

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Nne - Tarehe 20 Mei, 2016**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

**MWENYEKITI:** Hati za kuwasilisha Mezani, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:** Maswali.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 199

**Watoto Wenye Ulemavu Kuanza Shule Wakiwa na Umri Mkubwa**

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA** aliuliza:-

Elimu kwa watoto wenye ulemavu hupatikana kwa vikwazo na matatizo mengi kiasi kwamba wengi huanza shule katika umri mkubwa ukilinganisha na watoto wasio na ulemavu:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuongeza umri wa kustaafu kwa lazima kuwa miaka 65 kwa watu wenye ulemavu?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa upendeleo maalum wa ajira kwa watu wenye ulemavu katika Wizara na Taasisi zake pale ambapo mtu mwenye ulemavu atakuwa na sifa stahiki wakati wa zoezi la ajira?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wenye ulemavu kuhusiana na mambo mbalimbali kama vile upatikanaji wa elimu na ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kwamba elimu na ajira ni baadhi ya mambo muhimu kabisa yenye uwezo wa kumtoa mtu mwenye ulemavu kutoka katika hali ya unyonge na utegemezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, napenda kujibu swali namba 199 lenye sehemu (a) na (b) lililoulizwa na Mheshimiwa Dkt. Ely Macha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya Mwaka 2002, umri wa kustaafu kwa lazima kwa mtumishi ni miaka 60. Hata hivyo, suala la kuongeza umri wa kustaafu kwa watumishi wenye ulemavu litategemea mabadiliko ya sera na hasa kwa kuzingatia maoni ya wadau na ushauri mwingine utakaotolewa kulingana na uhalisia wa suala hilo.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetoa upendeleo maalum wa ajira kwa watu wenye ulemavu katika Wizara, Taasisi zake na Mashirika yasiyo ya Kiserikali pale ambapo mtu mwenye ulemavu anakuwa na sifa stahiki za ajira wakati wa zoezi la ajira. Kwa mujibu wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na. 9 ya mwaka 2010, kifungu cha 31(2) kinaeleza wazi kwamba kila taasisi au sekta binafsi yenye watumishi wapatao 20 basi asilimia tatu wawe ni watu wenye ulemavu.

Aidha, kifungu cha 32 cha Sheria hii kinaeleza kuwa kwa madhumuni ya kuendeleza na kulinda ajira ya watu wenye ulemavu, kila mwajiri anatakiwa

kufanya bidii ya kuendeleza ajira ya watu wenye ulemavu katika eneo lake la kazi. Serikali itaendelea na inaendelea kufuatilia utekelezaji wa sheria hii ili ajira za watu wenye ulemavu ziweze kupatikana kwa kuzingatia sheria na taratibu za ajira nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Macha swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ELLY M. MACHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sikuridhika sana na jibu lililotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri hasa katika kipengele (a). Kwa ajili hiyo basi, naomba kumuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, ni lini basi mchakato wa mabadiliko ya sheria utafanyika ili kuhakikisha kwamba sheria inawapigania watu wenye ulemavu kwa kuwaongezea umri wa kustaafu kwa kuwa umri wao wa kuanza shule unakua umechelewa ili waweze kupata nafasi ya kufanya kazi zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni *mechanism* gani ambayo Serikali imeweka katika kuhakikisha kwamba taasisi zake pamoja na sekta binafsi zinatenga asilimia tatu katika kila waajiriwa 20? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Elly Macha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza la ni lini, lazima niseme kwamba siwezi nikatoa *specific date* kwa sababu ili kubadilisha umri wa kustaafu kuna watu wengine wanahusika kama waajiri, taasisi zinazohusiana na hifadhi za jamii na watu wenye ulemavu wenyewe. Tayari *assignment* ya kwanza kuifanya baada ya kushika nafasi hii ilikuwa ni kukutana na watu wenye ulemavu na moja ya mambo ambayo tulikubaliana ni kwamba walete maoni yao yote ambayo yatapelekea kubadilishwa kwa Sheria Na. 9 ya mwaka 2010 ili kuboresha baadhi ya mambo yakiwemo masuala yanayohusiana na ajira kwa watu wenye ulemavu kwa sababu tunaamini katika ile *principle* inayosema *nothing for us without us* ambayo ni muhimu sana kwa watu wenye ulemavu. Kwa sababu maoni yao yanafanyiwa kazi siwezi nikatangulia kabla ya kupata maoni yao kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niseme tu natambua kwamba wako baadhi ya watu wengine walianza kufanya hivyo mwaka 2003 nchini Kenya, umri wa kustaafu wakati huo ulikuwa ni miaka 55 kwa lazima kwa watu wenye ulemavu ilikuwa ni miaka 60 lakini mwaka 2009 ikabadilishwa. Serikali ya Kenya

ilivyosema umri wa kustaafu kwa lazima ni miaka 60, mwaka 2013 ilipelekwa *Bill* ya kutaka kuongeza umri wa kustaafu kwa watumishi wenye ulemavu Kenya kufikia miaka 65 lakini mpaka navyozungumza *Bill* hii bado haijafanyiwa mabadiliko kutokana na sababu mbalimbali za kitaalamu zinazosababisha review ya sheria hiyo kuwa ngumu kidogo. Hata hivyo, hilo ni wazo zuri na tutalifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu mkakati uliowekwa, sheria imeonyesha wazi na tayari tumeshatoa maelekezo kwamba waajiri wote ni lazima watekeleze hili na Maafisa Kazi wanapokwenda kusimamia utekelezaji wa sheria baadhi ya mambo ambayo wanapaswa kuuliza ni utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ikiwemo *percentage* na mambo mengine kama *reasonable accommodation*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Elly Macha kwamba Serikali inafuatilia kwa makini usimamizi wa sheria hii kwa hiyo asiwe na wasiwasi wowote ule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana ambayo ameyaweka mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulihakikishia Bunge lako kwamba wakati tunatunga sheria hii kwa ajili ya kuhakikisha kwamba watu wenye ulemavu wanapata haki sawa katika nchi yetu, kifungu cha 12(1)(a) cha sheria hiyo kinalipa nguvu na mamlaka Baraza hili la Watu Wenye Ulemavu kuangalia matatizo na mambo mengine yote ambayo yamekuwa yakiwakumba watu wenye ulemavu nchini na kutoa mapendekezo na kuishauri Serikali nini cha kufanya. Kwa sababu tumeendelea kutenga fedha za kulifanya Baraza hili liwe linakutana, ningeshauri sana tufanye kazi kwa karibu na Baraza na yale ambayo wanayaona ni mambo ambayo yanatakiwa yafanyiwe mabadiliko ya kisheria, ya kikanuni na vitu vingine, basi wanaweza kulitumia lile Baraza tukashauriana na Serikali na tukaona lini na namna gani tunaweza tuka-consider hayo mambo ambayo ni ya msingi sana katika kuweka *welfare* ya walemavu nchini. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza Mheshimiwa Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *disability is not inability*. Kwa muda mrefu tumepiga kelele sana kwamba majengo hasa madarasa yawe *disability*

*friendly* ili watoto wenye ulemavu waweze kusoma, lakini mpaka leo tunashuhudia madarasa yanajengwa hayana ngazi za kuwasaidia au *ramps* ili hawa watoto waweze kusoma kama wenzao na kwa kufanya hivyo suala la kwamba waongezewe muda wa kustaafu halitakuwepo. Serikali inatoa kauli gani kuhakikisha kwamba majengo yote ya Serikali yanakuwa *disability friendly* ili watoto waweze kuingia madarasani toka wakiwa na umri mdogo? (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu wazi kwamba dhana ya elimu shirikishi au dhana ya kushiriki katika shughuli mbalimbali za jamii kwa watu wenye ulemavu inaendana kabisa na kubadilisha mazingira ili kumfanya mtu mwenye ulemavu afike pale anapotaka bila vikwazo vyovyote vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Ofisi ya Waziri Mkuu ilishatoa maagizo kwa Halmashauri mbalimbali ambazo zinahusika na ujenzi wa miundombinu mbalimbali kuhakikisha kwamba majengo yanayojengwa hasa ya shule yanakuwa ni shirikishi, yana hali ya kumfanya mtu mwenye ulemavu afike bila matatizo yoyote darasani. Siyo tu kwamba yalikuwa maagizo bali hilo ni takwa la Sheria Na. 9 ya mwaka 2010. Kwa hiyo, niseme tu kilichobakia ni kufuatilia utekelezaji wa sheria hiyo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 200

### **Ahadi ya Kulipa Wazee Pensheni**

**MHE. SAUMU H. SAKALA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza ahadi yake ya kuanza kuwalipa wazee pensheni?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaanza kutekeleza ahadi yake ya kuwalipa pensheni wazee mara baada ya maandalizi ya utekelezaji wake kukamilika. Maandalizi hayo ni pamoja na kuunda vyombo vya usimamizi wa mpango huo katika ngazi zote, kuweka mfumo na miundombinu muhimu kwa ajili ya kutekeleza mpango huo, kufanya utambuzi na usajili wa walengwa,

kutoa elimu kwa umma na kujenga uwezo wa watendaji wa mpango. Vilevile maandalizi haya yatahusu maandalizi ya ziada kama vile rasilimali fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu mkubwa wa mpango huu ndiyo maana inalishughulikia suala hili kwa umakini mkubwa ili tu mara utekelezaji wake utakapoanza uwe endelevu na wenye manufaa kwa wazee nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakala swali fupi la nyongeza.

**MHE. SAUMU H. SAKALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Suala hili la wazee kulipwa pensheni kila siku limekuwa likitajwa, lakini nashangaa kidogo nikisikia bado hata hayo maandalizi hayajaanza. Je, Serikali inaweza kusema nini kinakwamisha maandalizi hayo ambayo mpaka sasa hayajaanza na kwa kutambua umuhimu huo wa wazee?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, maandalizi hayo yataanza lini na yatamalizika lini? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Saumu Heri Sakala, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza limeuliza ni nini kinakwamisha. Kwanza kabisa nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ina dhamira njema kabisa ya kuhakikisha inatekeleza ahadi yake ya kuwalipa pensheni wazee kwa kutambua mchango mkubwa ambao wazee wameutoa katika Taifa hili katika sekta za huduma za jamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa hiyo, Serikali inatambua kabisa umuhimu wa wazee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kinachokwamisha hapa si kwamba kuna jambo ambalo linakwama, lakini mipango ya Serikali ilikuwa kwanza kuhakikisha inatengeneza miundombinu ambayo ndiyo itakwenda kulifanya jambo hili liwe endelevu. Kwa hiyo, katika uratibu wa zoezi zima, awali ilikuwa ni kutayarisha mpango rasmi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mpango huu unaanza kufanyiwa kazi na tayari mpango huu umekamilika zimebaki hatua chache tu za kuona ni namna gani mpango huu utaanza sasa kutekelezwa pale ambapo mamlaka husika zitahusishwa na fedha zitakuwa zimepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ameuliza ni lini itaanza. Nirudie tu katika jibu langu la msingi kwamba zoezi hili ni kubwa sana ambalo linahitaji umakini mkubwa sana na lengo la Serikali ni kulifanya kuwa endelevu. Hata

katika baadhi ya nchi ambazo wamefanya zoezi hili kwanza kabisa walifanya namna ambavyo ilikuwa inawapa picha waanzaje ndiyo baadaye waje walikamilishe kwa uzito wake. Kwa hiyo, na sisi kwa kutambua kwamba jambo hili ni kubwa na linahitaji rasilimali fedha, Serikali imeanza kwanza na ujenzi wa miundombinu ya kuratibu zoezi zima ili baadaye kuweza kuwafikia wazee hawa kwa maana ya kuwalipa pensheni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia jambo hili tulikwenda kujifunza katika baadhi ya nchi ambazo zimefanikiwa sana. Ukienda kule Nepal ambao ni kati ya watu waliofanikiwa, wana kitu wanakiita *Nepal's Senior Citizens' Allowance* na wenyewe walianza katika utaratibu huu huu. Walianza kwanza kuwalipa wazee kuanzia umri wa miaka 60 lakini baadaye wakaona namna gani waweze kuingiza na makundi mengine. Kwa hiyo, na sisi tunatafakari mpango huu mzima lengo letu ni kuufanya mpango huu uwe endelevu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza mimi nasikitika kwa sababu Serikali inaonekana haina nia njema juu ya jambo hili. Mimi nikiwa Mbunge mwaka 2004 Serikali ilitoa majibu haya haya, mwaka 2008 Serikali ikatoa majibu haya haya, mwaka 2012 Serikali ikatoa majibu haya haya. Mimi ni Mbunge kwa kipindi cha nne sasa, nasikitika sana juu ya majibu yenu ambayo ... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali kwa ufupi naomba tafadhali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni moja tu, uzee na kuzeeka nani ataukwepa, hakuna na kila mmoja ni mzee mtarajiwa. Serikali ituambie sasa ina mkakati gani wa ziada na kama mlivyosema kuwa hatua chache zimebakia, hizo hatua chache ni zipi? Je, ndani ya miezi mitatu mnaweza kumaliza suala hili ili wazee wapate pensheni zao hasa ukizingatia na wale baadhi waliopigana Vita vya Kagera? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE WALEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masoud, lakini nikiendelea kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina nia ya dhati ya jambo hili na ndiyo maana katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 jambo hili limewekwa na kutafsiriwa vizuri sana. Kipindi cha nyuma jambo hili halikuwa limechukua picha ya kutosha kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama

cha Mapinduzi. Hiyo tu kwanza ni nia ya dhati ya Serikali kuhakikisha jambo hili linatekelezeka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri hapa ameeleza vizuri sana na naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba suala hili sio la kulala na kuamka ndani ya miezi mitatu halafu ukasema unaanza tu kulipa pensheni, hapana.

Narudia kusema Serikali imeshaanza kutengeneza miundombinu ya kulifanya jambo hili liweze kutekelezeka.

Sheria inayompa mamlaka Mdhibili wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, kifungu cha 5(1)(e), kimemuagiza na kumwelekeza Mdhibili kuhakikisha anasimamia suala zima la kuona namna gani Watanzania wengi wanafikiwa na sekta ya hifadhi ya jamii ikiwemo wazee.

Kwa hiyo, naomba kulihakikishia Bunge lako Tukufu Serikali inalifanyia kazi suala hili na mara litakapokamilika litaanza kuchukua nafasi yake na wazee watapata pensheni. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Na. 201

### **Kukipandisha Hadhi Kituo cha Afya cha Mangaka**

**MHE. CECILIA D. PARESSO (K.n.y. MHE. WILLIAM D. NKURUA)** aliuliza:-

Wilaya ya Nanyumbu ilianzishwa mwaka 2005 lakini mpaka sasa haina Hospitali ya Wilaya hivyo kuwalazimu wananchi kufuata huduma hiyo katika Hospitali ya Wilaya ya Masasi lakini pia kumekuwa na jitihada za kuomba kukipandisha hadhi Kituo cha Mangaka kuwa Hospitali ya Wilaya ya Nanyumbu lakini mpaka sasa hakuna mafanikio yoyote.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kukipandisha hadhi kituo hicho ili kuwa Hospitali ya Wilaya na kunusuru afya za wananchi wa Nanyumbu hasa akina mama wajawazito kwa kulazimika kupelekwa Wilaya jirani ya Masasi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.



**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Dua Nkurua, Mbunge wa Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha Wilaya ya Nanyumbu inakuwa na Hospitali ya Wilaya, tayari Serikali imetoa kibali na kupandisha hadhi Kituo cha Afya cha Mangaka kuwa Hospitali ya Wilaya baada ya kukidhi vigezo na taratibu zilizowekwa. Kibali hicho kimetolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia barua ya tarehe 27 Februari, 2016. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kuuliza ...

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Nimefika.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

**MHE. WILLIAM D. NKURUA:** Nimefika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso naomba uendelee.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walikuwa wakizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pareso naomba uendelee.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hospitali zetu mbalimbali nchini zina upungufu mkubwa wa dawa, je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha dawa za uhakika zinapatikana katika hospitali zetu nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali dogo la pili, kwa kuwa MSD pia inaidai Serikali fedha nyingi, je, ni lini Serikali itahakikisha inalipa deni la MSD? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Cecilia Paresso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulivyoeleza hapa katika vipindi tofauti, jukumu kubwa la Serikali ni kuhakikisha tunaondoa upungufu wa dawa na vifaa tiba. Katika swali la kwanza linalosema Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba dawa zinapatikana, ni kama tulivyoeleza hapo awali kwamba jukumu letu kubwa hivi sasa ni kuhakikisha kwanza tunajielekeza zaidi katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipindi tofauti nimesema kwamba ukusanyaji wa mapato kwa kutumia mifumo ya kielektroniki ni kuongeza ukusanyaji wa fedha katika hospitali, zahanati na vituo vyetu vya afya. Tutakapofanya hili kwa upana wake maana yake ni kwamba vituo vya afya vitakuwa na dawa za kutosha kwa sababu mwongozo unasema jinsi gani pesa zinazopatikana zitaenda kwenye ununuzi wa dawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la deni la MSD Waziri wa Afya alipokuwa aki-*table* bajeti yake na katika mijadala mipana iliyojitokeza imejielekeza kuhakikisha deni la MSD linalipwa lengo likiwa ni MSD kuwa na uwezo wake wa kusambaza dawa. Waziri wa Afya alieleza suala hili kwa upana sana na Wizara ya Fedha ilichukua *commitment* ya kuhakikisha kwamba MSD deni lake linalipwa ili mwisho wa siku MSD iweze kusambaza dawa katika hospitali, zahanati hali kadhalika vituo vya afya na hospitali za mkoa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwamoto swali la nyongeza.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa swali la msingi lilikuwa linahusu kuhusu kupandisha vituo vya afya; na kwa kuwa Wilaya ya Kilolo toka ilipoanzishwa mwaka 2000 haijawahi kuwa na hospitali ya Wilaya, imekuwa na Kituo cha Afya cha Dabaga na hivyo imepelekea ili wananchi kufuata huduma za hospitali inabidi waende Ilula kilometa zaidi ya 120.

Je, Serikali sasa haioni kuna umuhimu wa kupandisha hadhi kituo hicho cha Dabaga kuwa hospitali ya wilaya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwamoto, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba tupokee huo mtazamo kwamba Kilolo hakuna Hospitali ya Wilaya kwa hiyo ina maana lazima watu waende Ilula kwa ajili ya kupata matibabu. Nilieleza hapa katika vipindi tofauti kwamba mchakato wa kupandisha ama Zahanati kuwa Kituo cha Afya au Kituo cha Afya kuwa Hospitali ya Wilaya kuna utaratibu wake muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wake unaanzia kwenye WDC kwa maana ya Mabaraza ya Madiwani mwisho wa siku unafika Wizara ya Afya ambao ndiyo wenye dhamana. Wizara wakishafanya uhakiki kwamba kituo hicho kimekidhi kuwa hospitali ya wilaya basi inapandishwa moja kwa moja kama nilivyozungumzia katika suala la wenzetu wa Nanyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo haya, naomba nimuelekeze Mheshimiwa Mbunge kwa sababu najua yupo makini sana katika Kamati ya TAMISEMI, ahakikishe kwamba ule mchakato wa awali unaenda na kuangalia vigezo vinafikiwa mwisho wa siku na sisi TAMISEMI tutaweka nguvu na Wizara ya Afya wataangalia vigezo vikikubalika kituo hicho cha afya kitapandishwa hadhi lengo kubwa likiwa ni kuwafikia wananchi kwa karibu zaidi. Ni kweli haiwezekani wala haiingii akilini mwananchi kutembea kilometa 100, ni umbali mkubwa sana.

Kwa hiyo, hili ni jambo la msingi na naomba mchakato uendeleo kwa kufuata utaratibu unaoelekezwa, nadhani Serikali italiangalia kwa jicho la karibu zaidi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 202

### **Ukosefu wa Vifaa Tiba Hospitali ya Makambako**

**MHE. DEO K. SANGA** aliuliza:-

Serikali ilipandisha hadhi Kituo cha Afya cha Makambako kuwa Hospitali lakini tatizo kubwa lililopo ni ukosefu wa vifaa tiba na kufanya watu wengi kwenda kutibiwa Kibena, Njombe au Ilembula.

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa hivyo ili watu wasipate taabu ya kwenda kutibiwa Kibena, Njombe au Ilembula?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mbunge wa Makambako, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupandisha hadhi Kituo cha Afya Makambako kuwa Hospitali, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilitoa vifaa mbalimbali vikiwemo vifaa vya umeme chumba cha upasuaji, kitanda cha kufanyia upasuaji na seti tatu za vifaa vya upasuaji akina mama wajawazito na seti mbili za upasuaji mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizo, tukiri kwamba bado upo upungufu wa vifaa kama vile *X-ray, Ultrasound, ECG machine* na mashine ya dawa za usingizi, *pulse oxymeters, monitors*, seti ya mashine ya kufulia nguo na vifaa vya meno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 imetenga shilingi milioni 20.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba kupitia vyanzo vya mapato ya ndani. Aidha, Halmashauri imepanga kukopa shilingi milioni 154.2 kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanga swali la nyongeza.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru majibu mazuri ya Waziri ya kutununulia baadhi ya vifaa vya upasuaji ili tupate huduma hii. Kama nilivyosema vifaa hivi vimekaa tu haviwezi kufanya kazi, ni sawa na mifugo umechukua majike umeyaweka hujapeleka madume hakuna kitu ambacho kitaendelea pale. Serikali haioni sasa uko umuhimu wa kupeleka kwa mfano hizi dawa za usingizi ili shughuli za upasuaji ziweze kuanza? (Makofi)

Mheshimiwa mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Rais alipopita pale aliahidi kuwaondolea kero wananchi wa Makambako ili wasiende kufanyiwa upasuaji Njombe na Kibena kama nilivyouliza kwenye swali la msingi. Hawaoni sasa iko haja ya kuchukua fedha za dharura kununua vifaa hivi pamoja na vile vilivyopeleka ili shughuli za upasuaji zianze?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deo Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nikiri nilifika pale Makambako na nikaenda mpaka Hospitali ya Kibena wakati nilipotembelea Makambako mpaka Njombe. Kihistoria ni kwamba watu wa Makambako walikuwa wakitibiwa katika Hospitali ya Kibena na ni kweli Hospitali hii inakabiliwa na changamoto kubwa sana na nimshukuru Mbunge kwa kweli lazima niweke wazi, ni miongoni mwa Wabunge ambao kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana na nilitembelea mpaka miundombinu ambayo yeye mwenyewe alishirikiana na halmashauri yake kuiweka sambamba na miundombinu ya elimu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tunakupongeza kwa hilo kama Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwamba vifaa viko pale havifanyi kazi ni kweli na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema vifaa vile havifanyi kazi. Pia hata lile jengo nadhani ukarabati ulianza kufanyika na hata mfumo wa maji zile koki zenyewe zilikuwa hazifanyi kazi vizuri. Kulikuwa kunatakiwa koki maalum ambazo unagonga kwa mkono inafunguka badala ya kushika ku-avoid contamination. Zoezi hilo limeenda vizuri ikiwa ni pamoja na urekebishaji wa mitaro, lakini changamoto kubwa pale imekuwa ni fedha. Jukumu letu kubwa ni kuhakikisha ile bajeti iliyotengwa iweze kufika angalau lile jengo lifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia amesema wazi Mheshimiwa Rais alipita kule wakati wa kampeni na aliahidi kushughulikia hospitali ile ya Makambako ili ifanye kazi vizuri. Kuhusu kutenga pesa za dharura, mimi nasema jukumu letu kubwa katika kipindi hiki cha mwaka wa fedha tunaoenda nao ile bajeti ambayo ilielekezwa kwenda pale ambayo kwa bahati mbaya haijafika vizuri basi tutawasiliana ndani ya Serikali yetu ili iweze kwenda. Sasa hivi tumesema tumeongeza sana ukusanyaji wa mapato tutahakikisha yale mapato yanayokusanywa kwa zile bajeti zilizopangwa ambazo pesa hazijapelekwa ziweze kupelekwa ili miradi iweze kutekelezeka na wananchi wapate huduma.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mzee Deo Sanga naomba nikiri kwamba tutakuwa pamoja kuhakikisha kwamba wananchi wa Makambako hasa tukijua ni center kubwa sana kwa watu wa Mbeya na Songea, tutasaidia eneo lile liweze kupata huduma bora za afya. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tatizo la afya au linalohusiana na zahanati kwa ujumla linagusa maeneo mengi katika nchi hii ya Tanzania. Mojawapo ni Zahanati ya Nduruma iliyopo katika Kata ya Nduruma, Wilaya ya

Arumeru. Zahanati hii imepandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya lakini hakuna jengo la upasuaji, hakuna vifaa na inahudumia vijiji karibia kumi. Je, Waziri anatuambia nini kuhusiana na kituo hiki cha afya ambacho hakina vifaa na wananchi wanalazimika kwenda Hospitali ya *Mount Meru* iliyoko mkoani Arusha?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Mollel, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wiki moja iliyopita Mheshimiwa Amina Mollel aliniambia kuhusu zahanati hiyo ambayo imepandishwa hadhi kuwa Kituo cha Afya na mimi nilimpa ahadi kwamba tutafanya kila liwezekanalo, huenda kabla Bunge hili halijaisha tutafika pale Arusha kuangalia zahanati hii. Pia ameniambia mambo mengine zaidi kwamba wataalam wengine wameondoka na zahanati ile haifanyi kazi. Naomba nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza safari yetu itakuwa palepale mimi na yeye, tutaenda pale Nduruma kuona changamoto za zahanati ile kwa karibu zaidi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wale kutoka pale kwenda *Mount Meru* na Arusha ni jiji linalokuwa na *population* inaongezeka. Ni lazima maeneo ya pembeni tuyaimarishe ili kupunguza ile *referral system* kwamba siyo kila mtu ugonjwa mdogo aende katika Hospitali ya Wilaya. Serikali kupitia TAMISEMI na tutakapokwenda pamoja tutahakikisha ule upungufu tunaubaini na kupanga mpango mkakati wa jinsi gani tutafanya ili kituo hiki cha afya kiwe na vifaa tiba na wataalam kiweze kutoa huduma katika maeneo hayo na kata zinazokizunguka. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango.

Na. 203

### **Hitaji la Benki na Mafunzo kwa Wanawake Wajasiriamali**

**MHE. ZAYNABU M. VULU (K.n.y. MHE. ANNA R. LUPEMBE)** aliuliza:-

Wanawake wengi wa vijijini hawakopesheki kwa sababu benki haziwafikii huko vijijini lakini pia hawana mafunzo maalum ya kuwasaidia ujuzi wa namna ya kufikia huduma hiyo ya kukopeshwa.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka huduma ya benki kwenye vijiji ili wanawake wa huko waweze kupata mikopo?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa akina mama hao mafunzo maalum yatakayawasaidia katika kujipanga kukopa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mipango ya Serikali kupeleka huduma ya benki kwenye vijiji ili wanawake waweze kupata mikopo, napenda ikumbukwe kwamba kufuatana na mabadiliko ya mfumo wa kifedha nchini unaotekelezwa tangu mwaka 1991, Serikali imejitoa katika kuhusika moja kwa moja na uendeshaji wa shughuli za benki na badala yake Serikali inafanya juhudi mbalimbali za kuboresha mazingira ya utoaji huduma za kibenki ili huduma hizi ziwafikie wananchi wengi. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania, Serikali imefanya msukumo wa kuhakikisha kuwa huduma za kibenki zinawafikia wananchi ili kurahisisha shughuli zao mbalimbali za kiuchumi mijini na vijijini. Benki kadhaa zimeanzisha huduma za kibenki kupitia mawakala na huduma za kifedha kupitia simu za mkononi ambazo zimewasaidia sana wananchi sehemu ambako hakuna matawi ya benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Benki Kuu inaendelea kuweka mazingira wezeshi na taratibu rafiki ili kusaidia nguvu za wananchi na sekta binafsi kuanzisha benki au taasisi za fedha. Juhudi hizi zimesaidia wananchi kuanzisha benki za kijamii na taasisi ndogondogo za fedha katika maeneo yao. Ni matarajio ya Serikali kuwa wananchi watatumia fursa ya mazingira mazuri ya uwekezaji yaliyopo hapa nchini kuwekeza wao wenyewe au kuzishawishi benki kuanzisha huduma za kibenki katika maeneo yao. Aidha, Serikali pia itaendelea kushawishi benki nchini kupanua shughuli zao ili ziwafikie wananchi wengi hasa wale wa vijijini wakiwemo akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikishirikiana na Benki Kuu ipo tayari kutoa mafunzo maalum ya elimu ya fedha kwa wananchi wote wakiwemo akina mama. Benki Kuu kupitia Kurugenzi yake ya Utafiti na Uchumi ina mpango wa kuelimisha umma (*consumer literacy program*) kuhusu utumiaji wa huduma za kifedha nchini ili kuleta uelewa mpana wa upatikanaji wa huduma za kifedha ikiwemo taratibu zinazohusu mikopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaynabu swali fupi la nyongeza.



**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza ni kutaka kujua Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia akina mama walioanzisha VICOBA kwa kuongezewa mtaji wao? Pia Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha taasisi binafsi zinazotoa mikopo kuacha kunyanyasa akina mama wanapochelewa kulipa mikopo yao kwa kuwanyang'anya vifaa vyao vya matumizi na vinavyowaendeshea maisha? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni lini Serikali itashawishi mabenki kutupelekea benki kwenye Wilaya ya Mafia na Jimbo la Utete? Kwa sababu Makao Makuu ya Wilaya ya Rufiji ni Utete lakini mpaka leo hapo Utete hakuna huduma inabidi waende Kibiti kufuata huduma. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili japo yameonekana kama manne ya Mheshimiwa Zaynabu Vulu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza ni akina mama kuongezwa mtaji kwa kuwa wameanzisha VICOBA. Kwanza kabisa naomba niwapongeze akina mama wote nchini kwa kuonesha ujasiri wao katika kuungana katika vikundi na kuanzisha VICOBA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba Serikali imeweka mazingira mazuri na tayari taasisi za kifedha au benki za jamii zinaanzishwa hivyo nawashauri akina mama hawa na mimi nitashirikiana nao kama mama kuhakikisha kwamba tunaanzisha taasisi au benki yetu ya kijamii ya wanawake sehemu yoyote ile. Naomba nitoe nafasi hiyo, tushirikiane kwa pamoja Wabunge wanawake ili tuweze kuungana na akina mama hawa kuanzisha benki ya wanawake ya kijamii sehemu yoyote ile ndani ya nchi yetu ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ya swali hili la kwanza ilikuwa ni taasisi za kifedha zinazokopesha ziache kuwanyanyasa akina mama. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kama nilivyojibu wiki moja iliyopita Serikali inaanzisha rasimu ya sera kwa ajili ya taasisi hizi ndogo za fedha ili sasa kuweza kuzikagua na kuziwekea sheria na taratibu ya kuweza kufanya kazi na kuacha kuwanyanyasa akina mama. Sera hii itakapokuwa tayari, nina uhakika kabisa taasisi hizi zitaacha kuwanyanyasa akina mama. Pia naomba niwashajihishe taasisi zote hizi zinazotoa mikopo kwa akina mama ziache utaratibu huu wa kuwanyanyasa akina mama. Tufuate taratibu zote za utoaji



wa mikopo kama vile kuangalia uwezo wa mlipaji anayekopa kabla hujamkopesha kuliko kumkopesha tu kwa kuonekana wako kwenye kikundi halafu baadaye unakuja kuwanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, nilisema ameuliza maswali mawili lakini yanaonekana kama manne, kwa hiyo, kulikuwa na *sub-questions*. Napenda kulijibu swali hili, kwamba ni lini Serikali itaweza kuzishawishi benki kupeleka matawi yao Mafia na Rufiji?

Namuomba Mheshimiwa Zaynabu Vulu tushirikiane tuone ni jinsi gani ya kuongea na benki zetu na hasa benki yetu ya NMB na CRDB, nina uhakika wakienda ku-access mazingira ya Mafia wataenda kufungua tawi lao sehemu hii. Naomba tukae na Mheshimiwa Zaynabu Vulu tuone ni jinsi gani ya kushughulikia suala hili.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Na. 204

### **Maafisa Uhamiaji katika Balozi Zetu**

**MHE. SALUM MWINYI REHANI (K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA AMJADI)**  
aliuliza:-

Hapo kwanza Maafisa Uhamiaji wetu walikuwa wakipelekwa kwenye Balozi zetu kufanya kazi ya kutoa viza kwa wageni wanaotaka kuja Tanzania lakini hivi sasa Maafisa hao hawafanyi tena kazi hiyo na badala yake kazi hizo zinafanywa na Maafisa wa Wizara ya Mambo ya Nje na hutoa viza hata kwa waombaji wasiotakiwa kupewa:-

(a) Je, kwa nini Maafisa hao wa Uhamiaji waliondolewa kwenye Balozi hizo?

(b) Je, ni sahihi kwa Maafisa wa Mambo ya Nje kufanya kazi za kutoa viza kwa wageni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, lenye sehemu mbili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Balozi zake mbalimbali nje ya nchi na Ofisi za Wawakilishi wa Heshima (*Honorary Consuls*) imeendelea kutoa huduma ya viza kwa wageni mbalimbali wanaokusudia kusafiri kuja nchini Tanzania kwa madhumuni mbalimbali. Kazi ya kutoa viza hufanywa na Maafisa wa Serikali ambao wapo Ubalozini kwa nchi zenye Uwakilishi wa Kibalozi na Wawakilishi wa Heshima (*Honorary Consuls*) kwa maeneo ambayo Tanzania haina uwakilishi wa Kibalozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi huwa na Maafisa wa aina mbalimbali wakiwemo Maafisa Mambo ya Nje, Maafisa kutoka Idara ya Uhamiaji, Waambata Jeshi pamoja na Maafisa kutoka Idara mbalimbali za Serikali kwa kadri ya mahitaji ya Ubalozini husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, sehemu kubwa ya Maafisa katika Ofisi za Ubalozini huwa ni Maafisa wa Mambo ya Nje. Kutokana na Idara ya Uhamiaji kutokuwa na Maafisa Uhamiaji katika baadhi ya Balozi zake, kazi ya utoaji viza katika baadhi ya Balozi zisizo na Maafisa wa Uhamiaji hufanywa na Maafisa wa Mambo ya Nje. Kazi hiyo huongozwa na taratibu na misingi maalum ya kisheria kama ilivyocainishwa katika Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Maafisa Uhamiaji katika Balozi hizi ni kama ifuatavyo:-

- (i) Utoaji wa viza kwa wageni wanaotaka kutembelea Tanzania;
- (ii) Kushughulikia pasi za kusafiri za Watanzania wanaoishi katika nchi za uwakilishi;
- (iii) Kutoa hati za kusafiria za dharura kwa Watanzania walipoteza pasi zao za kusafiria au ambao wameingia nchi za uwakilishi bila pasi za kusafiria;
- (iv) Kutembelea magereza zenye wafungwa ambao ni raia wa Tanzania; na
- (v) Kuthibitisha uraia wa wageni ambao hufika Ubalozini na kujitambulisha kuwa ni Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji wa Maafisa Uhamiaji katika Balozi zetu hufanywa na Idara ya Uhamiaji. Maafisa hao hupangwa katika Balozi zetu kulingana na mahitaji ya Idara hiyo. Mathalani Idara ya Uhamiaji iliwatambuliwa Bwana Sylvester Ambokile aliyekuwa Afisa Uhamiaji London na kuteuliwa kuwa Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Makao Makuu na Bwana Johari Sururu ambaye alikuwa Afisa Uhamiaji Abu Dhabi na kuteuliwa kuwa Kamishna wa Uhamiaji

Zanzibar. Hivyo, jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni kuwezesha maafisa hawa kutekeleza majukumu yao pindi wanapokuwa vituoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kama ilivyokwishaelezwa si Balozi zote za Tanzania nje ya nchi zina Maafisa Uhamiaji. Hivyo, uwepo wa Maafisa Mambo ya Nje au Maafisa wengine wa Serikali katika Balozi hizo wanaotoa viza kwa wageni mbalimbali wanaokusudia kuja Tanzania hauna madhara yoyote kwa kuwa shughuli hiyo hufanywa kwa kuongozwa na utaratibu na misingi maalum ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu haina taarifa inayoonyesha kuwa kuna Maafisa Mambo ya Nje ambao wamekuwa wakitoa viza kwa waombaji wasiostahili katika Balozi zetu zilizo nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ussi Pondeza swali la nyongeza. Hayupo?

**MBUNGE FULANI:** Hana?

**MWENYEKITI:** Hana. Haya Mheshimiwa Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuuliza swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wetu wanavyokwenda katika nchi ya Zambia hasa katika Jimbo la Copperbelt wamekuwa wanakamatwa wakiwa *stand* na wanapelekwa gerezani bila kupelekwa Mahakamani. Je, Serikali inasema nini kuhusiana na jambo hili kwa sababu kuna vijana wengi sana ambao wako magereza na hawajapelekwa Mahakamani mpaka sasa hivi? Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili nalipokea na Wizara yangu pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani tutalifanyia kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona. Pamoja na hawa *professional staff* kutofanya kazi zinazopaswa katika Balozi zetu, mimi nilitaka kujua tu *effectiveness* ya *commercial attaché* wetu katika balozi hizo kwa sababu wako *dormant*. Kujumla nataka kujua suala zima la utalii pamoja na uwekezaji katika kuongeza pato la Taifa na vilevile kuitangaza nchi linashughulikiwa vipi na Balozi zetu? Naomba majibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza za Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, amelisema kwa ujumla kwamba kama kuna watu wanapelekwa ambao siyo taaluma yao wanafanya hawafanyi kazi vizuri lakini vilevile amesema kwamba baadhi ya Maafisa huwa hawatekelezi kazi zao vizuri. Kama anavyojua hii ni Wizara mpya, sasa hivi kuna mpango wa kuwaangalia hawa Maafisa wote na kupima utendaji kazi wao na wale ambao wataonekana hawatekelezi kazi zao vizuri tutawarudisha na kuwapeleka wale ambao wanastahiki.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Na. 205

### **Askari Kuboreshewa Makazi yao**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA (K.n.y. MHE. DEVOTHA M. MINJA)** aliuliza:-

Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza wanaishi katika nyumba chakavu zisizokuwa na hadhi ikilinganishwa na kazi zao wanazofanya kwa jamii:-  
Je, Serikali ina mpango gani kuwaboresha makazi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yalivyowahi kujibiwa maswali kadhaa ndani ya Bunge lako Tukufu kuhusu askari kuboreshewa makazi, Serikali inafahamu kuwa lipo tatizo la baadhi ya askari wa Jeshi la Magereza na Polisi

kuishi katika nyumba chakavu zisizokuwa na hadhi. Namwona rafiki yangu hapa anashusha kichwa ananyanyua. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na tatizo hilo, Serikali imeendelea na mpango wake wa kuzifanyia ukarabati mkubwa baadhi ya nyumba na kwenye baadhi ya magereza kujenga nyumba na vilevile kuendelea kuona mahitaji ya nyumba na hivi sasa ni nyumba 14,500 wakati zilizopo ni 4,221 hivyo kuwepo upungufu wa nyumba 10,279 ambao unalazimisha baadhi ya askari kuishi nje ya Kambi za Jeshi la Magereza. Hata hivyo, kasi ya utekelezaji wa mpango huu umekuwa ni mdogo kutokana na kuathiriwa na ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kupande wa Jeshi la Polisi, Serikali inakusudia kujenga nyumba 4,136 katika mikoa 17 ya Tanzania Bara na Zanzibar kama nilivyozungumza kwenye bajeti yetu. Aidha, Serikali itaendelea kutatua changamoto ya uhaba wa nyumba kwa kutumia njia mbadala ikiwemo mikopo yenye riba nafuu, Miradi Shirikishi (PPP) na kwa kutumia fedha za bajeti ya Serikali kadiri hali ya uchumi itakavyokuwa ikiimarika. Mkakati huu utakwenda sambamba na mipango. Nirudie tena, mkakati huu utakwenda sambamba na mipango ya maendeleo ya Serikali ikilenga kufikia idadi ya nyumba za makazi kwa askari wote waliopo sasa na watakaojiriwa baadaye. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ingawaje dah, Waziri kajibu kwa pozi kweli kweli mistari michache tu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, anasema kwamba wanaendelea kujenga, hivi miaka 51 ya Uhuru upungufu nyumba 10,000 wapewe miaka mingapi ili wamalize hili tatizo katika nchi yetu? Magereza nimeshuhudia mwenyewe kwa mfano katika Wilaya yetu ya Kilombero kuna magereza mawili ya Idete na Kiberege wafungwa wanaenda kujenga nyumba za watu binafsi kwa nini msitumie nguvu kazi ya wafungwa hawa ili kwenda kujenga nyumba na Serikali muongeze hela kule juu kumalizia majengo haya? Hiyo nguvu kazi ya hawa wafungwa walioko magerezani mtafanya lini huo mpango? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la Polisi yaani kama kuna tatizo kubwa ndani ya Mkoa wa Morogoro ni suala la nyumba za Polisi hasa Wilaya ya Kilombero likiwemo na Jimbo la Mlimba. Kwanza Wilaya ya Kilombero pale Ifakara kulikuwa na majengo ya Kituo cha Polisi, Mlimba hakuna kabisa wanategemea TAZARA...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ulize swali tafadhali.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Na zile nyumba zimeuzwa ule mwaka zilizouzwa nyumba za Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ulize swali kwa ufupi.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Sasa hivi hawana nyumba kabisa. Je, Serikali katika huo mpango wao wana mpango gani wa kujenga nyumba na Vituo vya Polisi ndani ya Wilaya ya Kilombero, Ifakara na Jimbo la Mlimba ambapo wanakaa kwenye vituo vya TAZARA?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu ni rafiki yangu sana. Ananiuliza tupewe miaka mingapi, yeye ana miaka mingapi? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza na nirudie tena tunafanya kila linalowezezana tuhakikishe askari wetu wanakuwa na mahali pazuri pa kukaa. Ndiyo jibu sahihi, tunafanya kila linalowezezana askari wetu wawe na mahali pazuri pa kukaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili nalo ni kwa sababu yeye ni rafiki yangu namjibu, mpango gani? Mpango nimeeleza kwenye jibu langu la msingi na nimhakikishie tu kwamba tutafanya kwa jinsi tulivyoeleza katika mpango wetu kuhakikisha kwamba askari wote wanapata nyumba nzuri na mahali pazuri pa kukaa. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**MWENYEKITI:** Kutokana na muda tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Na. 206

### **Kituo cha Redio Mwangaza Kuzuia Masafa ya Redio Nyingine**

**MHE. YAHAYA O. MASSARE** aliuliza:-

Kila Mtanzania ana haki ya kupata habari wakiwamo wananchi wa Itigi.

Je, kwa nini wananchi wa Itigi na maeneo ya jirani wananyimwa haki ya msingi kutokana na Kituo cha Redio Mwangaza kuzuia masafa ya redio nyingine ikiwemo Redio ya Taifa TBC na TBC FM?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua kuwa kila Mtanzania ana haki ya kupata habari wakiwemo wananchi wa Itigi. Upatikanaji wa matangazo yanayotolewa katika masafa ya mawasiliano ya FM hutegemea na ukaribu wa mahali kilipo kituo cha utangazaji husika. Itigi iko umbali mkubwa kutoka vituo vya utangazaji vinavyoweza kusikika katika eneo hilo. Kwa sasa Itigi ni moja ya maeneo ambayo mawasiliano ya vituo vya utangazaji vilivyo mbali hayapatikani vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Itigi ni Wilaya iliyoko Mkoa wa Singida takribani umbali wa kilometa zaidi 150 kutoka mji wa Dodoma na kama kilometa 100 toka Singida Mjini ambako vituo vingi vya redio vinarushia matangazo yake. Hii inafanya redio nyingi kutosikia vizuri eneo kubwa la Wilaya ya Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uwekezaji wa redio za FM ikiwemo TBC umefanyika katika miji ya Singida na Dodoma ambapo kitaalam mawimbi ya redio hufifia na kusababisha kutokuwepo na usikivu mzuri wa redio katika eneo la Itigi toka miji hiyo. Vilevile Redio Mwangaza imesimika mitambo ya kurusha matangazo (*booster stations*) Itigi katika kujikwamua na tatizo la usikivu usio wa uhakika toka Dodoma kwa kuzingatia masharti ya leseni katika eneo la Itigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhimiza TBC kusimika mitambo ya kurusha matangazo kwa ajili ya wakazi wa Itigi ili waweze kupata haki yao ya kupata habari.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahaya swali la nyongeza.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni haki ya kila mwananchi hasa Mtanzania kupitia kodi zao kusikiliza redio ya Taifa hasa TBC. Je, ni lini Serikali

sasa itaweka *booster* yake ya *TBC* katika Mji Mdogo wa Itigi ili na wananchi wale wasikie redio yao ya Taifa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kwenye gari yake yenye redio nzuri ili atakapofika Itigi asikie matatizo yaliyoko pale?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba usikivu wa redio hasa Redio ya Taifa pale Itigi siyo mzuri lakini hii imetokana na mabadiliko ya teknolojia kutoka *Mediam Waves (MW)* kwenda *FM*. *TBC* kwa sasa inamalizia zoezi la kufanya uchambuzi wa kuangalia mahali ambapo tunatakiwa kuweka *booster* na maeneo mengine tunalazimika kupeleka mtambo. Sasa ni lini usikivu utaboreka, ni pale utaratibu huu wa kufanya uchambuzi utakapokamilika na ni hivi karibuni kwa sababu tupo mwishoni kabisa, upembuzi ukimalizika tutaamua sasa Itigi tunaweka mtambo au *booster*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mimi kama Waziri wa Habari nipo tayari kuambatana naye na yeye anajua kwamba Singida ni nyumbani kwetu. Najua usikivu pale ni mbovu ndiyo maana tunafanya kila liwezekanalo kazi hii ikamilike mapema tuweze kuongeza usikivu wa Redio ya Taifa kwenye eneo la Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sevelina Mwijage.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa matatizo ya Itigi ni sawasawa na matatizo ya Wilaya ya Biharamulo hasa msitu tunaokatisha wa Kasindaga Muleba una matatizo ya mawasiliano na pale kuna *barrier* nyingi za maaskari ambao wanakaa pale saa zote. Ni lini Serikali itaweza kuwawekea mawasiliano pale hata mnara mmoja angalau wa Tigo au Vodacom?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASIALINO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha wa 2016/2017 Serikali ina mpango wa kupeleka mawasiliano maeneo yote ambayo yana matatizo ya mawasiliano. Moja kati ya eneo hilo ni hilo alilosema Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji.



Na. 207

## **Unyonyaji na Ukandamizaji Unaofanywa na Wachuuzi**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itasimamia kwa dhati sheria zake na kuondosha unyonyaji na ukandamizaji unaofanywa na wachuuzi kwa kununua mazao ya wakulima kwa utaratibu wa kufunga lumbesa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondokana na unyonyaji na ukandamizaji unaofanywa na wachuuzi, Serikali imeamua kufanya mapitio ya Sheria ya Vipimo, Sura ya 340 ili iendane na mazingira ya sasa. Lengo la Serikali ni kumlinda muuzaji kwa kuwadhhibiti wanunuzi wanaotumia njia za udanganyifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya sheria tajwa kwetu ni suala la kipaumbele. Katika kipindi kifupi kadri iwezekanavyo Wizara yangu itawasilisha mabadiliko hayo Bungeni ili Bunge lako Tukufu lifanye marekebisho yanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho ya Sheria ya Vipimo yaliyotajwa hapo juu, Wakala wa Vipimo imewasilisha kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, mapendekezo ya kutungwa kwa sheria ndogo (*by laws*) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zitakazowaongoza wakulima na wafanyabiashara kufungasha mazao kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo na Kanuni zake. Ili kurahisisha usimamizi wa matumizi ya vipimo rasmi katika ununuzi wa mazao, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitaainisha vituo maalum (*buying and selling centre*) katika vitongoji nchi nzima na kwa mazao yote na hivyo hakuna mfanyabiashara atakayeruhusiwa kusafirisha mazao ambayo yamefungashwa kinyume na Sheria ya Vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Wakala wa Vipimo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali za Mitaa itaanzisha vituo maalumu vya ukaguzi bila kusababisha usumbufu katika ufanyaji biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwatangazia Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuunga mkono juhudi za

kupiga vita matumizi ya vipimo batili katika ununuzi wa mazao ya wakulima ikiwa ni pamoja na kutenga na kuyasimamia maeneo maalum ya kuzuia mazao (*buying and selling centres*). Maafisa Ugani walioko vijijini watumike kusimamia matumizi ya vipimo rasmi katika vituo hivyo na kutoa taarifa zote muhimu kwa Wakala wa Vipimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi swali fupi la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri napenda kumfahamisha kwamba tunakwenda kwenye Tanzania ya viwanda na kule Mlalo tunalima kabichi, karoti, viazi, hoho pamoja na mazao mbalimbali ya mboga mboga. Je, haoni kwa kuwa sisi tutakosa viwanda wakatutafutia soko zuri la kuweza kupata tija kwenye mazao haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa mazao na bidhaa nyinginezo zinafungwa katika vipimo ambavyo vinaeleweka, haoni sasa ni wakati wa Serikali kuweka mkazo kwamba na mazao ya wakulima nayo yaweze kufungwa katika utaratibu ambao utawaletea tija wakulima? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la mazao, katika maelekezo ambayo Serikali imetoa na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake amesisitiza ni kwamba Halmashauri zote kuanzia ngazi ya Kijiji, Kata mpaka Wilaya tunapaswa kutenga maeneo ambayo moja itakuwa sehemu ya kujenga viwanda vidogo, pili itakuwa sehemu ya kujenga hifadhi na tatu itakuwa sehemu ya kufanyia biashara. Kwa kutengeneza zile *business centers*, wateja wataweza kufika na kuweza kununua mazao yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao ya wakulima yakifungashwa vizuri yatapata soko, nakubaliana na hilo. Jambo la kufanya ni kwamba tunapohimiza ujengaji wa viwanda huko vijijini vinaongeza thamani na unapoongeza thamani ya bidhaa inahusisha pamoja na ufungaji. Kwa mfano, tungependa watu wa Lushoto na Tanga zile tangawizi na hiliki mkishazichakata kwenye viwanda vidogo pale ndiyo zinaingia kwenye *packaging* ambayo itakuwa inaeleza kama ni kilo au ni *volume* gani.

Mheshimiwa Shangazi tutawasiliana zaidi kusudi niweze kukupa maelekezo ya kiutendaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata kwa ufupi sana.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa tatizo la lumbesa linasababishwa na viroba ambavyo vina vipimo tofauti tofauti. Kwa kuwa nchi yetu ilikuwa na kiwanda cha magunia ambayo yalikuwa na kipimo na ujazo ulio sawasawa.

Je, Waziri yupo tayari kwenda kukifufua kiwanda kile ili tuweze kuwa na vipimo vinavyolingana kuepuka kuwadhulumu wananchi wetu? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viroba au vifungashio vyenye ukubwa tofauti suluhisho lake ni kuwa na mizani kwenye *buying centre* ambao utabainisha kilo stahiki, ukubwa wa gunia sio hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la viwanda vya magunia, kwa nini viwanda vya mgunia vya Tanzania vilikufa ikiwemo kile cha Kilimanjaro. Magunia yanayotoka nchi za Asia ikiwemo Bangladesh yanapoingia *East Africa* hayatozwi ushuru, magunia yanayotengenezwa na viwanda vya Tanzania yanatozwa ushuru katika mazingira hayo lazima tuanguke. Kwa hiyo, mapendekezo ni kwamba lazima tuangalie ulinganisho wa ushuru na gharama za bidhaa zinazotoka nje na zinazoingia ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limeshafikishwa kwa wahusika na tutaweza kulishughulikia namna hiyo. Kwa hiyo, viwanda vya Kilimanjaro, Singida na Tanzania nzima vitaweze kufufuka kwa namna hiyo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji.

Na. 208

### **Fedha za Mradi wa Skimu ya Umwagiliaji - Kijiji cha Endagaw**

**MHE. DKT. MARY M. NAGU** aliuliza:-

Serikali ilitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 400 za awamu ya kwanza kwa ajili ya skimu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Endagaw na mradi huo kwa ujumla unagharimu shilingi milioni 800:-

Je, ni lini Serikali itamalizia kiasi cha fedha kilichobaki ili kukamilisha mradi huo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIANI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Skimu ya Endagaw ina jumla ya eneo la hekta 256 linalofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji. Kwa sasa eneo linalomwagiliwa ni hekta 200. Wananchi wa Skimu ya Endagaw kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Hanang waliibua miradi wa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang iliwasilisha maombi ya kupatiwa fedha yenye jumla ya shilingi milioni 800 kutoka Mfuko wa *DIDF* kwa ajili ya kuboresha mfumo wa umwagiliaji. Katika mwaka wa fedha 2011/2012, Halmashauri ilipokea kiasi cha shilingi milioni 410 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa skimu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kujenga mfereji mkuu wa upande wa kushoto wa kijito cha Endagaw kwa kuusakafia ili kudhibiti upotevu wa maji ardhini kwa urefu wa meta 3,000 na maumbo sita ya kudhibiti mwenendo wa maji ya umwagiliaji. Aidha, katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali imepanga kuendelea na ukamilishaji mfereji mkuu wa upande wa pili wa kijito wenye urefu wa meta 3,000.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maji ya kijito cha Endagaw yamekuwa mengi kuliko utaalamu ulivyoona na kwa hivyo mfereji mmoja unaweza ukafanya ukuta uliojengwa kubomoka.

Je, Waziri anaweza kuwahakikishia watu wa Endagaw na wa Hanang kwamba huu upande wa pili utajengewa mfereji mara moja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, palipokuwa na kijito cha Endagaw kulikuwa na wananchi ambao walikuwa na shughuli zao na makazi yao na wakaondolewa kwa ajili ya skimu hiyo.

Je, Serikali inaweza kutusaidia kuwapa fidia wale watu ambao wameondoka pale kwa ajili ya mradi huu? Namuomba Mheshimiwa Waziri

aweze kutembelea eneo hilo na kuona umuhimu wa maswali haya mawili ya nyongeza niliyoyauliza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze kwa kuibua swali hili. Tunasema kwamba ili tuweze kupata chakula cha kutosha lazima tuende kwenye kilimo cha umwagiliaji. Sasa hivi Taifa letu tumeshaanzisha Tume ya Umwagiliaji itakayosimamia eneo hili. Mpaka sasa Taifa linalima hekta 461 tu tunataka katika miaka mitano ijayo tufikishe hekta milioni moja. Sasa kwa kuanzia na hiki Kijiji cha Endagaw ambapo tayari tumeahidi kuendelea kujenga skimu ile, hizo laki nne tutazipeleka lakini tutaboresha kwa namna ambavyo anashawishi Mheshimiwa Mbunge ili wananchi wale waweze kupata faida ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili nitakwenda kuangalia katika kuwahamasisha wale wananchi tutaona namna gani ya kuwafidia. Jambo moja zuri ni kwamba fidia nzuri ni ile kuwajengea skimu ambayo wataweza kuendelea kulima kuliko wakipewa fedha lakini wasiendeleo kulima. Kwa hiyo, tutaangalia namna bora ya kuwafidia kwa kujenga skimu ili walime kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza session ya maswali na majibu na sasa ni matangazo ya wageni waliopo ukumbini asubuhi hii.

Kwanza ni wageni 60 wa Mheshimiwa Charles M. Kitwanga, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Madiwani kutoka Misungwi wakiongozwa na Ndugu Anthony Bahebe - Mwenyekiti wa Halmashauri ya Misungwi na Ndugu Donald Magesa - Katibu wa CCM Wilaya ya Misungwi. Karibuni sana. Wengine ni wageni kumi wa Mheshimiwa Dkt. Abdallah Possi, Naibu Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Watu Wenye Ulemevu) ambao ni wanachama wa Chama cha Wasioona Tanzania (TLB) wakiongozwa na Ndugu Luis Benedictor - Mwenyekiti na Ndugu Robert Bundala - Makamu Mwenyekiti. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni 47 wa Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Mkoa wa Ruvuma. Karibuni wanafunzi wetu. Wageni wengine ni wageni sita wa Mheshimiwa Frank Mwakajoka ambao ni walimu wa shule ya msingi na sekondari kutoka Tunduma wakiongozwa na Ndugu Pili Njebete na Ndugu Idrisia Ntakasime, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa wawili wa Mheshimiwa Josephine Genzabuke kutoka Kasulu Kigoma ambao ni Mwalimu Adassa Konakuze na Ndugu Rehema Ngelula. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Desderius Mipata ambao ni walimu na wapiga kura wake kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wakiongozwa na Ndugu Mkondya George, karibuni sana. Pia kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Boniventura D. Kiswaga ambao pia ni wapiga kura wake kutoka Jimboni wakiongozwa na Ndugu Ayoub Bindule. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni 29 wa Mheshimiwa Kasuku Bilago ambao ni viongozi wa Chama cha Walimu, Kitengo cha Wanawake kutoka Jimboni kwake wakiongozwa na Ndugu Leah Ulaya - Makamu wa Rais Chama cha Walimu, karibuni sana wageni wetu wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, lifuatalo ni tangazo kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Shughuli za Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa ratiba ya Mkutano huu wa Tatu wa Bunge unaoendelea ina mabadiliko kidogo, hotuba ya bajeti ya Serikali sasa itasomwa Bungeni siku ya Jumatano tarehe 8 Juni, 2016 badala ya Alhamisi tarehe 9 Juni, 2016 kama ilivyokuwa imepangwa awali. Katika tarehe hiyo, hotuba za bajeti kwa nchi nyingine za Afrika Mashariki pia zitasomwa kama kawaida. Waheshimiwa Wabunge mtapatiwa nakala ya ratiba mpya. Hata hivyo, siku ya kuahirisha Mkutano huu wa Tatu wa Bunge inabaki kuwa tarehe 1 Julai, 2016.

Tangazo lingine pia ni la Mkurugenzi, Idara ya Shughuli za Bunge anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba leo Ijumaa tarehe 20 Mei, 2016 kutakuwa na semina kwa Wabunge wote kuhusu Benki ya Maendeleo ya Kilimo. Semina hiyo itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa kuanzia saa 7.30 mchana, Wabunge wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge, lifuatalo ni tangazo la msiba, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo anatangaza kifo cha mdogo wake anayeitwa Michael James Wambura kilichotokea tarehe 19 Mei, 2016 katika Hospitali ya Mkoa wa Mara iliyopo Musoma Mjini. Mipango ya mazishi inafanywa na familia ya marehemu. Mheshimiwa Anastazia Wambura kwa sasa yupo nyumbani kwake maeneo ya Kisasa kwenye nyumba za TBA akifanya maandalizi ya kusafiri kwenda Musoma. Kwa wale wanaotaka kwenda kumpa pole wapige simu namba 0713 493230 kwa ajili ya kuwaelekeza mahali nyumba ilipo. Pole sana Mheshimiwa Nape, Mwenyezi Mungu atamlaza mahali pema peponi marehemu na Mwenyezi Mungu akupe moyo wa subira.

**WABUNGE FULANI:** Aaaah.

**NDG. RAMADHANI ISSA ABDALLAH - KATIBU MEZANI:** Aliyefiwa ni Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**MWENYEKITI:** Samahani, aliyefiwa ni Mheshimiwa Anastazia, tunampa pole sana. Mwenyezi Mungu atampa subira.

Tunaendelea na tangazo lingine limetoka Utawala, Waheshimiwa Wabunge wote mnatangaziwa kuwa Mheshimiwa Stanslaus Mabula pamoja na Taasisi ya Flavian Matata wameandaa ibada maalum ya kumbukumbu ya miaka 20 ya ajali ya MV Bukoba itakayofanyika tarehe 21 Mei, 2016 katika makaburi ya MV Bukoba yaliyopo Igoma, Mwanza kuanzia saa nne asubuhi. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnaalikwa kushiriki ibada hiyo maalum.

Mwisho ni tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla, Mwenyekiti wa *Bunge Sport Club* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho saa kumi jioni kwenye Uwanja wa Jamhuri kutakuwa na michezo ya *football* na *netball* kati ya Waheshimiwa Wabunge na wafanyakazi wa Bunge, wote mnaombwa kuhudhuria kwenye mechi hiyo kabambe. Mgeni rasmi kwenye mechi hiyo ni Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Naibu Spika wa Bunge. (Makofi)

Katibu tuendelee.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(g) miongozo yote tutachukua baadaye.

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

#### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017 - Wizara ya Nishati na Madini**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaanza majadiliano na tutaanza na Mheshimiwa Stephen Ngonyani atafuatiwa na Mheshimiwa Jasson Rweikiza na Mheshimiwa Agness Marwa.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi nianze kwa kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini hasa Profesa mwenzangu maana maprofesa tupo wawili tu humu ndani ya Bunge.



**MBUNGE FULANI:** Watatu.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Aaah tumekuwa watatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Nishari na Madini kwamba sisi wengi Wabunge tuliorudi safari hii ni heshima yako Mheshimiwa Profesa. Nasema hivyo kwa sababu sehemu zote ulizoweka umeme ndiyo watu wamepata neno la kuongea na leo hii Wabunge tumeingia hapa. Tunamshukuru sana yeye pamoja na taasisi zako zote na tunaomba waendeleo na moyo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa neno dogo. Katika utaratibu wa umeme kuna sehemu vimejitokeza vitu ambavyo vinatakiwa vifanyiwe kazi haraka sana na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mita zetu za LUKU Watanzania wengi wamekuwa wanakatwa ikifika mwisho wa mwezi. Kama ni kukatwa pesa ni afadhali mtu awe anataarifiwa kwamba katika kuwekewa LUKU yako LUKU hiyo imekutwa na matatizo, huko nyuma ulikuwa una deni na kama ni deni tujue kwamba, ilikuwa ni kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini kumekuwa na taratibu ndani ya TANESCO mtu anatarajia katika simu yake ana shilingi 20,000; anaweka LUKU lakini ikifika pale anaambiwa pesa yako haitoshi, wakati hana pesa nyingine na anahitaji msada wa umeme. Unaweka shilingi 30,000 unaambiwa pesa yako haitoshi. Sasa kama haitoshi kwanini vitu hivi mtu asikuambie mapema kwamba, unawekewa LUKU lakini siku za nyuma ulikuwa una deni kiasi fulani unatakiwa ulipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mnawangoja walala hoi inafika siku ya mwisho wa mwezi mtu analipia LUKU yake kwa misingi kwamba nyumba yake ipate umeme, unakatwa pesa yako. Mheshimiwa Waziri naomba sana kama utaratibu huu huufahamu tunataka tukuambie kuna tatizo hili kwa Watanzania wa chini ambao hawajui kwamba maisha yao ya baadaye yanakuaje wanakatwa pesa zao hovy hovy.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, watu wanaowekewa REA waliambiwa kwamba wanawekewa umeme kwa shilingi 27,000. Na Watanzania wengi walipata nguvu kubwa sana kwamba sasa tunawekewa umeme kwa shilingi 27,000. Lakini kunatokea mabadilika, mtu anakwenda kutafuta pesa hata kwa kukopa kwa mtu, anaweka *line* katika nyumba yake, siku anayotarajia anaambiwa kwamba leo REA imekiuka sio hii tena shilingi 27,000 inapanda bei kiasi ambacho Mtanzania wa chini anashindwa wakati nyumba yake tayari imekuwa na LUKU tayari ameshaifanyia kila kitu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri, kama umeme wa REA ameufanyia jitihada kubwa sana kwa Watanzania, wameupata, lakini sasa inafika mahali wanabadilishiwa viwango vya kuweka umeme, hatuwatendei haki kwa sababu umeme huu umeletwa na Watanzania na hii pesa ya Watanzania na ni kodi ya Watanzania. Kama kweli tunataka kuwasaidia Watanzania basi wawekewe kiwango kile kile kiwasaidie Watanzania wa chini na wao wawe na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunakuja umeme. TANESCO wanafanya kazi nzuri sana usiyemkuta mtu anayemshukuru mtu wa TANESCO au watu wote wa TANESCO basi mwangalie huyu mtu ana mapungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ila nataka niwashauri kitu kimoja Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi. Umeme tunao utumia sasa hivi ni wa gharama kubwa sana kwa sababu unatumia mafuta na vitu vingine, na wengine mnakodi mitambo. Lakini kuna vituo vya nguvu vya umeme ambavyo vinatumia maji. Vituo hivi ndivyo vinavyofanya leo Uganda wanakuwa na umeme ambao haukatiki mara kwa mara, na umeme huo wa Uganda umefika mpaka Tanzania kwa kutumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini eneo la Hale, Kihansi, Bwawa la Nyumba ya Mungu na Bwawa la Mtera tusiyaendeleze kwa kuweka mitambo ya kisasa badala ya kutegemea hawa watu wanaotoka nje ya nchi kuja kutuibia Watanzania? Wanatuongezea *bills* zisizokuwa na maana, matokeo yake wanataka watupeleke mahakamani? Hawa watu walikuja kwetu kuchuma au walikuja kuwasaidia Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama kuna uwezekano, haya meneo ambayo tuliyaanzisha sisi; Watanzania walikuwa wanategemea sana umeme wa nguvu za maji leo Zimbabwe na Zambia wanategemea nguvu ya maji tu. Na hii nguvu ya maji inasaidia haina gharama kubwa kama hizo wanazotupa hawa wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Mheshimiwa Waziri, yeye ni msikivu sana, tena ni Profesa mwenzangu naomba aliangalie suala hili ambalo mimi bila yeye nisingerudi pale jimbo la Korogwe Vijijini. Alifanya kazi ya ziada kulisambazia umeme, lakini pamoja na umeme ule ambao ameusambaza namshukuru na uendeleo na jitihada zake. Lakini swali ambalo ninajuliza, kuna baadhi ya maeneo ambayo hayana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo la Korogwe katika Mkoa wa Tanga, Jimbo la Korogwe Vijijini ndiko kwenye nguvu za umeme aina mbili, iko Hale, iko Chemka. Lakini nguzo nyingi za umeme zimepita kwenye nyumba za watu zimekwenda kwenye mashamba ya mkonge ambayo leo hii hayaendelezwi.

Sasa badala ya kuchukua nguzo nyingi kupeleka kwenye maeneo, na kuna vijiji ambavyo vimepitiwa na maeneo yale, kwa nini wasipeleke nguzo moja badala ya kupeleka nguzo 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusitumie vielelezo hivi? Kwa mfano nina kata pale toka Uhuru umeme wanausikia kwenye redio, kata ya Kizara, kata Vugiri katika vijiji vya Mlalo, kata ya Mpale katika kijiji cha Mpale na Mali hakuna kitu cha aina yoyote. Kata ya Mkalamo, Mswaha hakuna umeme, sasa na ndio umeme umetokea huko kwangu. Mheshimiwa Waziri, naomba ulivyonisaidia wakati nikiumwa, nikiwa India ukanipeleka na watu wako wa REA wamefanya kazi nzuri sana hebu nimalizie hili na mimi nijijue kwamba mwaka 2020 basi tunakuwa watu wa kupeta tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la madini. Madini ni kitu muhimu sana kwa Tanzania. Mimi kwenye jimbo langu kuna sehemu kubwa tu za kutoa madini, lakini watu wa madini hawapati faida yoyote ya madini yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma Serikali iliahidi kwamba itakwenda kule kuwapelekea wachimbaji wadogo wadogo, watakwenda kuwafungulia SACCOS zao za kupata pesa kwa ajili ya wao kuendeleza miradi yao ya madini, lakini cha kushangaza mpaka leo hii katika Jimbo langu kule Kalalani hakuna hata mtu mmoja ambaye amesaidiwa. Sasa hawa wachimbaji wadogo wadogo kwanini hatuwathamini wakati wao ndio wanaoonesha njia kwamba, hapa ndiko kwenye madini na ndipo wanapoonesha njia na Serikali inakuja kuchimba inapata faida kubwa, wawekezaji wanakuja; lakini sio kwa Serikali peke yake bila kushirikiana na hawa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ni msikivu na Wizara yake ni sikivu. Mimi nimeita kwenye Kamati yangu, tumeona matatizo yake na mmejaribu kuyarekebisha. Katibu wako Mkuu, anafanya kazi vizuri, Katibu Mkuu wa REA anafanya kazi vizuri. Naomba sana hii shughuli hebu imalizie kwa sababu wengine hatuwezi kusimama hapa kila siku kupinga wakati Serikali imefanya. Si mimi tu hata upinzani kuna majimbo mengi yamepewa umeme na kama yamepewa umeme ni kwa ajili yako na ndio maana wengine hapa leo hata kusema yale maneno makubwa makubwa hatuwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia, Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Stephen, tunaendelea na Mheshimiwa Jasson Rweikiza na baadaye Mheshimiwa Agness Marwa na Mheshimiwa Vicky Kamata Likwelile wajjandae.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kuchangia asubuhi hii. Mimi nianze kwa kuwashukuru na kuwapongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri wanayoifanya, maana unapotaka mambo yapelekwe kwako au yasogezwe kwenye eneo lako vilevile lazima utambue kazi ambayo imefanyika. Kazi kubwa imefanyika na inaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kusema hivyo sina maana kwamba tumemaliza, bado tuna kazi za kufanya na tunaendelea nao. Lakini nalinganisha na miaka nyuma ambapo umeme ulikuwa unakatika mara kwa mara, kila mahali giza, sasa hivi hali hiyo haipo tumeweza kupambana nayo na tumekabiliana nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mbalimbali inayoendelea, tunaona miradi mingi, tumepata gesi ya Mtwara, kutoka na gesi hiyo tumefungua miradi mikubwa ya kufua umeme pale Kinyerezi ambayo ikikamilika tutapiga hatua kubwa sana katika kuwa na umeme wa kutosha na mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna miradi mingine, kwa mfano ile njia kubwa ya umeme kutoka Iringa kwenda Shinyanga ambayo ikikamilika ni kama *backbone*, ina-cross kuanzia Iringa kwenda Shinyanga, itakuwa ni chanzo cha kupeleka umeme mikoa mengine ambayo imezungukwa mikoa hiyo, ambao ni umeme mkubwa KV 400. Hili ni jambo la kujisifia na kuishukuru Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niisemee REA. REA kazi yao vilevile ni nzuri sana, vijiji vingi nchi nzima vimepata umeme. Mimi najiuliza ingekuwa hakuna REA tungekuwa wapi? Kazi ya REA ni nzuri, nawashukuru na kuwapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema pamoja na kazi nzuri bado tuna kazi kubwa ya kufanya. Pale Kagera Mkoa mzima kuna tatizo la umeme kubwa sana. Hata leo ninavyoongea hivi sasa hivi hakuna umeme umezimika, jana hivyo hivyo, juzi hivyo hivyo, kila siku, mwaka mzima; wanazima umeme asubuhi unarudi jioni au haurudi kabisa, tatizo ni kwamba hatuko kwenye Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Kagera unatokea Uganda, tunanunua Uganda hivi leo Uganda wanashida kubwa ya umeme, umeme ni pungufu. Kwa hiyo, wanakata umeme, Kagera tuko gizani muda mwingi sana. Kwa hiyo niombe Kagera iunganishwe kwenye Gridi ya Taifa. Nafahamu umesogea kama si Geita basi ni Chato wa Gridi umefika umeme. Kazi ifanyike kwa jitihada kubwa ufike mpaka Bukoba, mpaka Karagwe, mpaka Ngara kote tupate umeme wa Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna mradi mwingine pale Rusumo wa umeme wa kuzalisha *megawatts* 80. Mradi huu umeanza kwa ushirikiano wa nchi tatu, Rwanda, Uganda na Tanzania, lakini kasi yake si kubwa hairidhishi. Kasi iongezwe kusudi mradi huu ukamilike tupate umeme huo. Umeme huo ukipatikana ni mwingi, *megawatts* 80 kwa Kagera tutapata *megawatts* 27 utatosha mahitaji yetu na utatusaidia kwa shughuli mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia miradi ya REA. Pale kwangu Bukoba Vijijini kwanza nishukuru vijiji vimepata umeme baadhi, lakini siyo vyote. Kuna vijiji vingi havijapata umeme, Kata nzima ya Kibirizi haina umeme. Kijiji cha Kibirizi chenyewe, Omubweya na Kamuli havina umeme. Kata nzima ya Rukoma haina umeme, Rukoma yenyewe, Nsheshe na kwingineko hakuna umeme. Kata ya Kikomelo umeme haujakanyaga. Niombe sana vijiji na kata hizi zipelekewe umeme na kwenye Ilani ya CCM ya uchaguzi ya mwaka jana kata hizi zimetajwa kwamba kutapelekwa umeme kwenye awamu hii ya mwaka 2015/2020. Niombe kazi ifanyike na umeme usogee Kata ya Kibirizi, Kata ya Lukoma na Kikomelo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hata vile vijiji vingine ambavyo umefika, jambo ambalo nafikiri REA hawakulifanyia kazi vizuri, vijiji vya Bukoba ni vikubwa sana, vikubwa kweli kweli; unakuta kijiji kina kaya 400 wamepeleka umeme kaya 15, 20 au 10. Ni kweli kwenye kijiji umeme umefika lakini wananchi hawajapata umeme kama inavyostahili. Niombe sana kwamba jitihada ziendeleo kwenye REA III, vijiji hivi viongezewe mgao au kazi isogee ndani zaidi kwenye vijiji ambako tayari wamefika lakini hawajafika maeneo mengi ya kutosha na vitongoji vingine ambavyo havijafikiwa nako vifikiwe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nimalizie kusema kwamba, umeme huo tunapoupeleka vijijini bado kuna mapungufu fulani fulani. Kwa mfano taasisi kama shule za sekondari au zahanati au sehemu kama hizo tunasema wananchi wajiwekee wenyewe ni kazi kubwa sana kufunga umeme kwenye sekondari uwake madarasani, maabara wafunge *wiring* mle ndani, nyumba za walimu, wananchi hawawezi, Serikali nayo iangalie uwezekano wa kufanya kazi hii yenyewe, iwe ni sehemu ya mradi, wasiishie tu kupeleka umeme kijijini labda kwenye center halafu wakaondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi kama shule REA yenyewe ifunge umeme mle ndani kwenye taasisi za Serikali; iwe shule, iwe zahanati kusudi matunda ya umeme yaonekane kwa wananchi walio wengi, taasisi zipate umeme, kama ni hospitali ziweze kuboresha huduma pale tuwe na beni za damu (*blood bank*) na huduma nyingine kutokana na kutokuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi hii naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rweikiza, ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Agness Marwan a baadaye Mheshimiwa Vicky Kamata ajiandae.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kipekee zaidi naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Muhongo kwa kazi kubwa anayoifanya. Kwa kweli Mheshimiwa Muhongo unastahili sifa na nafasi hiyo ulistahili hasa ndiyo maana umerudishwa tena pamoja na majungu yote yaliyotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendeleo pia kuishukuru au kupongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi kubwa wanayomsaidia Waziri Muhongo pamoja na Naibu wake kwa sababu kumekuwa kuna mgogoro wa muda mrefu sana kati ya wananchi wa Tarime kule mgodini na wawekezaji wa Mgodini wa Acacia. Lakini Mheshimiwa Waziri amekuwa ni chachu kubwa ya kuonyesha yeye anasababisha ule mgogoro unafikia mahali anaumaliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo basi Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake nilizoziona au wananchi walizoziona Mheshimiwa Waziri alituma watu waende wakaangalie matatizo ya wananchi, Mheshimiwa Waziri alimteua akiwemo Mbunge wa kule kule mgodini kaka yangu Heche na yeye pia alikuwa kati ya watu walioenda kule kuangalia matatizo ya wananchi, kwa hiyo nafikiri mambo yatakuwa mazuri tu nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri endelea hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona hapa kwenye mkataba wa Mgodini wa Acacia. Mgodini wa Acacia ulikuwa na leseni ya utafutaji wa madini ndani ya Halmashauri ya Tarime katika Kata ya Turwa na Kinyamanyori. Kwakuwa leseni hiyo muda wake ulishakwisha naiomba Serikali ikabidhi maeneo yale kwa wananchi ili waendeleo na uchimbaji mdogo mdogo. Na Serikali kwa mpango wake endelevu iliyonao mzuri wa kuwasaidia hao wachimbaji wadogo wadogo, wachimbaji hao watakaporudishiwa eneo hilo iwasaidie mashine za kisasa kama ilivyo kwa maeneo mengine ili uchimbaji wao uwe na tija na uwanufaishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri, pamoja na juhudi zake kubwa sana za kuanzisha mradi wa REA ambao umewasaidia ndugu zetu wengi sana Vijijini ikiwemo Mkoa wa Mara; Mheshimiwa Waziri nikuombe kuna baadhi ya vijiji mkoani Mara ambavyo vimebaki; kwa mfano Wilayani Rorya kuna vijiji vya Kemwame, Kibui, Mkengwa na Baraki Tarafa ya Suba vimekwama baada ya kuwa vimewekewa nguzo toka mwaka 2015 na kinachoendeleo wananchi wale hawakijui mpaka sasa hivi wamebaki kwenye sintofahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri atakapofunga hoja yake anipe majibu juu ya suala hili la umeme, ni lini wananchi wa Wilaya ya Rorya wataupata umeme? Lakini pia anipe majibu ya kuwarudishia wachimbaji wadogo wadogo wa Tarime eneo lao ili nao waifadike nalo? Kwa sababu kuna wachimbaji wengi wadogo wadogo kule ambao wanaitwa tu wachimbaji wadogo wadogo lakini hawana maeneo ya kuchimba kwa sababu yale maeneo ni ya watu, watu ndio wameyamiliki. Kwa hiyo, nikuombe kipekee zaidi unishughulikie sana suala, hili usiliache.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu wapendwa, Wabunge wenzangu; mwisho naomba kumalizia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao wameniweka wimbo kwenye simu yangu unasema CHADEMA, CHADEMA peoples power nina imani kabisa ni wale majirani zangu. Lakini watani wangu naomba niwaambie mimi ni nyara ya CCM, kwa hiyo huo wimbo hautafanya chochote. Tunapoingia humu ndani Bungeni bangi tuweke pembeni na kazi tuweke pembeni.

Kwa hiyo, ndugu zangu niwaambie hamtanikatisha tamaa, CCM ina vijana, ina wazee ina watoto ina kila mtu na CCM ni ile ile mwaka 2020 mtaisoma namba. Ahsante mimi ndiye Agness kutoka Mkoa wa Mara, nyara ya CCM ahsanteni. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agness tunaendelea sasa na Mheshimiwa Vicky Kamata na baadaye Mheshimiwa Ally Saleh ajiandae.

**MHE. VICKY P. KAMATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa ninamshukuru Mungu kwa afya njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nianze kwa kusema kwamba ninaunga hoja hii mkono kwa asilimia mia moja lakini pia ninampongeza sana Profesa Muhongo kwa kurudi tena katika Wizara hii. Imani kubwa aliyokuonyesha Mheshimiwa Rais John Joseph Pombe Magufuli, ni imani kubwa ambayo Watanzania wengi tulioko huko nje pia tunayo kwako pamoja na Naibu wako Dkt. Kalemani. Tuna imani kubwa sana, kwamba kazi itafanyika na matokeo yataonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza na narudia tena kusema kwamba Rais amekuamini Profesa Muhongo, amekurudisha kwa sababu anakujua. Tunataka kwenda kwenye uchumi wa kati ambao unategemea viwanda. Mheshimiwa Mwijage, Profesa Mkenda pamoja na Dkt. Meru hawana muujiza wowote ule watakaoweza kuufanya ili Tanzania iwe kweli ya viwanda iwapo ninyi



hamtafanya kazi nzuri ya kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika unapatikana ili kuwezesha Tanzania ya viwanda iweze kufikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Kamati yangu tulienda Arusha, tulitembelea Kiwanda cha kutengeneza transfoma, *TANELEC*. Kiwanda kile kinafanya kazi nzuri sana, kinatengeneza transfoma zenye ubora mkubwa sana. Transfoma zile zinanunuliwa Kenya, Uganda na nchi nyingine lakini sio Tanzania, kwa maana ya kwamba *TANESCO* hainunui zile transfoma zenye ubora mkubwa. Wanunua transfoma kutoka India, zinakuja hapa zinafika kwa gharama kubwa pengine kuzidi hizi za hapa kwetu na bado hazina ubora wa kutosha, zinalipuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajumbe wengi wameeleza kwamba kwenye maeneo yao yametokea matukio ya hatari sana kwa sababu zile transfoma zimekuwa zikilipuka, wanashindwa kununua transfoma kutoka *TANELEC*. Kamati yangu ilipata uchungu sana baada ya kujionea kazi nzuri ya kiwanda kile, lakini kuna malalamiko na changamoto kubwa wanazokutana nazo. Kamati ilipata uchungu na ilipata hasira sana. Ninaamini kama kamati yangu ingekuwa na mamlaka, ingekuwa na uwezo siku ile ile tungeweza kutumbua majipu fulani fulani.

Lakini tulijiuliza, kama tunaweza kumtumbua Mkurugenzi wa *TANESCO* tukamuita jipu, tutakuwa tunamuonea kwa sababu tatizo sio Mkurugenzi wa *TANESCO*, tatizo si Idara ya Manunuzi, tatizo ni Sheria ya Manunuzi. Sasa kama tunazo sheria ambazo zinakuwa kikwazo, sheria ambazo hazitusaidii, tunataka kukimbia sheria zinatufunga miguu tushindwe kwenda tunakoenda, kwa nini hizo sheria zisiletwe haraka tuzifanyie marekebisho ndani ya Bunge hili? Tuifanyie marekebisho hiyo Sheria ya Manunuzi kusudi tuweze kufanya kazi vizuri kwasababu hii Sheria ya Manunuzi imekuwa kichaka, tutakuwa tunawaonea watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikasirika sana siku ile na Mkurugenzi wa *TANESCO* tukasema kwanza yeye ni Mjumbe wa Bodi inawezekanaje wanunue *transformer* India zenye ubora mbovu? Lakini tunakuja kujua kumbe si yeye, tatizo ni sheria yetu ambayo tuliipitisha wenyewe humu. Sasa tulete hiyo sheria haraka sana ifanyiwe marekebisho kusudi tuweze kufanya kazi vizuri na *TANELEC* iweze kuuza transfoma zake hapa hapa Tanzania; na kiwanda chetu kama kweli tunataka Tanzania iwe ya viwanda basi tuanze na viwanda vilivyomo humu kuvipa uwezo wa kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ningependa nizungumzie wachimbaji wadogo wa Geita. Mheshimiwa Profesa Muhongo na kaka yangu Dkt. Kalemani; tena Dkt. Kalemani unaona kabisa hali halisi ya watu wako wa Geita maana wewe unatoka Geita, wewe ni Mbunge wa Chato. Maisha ya

wananchi wa Geita ni magumu na Serikali imekuwa ikiahidi kila siku kwamba itawapa maeneo ya kuchimba lakini sielewi tatizo ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Muhongo ulianza vizuri sana kipindi kile, uliwapa matumaini makubwa sana wananchi wa Geita hususani hawa watu ambao wanachimba, walijiunga kwenye vikundi vya SACCOSS mpaka leo vikundi vinakufa kwa sababu hakuna maeneo ya kuchimba. Naamini pale ulipoishia kipindi kile baada ya matatizo yale kutokea, umerudi tena, ni kwa mpango wa Mungu na kwa makusudi mazuri na nia njema ya Rais kwamba uwasaidie wachimbaji wadogo wadogo wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa taarifa nilizonazo, lile eneo la STAMICO lina-expire Julai, 2016 yaani mwaka huu, tuna mwezi mmoja tu lile eneo lina-expire. Huoni umuhimu Mheshimiwa Waziri wa kuwapatia sasa wananchi hilo eneo la STAMICO ili waweze kugawana SACCOSS zile ziweze kuanza kufanya kazi? Wananchi wa Geita wanategemea uchimbaji, sasa hawafanyi kazi matokeo yake watu wanaanza kufanya vitendo vya uhalifu kwa sababu hawana kazi za kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninaomba sana kupitia bajeti, nina uhakika bajeti hii itapita kwa sababu ni nzuri na tena kama ulivyosema asilimia 94 ni kwa ajili ya maendeleo, kwahiyo ninaamini kabisa Geita itapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Muhongo juzi umeenda umekutana na Watanzania wanaoishi Geita, umewapa matumaini na umerudisha imani kubwa, wana imani na wewe na mimi Mbunge wao nasema waendeleo kuwa na imani na wewe kwa sababu wewe ni mnyoofu, ni muadilifu na ahadi zako hazipindi pindi. Nina uhakika safari hii maeneo ya wachimbaji wadogo yatapatikana, tukianza na hilo linalo-expire mwezi Julai.

Lakini vilevile Mheshimiwa Muhongo unauwezo wa kwenda kuzungumza na GGM. GGM wamehodhi maeneo makubwa sana. Kuna lile eneo la Nyamasagata, kuna la Semina, kwanini usiongee na GGM wakawagawia haya maeneo, wakawaruhusu basi hata wakachimba kwa sababu wenzetu wa Ghana wamewezaje wachimbaji wadogo na wakubwa kuogelea kwenye bwawa moja bila kuleta madhara yoyote? Ni utaratibu tu uwekwe, hawa wachimbaji wadogo wachimbe na hawa wakubwa pia wachimbe, hawa wadogo kwanza wanachimba kwanza hawana vifaa vikubwa kwa hiyo hawawezi wakachukua dhahabu nyingi ya hawa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itawasaidia tu kuweza kuendesha maisha yao ya kawaida na kelele pia zitakwisha. Nikuombe Profesa Muhongo na Naibu wako, Katibu Mkuu; sisi tuna imani kubwa sana na ninyi, kwa hiyo ninaamini



kabisa, mara baada ya hii bajeti kupita, utafika Geita, utawasaidia wachimbaji wadogo, SACCOSS zitaanza kufanya kazi na Geita itafanana kwamba huu kweli ni mji wa dhahabu maana maisha wanayoishi Watanzania pale kwa kweli hayaridhishi hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijagongewa Kengele pia nipongeze na mimi kidogo umeme wa REA. Kwa kweli kwa Mkoa wetu wa Geita mmejithadi, tunakwenda vizuri, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo nguzo zimepita muda mrefu sana na mpaka sasa imefikia mahali wananchi wanaanza kupata hasira wanataka kukata zile nyaya kwamba kwa nini umeme umepita umeenda maeneo mengine na sisi tumerukwa, na sisi tuko kwenye kata ambayo ni makao makuu ya kata? Kuna vituo vya afya pale, kuna sekondari pale, kuna shughuli nyingi za maendeleo ziko pale lakini umeme umepita juu. Juzi juzi nilikuwa naongea na Diwani wa Nyaruyeye, kaniambia kweli nimekuwa na kazi kubwa ya kuzuia watu kwenda kuangusha zile nguzo kwa sababu zimepita hapa muda mrefu na sisi hatuna umeme.

Kwa hiyo, ninaamini kabisa baada ya bajeti hii kupita, maeneo ya Nyaruyeye, Nyarugusu na mengineyo yote ambayo bado hayajapatiwa umeme lakini nguzo zimepita basi ule umeme ushuke ili watu wote tuweze kunufaika na huo umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo machache, narudia tena kupongeza Wizara hii na kuwatakia kila la heri, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kulinda muda. Mheshimiwa Ally Saleh na Mheshimiwa Heche ajiandae.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Unapotazama bajeti hii lazima takuwa-*impressed* na takwimu hasa kwenye kipato ambacho nchi hii inapata. Lakini utakuwa unajjuliza kama mwananchi kwa sababu utakuwa na matumaini kwamba tunaweza kutoka kwa mali ambayo tunayo katika nchi hii, mbali ya mali nyingine za misitu na bahari na kitu gani. Picha ya utajiri tulionao katika nchi kwa upande wa madini haionekani katika picha kubwa ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaamini kwamba madini yangeweza kutotoa kwa sababu wako watu wana madini au wana *resource* moja, mbili na wametoka na nchi zao zimekwenda mbele sana. Sasa sisi kama nchi ukitazama katika kitabu hiki unaona kuna mapato mengi, lakini unaweza ukajjuliza *is this our level best, have we done our best* katika suala la madini au la gesi? Kwa sababu siyo tu kuna *room to improve*, lakini naona kama kwamba unajjuliza, tatizo ni nini? Ni sera, ni mipango, ni utekelezaji, ni kitu gani? Kwa sababu zipo nchi ambazo zimeweza kutoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Angola ilikuwa na vita kwa muda mrefu, lakini baaa ya kutoka kwenye vita wamejipanga, sasa hivi wana kipato kizuri kinachopita dola 8,000 kwa kila mtu. Botswana nchi ndogo, ina GDP ya 38 au 39 *billion dollars*. Sasa hivi Mbotswana anapata dola 18,000 *per capita* yake na *resource* yao ni chache, *uranium* kubwa kabisa na vitu vingine vidogo vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sisi Tanzania tunayo madini ambayo mtu mwingine katika Nchi nyingine angeweza kujiuliza *why are you poor?* Tusifananishwe na nchi kama Congo ambayo inautajiri mkubwa. Lakini Congo wana tatizo moja kubwa katika suala la utawala bora, lakini sisi tuna utulivu wa kutosha. Kwa hiyo, pamoja na uzuri wa kitabu hiki lakini ukisoma vitabu vingine viwili vya Hotuba ya Kamati na Hotuba ya Upinzani unaona kwamba kumbe tuna mengi ya kufanya ili tuweze ku-*realise* utajiri ambao Mungu ametujaalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na Mungu ametujaalia utajiri ule, ameuleta kwa *sequence*. Kila baada ya muda tunavumbua kitu kingine ambacho ni kizuri zaidi kuliko kitu kingine. Tulikuwa na almasi tangu miaka ya *boers*, imeondoka almasi ikaingia dhahabu sasa hivi Mungu katujaalia kuna madini makubwa zaidi ya *graphite*, tuna *uranium* inakuja lakini tunajipangaje katika hivi? Sasa mimi najiuliza, kwa mfano, tuna *uranium* na *graphite* ambayo ni madini *very strategic*, lakini je, tunayo sisi wenyewe *strategic mineral policy*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua madini yanatumika yanakwisha lakini tunajipangaje madini haya yawe ya kututoa. Je, tunatengeneza *sovereign fund* kutokana na madini haya? Madini yatakwishia lakini nchi itabakia. Nchi inajitayarisha kwa mfuko ule ambao utaweza kuwa akiba kwa siku za mbele?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Qatar kweli ina gesi, Angola kweli ina petroli na vitu vingine lakini wana *sovereign fund* ambayo wanaweka akiba kwa ajili ya baadae. Sasa utajiri wote ambao tunao hivi sasa tunaojivunia, hatutawekea vizazi vyetu huko mbele lakini pia hatutoweza kufanya uwekezaji wa uhakika kwasababu kama nchi hatuna mfuko wa *sovereign fund*. Jambo hilo nimelisema hapa kabla na ninalisema tena kwa sababu mtu yeyote anaye *study* Qatar, Norway na wengine wamefaidika katika hilo. Sasa nilisema ukisoma hotuba ya Waziri, soma na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye REA. REA tunasema fedha zake zinajulikana zinapatikana njia gani na zimetengewa sheria kwamba lazima zitumike kwa njia ile. Jana tumeambiwa hapa kwamba shilingi bilioni 73 hazikutumika inavyopaswa. Unajiuliza kama shilingi bilioni 73 hizi zingetumika tungepata umeme kiasi gani kwa vijiji vyetu? Na kwa nini hazikutumika na zimekwenda wapi? Kama ambavyo wamesema watu wengine pia ningependa kumuuliza Bwana Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makaa ya mawe ya Mchuchuma, Liganga kila mtu Tanzania amekuwa akiisikia. Kama nchi tuliwahi kujitayarisha kutumia sisi wenyewe ndani? Tumekuwa na mkakati wa kuongoza nchi kwamba hatuwezi kutumia makaa ya mawe? Makaa ya mawe haya kwa maana nyingine yapo lakini ni kama, kule Zanzibar wanasema kama joka la mdimu, yapo hayatusaidii kitu. Tumekaa nayo, hatuyauzi nje wala hatutumii hapa ndani kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni madini. Kama nilivyosema pale mwanzo, tuna madini ya kutosha, kumekuwa na malalamiko mengi hapa. Hata ile alama ya Tanzania (*Tanzanite*) bado hatutumii inavyopaswa. Lakini mbali ya hayo, madini mengine mengi ambayo tunayo katika nchi yetu, hatujayatumia kiasi cha kutosha. Mimi naamini kama tungekuwa tumejipanga basi haya yangeweza kututoa. Tumeambiwa katika *report* ya Kamati kwamba kipato kwenye madini kimeshuka kwa asilimia 19, unajiuliza kitashukaje kwa sababu madini bado yapo kama kuna mikakati mizuri na mipango mizuri ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahivyo mimi naamini tungefanya kazi vizuri katika eneo hili. Eneo lingine kama nilivyosema pale mwanzo, ni *uranium* na *graphite*. Tanzania, watu wengine wamesema hapa tunaweza kuwa katika kumi bora wa matumizi ya *graphite*. *Graphite* imekuja kama akiba yetu, kama hamadi kibindoni ambayo tunaweza tukaitumia ili nchi tuweze kusimama sawa sawa. Lakini kama nilivyosema mwanzo kama hatujakuwa na *strategic mineral policy* ambayo itatuongoza namna ya kuzuia vitu vyetu hivi basi hatutafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, jana nilisikia wazo ambalo nililipenda kidogo, wazo la *STAMICO*. Tunawekeza sana katika *STAMICO*, na dada mmoja hapa amesema, sehemu nyingine walizonazo *STAMICO* ziruhusiwe kwa wachimbaji wadogo wadogo; lakini lilikuja wazo zuri hapa. Wazo lenyewe ni kwamba badala ya *STAMICO* kung'ang'ania kuwekeza na kushindana na makampuni makubwa, kwa nini tusibadilishe *format*, *STAMICO* ikawa inanunua *shares* ambazo zitakuwa zina uhakika, kwa hili wazo ilitolewa na upande wa upinzani ambazo zitaweza ku-*maintain* hii kuliko kung'ang'ania kitu ambacho *STAMICO* hiyo enzi na enzi haijatutoa popote pale na bado tuko pale pale tulipo. Wazo hilo nimelipenda na ningependa Waziri alifikirie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kuhusiana na suala la gesi. Ni kweli kama nchi tunajipanga kwamba tunataka kutumia gesi ikifika mwaka 2023. Lakini tujue tunajipanga, tuna majirani zetu Mozambique nao wana gesi ambayo inaweza ku-*equal* na kile ambacho tumekipata hivi sasa. Kwa hiyo, tujue tutakuwa na ushindani wa karibu, tena maeneo ambayo yamekaribiana. Kwahivyo mtu anaweza akachagua kuja Tanzania au kwenda Mozambique kwa sababu kijiografia ni maeneo yako karibu na kwahivyo kama hatujajipanga sawa sawa hatutaweza kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeshauri, suala la LNG lingetazamwa mapema na namna ambavyo tutafaidika kwa sababu watu wote waliopata gesi wametoka. Qatar, Norway na wengine wote lakini kwa ambavyo mara nyingi naona katika nchi yetu tunaweza kuwa na gesi lakini bado tutakuwa maskini kwa sababu umaskini wa Tanzania kwa sehemu kubwa ni umaskini wa kujitakia. Ndiyo maana nakubaliana na hoja ya Kamati ambao wamesema, Serikali iandae mpango mkakati wa usimamizi wa gesi asilia pamoja na kutafuta masoko mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia ya ushindani, tujipange kwa muda mrefu. Gesi na vitu vingine vinaweza kututoa lakini kama sivyo tunaweza tukabakia hivi badala ya kuwa *economically giant* tukawa *economically dwarfs*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Saleh. Tunaendelea na Mheshimiwa Heche na baadae ajiandae Mheshimiwa Upendo Peneza ajiandae.

**MHE. JOHN W. HECHÉ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia. Na mimi pia nimshukuru Profesa Muhongo kwasababu kwenye Bunge la mwanzo mwezi wa pili aliunda kamati ya kwenda kuchunguza suala la Nyamongo na ndugu yangu Agness pale anasema aliniteua, mimi sikuteuliwa na Profesa ni vyema nikaweka wazi haya mambo yakajulikana.

Kwa hiyo, nampongeza Profesa kwa ile kazi na wananchi wa Nyamongo wanasubiria majibu yao kwa matatizo yale makubwa ambayo yamekuwa pale kwa miaka yote. Leo nilitaka tu niseme kidogo kuhusiana na historia ya mgodi ule wa Nyamongo na utofauti wake na migodi mingine ili Profesa uelewe unapokwenda kutoa majibu ya wale wananchi, utoe majibu ukijua hilo kichwani kwako.

Kwanza ule mgodi ni tofauti na migodi mingine ambayo wazungu wanakwenda wanapata eneo porini huko, wanaanzisha uchimbaji, wanafanya *exploration* na wanaanza kuchimba. Ule mgodi ni mgodi wa wananchi tangu mwaka 1911, watu wa pale walianza kuchimba madini pale kabla hata ya ukoloni na kabla ya Uhuru. Watu wa eneo lile hawana hata eneo la kulima, kwa hiyo waalikuwa maisha yao yote yanategemea uchimbaji wa madini ya Nyamongo, ndivyo maisha yao yalivyokuwa kwa miaka yote. Mwaka 1994, Serikali haya maamuzi ya kuamuliwa Dar es Salaam; Serikali ikachukua leseni ikawapa wazungu. Ina maana ikabadilisha *economic activity* ya watu, kama mimi nafanya biashara ya duka, leo unakuja unafunga duka langu, hunioneshi

kazi nyingine mbadala ya kufanya. Kwa hiyo, Serikali ikachukua leseni ikawapa wazungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazungu wakaja wakatwaa eneo na ule mgodi uko katikati ya makazi ya watu. Wakatwaa eneo, migogoro ikaanza tangia mwaka 1994. Mauaji kila mwaka, tena siyo kila mwaka, karibia kila siku na juzi tarehe 7 mwezi huu umesikia ndiyo mauaji ya mwisho yametokea. Wananchi wale tumebadilisha uchumi wao, hatutaki kuwaandalia njia mbadala, hatujawapa hata mita moja. Nimesoma hapa Profesa uje ufafanue, umesema kwenye ukurasa wa 50 kwamba mmewatengea eneo, liko wapi? Hilo eneo mmewapa wachimbaji wapi? Kwa sababu mimi na wewe tulikuwa pale na *demand* yao ni hii na mimi najua hujatoa taarifa, hujapeleka taarifa ile kwa wananchi lakini umesema ukurasa wa 50 kuna eneo limetengwa kwa wachimbaji wale, akina nani? Hilo eneo halipo na hii ndiyo imekuwa mgogoro siku zote Profesa, pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanataka kuingia pale wachukue kwa sababu hawawezi kufa kwa njaa, wakati mali yao wanachukua wazungu wanaondoka nayo, haiwezekani, ni lazima kutafuta suluhu. Tangia mwaka 1994 Watanzania wenzetu zaidi ya 400 wameuawa pale mgodini. Watu wamebaki na vilema vya maisha, wengi tu ambao hawana idadi. Na hili suala ni suala ambalo kama hatutatatua kwa kuwapa wananchi eneo la kuchimba, hakuna suluhu pale. Wale wazungu wametumia shilingi bilioni 21 kujenga ukuta, yaani baddala ya kutengeneza mahusiano na wananchi kwa kupeleka hizo pesa kwenye maendeleo wamejenga ukuta zaidi ya kilometa 10 na kitu, shilingi bilioni 21 ukuta mrefu na bado haiwi suluhu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi Mkuu wa Wilaya anasema kwamba mtu aliyepigwa risasi alikuwa ameenda *rompad* kuiba madini. Eti anasema *rompad* kuna madini. Mimi nimefanya kazi pale mgodini Nyamongo, *rompad* hawaweki madini, wanaweka mawe na mawe yanakuwa pale zaidi ya tani 2,000, 3,000. Mtu anaenda na kamkoba kuchukua jiwe pale ambalo halifiki hata kilo moja unampiga risasi una-*justify* kifo chake eti alikuwa ameenda *rompad* kuchukua madini, hata hajui amekurupuka tu. Mkuu wa Mkoa anakuja bila heshima anasema waliopigwa risasi ni wahuni kwamba wananchi wa Tarime wanauawa halafu mnawaita wahuni? na nilitamani Waziri Mkuu awe hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatutakubali kauli za aina hiyo kwa wananchi wa Tarime ambao mali yao imechukuliwa, inasafirishwa kila siku na Profesa hapa leo mimi nimekuwa mpole sana kwa sababu nategemea utatoa majibu ambayo ni *positive*, lakini kauli kama zile za Magesa Mulongo kwa watu wa Tarime na watu wa Mkoa wa Mara; Profesa wewe unajua sisi sio wanafiki – nyeupe ni nyeupe. Nilikuwa naona wengine wanakupongeza huko ambao tu walitumika mwaka jana kuku-*crucify*. Bora sisi ambao tumesema na msimamo

wetu umebaki pale pale. Sisi si wanafiki. Wengine ooh Profesa tunashukuru Mungu amekuleta tena, hawa hawa! (Makofi/Vicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Profesa, ninakuomba tatua mgogoro wa watu wa Nyamongo. Nilipokuwa *form two* nasoma historia wanasema sababu zilizosababisha kukua kwa miji kama Johannesburg, ni kuwepo kwa madini pale. Lakini wewe umeenda Nyamongo pale hata mita moja ya lami tangu mwaka 1994 hakuna. Halafu mnataka Wakurya waendeleo kupigia makofi mambo yale, madini yanaondoka. Tunabaki na mashimo, milima, unakuta vijana zaidi ya 2,000 wako kule juu ya mawe. Siku mgodi ukifungwa sijui watakwenda wapi? Mkoa wa Mara hautakalika. Serikali haioni, sisi tunaolia kila siku saidieni hawa watu. (Makofi)

Mheshimiwa wenyekiti, Waziri Mkuu angekuwa hapa asikie, Waziri wa Mambo ya Ndani na Mawaziri wengine msikie. Mgodi unalipa mpaka askari, mimi naamini askari analipwa kulinda mwekezaji na analipwa na Serikali. Lakini mgodi sasa hivi unalipa askari kila siku shilingi 50,000, askari wanaokwenda kulinda ule mgodi na ndiyo maana wamekuwa *loyal* kwa mgodi. Mtu wa mgodi akiwaamrisha kupiga Mtanzania risasi wanapiga tu, hawajali. Askari wamekuwa wanyama pale. Juzi wanakwenda kwenye Kituo cha Afya, wanapiga risasi Kituo cha Afya? Kuna watu wanafanyiwa upasuaji pale, kuna watu wana *pressure* pale, wanapiga mpaka mama ambaye anachukua dawa pale, na Tanzania mambo haya mnaona ni sawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema na hii ni kauli yangu na ni kweli tupu, lazima yale mauaji yakome pale. Yasipoisha askari wenu wale wataniua mimi, nawaambia ukweli. Wataniua mimi kabla sijamaliza Ubunge wangu. Siwezi kukubali tena waendeleo kuu wananchi pale. Nitawapelekea wananchi laki moja pale, watatupiga risasi hawatatumaliza, watajiua wenyewe baadaye. Tangu mwaka 1994 Wakurya wanauawa kama wanyama hata Profesa Maghembe hapa ukigusa swala pale porini hawezi kukubali. Huyu hapa na TANAPA yake gusa swala mle ndani uone kama atakubali, sembuse mtu? Watu wanauawa kama wanyama halafu sisi tukae hapa tunapiga makofi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba Profesa tunaomba suala la wachimbaji wadogo lile lipatiwe ufumbuzi. Watu wapate eneo kwa sababu mzungu amekuja akawakuta wanachimba Nyabirama, amewakuta wanachimba pale Nyarugusu, amechukua lile eneo hamjatengea wananchi maeneo. Bila kufanya hivyo mgogoro ule hautaisha, tutakuwa tunatwanga maji kwenye kinu, tutaunda kamati na kamati. Achilia mbali DC amekwenda pale amehamisha mto, tulikuwa na wewe unaona pale, umemuhoji bila aibu DC anafanya maamuzi ya kuhamisha mto sasa ule mto mvua ikinyesha una *flood* kwenye mazao ya watu kwa sababu ya maslahi ya wazungu. (Makofi)



Mheshimiwa Mwenyekiti, DC anakuja pale siku mbili anajifanya mkali, wazungu wanamchukua wanamweka mfukoni tayari anaanza kuimba nyimbo za wazungu kama yule wa pale. Sasa hivi ukigusa mgodi anasema ua, ndiyo suluhu anayoona. Kwa hiyo ninakuomba Profesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili yale magari ya mgodi yanayosomba mafuta, tuko karibu kuyawekea magogo kuyazuia yasitembee kwenye barabara zetu, kwa sababu yale magari wazungu wale hawarekebishi barabara, Halmashauri tunahangaika na barabara kwa vifedha vyetu vidogo wao wanatembeza mzigo mkubwa. Kama wanataka warekebisha ile barabara yao ya chini ya mgodi, ile ya kule chini watembeze magari yao. Wakipita huku juu ntawahamasisha wananchi wataweka magogo watayapiga mawe. Hatuwezi kukubali watembeze pale, hawaleti hela pale wanataka watembeze, wanatembezaje magari kwenye barabara yetu pale? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, Profesa kuna uamuzi unaweza ukafanya ambao hautakusababisha upigiwe makofi sana...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Heche, muda wako umemalizika. Sasa hivi namkaribisha Mheshimiwa James Millya na baadaye Mheshimiwa Upendo Peneza ataendelea. (Makofi)

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya watu wa Simanjiro, kwanza kwa sababu nasimama mara ya kwanza niwashukuru sana kwa kunichagua na kunipa heshima ya kuwa Mbunge wao na kusaidia kuwaondolea kelele hapa Bungeni. Mimi namshukuru Mungu sana kwa hilo na nawashukuru kwa ajili ya heshima waliyonipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Profesa Frantz Fanon wakati fulani alinukuliwa akisema haya, nanukuu kwa kiingereza; *“every generation out of relative obscurity must find it's own mission and either fulfill it or betray it.”* Kwa tafsiri isiyokuwa rasmi sana kwamba kila jamii kwa wakati fulani lazima ikubali kutafuta njozi yake na labda waamue kuikamilisha au kuikataa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la nchi yetu ni kubwa na tatizo hili kwasababu limetokea CCM wakati fulani si lingine bali ni unafiki na uongo. Unakuta viongozi wanaotegemewa na Taifa hili wanaongea uongo kwa sababu ya kujipendekeza, nilishindwaga mimi, nilishindwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasemahaya? Ugonjwa huu ni mkubwa kwa sababu unakuta makada ninaowafahamu kwa majina wanajaribu kujivua u-Membe, wanajaribu kujivua u-Lowassa kwa kujipendekeza na Serikali iliyoko



madarakani wanawaacha wananchi wanateseka hawasemi ukweli. Huu ugonjwa ni mkubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mifano michache wengine wanasema nisitaje lakini kwasababu sitaki kuwa mnafiki, alikuja Mwenyekiti wa Tume ya mabadiliko ya Katiba, ugonjwa huu ni mkubwa. Katoka kwa wananchi akatetea Katiba nzuri, iliyotoka kwa wananchi kwa mapendekezwa ya wananchi baadaye alipoguswa mahali na CCM akakana matokeo ya wananchi, ni unafiki mkubwa. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa na kama viongozi hatutapona katika hili nchi hii itaenda pabaya. Ninamkosa Baba wa Taifa kama Nyerere, kama Sokoine ambao wakisimama kwa ukweli, watasimamia hiyo kweli na hiyo kweli itawaweka huru milele. Nimewakosa watu hawa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudi kwenye hoja za madini. Sisi watu wa Simanjiro tuna madini ya *Tanzanite*, kwa miaka mingi sana ukienda Naisinyai, kuienda Mererani – Simanjiro watu ni maskini kweli kweli. Eneo lenye watu karibu 50,000 Mererani na Naisinyai hawana maji, *Tanzanite* ipo pale, wanachukua wazungu, wanachukua wazawa, watu wetu wanaachwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, Mheshimiwa Profesa Muhongo ninakuheshimu sana na unajua, nikuombe hata kutokana na yale ambayo yanasemekana si hasara, *corporate social responsibility*, tusimamie, watu wetu wanaumia sana, wanaonewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa leo hii niongee kwa masikitiko makubwa. Tulikuwa na mgodi mkubwa unaoitwa *Tanzanite One*, hata Kamati imegusia na kwenye taarifa mbalimbali ipo. Mgodi ambao Serikali ni mbia, *STAMICO* na mwekezaji uliuzwa kiholela na mimi najiuliza kama Mbunge na ningeomba nipate majibu wakati unakuja kuhitisha hotuba na hoja yako; hivi mgodi ule na ubia ule ulipatikanaje kwa Kampuni ya *Sky Associates* ambayo nimeaminishwa na najua kwenye maandiko si Kampuni ya Tanzania, wametokea wapi watu hawa? Je, *tender* hii ilitangazwa lini ili watu wote wa-*compete fairly* halafu wapewe. *Sky Associates* kama alivyokuwa anasema Dkt. Mwakyembe kuwa wakati fulani aki-present hoja yake ya *DOWANS* hii ni kampuni ya mfukoni, ni ya watu wachache waliotengenezewa ulaji na baadhi ya Mawaziri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hapa, sintachelea kusema Simbachawene anahusika kwenye hili. Kampuni hii leo hii inanyanyasa wananchi wote, wachimbaji wadogo naomba niwataje kwa majina, Simbachawene amesainije mkataba kampuni iingie kwenye ubia na Serikali lakini hakuna mtu alieshindana naye? Eti walitangaza kule *London Stock Exchange*, Watanzana wangapi

wangeweza kuona London Stock Exchange? Leo wachimbaji wadogo wanaonyanyaswa kwenye mkataba huo, Mathias Mnama, Sunda, One, Olomi, Mwarabu na mwingine kapoteza maisha kwa sababu ya mitobozano. (Makofi)

Mheshimiwa Profesa, wewe uliunda Tume wakati fulani, Tume mbalimbali zimeundwa kwa ajili ya mitobozano huko ardhini lakini bahati mbaya kuna Tume yako wewe, kuna Tume ya Dkt. Kipokola, kuna Tume ya Jenerali Mboma, wachimbaji wadogo wanaonewa na mgodi huu kwa muda mrefu.

Ninaomba kwa mara ya kwanza unisaidie kama Mbunge na unisaidie kama mwananchi mwakilishi wa wananchi wengi wanaotaka kunufaika na mgodi wao. Hawa Sky Associate waundiwe tume, ni wezi, hawanufaishi Simanjiro. Ninakuomba, wanaiba madini, wananunua mpaka Maafisa wetu wa Serikali, wengi! Naomba Mheshimiwa Profesa utusaidie kwenye hili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine; Mheshimiwa Profesa madini yanaibiwa kila siku na kampuni hii. Na bahati mbaya, mimi nimeahidi mara nyingi nitakuwa mkweli mpaka nitakapokufa. Wanapata wapi kiburi cha kufukuza wafanyakazi 201 halafu wamewafukuza, baada ya kuwafukuza wanawapeleka mahakamani hawajawalipa mafao na sheria za kazi zinajulikana, bahati mbaya mama yetu Mhagama naye anatajwa humu ndani kwamba ni shemeji wa mmoja wa mbia wa hapo. Dada anaitwa Asia Gongga ameolewa na Martin Mhagama au Yusuph Mhagama, sasa sijui....

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Taarifa Mheshimiwa Mwenyekiti.

## T A A R I F A

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba afahamu katika nchi yetu ya Tanzania jina la akina Mhagama ni ukoo mkubwa na ukoo wangu mimi wa akina Mhagama hauna huyo mtu anayemtaja.

Sasa ninaomba kumpa taarifa anachokisema si sahihi na hakikubaliki na asichafue ukoo wetu wa akina Mhagama kwa sababu ya majina kufanana bila yeye kufanya utafiti. Kwa hiyo ninaomba kabisa kumpa hiyo taarifa na kwa kweli ikiwezekana aache na asipoacha nitatumia kanuni nyingine ili kuchukua hatua. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Millya, taarifa hiyo.

**MHE. JAMES K. MILLYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba ukoo wake ni mkubwa na mimi ni kwamba nimepata taarifa. Nimetaja taarifa tu kwamba anatajwa. Angesema tu mimi huyo sihusiki naye, *simple*. Lakini watu hawa wanapatiwa kiburi na nani? Wanafukuza Watanzania halafu sekta yako inayosimamia wafanyakazi haiwasaidii, kwa nini nisihusishe jina hilo na jina lako? (*Makofi*)

Baada ya kusema haya mgodi huu tunataka tunufaike nao. Madini haya yamechukuliwa kwa muda mrefu lakini kampuni hii ya kitapeli iondolewe mara moja, Wanasimanjiro na Mheshimiwa Waziri nikuombe ukutane na wananchi hawa ukutane na wachimbaji wadogo usikie kilio chao. *Tanzanite* kwa mara ya kwanza na EPZA, kwa nini msijenge EPZA, madini yetu yanatoroshwa kila siku. Tumeto aeneo kama Simanjiro, liko eneo la EPZA, mnachelewa kulijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Millya, tunaendelea na Mheshimiwa Upendo na baadaye Mheshimiwa Kanyasu John na Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje wajiandae.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii, na naomba pia niweze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia tena fursa nyingine na kuweza kuzungumza ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kusoma ripoti ya *committee* maalum iliyoungwa na Rais nimepata kutambua ya kwamba yawezekana kama nchi na katika vipindi vilivyopita na leo hii katika juhudi zinazofanywa na Rais wa sasa za kutafuta mapato mbalimbali lakini Serikali kwa vipindi vilivyopita ilishiriki kikamilifu kusababisha ukwepaji wa mapato ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema kauli hiyo ukiangalia katika mikataba ambayo iliingiwa na nchi hii, katika mkataba wa Bulyanhulu ambao uliingiwa mwaka 1994 kutokana na ripoti maalum ya *committee* ya Rais inaonesha ya kwamba suala la *fuel levy* ama mapato au misamaha ya kodi inayotokana na mafuta yanayotumiwa mgodini ilipitishwa kama *government notice* mwaka 1999. Lakini mgodi huu ulipata mkataba mwaka 1994 ambapo Bulyanhulu ni sehemu ya migodi ambayo inapokea misamaha ya kodi kwenye mafuta. Mwaka 2014 Bunge hili hili tukufu lilitunga sheria na kuilinda mikataba ile ambayo imepita kwamba watu hawa hawafai kuguswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kwamba tusifike hatua tukasema tufunike kikombe tuendeleo na mambo mengine, lakini kuna haja ya kupitia pale tulipotoka tuweze kuona kwamba kama kuna

mapato mengine tunaweza tukayapata na tusifunike tu kwamba mikataba tulishaifanya basi, sehemu maalum ziangaliwe kuangaliwa ili kuweza kuongeza mapato ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna suala la *service levy*, mapato yanayolipwa na migodi ambayo ni asilimia 0.3 ya *turn over* ya migodi hiyo. Kwa miaka iliyopita Serikali iliweka *fixed cost* kitu ambacho ni tofauti kabisa na Sheria ya Serikali ya Mitaa ya mwaka 1982. Wakaweka *fixed cost* ya dola za Kimarekani 2,000 ambazo ndizo zinazofaa zilipwe katika Halmashauri zetu. Lakini mwaka 2014 yalifanyika mabadiliko na sasa *service levy* inalipwa kwa 0.3, ile ile ya *turn over*. Sasa naitaka Serikali iweze kusimamia na kuhakikisha kwamba inazisaidia Halmashauri hizi ili kuweza kutambua ni kiasi gani ambacho ni *turn over* wanayostahili kama Halmashauri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Halmashuri zetu hazina uwezo mkubwa kwa hiyo Serikali iweze kulifanya hilo na kuweza kusaidia. Lakini vilevile tuna TMA na wao wahusike kuangalia, isiishie tu udhibiti kwa maana ya madini lakini waangalie katika eneo kubwa la kuangalia kiasi gani ambacho Halmashauri zetu zinastahili ili kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa Wizara zingine hasa ile inayohusiana na Mambo ya Serikali za Mitaa ni muhimu pia wakatambua ya kwamba dhahabu au madini yoyote yale hayatarudi tena kuwepo kwenye ardhi. Kwa hiyo, ni vyema basi tukaweza kuzishauri Halmashauri zetu, tukashiriki kikamilifu ili walau kiasi kinachotolewa kwa ajili ya *service levy* kitumike kwa ajili ya kuendeleza Halmashauri, kuweka mikakati au uwekezaji mkubwa ndani ya Halmashauri zetu lakini pia kuendeleza huduma za kimaendeleo badala ya hizo hela kutumika kwenye OC ili Serikali nayo ipange mambo mengine lakini pesa zitumike kwa shuguli za maendeleo zilizokusudiwa kwa ajili ya wananchi wa eneo husika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Geita na katika maeneo ambayo yanapata shida kubwa sana kutokana na uwekezaji wa kampuni ya *Geita Gold Mine*, ni wananchi wa Geita. Wananchi hawa katika maeneo ya Katoma, Nyamalembo na Compound. Wananchi hawa wamekuwa wakiathirika na mitetemo, vumbi inayotoka migodini. Vilevile nyumba zao zimekuwa zikiathirika kwa nyufa. Mheshimiwa Naibu Waziri aliweza kuwatembelea wananchi hao na akagundua kasoro ambazo zipo na akaona matatizo ya kuchafuka kwa maji kwa maeneo ambayo wananchi wanaishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha kusikitisha, Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa agizo kuwa mgodi kwanza kuziba mtaro ili maji yasiende kwenye visima vya maji, lakini pia kuhakikisha ya kwamba wananchi hawaendelei kunyanyasika katika eneo lao. Lakini nikutaarifu kwamba ni kitu cha

kushangaza, mgodi huu una kiburi cha ajabu yaani hata agizo la Serikali hawakuweza kulitimiza na mpaka leo hii hicho hakijafanywa na badala yake Serikali inaangalia namna mbadala ya kuongea nao, badala ya kusaidia maisha ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna kesi mbalimbali ambazo zimejitokeza Geita, Mheshimiwa Waziri unafahamu kuna wananchi wa Maili Mpya katika eneo lile. Wananchi ambao walifukuzwa kwa kudhalilishwa, maeneo yao yakafukiwa, mgodi umechukua hilo eneo, lakini bado kuna wananchi wa Katoma ambao wengine hawakulipwa fidia hata kidogo, wamefukuzwa katika maeneo yao. Sasa haiwezekani kwamba tuna Serikali; kuna kipindi niliendelea kuitembelea nchi ya Norway katika mafunzo wakatuambia kwamba wafanyakazi walivyokuwa wananyanyaswa walifananisha manyanyaso yao na wafanyakazi wa Kiafrika wanaonyanyaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini leo tunanyanyaswa sisi ndani ya nchi yetu na wawekezaji hawa hawa bila kuzingatia haki za binadamu na uhuru wetu na afya zetu ndani ya Taifa letu. Kwa hiyo, ninaiomba sasa Serikali iweze kuangalia ni namna gani mtawasaidia wananchi wa Geita. Kutakuwa hakuna maana kwa wao kumpigia Rais Magufuli kura nyingi na kwa imani kubwa waliyonayo tena Rais kutoka nyumbani, halafu wakabaki na manyanyaso makubwa yanayofanywa na mgodi wa *Geita Gold Mine*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mtaa wa Nyakabale ni eneo ambalo liko ndani ya *beacon* ya mgodi. Eneo hilo wananchi wa Nyakabale kama unavyofahamu limefungiwa hata nyia yake. Wananchi hawawezi kutumia njia maalum waliokuwa wanatumia zamani kuelekea mjini, badala yake mgodi umeweka mabasi asubuhi na jioni, mgodi ume-*limit movement* ya wananchi katika eneo husika. Pia limechimbwa shimo la takataka ndani ya eneo lao ambapo sumu za mgodi zinamwagwa ndani ya Nyakabale katika Kata ya Mgusu. Hii inaathiri afya za wananchi wa Geita, zinaathiri afya za wananchi wa Nyakabale. Ninaomba Serikali mfuatilie hilo ili hali iweze kukomeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni suala la wachimbaji wadogowadogo. Katika kipindi kilichopita Serikali iliwahamisha wananchi wa Samina na kusema kwamba inawapatia eneo lingine la uchimbaji. Kwa masikitiko makubwa sana Serikali ilitoa eneo ambalo halijapimwa na ilitoa pia sehemu ambayo utafutaji wa madini kwenda chini uko mbali sana. Sasa Serikali yetu hii naiomba inavyotoa maeneo ya madini yaliyo karibu kwa wawekezaji wawafikirie wazawa Watanzania ili waweze kufanya shughuli za uzalishaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuwakumbuke wanawake katika hiyo ruzuku uliyoitaja wachimbaji wadogo wadogo, wanawake wawe ni sehemu ya

ushirikishwaji katika maeneo ya uchimbaji wadogo wadogo. Kwa sababu wanawake wanapiga mawe, wanawake wanafanya shughuli za kwenye makarasha, wanawake wanafanya shughuli mbalimbali katika maeneo ya migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia Wizara iweze kuliangalia hilo katika hizo ruzuku wanawake wa Geita pia ziweze kuwafikia na ziweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wananchi wa Nyarubuso, ni wananchi wanao athirika kutokana na shughuli za *ellusion* ama uchenjuaji wa dhahabu. Serikali naomba itoe elimu nzuri kwa wananchi wa Geita, kwamba pamoja na uchenjuaji huo lakini waweze kufanya shughuli ya makusudi ya kwamba uchenjuaji usiathiri vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ninaiomba Serikali itoe kauli humu ndani, Iitoa ahadi kwa wananchi wa Geita kuwapatia magwangala ama mabaki ya dhahabu, lakini tunafahamu Serikali haijafanya uchunguzi kujua ni kiasi gani watapata dhahabu katika magwangala hayo. Ninaomba Serikali itoe kauli ili mchanga huo basi wananchi kwa sababu wamekosa maeneo ya kuchimbia, sasa wanatafuta mabaki ya mchanga wa dhahabu kutoka katika kampuni ya *Geita Gold Mine*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itoe kauli ili kauli iliyotangazwa na Makamu wa Rais Mama Samia Suluhu tuweze kuelewa ina faida ama haina faida na lini itatekelezwa kwa wananchi wa Geita ili walao kama hamjawapatia maeneo walau wapatieni huo mchanga ili waweze kujifanyia shughuli zao za maendeleo, ahsanteni sana. *(Makofi)*

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7), 64(1) (a) na 63(4).

Mheshimiwa Mwenyekiti, inataka kuzuka tabia humu ndani tena ya makusudi kabisa ya watu kutaka kuchafua majina ya wenzao bila sababu ya msingi kwa kutumia maneno ya uongo, ambayo ni maneno yasiyoruhusiwa ndani ya Bunge hili. Mbunge Millya alipomaliza kusema hapa na mimi nilipompa taarifa bado akaendelea kusema ninakiri kwamba huyo mtu ni shemeji yangu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Mwongozo wako kwa Mbunge huyu aliyesema uongo na mimi nathibitisha na nina uhakika kabisa huyo siyo shemeji yangu, ninaomba Bunge lako limtake Mheshimiwa Millya alete ushahidi na kuthibitisha ushemeji wangu kati yangu mimi na huyo mtu aliyosema na kama hatauthibitisha, Bunge lichukue hatua ili kukomesha tabia hii ya Wabunge kutaka kupakaziana tu masuala ambayo hayana ukweli ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ahsante nimepokea Mwongozo tutautolea baadaye. Tunaendelea na Mheshimiwa Kanyasu C. John na baadaye tutaenda na Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Nakushukuru sana Mwenyekiti, na naomba nimshukuru pia Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema, niwashukuru pia wapiga kura wangu wa Jimbo la Geita Mjini na wananchi wa Geita kwa ujumla wake kwa uvumilivu wao mkubwa wanaoupata kwenye matatizo ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwanza kwa kusoma kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 15 ambapo amesema Serikali iliajiri kampuni ya *Shaka Consult Group* ya Misri kuwa mshauri mwekezaji wa kusimamia utekelezaji wa mradi wa Bulyanhulu - Geita KV-220 kwenye urefu wa kilometa 55.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameendelea kusema hapa lakini *interest* yangu ni kule chini; anasema gharama za mradi huu ni dola milioni 23 sawa na takriban bilioni 41. Jumla ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni shilingi bilioni sita, *very interesting*, na unatarajiwa kukamilika 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa mradi huu ambao ameukusudia kupeleka Geita. Ninaamini kwamba una nia njema, lakini natazama fedha zilizotengwa sasa na pia natazama muda ambao umejiwekea kutekeleza nayaona matatizo makubwa ya umeme katika Mji wa Geita kwa sasa yataendelea kuwa kero kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anafahamu nimsumbua sana mara kwa mara, umeme wa Geita Mjini unazimika kila saa, umeme wa Geita Mjini ambao unatokea Sengerema kuja Geita ni mdogo, ulikuwa umefikiriwa kwa ajili ya Mji wa Sengerema na baadaye ukapelekwa Geita. Umeme ule inapofika saa moja jioni unawaka lakini taa haziwaki. Nimemueleza hili Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri analijua, sasa nilitarajia kwenye taarifa yake hii atakuwa angalau na mpango wa dharura kwa sababu Geita



pale ni Mji mkubwa, lakini ni Mkoa ambao tungeweza kuweka mpango mzuri wa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninayo mapendekezo, tunao umeme kilometa 22 tu kutoka Geita Mjini ambao uko Katolo ambao ni umeme wenye nguvu. Wakati unafikiria mradi mkubwa huu ambao utaisha 2018, na inawezekana ukaisha 2020. Umeme huu ambao uko kilometa 22 tu kutoka Katoro kuja Geita, na ambao gharama yake inakadiriwa haifiki bilioni moja kuuvuta kuufikisha Geita Mjini, ingelikuwa ni suluhisho la kwanza la kupeleka umeme katika Mji wa Geita. Hivi ninavyozungumza na wewe kata zinazotengeneza Mji wa Geita wenyewe, kata za Nyankumbu, Bombambili, Buhalahala, Mtakuja zote hazina umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani umeme upo pale pale kati kati ya Mji lakini Vitongoji vyote vya Geita Mjini havina umeme. Pamoja na huo uliopo kutokuwa hautoshi lakini havina umeme. Kuna sehemu wameweka transfoma ambayo kila inapofika jioni saa moja umeme unazimika. Nilikuwa nakuomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na nia njema ya mradi huu unaokwenda mpaka 2018 ambao pia naona fedha zake zimewekwa za kuanzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe suluhisho la sasa, kwa sababu umeme uliopo Katoro una nguvu, utolewe umeme upelekwe pale. Bahati nzuri sana Geita tuna Meneja mzuri wa TANESCO, ana-respond haraka, hana matatizo makubwa, kinachosumbua pale sasa ni kumwezesha ili aweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niende kwenye umeme wa REA. Katika Jimbo la Geita Mjini umeme wa REA bado katika kata zote 13 haujaenda, nimefanya mawasiliano na Meneja wa REA wa Kanda ile amesema ametuingiza kwenye awamu hii, lakini nilikuwa naomba sana, kwa sababu tatizo hili naliona hata katika Jimbo la Geita Vijijini, kazi ya mkandarasi imekamilika mpaka sehemu ya kutoka Nyamadoke tayari; pale panatakiwa tu kuunganishwa ule umeme, leo karibu miezi sita hapajaunganishwa. Nilikuwa naomba sana kwenye umeme wa REA Mheshimiwa Waziri suala hili lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni suala la wachimbaji wadogo wadogo. Mheshimiwa Waziri alikuwepo Geita, na nashukuru kwamba tulifanya mkutano naye na akatoa takwimu nyingi sana. Lakini anakumba nilitoa ushauri wangu pale sikumpinga nilitoa ushauri, ana takwimu nyingi sana zinazoonesha wachimbaji wadogo wamepewa maeneo lakini wanaopewa ni wale wale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayepewa leo London – Singida, anayepewa leo Nyarugusu, anayepewa Kahama, majina ni yale yale. Nilimshauri

atengeneze *database*, atagundua yako majina yale yale yanazunguka. Kila yanapogunduliwa madini wanakwenda wanafukuza wenyeji, wanaunda ka-SACCOS wananunua watu wanahamia pale. Nashauri kwamba wananchi wale wa kawaida bado hawapati maeneo, na ndio maana kelele za magwangala zitaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakati tunazungumzia maeneo ya wachimbaji wadogowadogo lazima tuangalie watu wanaojirudiarudia, watu ambao kila mara yanapogundulika madini wanakwenda pale kwenda kutafuta maeneo mapya. Tulipokutana na Mheshimiwa Waziri kwenye ziara yetu Geita tulimrusia kuhusu milipuko. Mheshimiwa Naibu Waziri tulikuwa naye Geita, tulikwenda kwenye nyumba ambazo zimeathiriwa na milipuko, tulikwenda kwenye nyumba ambazo vigingi vya GGM viko ndani ya makazi yao, wale watu hawaruhusiwi kupima, hawaruhusiwi kuuza, wanaonekana eneo ni la mgodi lakini mgodi wanasema hawana kazi nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishauriana na Mheshimiwa Naibu Waziri na akatoa muda, akawaambia wafanye *declaration* kama wanalihitaji lile eneo walipe fidia watu watoke na kama hawalihitaji, wawaruhusu watu waendeleo na maisha yao mpaka leo hili suala halijafanyika, matatizo ya watu yanaendelea kuwa pale pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu niseme kwamba kuendelea kukaa katika vigingi watu hawa wanaendelea kuwa maskini. Hawawezi kupima, hawawezi kukopeshwa, hawawezi kujenga nyumba za kudumu. Kwa hiyo, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutoa majibu atuambie anafanya nini kwa sababu hali hii inasababisha wananchi wangu wa Jimbo la Geita kuendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kidogo kuhusu magwangala. Kama wanavyosema wenzangu magwangala inatokana na vijana wengi na wanataka biashara za madini kukosa maeneo ya kuchimba; si suluhisho la matatizo ya wachimbaji wadogo wadogo kwa sababu nina uhakika magwangala yale hata yakitolewa leo baada ya miezi miwili, yatakwisha na yatakapokwisha yale magwangala tutatengeneza tatizo jingine kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka kusema pamoja na nia njema ya kutoa magwangala haya ambayo wananchi wanayapigia kelele, wananchi walikuwa na maeneo yao walikuwa wanachimba ya asili pale Geita, kama Nyamatagata, Samina wakaja wakatolewa, lakini maeneo yale dhahabu yake iko juu juu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alipokuwa Geita akisema yeye hawezi kubadilisha hata mtu ampige risasi. Mimi nataka nimshawishi

Mheshimiwa, sheria inasema kila baada ya muda, wanapofanya *revision* ya *license* kuna maeneo watu wanayaachia, ni vizuri sana Mheshimiwa Waziri maeneo ambayo wanayaachia yawe ni maeneo ambayo wananchi wanaweza wakachimba wakapata dhahabu ya juu juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo tuliyonayo sasa hivi Geita ni kwamba hata kama watu wa GGM wangejenga hospitali, shule na barabara kama jamii inayowazunguka pale inalala njaa, kama jamii inayowazunguka pale bado wanaishi katika mazingira kama wako utumwani bado wataendelea kuwachukia wawekezaji na tutaendelea kuuchukia mgodi.

Kwa hiyo, mimi nilitaka niwashauri kwamba ni lazima wananchi wapewe maeneo ya kuchimba, na hili liko ndani ya uwezo wako kwa sababu maeneo tunayo. Tatizo kubwa ni moja walipelekwa maeneo ya Isamilo, wakapewa *license* karibu 17 za SACCOS wamechimba watu wameweka karibu milioni 200 madini hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamechimba pale wanakutana na maji madini hakuna, kwa hiyo mara nyingi migodi inaachia maeneo ambayo imefanya utafiti imegundua kwamba dhahabu zilizopo pale ni ndogo na hazifai. Kwa hiyo nikuombe sana utakapotaka kutoa maeneo tuhakikishe kwamba maeneo haya yana madini ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la *service levy*. Mheshimiwa Waziri alipokuwa Geita, tulimwambia hatuna mgogoro na *Geita Gold Mine* ingawa mchango wao wa *service levy* ni mdogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Geita ule ni mgodi wa pili Afrika kwa dhahabu nyingi, wanatupa bilioni nne. Tuliuliza swali, hizi ni asilimia ngapi ya mapato yao? Kwa sababu tunaamini mapato yao ni makubwa sana, lakini la pili, wanatoa orodha ya kampuni 1,000 wanazofanya nazo kazi. Katika hizo asilimia 80 kampuni zile ziko Ulaya, Australia, New Zealand na Marekani, wanafanya nazo *electronic business*. Kwa hiyo, anampa Mkurugenzi wa Halmashauri aende akakusanye *service levy* kwa kampuni ambayo haina *license* Tanzania, hailipi kodi Tanzania, haina *address* Tanzania. Tulimwambia Mheshimiwa Waziri, watu wa mgodi walazimishwe kufanya kazi na kampuni za Tanzania ambazo tunaweza kuzi-*trace* na kujua zinapatikana wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi wanakupa kampuni iko New Zealand halafu wanakwambia ukusanye *service levy* kampuni hii haijulikani, haina leseni, hailipi kodi za Serikali, hata Tanzania haina *address* na Mheshimiwa hili niliwahi kufika mpaka ofisini kwako nikakutana na Katibu Mkuu wa Wizara, nikamshauri, nikazungumza naye na akasema atalishughulikia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hawa watu pamoja na kuwaibia Halmashauri ya Geita, bado pia wanaiibia Serikali. Huwezi ukalipa mtu dola milioni moja kampuni yake iko *South Africa*, Tanzania haina leseni, hailipi kodi, haina ofisi na Serikali ipo inakubali hizo hesabu wakati wa kufanya *Cooperate tax*.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana hili liangaliwe vizuri. Na inawezekana kabisa haya yanafanyika kwenye makampuni yote katika nchi hii, kwa sababu visingizio ni kwamba kuna vipuri ambavyo vinaagizwa Ulaya na Watanzania wengi hawana uwezo wa kuviuza, yes tunakubali, lakini *procedure* za kufanya biashara Tanzania zinajulikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Watanzania hamuwaruhusu hata kufungua kibanda cha soda bila kupata *TIN Number*. Kwa nini huyo anayellipa mamilioni ya shilingi anaanza kufanya biashara na Mgodini na analipwa pesa na inakuwa *declared* kwenye hesabu wakati hana leseni Tanzania na halipi kodi? Ushauri wangu Mheshimiwa Waziri asaidie kupata hizi fedha kwa sababu ni fedha nyingi na tunazihitaji kwa ajili ya maendeleo ya Mji wa Geita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama unavyoitaza Geita sasa hivi, kuna mashimo makubwa, ambayo tayari dhahabu zimekwisha. Inawezekana kabisa miaka ishirini ijayo tukabaki na mashimo yale na wananchi wa Geita wakaendelea kubaki maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu ni kwamba wakati mgodi unafikiria kufanya *CSR* washirikiane na Halmashauri kuangalia miradi ambayo sisi tunadhani ina tija kwetu. Siyo wao wanabuni mradi wao halafu ule mradi wanaugeuza kuwa mradi wa wananchi wa Geita. Tunaunga mkono juhudi zao tunapenda waendeleo kuwepo, tunataka wawekezaji zaidi lakini lazima waangalie mipango ya Halmashauri namna gani wataingia kwenye mipango hiyo kuliko kuja na mipango yao wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekwenda wameanzisha, chuo cha kushona cherehani wameanza na watu 90 sasa hivi wako watu kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja.  
(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kanyasu. Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Hassan Seleman Kaunje na baadaye Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima na Mheshimiwa Seleman Zedi wajiandae

**MHE. HASSAN S. KAUNJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Lakini kwa utamaduni wa Kitanzania unapofanyiwa jambo

jema ni vizuri ukatoa shukrani, na shukrani zangu za dhati, ziende kwa Profesa Muhongo, REA, TANESCO Lindi, lakini vilevile TANESCO zone ya Kusini kwa kushughulikia tatizo la umeme katika kata mbili za Ng'apa na Tandangongoro ambazo zimepitiwa na bombala gesi lakini umeme ulikuwa haujafika. Wamelitatua tatizo hili na ninawashukuru na kuwapongeza sana kwa juhudi hizo walizozifanya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninataka nizungumze *especially* kwenye suala moja tu la LNG inayoenda kujengwa Lindi. Na ningemuomba Mheshimiwa Waziri anisikilize kwa umakini ninayotaka kuyazungumza kwa sababu, kuna ninayotaka kuyashauri ya msingi sana ambayo anapaswa kuyachukua kuanzia sasa anapoanza safari ya kuelekea katika uwekezaji wa kiwanda hicho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 35 wa hotuba yake ameomba tuidhinisha shilingi milioni 800, anaenda kufanya maandalizi ya uchoraji wa ramani ambayo itaingia katika Mipango Miji katika Manispaa ya Lindi ya kiwanda hiki anachotaka kujenga, lakini vilevile maandalizi ya uwanja wa ndege wa Lindi kwa ajili ya programu inayokuja. Sasa wakati anayafanya haya nimuombe Mheshimiwa Waziri aende sambamba na kulipa fidia kwa wakazi ambao wanaoondoka katika eneo ambalo litaguswa na mradi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimuombe Mheshimiwa Waziri afanye yafuatayo katika eneo hilo, anaenda kuandaa mchoro wa kiwanda, ila eneo la Lindi Manispaa halina *master plan* ya Mji, kwa hiyo, aongee na Waziri mwenzie anayehusika na *master plan* wahakikishe *master plan* ya Mji wa Lindi inapatikana kabla ya michoro hiyo inayoenda kuandaliwa na kuingizwa haijaweza kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo anaenda kuyafanya hayo anayotaka kuyafanya, atusaidie kutupelekea pesa zetu kwa kumwambia Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwamba zoezi la kuandaa mpango kamambe huu ambao ni *master plan* unakwama kutokana na kuzuiwa kwa zaidi ya shilingi milioni 700 ambazo ni *retention money* ambazo ziko kwake zinazotokana na uuzwaji wa viwanja. Tupelekee fedha hizi katika Manispaa ya Lindi, ili tuweze kuandaa mpango kamambe. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, anapeleka mradi huu ambao unatarajiwa kupeleka zaidi ya wafanyakazi na watu wengine watakaokadiriwa kuwa 20,000 na Mji wa Lindi una watu takribani 100,000 kwa hiyo, unapopeleka watu 20,000 ni idadi kubwa ya watu. Lakini wananchi wa Lindi wana matumaini makubwa na mradi huu unaenda kutatua, historia yao inaenda kufutwa ya umaskini uliokithiri kupitia ajira zitakazotokana na mradi huu, lakini watu wa Lindi

wana tatizo moja kubwa la kihistoria, umaskini wao ni pamoja na kukosa elimu, hawana elimu, yanayoendelea katika mradi huu hata yaliyoanza sasa hivi ajira zile ndogo ndogo za maandalizi wanashindwa kupata kutokana na kukosa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, anapopeleka kiwanda hiki ambacho ujenzi wake utakamilika sio chini ya miaka kumi kutoka sasa hivi, basi aungane na Waziri wa Elimu kuweza kuandaa mpango utakaowafanya wananchi wa Lindi waweze kuwa na sifa hitajika na kuingia katika ajira zitakazotokana na kiwanda hiki pale kitakapokamilika. Nasema hivi mpango uwe maalum kwa sababu Serikali kwa mara nyingine au mara zingine imeshawahi kuchukua hatua stahiki za kusaidia baadhi ya maeneo kutatua kero zinazowasumbua *especially* za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona maeneo yale ya Wamasai ilipeleka programu maalum ya kuwafanya wasome, lakini vilevile kwenye maeneo ambayo ukeketaji kulikuwa na shida, Serikali ilichukua jukumu maalum la kuhakikisha kwamba tatizo hili linaondolewa. Nimuombe yeye na Waziri husika na Serikali kwa ujumla, wananchi wa Lindi walio wengi hawana elimu na uwezo wa kuweza kufanya kazi katika kiwanda hiki kitakapokamilika, tuwasaidie kwa kuanza na programu hii anapoanza sasa kuelekea kule kukitengeneza kiwanda hiki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulisimama hapa Mbunge mwenzangu wa Nachingwea, aliomba Mheshimiwa Waziri wa Viwanda apeleke wawekezaji watakaoweza kuwekeza *processing* ya samaki kwa sababu tuna ukanda wa kilometa 112 Lindi Mjini ambazo ni za bahari. Na kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri alisema tusiwahishe shughuli anatuletea kwanza viwanda vya mihogo; lakini lengo letu la kuzungumza viwanda vya samaki tunamaanisha kwamba kuna wavuvi ambao watahitaji soko lile na kwa sababu tunapeleka watu ambao watakuwepo katika kiwanda hiki, tunapaswa tujipange na tuwawezeshe wavuvi hawa waweze kuwa na soko la uhakika, ili waweze sasa na wao kuingia katika uchumi unaoenda wa kiwanda hiki cha gesi. Nimuombe basi, amwambie Waziri pamoja na kiwanda cha mihogo ambacho anatupelekea, basi atusaidie kutupelekea watu watakaowekeza katika sekta ya samaki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika eneo lingine. Eneo hili nataka nishauri kwa ujumla katika mambo yanayohusu uchumi wa Taifa ambao unaendana na Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ununuaji wa mafuta wa jumla ambao kwa kifupi unaitwa *BPS*. Na katika uagizaji ule wa mafuta makampuni yanayoleta mafuta ambayo yana zabuni ile mengi yamekuwa *registered* nje ya Tanzania.



Matokeo yake kwamba makampuni yale yanakwepa baadhi ya kodi ambazo zingepaswa kulipwa kama tu wange-register BRELA, Tanzania. Nimuombe Mheshimiwa Waziri alifanyie kazi jambo hili, ili kampuni hizi zinazoingiza mafuta ziweze kulipa kodi stahiki ambazo zitaendeleza Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo kuna jambo la vinasaba vya mafuta vinavyowekwa katika mafuta tunayoyatumia. Jambo hili linapigiwa kelele na wadau tofauti, wazo langu ni lifuatalo; Mheshimiwa Waziri lengo la kuweka vinasaba katika mafuta tunayoyatumia ni kuhakikisha kwamba tunakuwa na mafuta salama kwa ajili ya vyoimbo vyetu. Kuna wadau wanaozungumza kwamba jambo hili si zuri. Tunaweza tukaungana nao mkono, lakini tutaungana nao mkono tu pale tutakapohakikishiwa usalama wa vyombo vyetu, hivyo nimshauri Mheshimiwa Waziri jambo hili liendelee mpaka suluhu yake itakapopatikana na kuonekana jambo hili linaweza kutatuliwa kwa namna nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyazungumza haya nimuombe Mheshimiwa Waziri asiponijibu vizuri lini atawalipa fidia wananchi wa Mbanja, wananchi wa Likong'o, wananchi wa Kikwetu kupisha ujenzi wa kiwanda chake, nakusudia kuondoa Shilingi katika bajeti yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa wasaa huu wa kuchangia katika Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Sima na baadae Mheshimiwa Selemani Zedi.

**MHE. MUSSA R. SIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kukushukuru, lakini pia nimpungeze sana Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini kwa kazi yake. Hakuna ubishi kwamba mzee huyu kwa kweli ana-fit kwenye nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na umeme; katika Jimbo langu la Singida Mjini ninavyo vijiji 13 na mitaa 13 ambayo haina umeme. Katika taarifa yake Mheshimiwa Waziri, imeonesha wazi kwamba kutakuwa na KV 400 zinapita Singida kwenda Shinyanga, lakini pia kwenda Namanga. Nimuombe sana tusiwe watazamaji, lakini tusiwe watu wa kupisha mradi unapita unaenda kwa wengine na sisi tuwe sehemu ya mradi. Naomba Mheshimiwa Waziri utushirikishe na ikiwezekana sasa vijiji vyangu vyote hivi nilivyovitaja na mitaa viweze kupatiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeguswa kidogo na suala la vinasaba. Kabla sijaendelea na mimi nichukue fursa hii kumpungeza Mheshimiwa Waziri kwa kuweka vinasaba ambavyo vimetusaidia kwa kiasi kikubwa sana; vimepunguza



uchakachuuji wa mafuta kwa asilimia kubwa na kama haitoshi vimedhibiti mafuta ya magendo (*smagling product*). Vinasaba hivi vimedhibiti pia *on transit product*. Yale mafuta yanayopita hapa kwenda nchi za jirani vimedhibiti, lakini pia hata yale mafuta ambayo yanasamehewa kodi, vinasaba hivi vimetusaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi vimeongeza makusanyo ya kodi na vimeleta ushindani kwa wafanyabiashara wa mafuta nchini. Nikuombe sana na niwaombe Waheshimiwa Wabunge na wananchi tufike mahali tuiunge mkono Serikali, tuwe waadilifu na kama haitoshi kwa wale wafanyakazi wetu ambao tunawatuma kwenda kubeba mafuta haya sasa wawe makini na kazi hii kwa sababu Serikali kwa kweli ina mkono mrefu na nikuombe Mheshimiwa uifanye kazi yako vizuri, nakupongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie suala la madini. Kwa kweli, kwa Mkoa wangu wa Singida tunayo madini mengi sana na ya kutosha, lakini hali tuliyonayo pale haifanani na yale madini tuliyonayo pale. Nataka niombe Serikali sasa iwaangalie wale wachimbaji wadogo waweze kupewa fedha na kama haitoshi, wachimbaji wadogo wale waweze kupewa elimu, kwa maana sasa waendane na teknolojia ya uchimbaji ya sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo ninaloliona pale, naliona tatizo kubwa moja, *GST*. Mamlaka ya *GST* siyaoni, *GST* wanavyoonekana kwa sasa kazi yao haina meno. *GST* wakati umefika sasa wafanane kama *EWURA* kwa sababu, na wao nao ni wakala, wapewe hatimiliki. Sasa hivi makampuni yote tunayoyaona makampuni makubwa ndio ambayo yanafanya utafiti na wakishamaliza utafiti ule hawako tayari kutupa hali halisi ya madini tuliyonayo pale kwenye maeneo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejionea, nitoe mfano wa *Shanta Company Limited* pale Singida walitoa eneo la Mwintiri kwa wachimbaji wadogo, lakini eneo lile wachimbaji wadogo wameshindwa kuliendeleza kwa sababu hawana utafiti, hawajapewa ramani nzima ya eneo lile lililopo pale. Sasa kwa hali hii ni lazima Serikali ije na mpango kama ni sheria, kama ni nini, ije tuweze kuisimamia. *GST* wapewe mamlaka wawe mawakala ambao wanaweza kusimamia *raw data* na sio watu wa kupewa *processing data*. Huu sio wakati wa *processing data*. Wawe ni watu ambao wana *raw data* na wawekezaji wote wanaokuja waanzie *GST*, hii inaweza kutusaidia sisi na wale wachimbaji wetu wadogo walioko kule wanaweza kupata mwelekeo wa kuchimba madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama ambavyo alitangulia msemaji mmoja tuko naye kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara alizungumzia namna ambavyo *TANELEC*, kiwanda ambacho sisi tuna hisa, kiwanda ambacho kimefika mahali sasa Serikali imekitelekeza. Mimi nizungumzie upande mdogo

wa REA. REA waliwapa kazi Symbion, Symbion wamekwenda kuomba kutengenezwa transfoma TANELEC, hivi tunavyozungumza zimetengenezwa transfoma za zaidi ya shilingi bilioni mbili zimekaa pale. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia kama Kamati transfoma ambazo Symbion walizi-order ziko pale TANELEC, kwa hiyo, wametuingizia hasara Serikali. Nikuombe Mheshimiwa Waziri na kuna taarifa kwamba ulifika pale na ukatoa maagizo. Na sisi tukuombe ifike mahali sasa hawa watu wanaopewa tender, tender hizi lazima ziangalie kwanza viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka wakati nachangia kwenye viwanda nilitoa ushauri kwamba kabla hatujaenda kwenye kutangaza tenda ya kuingiza viwanda vyetu kwenye tender ni lazima kwanza ikiwezekana 40% ibaki kwetu, 60% waende wakashindanishwe kwenye tender, hali hii itatusaidia sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia wenzetu wa Symbion wanaagiza transfoma kutoka India. Na nilitoa mfano siku ile wenzetu kule wanatoa ruzuku kwenye viwanda vya ndani 10% kwa kila kiwanda. Uzalishaji unakuwa mwingi kwa hiyo, wanatafuta sehemu ya *dumping*, sasa sisi hatuwezi kuendelea kuwa *dumping place*. Niombe sana na sisi sasa tufike mahali tuone umuhimu wa viwanda vyetu vya ndani, hali hii itatusaidia kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa nchi yenye viwanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Singida Mjini tumejaaliwa kuwa na chanzo cha umeme ambacho ni upepo na mpaka sasa sioni juhudi za Serikali kuhakikisha kwamba rasilimali hiyo ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia tunaweza kuitumia ipasavyo, sioni. Maana tunakoelekea tunaelekea kwenda ku-*misuse* rasilimali ambayo Mwenyezi Mungu ametupatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niuone mpango wa Serikali wa kuhakikisha rasilimali ile iliyojitokeza kwenye eneo letu la Singida Mjini ya umeme wa upepo, Serikali inakuja na mpango wa kuwekeza ama kutafuta wawekezaji. Na kwa bahati nzuri tayari walishajitokeza wawekezaji, kwa bahati mbaya sijajua wameishia wapi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako *Wind East African Company* walijitokeza, lakini kama haitoshi wako *Power Pull* nao walijitokeza. Sasa niombe Serikali, kama wawekezaji walijitokeza na wameonesha nia, kama kuna mahali tunaweza kuwa-*support* basi tuwa-*support* waje wawekeze umeme pale Singida. Tunajua umuhimu wa umeme kwenye maeneo yetu, sisi tumejaaliwa hilo na maeneo yetu tuna uzalishaji mkubwa sana. Tunauhitaji umeme huu kwa kasi kubwa, utatusaidia kuinua uchumi wetu hasa kwa maeneo yale ya Kisasida

ambayo tayari pale tuna uzalishaji na ndio tuna kilimo cha umwagiliaji cha mboga mboga.

Mheshimiwa Waziri nikuombe sana ifike mahali, sisi ndugu zetu wa Singida Mjini pale tunakutakia kila la heri, tunakuomba ufike ili uweze kutuwezesha na sisi kuweza kuupata huu umeme na uchumi wetu uweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya na mimi nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kweli kumteua baba huyu ametusaidia sana sisi. Ameionyesha dhamira ya dhati ya nchi yenye viwanda kwamba inawezekana kwa sababu tayari tuna uwezo wa kupata umeme kwa kila eneo. Baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mussa. Tunaendelea na Mheshimiwa Joram Hongoli na baadae Mheshimiwa Boniventura Kiswaga na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu ajiandae.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi hii. Nami nianze kwanza kabisa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumbua wote wabadhirifu na mabaradhuli wote wanaoharibu uchumi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa namna ya pekee niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri wote na Manaibu Waziri kwa kazi kubwa wanazofanya hasa za kuhakikisha kwamba uchumi wan chi hii unakua. Lakini nimpungeze pia Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Profesa Muhongo na Naibu wake Waziri kwa kazi kubwa wanayofanya kwa kuhakikisha kwamba Tanzania inakuwa na umeme wa kutosha na hatimaye tuweze kuwa na viwanda vya kutosha na shughuli nyingine za uchumi ziweze kuboreshwa kupitia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nimpungeze tena Mheshimiwa Waziri, nirudie, kwa kuhakikisha kwamba Jimbo langu la Lupembe pia linapata umeme. Nashukuru katika wiki hii vijiji viwili vimeweza navyo kupata mwanga wa umeme kwa mara ya kwanza kati ya vijiji 45; kwa hiyo, bado vijiji 33 havina umeme kati ya vijiji 45. Niombe Mheshimiwa Waziri na vile vijiji 33 vilivyobakia tuendeleo kuvipigania ili viwe na umeme nao wajisikie wapo nchini Tanzania kama Watanzania wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema kwamba maendeleo ni umeme. Uwepo wa umeme kwa maana ya nishati ya kutosha ya umeme na nishati yenye uhakika, lakini pia yenye bei nafuu ndipo tutaweza kuwa na maendeleo, lakini kama nishati itakuwa bado bei yake ipo juu wananchi wengi hawawezi ku-*afford* kuipata bado hatutaweza kuhakikisha kwamba tunaenda kwenye uchumi ambao tunauhitaji.

Niseme kwanza nipongeze kwa kupunguza bei, na umeme toka 1.5% mpaka 2.4%, lakini pia nipongeze kwa kutoa tozo la maombi ya uunganishaji wa umeme ambayo ni *application fee* shilingi 5,000; lakini pia nipongeze kwa kutoa *service charge*, hii ilikuwa inawakwaza wananchi wengi sana. Na nipongeze kwa niaba ya wananchi wangu wa Lupembe kwa kupunguza hii kodi maana wananchi kipato cha chini, wataweza kuingiza umeme kwa kutumia tu angalau shilingi 5,000 wanaweza wakapata umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia kuhusu mradi wa REA. Katika eneo langu na katika Jimbo langu mradi wa REA Phase I hatukupata, lakini tukapata mradi wa REA Phase II, lakini kwa bahati mbaya hatukuweza kupata umeme hata kijiji kimoja katika REA II. Basi tunaomba vijiji vyote hivi viingizwe kwenye REA III kwa maana ya vijiji vyote 33, tunaomba mtusaidie kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari kuna Shirika ambalo linafanya kazi kule kwa ushirikiano wa Serikali, Shirika la CEFA ambalo limeingiza vijiji viwili, sasa tatizo bado ni kadri ya mkataba ile asilimia ambayo Serikali ilitakiwa ichangie naomba tujitahidi tuweze kuwapatia lile Shirika ili liweze kuendelea na kuhakikisha kwamba linasambaza umeme kwenye vijiji vingine ambavyo tayari nguzo zimechomekwa lakini bado nyaya hazijafungwa na hawajazambaza umeme, kwa hiyo niombe hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niombe kupitia ile mradi ambao wa kwanza ulikuwa TANESCO, ile Gridi ya Taifa iliyowenda mpaka vijiji vile vya Lupembe na Igombora, basi kuna baadhi ya vijiji vilirukwa haukushushwa umeme, umeme umekatiza tu umepita katikati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mara nyingi wananchi wamekuwa wakilalamika kwamba umeme umepita kwenye vijiji vyao, lakini vijiji hivyo havina umeme au vitongoji mbalimbali ambavyo umeme umepita juu haujashushwa. Tuombe tunapopeleka umeme kwenye maeneo hayo au kwenye maeneo mengine tuhakikishe kwamba yale maeneo ambako umeme unapita basi wananufaika na nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe pia bei ya umeme ilivyo sasa hivi pamoja na kwamba tumepunguza kutoka kwenye asilimia 1.5 mpaka 2.4 bado bei hizi ziko juu. Kuna baadhi ya wananchi wengi wanashindwa kulipia gharama hizi, tuangalie uwezekano wa kupunguza gharama za umeme angalau zishuke kabisa kutoka kwenye ile asilimia ziende chini kidogo ili wananchi wengi wa kipato cha chini waweze kununua na kutumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyo sasa hivi, tunasema mazingira yanaharibika kwa kutafuta mkaa, wananchi wanatumia mkaa walio wengi lakini pia

wanatumia kuni katika kupata nishati. Tukishusha bei ya umeme ukawa wa gharama ndogo au ukawa gharama ambayo wananchi wa kipato cha chini wanaweza wakaununua basi yale madhara ya misitu kwa maana ya kutafuta nishati ya mkaa na kupata kuni yatapungua. Wengi wao watahamia kwenye umeme kwa kuwa umeme utakuwa una bei ndogo, utakuwa wa bei rahisi na wataweza kununua umeme na kwa upande mwingine tutakauwa tunapunguza madhara ya kupotea kwa misitu, tutakuwa tunapunguza uharibifu wa mazingira kupitia kutumia hizi nishati za mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba tujitahidi tuweze kuhakikisha kwamba umeme unapungua uwe na bei ndogo ili tuweze kuokoa mazingira yetu na misitu yetu ambayo kila siku tani za miti zinakatwa kwa ajili ya kupata nishati hii ya kupikia kwa maana ya mkaa na kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme kwamba huduma ya umeme hii lazima tufikirie kuisambaza hasa kwenye maeneo yenye taasisi kama vile shule, maeneo ya Hospitali, na maeneo ya huduma muhimu za binadamu. Kwa hiyo lazima tufikire hilo pia tunasema kwamba tunataka shule zetu ziwe na *E-schools*, tuwe na *E-learning* ni lazima tuweze kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme ili mipango ya kuwa na *E-learning*, *E-schools* kwenye shule zetu uweze kukamilika. Kwa hiyo, tunaomba tupeleke pia kwenye huduma hizi za kielimu na huduma nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia naona kuna Waheshimiwa Wabunge wengi wamelalamika sana juu ya kuweka vinasaba kwenye nishati ya mafuta. Kwanza lazima tujulize sababu zipi zilizosababisha Serikali iweze kuhakikisha kwamba inaweka vinasaba. Ni kutokana na kwamba kulikuwa na uchakachujaji wa mafuta kwa kiasi kikubwa, magari yamekuwa yakiharibika, pampu za magari zikiharibika mara kwa mara na baada ya sisi wananchi kulalamika na Wabunge tukaja tukaa na tukajadili, tukaamua kwamba tupitishie sheria ya vinasaba. Kwa hiyo, vinasaba hivi ni muhimu, naomba Waziri na Baraza zima la Mawaziri viendeleo, kama kuna matatizo madogo madogo basi yafanyiwe uchunguzi tuweze kuyatatua lakini sio kusimamisha hili suala la vinasaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeona faida zake, udhibiti wa uchakachuzi wa mafuta umepungua lakini pia Serikali imekuwa inapoteza mapato mengi sana hasa kwenye mafuta yale yaliyopo *on transit* kama walivyosema wenzangu. Kwa hiyo, kwa kuweka vinasaba tunaweza tukabaini kwamba haya mafuta yamepitiwa na vinasaba, watu wanaokagua vinasaba na haya mafuta hayajapitiwa. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo tutadhibiti upotevu wa kipato cha Serikali na hivyo Serikali itaweza kupata pato lake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia hasara kubwa kama nilivyosema ya haya mafuta kulikuwa na wizi mkubwa sana wa mafuta ambayo yanakuwa

kwenye *on transit*, kulikuwa na wizi mkubwa sana wa mafuta yaliyopo kwenye migodi. Kwa hiyo, kwa kufanya hivyo maana yake tutapunguza madhara ya wizi wa mafuta ambao ulikuwa unapelekea hasara kubwa hasa wenye migodi wenyewe, lakini kwa upande mwingine ulikuwa unapelekea hasara Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja, ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Hongoli, tunakwenda na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, yeye amesema atachukua dakika tano na atamgawia dakika tano Mheshimiwa Ngeleja. Kwa hiyo, tunaanza na Mheshimiwa Boniventura.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza nianze tu kuipongeza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati kadri ambavyo imejielekeza namna ya kutatua matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Profesa Muhongo anaondolewa kwenye Wizara hii wananchi wa Tanzania walisikitika sana na wakati amerudishwa wananchi wa Tanzania wameshukuru sana, kwa hiyo, endelea kuchapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba katika Wizara, Wizara hii ni ngumu sana, dunia yote hutafuta madini, hutafuta kupata utajiri kupitia madini, hii ni Wizara ngumu sana. Kwa hiyo lazima tukupongeze wewe pamoja na Naibu wako kwa kadri ambavyo mnachapa kazi Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina vijiji ambavyo vimepitiwa na REA Phase II, lakini vijiji hivyo ni Ng'haya, Bundlya, Kabila, Kigangama na Kisamba zimewekewa nguzo chache sana na sehemu zingine hata shule za msingi, makanisa na zahanati hazijapata umeme. Shahidi ni Naibu Waziri wa Nishati, tulitembelea maeneo hayo. Naomba mtakapokuja kujibu msem pia kwamba mnaongeza vijiji hivyo ili vikamilike vionekane kwamba kweli REA Phase II, imevitendea haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyo vijiji viwili pia ambavyo havikuwekewa umeme, umeme huu umekwenda kwenye vijiji vingine, kwa mfano Nyashigwe, iko kwenye REA Phase II, lakini umeme wake umekwenda kitongoji cha Mawe ambacho ni kijiji cha Welamasonga. Kwa hiyo, kijiji hiki hakijawekewa umeme, mtakapokuja kutoa majibu mniambie je, mtakiingiza kwenye Phase III, aumtakipelekea umeme sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipo kijiji kingine cha Kitongo Ndagalu ambapo makao makuu ya kijiji ambayo ni center kubwa haijawekewa umeme, umeme



umewekwa kitongoji cha Misungwi, napo mje mniambie ili wananchi hawa waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ha utaingia sasa hivi *REA Phase II*, basi uingizwe *REA Phase III*. Lakini umeme ambako wamekamilisha kama Kabila, Ng'haya haujawaka, naomba Wizara kwa maana ya Waziri muhimize ili kama umekamilika umeme huu uweze kuwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vya Magu havina umeme asilimia 70, ninaomba sasa kupitia *REA Phase III*, vijiji hivi viwekewe umeme, nimeongea na wewe Mheshimiwa Waziri, nimeongea na Naibu Waziri, nimeongea na Meneja wa Kanda, naomba sasa vijiji hivi kwa kweli viweze kupatiwa umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni *declare interest* nilikua mchimbaji mdogo mwaka 1993 katika machimbo ya Ulyankulu na huko ndiko nimeanzia maisha. Wachimbaji hawa wanateseka sana kila siku, wanahama kila leo, lakini wachimbaji hawa ni ajira yao. Tunapozungumzia *Tanzanite*, wachimbaji wale sio wa Arusha tu, wa Magu wapo, wa Bariadi wapo, wa Sengerema wapo. Tunapozungumzia almasi, wachimbaji wa nchi nzima wako kule na wa Magu wapo, tunapozungumzia dhahabu, wachimbaji wa Magu wapo. Kama walivyolalamika Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ninaomba hawa wachimbaji wadogo wadogo kama azma ya Serikali ni kuwatafutia maeneo iwatafutie maeneo ili waweze kupatiwa maeneo ya uchimbaji, hiyo ndio ajira yao ya kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako malalamiko kwamba mikataba ya madini tunapata fedha kidogo sana kama nchi. Ninaomba sasa haya nayo ni maeneo ambayo yanalalamikiwa na kila mmoja wetu ili yaweze kupitiwa na kuangaliwa ili Serikalil iweze kupata mapata ambayo kwa kweli yatanufaisha Taifa letu la Tanzania. Maana tunaweza kuwa na madini baadaye tukaachiwa mashimo na nchi isinufaike. Naishauri Serikali iangalie kwa uhakika ili kuhakikisha kwamba mikataba hii inawanufaisha watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ambayo yamewekewa umeme wa *REA* wananchi wanashukuru sana, sasa niguse tu kwamba tutakapokamilisha maeneo ya vijiji, viko vitongoji ambavyo navyo ni kama vijiji, kwa hiyo, tusiishie *REA Phase III*, lazima tuende na *REA Phase IV*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishie hapo na niunge mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante tunaendelea na Mheshimiwa Ngeleja dakika tano.



**MHE. WILIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nimshukuru sana na jirani yangu Mheshimiwa Kiswaga kwa ukarimu wake kwa kunipa dakika tano hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naungana na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo pamoja na Naibu wake Dkt. Kalemari kwa kazi kubwa wanayoifanya. Lakini nianze kwa kupeleka salamu maalum za shukrani kuungana na watanzania wengine kwa Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna alivyosimamia uamuzi wa kushirikiana na Uganda kujenga lile bomba la mafuta kutoka Uganda kuja kupitia Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba ujenzi wa bomba lile ulikuwa na ushindani mkubwa, ni hitajio la kila nchi inayopatikana ndani ya mipaka ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lakini Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uamuzi wae ule, pia umebadilisha siasa za nchi za Afrika Mashariki, kwa hivi tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo tunakupongeza sana kwa namna ambavyo ulisimamia utekelezaji ule ukiongoza kikosi cha wataalam hongera sana pamoja na timu nzima ya Serikali. Dkt. Kalemari miezi miwili iliyopita ulikuwa Sengerema, tunakupongeza sana kwa ziara iliyoifanya, mafanikio yake tumeshayaona, lakini kuna moja nilitaka nikukumbushe Mheshimiwa Kalemari, tulivyokuwa pale katika ule Mgodi wa Nyanzaga ulisema uliwapa siku 14 wale wachimbaji wenye leseni ile ambayo wamepewa ambayo ni ya Acacia, ulisema utawaandikia barua uwape *notice* ya siku 14, waeleze kama wana nia ya kuendeleza ule mgodi ama laa, na kama hawatakuwa na nia Serikali ichukue uamuzi mwingine kwa kutoa leseni ile kwa watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatarajia kwamba Mheshimiwa Waziri, utakapokuwa unafanya hitimisho/majumuisho yako ya jioni ya leo basi utatoa hatima na mwelekeo wa Mgodi wa Nyanzaga ambao unapatikana katika Jimbo la Sengerema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 30 wa hotuba ya Mheshimiwa Profesa Muhongo ambayo kwa kweli imebeba mambo mazito na mazuri, mojawapo ya mambo yanayozungumziwa pale ni kufikisha umeme katika baadhi ya maeneo ambayo hayafikiki kirahisi, hayafikiwi na umeme wa Gridi ya Taifa. Na mazingira ya maeneo hayo yanayozungumziwa ni pamoja na visiwa, Jimbo la Sengerema ambavyo msemaji ndio anaiwakilisha ina maeneo ambayo hayafikiki kirahisi, nina visiwa kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alivyokuwa anachangia jana Mheshimiwa Dkt. Tizeba alisema hapa, lakini mimi nataka niungane naye kwamba katika yale aliyozungumza ni pamoja na visiwa vya Juma Kisiwani, Chitandele, tuna kisiwa cha Chikomelo kule pamoja na Lyakanyasi. Nilikuwa naomba mtakapokuwa mnatafakari kuyafikia maeneo ambayo hayafikiki kirahisi msije mkasahau visiwa vinavyopatikana katika Jimbo la Sengerema na Wilaya ya Sengerema kwa ujumla ikiwemo Jimbo la Buchosa kwa ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba na maeneo mengine ambayo tunakumbwa na hilo jambo ambalo tuko katika maeneo ambayo hayafikiki kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri inatukumbusha kwamba malengo ya Serikali kufikia mwaka 2020 katika eneo la uzalishaji umeme tunakusudia tuwe tumefikia uzalishaji wa umeme kiasi cha megawati 4,915 kutoka kwenye 1,500 tulipo sasa. Nilichotaka kusema nimuombe Mheshimiwa Waziri atusaidie kufafanua, kuna miradi mingi imetajwa hapa, lakini kwa mahitaji haya na mkakati wa Serikali sasa hivi wa nchi ya Tanzania kuwa nchi ya Viwanda, tunaamini demand itaongezeka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka atusaidie katika mipango tuliyonayo, je, ni pamoja na uendelezaji wa miradi ya *Hydro*, inayotokana na nguvu ya maji ama vinginevyo kwa sababu tuna *potentials* kama *Stiegler's Gorge* lakini tuna Mpanga, Ruhuji, Mnyera, Rukose, tuna kule Kilombero, tuna maeneo mengi ambayo yanaweza kuzalisha umeme kwa kutumia nguvu ya maji. Tunataka kujua tu kama katika mpango wetu wa kulitoa Taifa hili, kufika hapo mbele tunakusudia kujumlisha hii miradi mikubwa ambayo inaweza kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji/

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, kwa sababu ni dakika tano tu, tarehe 21 Aprili, Shirikisho la Wachimbaji na Watafutaji wa Madini walitoa taarifa wakifafanua ushiriki na uwezesho na namna ambavyo wao wamechangia katika uendelezaji wa uchumi wa Tanzania. Katika baadhi ya mambo waliyoyazungumzia walitoa hisia zao na taarifa zilitoka kwenye vyombo vya habari vingi tu kwamba mpaka sasa hivi wameshachangia kiasi kikubwa. Lakini hoja ninayoizungumzia hapa ni kwamba tunaiomba Serikali itoe ufafanuzi itakapokuwa inafanya majumuisho, kwa sababu mchango wa kwenye Pato la Taifa wa sekta ya madini sasa hivi ni asilimia tatu pointi kadhaa. Lakini sisi tuna dira ya Taifa hapa inasema katika sekta ya madini tunakusudia mchangowa Taifa uwe umeshafikia asilimia 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema kwa sababu maandalizi ni sasa, miaka tisa, kumi iliyobaki sio mingi sana, pengine katika hatua hii Mheshimiwa Waziri, pamoja na Serikali nzima inaweza kukusaidia kutoa mwelekeo kwamba mikakati iliyopo kutoka kwenye asilimia tatu na ukizingatia changamoto zinazopatikana katika sekta ya madini duniani sasa hivi, ni

mikakati ipi tuliyonayo ya kutoka hapa kusogea mbele kufikia hiyo asilimia 10 ifikapo mwaka 2025?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naungana na Watanzania wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa tunayoifanya katika kuendeleza sekta. Lakini pia nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na Madini, wameanza vizuri sana wamefanya kazi kubwa sana, tunakushukuru sana na tunawatakiya kila la heri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ngeleja, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Dalaly P. Kafumu na baadae Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

**MHE.DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mungu kwa kupata nafasi hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu, na nakushukuru na wewe Mwenyekiti kwa kunipa nafasi. Lakini kama wenzangu walivyosema tuwapongeze Waziri na Naibu Waziri, pamoja na wataalam kwa kazi nzuri wanayofanya katika mazingira haya magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wana changamoto nyingi sana, mimi nilikuwa mmoja wao wakati fulani, kwa hiyo najua changamoto walizonazo, wanahitaji kuhudumia wananchi, lakini pia wanahitaji kuhakikisha wawekezaji wanaendelea kuja katika nchi yetu. Mnatakiwa kukaa katikati, ukihamia upande mmoja unaweza kuharibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nitasema maneno machache ya kutoa ushauri tu kwamba ukiangalia ukurasa wa 62 wa hotubua ya Mheshimiwa Waziri, kipengele 136, naomba nisome, kinasema; "Pamoja na bei ya madini ya dhahabu na nikeli kushuka katika soko la dunia, Serikali imeendelea kuhamasisha uendelezaji wa miradi mikubwa ya madini," mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Waziri kwa kusema haya maneno, lakini ningependa sasa haya maneno ya-reflect katika vitendo vya Serikali katika kuhamasisha uwekezaji mkubwa. Sasa hivi ukipita mitaani huko ukisikiliza wawekezaji na wachimbaji wadogo kuna kilio kwamba Serikali imegeuka kidogo. Zile juhudi tulizofanya kuanzia mwaka 1995 Awamu ya Tatu na ya Nne zinakwenda tofauti kidogo, kwa hiyo mimi ningependa niwashauri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, hebu ongezeni juhudi za kuhamasisha wawekezaji waje tusipohamasisha hatutakuwa na migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi utafutaji na ninyi ni mashahidi umepunga kweli na utafutaji unapopungua maana yake ni kwamba hatutakuwa na migodi siku za usoni, hii migodi ikifungwa basi. Napenda niseme kwamba Kamati ya Bomani ilitushauri tukatengeneza sera nzuri, tukatengeneza

na sheria nzuri, tumekosea wapi sasa mpaka tuanze kurudi nyuma? Ukiwasikiliza wawekezaji wengine wanasema Tanzania ninyi mnataka kurudi kwenye ujamaa, ukisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nashauri Mheshimwia Waziri, hebu tutoke hapo tulipo, tutengeneze mikakati sasa ya kuhamasisha. Kwa mfano tulikuwa tunaenda sana kwenye mikutano hii ambayo wawekezaji wote duniani wanakusanyika, tunawaalika. Miaka miwili iliyopita hatujaenda na wale wawekezaji wanaona Tanzania haimo tena kwenye kazi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaombeni sana tujitahidi tuwahamashe wawekezaji, wasikate tamaa, ninyi ni mashahidi leseni nyingi sasa hivi zimekaa *idle* kwa kweli, japokuwa tumetengeneza mfumo mzuri lakini hazifanyi kazi kwa sababu tumekosea wapi, wataalam wa nishati na madini toeni ushauri jamani kitu gani kimetokea? Mimi inaniuma sanamnapoona juhudi zile za Serikali ya Awamu ya Tatu na ya Nne zinakwenda nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia majirani zetu Mozambique hata Malawi walitangaza *geophysical results* zao mwaka jana, sasa hivi wawekezaji wanaenda kule kutafuta dhahabu hii hii ambayo imeteremka bei. Kwa hiyo, mimi naomba sana na sisi tutazame tena wapi tumejikwaa, tuamke, ni ushauri tu ambao kwa kweli utatusaidia kwenda mbele upande wa madini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napenda niseme juu ya ushiriki wa watanzania, tunaishukuru Serikali kwa kuwasaidia wachimbaji wadogo kuwapa hii mitaji. Lakini hebu wasaidieni pia na katika kutafuta madini. *Geological Survey of Tanzania* moja ya kazi yake kwa sera ile tuliyotengeneza ni kuyaangalia hayo maeneo ya wachimbaji wadogo na kuyapa *value* kidogo ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Lakini pia ni kuwasaidia katika *environmental impact assessment* ili waweze kuwa na tija katika uwekezaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulisema ni ushauri ambao hua natoa kila mwaka na sasa hivi natoa, mnaweza msinieleme sasa lakini baadaye mtanielewa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA), ni wakala unaofanya kazi nzuri kama walivyosema, lakini unalipa Taifa hili gharama kubwa kwa sababu unafanya kazi zinazofanywa na taasisi zingine. Ngoja nitoe mfano, wanaangalia kampuni itaweza kulipa kodi, kazi ambayo inafanywa na TRA mnaweza mkasema ni *audit*, lakini kazi ni ile ile ukimuuliza mwekezaji anayekaguliwa na TMAA, mwekezaji anayekaguliwa na TRA anayekaguliwa na yule mkaguzi wa kisheria kazi wanazofanya ni zile zile. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunafumia hela nyingi kufanya jambo moja, ukiangalia wanafanya kazi ya ukaguzi wa mazingira, NEMC anakwenda kufanya jambo lile lile. Wanafanya kazi ya kuangalia madini yanavyopelekwa nje, wametengeneza ma-desk pale kwenye viwanja vya ndege, kazi hii ilitakiwa kufanywa na Ofisi ya Kamishna wa Madini kwa Sheria ya Madini ya mwaka 2010. Mimi nasema *skills* na taaluma tuliyoijenga pale, hebu tuiweke mahali inapostahili, mimi ningependekeza na nimewahi kupendekeza kwamba hii kazi ifanywe na mtu mmoja sio watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunaweza tukaifanya TMAA ikawa Idara ya TRA yenye Kamishna wake wa ukaguzi wa migodi na hizo *skills* zote tukamuachia TRA, itasaidia sana badala ya kufanya kazi mara mbili. Taarifa ninayoipata lazima iende TRA na kama amekosea mtu, TRA ndio anaechukua hatua, TRA akiacha inakuwaje? Kwa hiyo TMAA imewekwa hapo kufanya kazi za watu wengine ili watu wengine wachukue hizo *information*. Tunatumia fedha nyingi sana, kufanya jambo lile lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri tena, sasa hivi naweza nisieleweke nasema lakini siku za usoni nadhani nitaeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kama nitapata muda, nataka nizungumzie mikataba ya madini. Mikataba ya madini watu wengi wanaisema tofauti, Sheria ya Madini...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Kafumu muda wako umeisha.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Ahsante sana.

**MWENYEKIT:** Tunaendelea na Mheshimiwa Lolesia J. Bukwimba na baadae Mheshimiwa Zitto Kabwe na Mheshimiwa Vedasto Ngombale pamoja na Mheshimiwa Othman Omar wajiandae.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana kwa kunipa nafasi, ili na mimi niweze kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini. Nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Busanda kwa kuniadini na kuendelea kunipa ridhaa na niwahakikishie kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa uaminifu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara kwa ujumla kwa kazi kubwa wanayoifanya. Kikubwa zaidi nimepitia kitabu cha bajeti ambacho kimejieleza vizuri sana katika ila hatua, kwa hiyo, napenda

kuipongeza sana Wizara kwamba wameweka mipango mizuri, cha msingi ninachoomba ni utekelezaji wa mipango hii ambayo wameiweka katika kitabu cha bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa umeme nimeona jinsi ambavyo ndani ya bajeti mmelezea vizuri sana katika aya zote 45 mpaka 49 nimesoma, nimeona jinsi ambavyo Wizara imejipanga kupeleka umeme kabambe katika maeneo ya vijijini. Kupeleka umeme kwa kuhakikisha kwamba wanaangalia taasisi muhimu katika maeneo hasa ya vijijini, kwa hiyo, hilo nalipongeza sana naipongeza Wizara, niombe tu muhakikishe basi muweze kutekeleza kulingana na mipango yenu mliyoiweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha pili, katika bajeti hii nimeona pia kuna ongezeko kubwa sana la fedha za bajeti za umeme vijijini kutoka shilingi bilioni 357 mpaka shilingi bilioni 534, ongezeko la asilimia 50. Kwa hiyo, ninaona jinsi ambavyo Wizara kusema ukweli imejipanga kufanya kazi kubwa na nina uhakika kwamba kupitia bajeti hii ya mwaka 2016/2017 wananchi wengi wataweza kunufaika zaidi.

Niombe sasa kulingana na mipango ambayo tumeipeleka, kwa sababu mimi nimeenda katika Mkoa wangu kupitia Ofisi ya TANESCO tumeweza kubaini vijiji ambavyo havijafikiwa na umeme. Niombe sasa Serikali iweze kutekeleza kulingana na jinsi ambavyo wamepanga ili tuweze kuona wananchi wanaweza kunufaika zaidi na upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika jambo la sekta ya madini ni kwamba katika upande wa madini, nimeona pia jinsi ambavyo Serikali imejipanga katika kuhakikisha kwamba inasaidia wachimbaji wadogo wa madini. Imesema kwamba mtapeleka mitaji kwa ajili ya kuwawezesha **wachimbaji wadogo, niombe Serikali iweze kulifanyia kazi hili, ni kilio cha kila siku. Kwa hiyo ninaomba Serikali iweze kuendelea kuwekeza, imetenga kweli shilingi bilioni 6.6 ni fedha nyingi, niombe Serikali ihakikishe inalifanyia kazi suala hili kusaidia wachimbaji wadogo.**

**Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko sehemu ambapo wachimbaji wadogo wako wengi sana na mara nyingi hili bado ni lalamiko kubwa kwa wachimbaji wanyonge wadogo wadogo. Kwa hiyo, niombe Serikali pia inapotekeleza majukumu yake, itushirikishe na sisi Wabunge ili tuone kwa sababu malalamiko Wabunge ndio tunaoletea kila siku kwamba mbona sisi hatujapata mitaji, lakini kwenye utekelezaji tunaona jinsi ambavyo Serikali inafanya kazi kubwa.**

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kule kwa wananchi hatuoni hayo mambo, kwa hiyo niombe Serikali safari hii hizo shilingi bilioni sita ilizotenga, ikumbuke pia



na wachimbaji wadogo wadogo wa Mkoa wa Geita hasa kule busanda ambako nina wachimbaji wadogo wengi ambao wanajikimu kwa kupitia shughuli za uchimbaji wa madini.

Vilevile katika suala la madini nichukue nafasi hii kwa kweli kuishukuru Serikali, kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wamefika Geita mara kadhaa. Kulikuwa na changamoto kubwa sana pale Nyarugusu STAMICO kwa mara ya kwanza katika bajeti ya mwaka huu, nimeona Serikali imezungumzia namna ambavyo inakwenda kutatua mgogoro huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na imesema kwamba katika mwaka 2016/2017 Serikali inaenda kumaliza hasa huu mgogoro na wananchi wataweza kupewa eneo la STAMICO. Jambo hili naipongeza Serikali na niombe utekelezaji sasa uweze kufanyika katika mwaka huu wa 2016/2017 na wananchi wana furaha kubwa sana kutokana na jambo hili kwa sababu imekuwa ni kilio cha muda mrefu. Miaka mitano iliyopita kila bajeti nilikuwa nikizungumzia suala hili. Kwa hiyo, mwaka huu mkitekeleza jambo hili, mimi nina uhakika wananchi wote wa eneo hilo la Busanda wataweza kunufaika, na sio tu wa Busanda kwa sababu masuala ya uchimbaji wanakuja watu kutoka sehemu mbalimbali na wanakuwa katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe Serikali katika hiyo aya ya 139 imezungumzia habari ya kuwapatia eneo la STAMICO watu wa Nyarugusu, ninaipongeza na naomba Serikali iweze kulifanyia utekelezaji suala hili ili wananchi waweze kufanya kazi zao sasa, waweze kufanya kazi na kunufaika zaidi katika kuwekeza katika shughuli za uchimbaji wa madini katika eneo hilo. Lakini vile vile Serikali iliahidi kwamba ingeweza kujenga kituo kikubwa sana cha wachimbaji wadogo eneo la Lwamugasa, jambo hili limekuwa ni la siku nyingi lakini katika bajeti nimeangalia Serikali inajenga vituo saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika maelezo nimeangalia Mkoa wangu haupo, niombe Serikali sasa iniambie wakati wa majumuisho, kwamba kituo cha Lwamugasa kimemezwa na nini hakipo tena na wala hakisikiki. Niombe muweze kuangalia bajeti zenu za nyuma na muhakikishe wananchi wa maeneo haya waweze kujengewa hicho kituo cha kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo. Hasa katika maeneo hayo ili waweze kunufaika na ruzuku, kwa ajili ya kununua zana mbalimbali za kufanyia kazi katika shughuli zao za uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba suala hilo liweze kufanyiwa kazi kwa kiwango kikubwa kwa sababu ni ahadi ya Serikali ya muda mrefu na ninyi wenyewe mliahidi, hatukuwa tumeomba lakini ninyi wenyewe mliweka kwenye utaratibu. Lakini vilevile kuna kituo mlianzisha pale Lwamugasa tulifanya uzinduzi



wa Benki ya Dunia kwamba ingeweza kusaidia wachimbaji wadogo, tumezindua tu lakini sasa hakuna kunachoendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali pia inipe majibu kwamba inasemaje kwa habari ya hicho kituo cha Lwamugasa, ambacho Benki ya Dunia ilikuwa imekubali kuweza kutoa fedha kwa ajili ya kusaidia wananchi wachimbaji wadogo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niombe Serikali iweze kuyazingatia hasa eneo la STAMICO Nyarugusu ambalo limekuwa ni kilio cha muda mrefu. Waheshimiwa Marais waliopita wamlizungumzia na kuahidi sana na Mheshimiwa Rais Magufuli alivyokuwa anafanya kampeini zake alisema suala hili limekwisha. Kwa hiyo naomba suala hili liishe lifike mwisho, ili wananchi waweze kufanya kazi zao sasa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilikuwa naomba kuzungumzia suala la afya katika sehemu za migodi. Ni kwamba nilikwenda workshop moja wiki iliyopita ya SADC, kuna suala la afya ambalo ni la msingi sana nilikuwa naomba Wizara iweze kulifanyia utafiti, inaonesha kwamba watu wanaoishi katika maeneo ya shuguli za uchimbaji wa dhahabu kuna vumbi la madini ya *silica* ambalo mara nyingi linasababisha ugonjwa unaitwa *silicosis* lakini vilevile inasababisha TB.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niliogopa sana na kushtuka, kwa hiyo, niombe Serikali iweze kufanya kazi ili wananchi wetu wasije wakaathirika na jambo hili. Kwa hiyo kupitia Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Afya mjaribu kufanya utafiti wa kutosha ili kuweza kubaini kama kweli hiyo *silica* ina-*affect* vipi wananchi wetu katika maeneo ambayo yako karibu na uchimbaji wa dhahabu. Ninaomba suala hili Serikali ilifanyie kazi kwa karibu ili tusije tukajikuta wananchi wetu wanathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na uwepo wa *silica*, ambao pengine wanakuwa wanaathirika na TB bila kujua na hatimaye baadae tukakosa nguvu ya Taifa, kwa sababu watu wataweza kuangamia kutokana na ugonjwa huo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkifanya hiyo tathimini na kuweza kuitolea ufafanuzi pengine itatuwezesha sisi pamoja na wananchi kwa ujumla kuweza kujua tatizo na kuweza kutafuta namna ya kujikinga ili kuweza kuondokana na kuweza kupata madhara hasa ya ugonjwa wa TB na magonjwa mengine ambayo yataweza kupunguza nguvu kazi ya Taifa kwa sababu wakiugua hawawezi kufanya kazi zote na pengine uchumi wa Taifa utaweza kutumika pia kwa ajili ya kupeleka fedha katika matibabu ya TB na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Serikali ilifanyie kazi hilo kwa sababu katika machimbo ya sehemu za Afrika Kusini inaonesha jambo hili

limeweza ku-affect watu wengi na sasa hivi ni kilio kikubwa na linazungumziwa sana katika nchi za Afrika ya Kusini. Sisi nchi ya Tanzania kama ni mojawapo ni vizuri Serikali iweze kuangalia suala hili kwa umakini, kikubwa zaidi kuweza ku-protect watu wetu ambao wataweza kuathirika na jambo hili kiafya.

Lakini vilevile na wale wanaofanya kazi migodini, mimi najua hawa wanaofanya kazi migodini wengi mwisho wa siku baada ya muda wanaathirika. Kwa hiyo Serikali ifanyie utafiti kwa watu wanaofanya migodini, ili wasije wakafika mahali sasa hata maisha yao yakaathirika na wakashindwa kufanya kazi zingine baadae baada ya kufanya kazi kwa muda fulani mgodini, baadae wanaathirika kiafya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema mambo hayo, niombe tu Serikali iendelee kuwekeza zaidi na napenda kushukuru naunga mkono hoja, nikiamini kwamba Serikali inaenda kufanyia kazi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunaendelea na Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika uendeshaji wa uchumi wetu kwa sekta zote ambazo ziko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo napenda niweze kupata mikakati ya Serikali, ni suala la mahusiano kati ya madini tunayozalisha, thamani tunayopata ya uzalishaji ya hayo madini na mapato ya Serikali kutoka kwenye makampuni husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangaliwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukitazama ukurasa wa 86 na 87 ametoa takwimu za sekta ya madini. Utaona mwaka 2015 dhahabu peke yake ilituingizia dola za Kimarekani bilioni 1.6 takribani trilioni 3.5 kwa maana ya thamani ya mauzo ya dhahabu nje. Lakini ukienda kuangalia mrabaha na mapato ya kodi kwa maana ya kodi zote ambazo zinakusanywa; kwa maana ya *corporate tax*, *value added tax*, *pay as you earn*, *skills development levy* na *withholding tax*, utakuta kwenye kodi tumekusanya shilingi bilioni 351 na kwenye mrabaha tumekusanya dola za Kimarekani 63.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua mapato haya, yaani *revenue* hii ya Serikali na fedha za kigeni ambazo makampuni ya madini yanapata kuuza dhahabu tu peke yake ni asilimia 15 tu ya dhahabu inayouzwa nje. Kwa hiyo, hii ni changamoto kubwa, najua tumetoka mbali tulikuwa tunapata chini ya hapo, tunahitaji kuongeza nguvu zaidi ili tuweze kufikia hatua kubwa zaidi ya mapato ambayo tunayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ambalo tunalo sasa hivi, ni tatizo la makampuni makubwa ya madini kutumia njia za kahasibu kuhamisha faida kutoka nchini kwetu kupeleka kule ambako wamesajiliwa, inaitwa *base erosion and profit shifting*. Hili ni jambo ambalo ni lazima tulishughulikie vizuri, na tukiweza kulishughulikia hatutakuwa na haya matatizo ambayo tunayo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kuweza kupata maelezo ya Serikali, leo hapa tunapozungumza ndani ya siku tano zijazo, hakuna ndege ambayo inaweza ikatua nchini kwetu kwa sababu hatuna mafuta ya ndege (*Jet A one*) na hii inatokana na zabuni ambayo ilitolewa kutoka kwa kampuni moja ya kigeni, kampuni ile ikaleta mafuta, mafuta yale yote yameonekana yako *contaminated* hayawezi kuingia kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa Serikali haijachukua hatua yoyote ile, mafuta ambayo yalikuwa yaende *Puma Energy* peke yake, yana thamani ya dola za Kimarekani milioni 13 mpaka hapa tunapozungumza, hifadhi yetu ya mafuta ya ndege imebakia ya siku tano tu, baada ya siku tano kama hakuna hatua ambayo Serikali imechukua, nchi yetu hakuna ndege ambayo itakayotua kwa sababu hawawezi kutumia mafuta ambayo yako nchini hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa naomba nipate maelezo ya Serikali, ni hatua gani ambayo wanachukua haraka kuweza kuhakikisha kwanza tunashughulikia jambo hili, tuweze kupata mafuta ya ndege ili ndege ziweze kutua. Tusipate aibu duniani, tusikose watalii ambao wanakuja nchini, lakini pili ni hatua gani ambazo zitachukuliwa dhidi ya watu ambao walitoa zabuni kwenye mafuta ambayo yameonekana hayafai kutumika katika nchi yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba nipate maelezo hayo ya Serikali, na nina barua za *Bulk Procurement Petroleum Agency*, ambazo zinahusiana na jambo hili, kama Waziri akizihitaji kwa ajili ya ufuatiliaji naweza nikampatia ili aweze kulifuatilia jambo hili, na kuweza kuleta suluhisho.

Jambo la tatu ni suala la uzalishaji wa umeme. Nimeona miradi ambayo imeorodheshwa, ni miradi mingi na miradi ambayo inapaswa kuungwa mkono. Kwa sababu juhudi zozote zile za kwenda kwenye viwanda, kama haziendani na uzalishaji wa umeme wa kutosha zinakuwa hazina maana yoyote. Ndio maana leo hii sisi kule Kigoma tunahangaika kutafuta wawekezaji, Waziri wa Viwanda anahangaika kutafuta wawekezaji, lakini swali la kwanza ambalo mwekezaji atauliza kuna umeme? Hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana tunapigana sana kuhakikisha kwamba mradi wa Maragalasi unafanikiwa na ninapenda niwapongeze kwa kuhakikisha kwamba mradi wa Maragalasi umeingia kwenye mpango na hili ni kilio cha watu wa Kigoma cha muda mrefu na napenda niwashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Kigoma na kwa niaba ya wabunge wengine wa Kigoma kuhakikisha kwamba mradi huu unakuja jinsi ambavyo unavyotakiwa. Hata hivyo umeme sekta ya uzalishaji (*generation part*) ya umeme is *liberalized*, ni eneo ambalo Sheria ya Umeme ya mwaka 2008 imeruhusu *private sector* kushiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kama tukitumia vizuri hiyo *mix* ya *public* na *private*, tutaweza kuhakikisha ya kwamba tunazalisha umeme wa kutosha. Kwa hiyo, nilikuwa namsihi Mheshimiwa Waziri kwamba mikataba ambayo tayari tumesaini, inaweza kuwa inahitaji *review* ni sawa, kwa sababu ni lazima tufanye *review* kuangalia maslahi ya nchi namna gani ambavo inakuwa. Lakini tusifanye makosa tuliyoyafanya nyuma kujikuta tunapelekwa mahakamani tunalipa gharama kubwa, nyote hapa mnafahamu kwamba ilibidi tuwalipe DOWANS kisiri siri zaidi ya bilioni 200, kwa sababu ya kesi ambayo tulipeleka mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusingie kwenye mtego wa kupelekwa mahakamani tena, Rais alitoa tamko pale siku anaweka jiwe na msingi la Kinyerezi kuhusiana na kuzalisha wenyewe, ni tamko sahihi kabisa, ni tamko la kizalendo kabisa, lakini halina maana ya kwamba tuingie kwenye migogoro na watu ambao tayari tuna mikataba nao, halafu tuanze tena ku-*negotiate* mahakamani, itakuwa ni *distraction* mtapoteza muda na Mheshimiwa Waziri itakuondolea muda wa ku-*concentrate* kuhakikisha ya kwamba tunapata umeme wa kutosha, vijijini na miradi ambayo tunayo hivi sasa. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri kwamba Serikali ijaribu kuangalia jambo hili na kuweza kuhakikisha kwamba tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni suala la TMAA na Dkt. Kafumu amelizungumza. Mimi nadhani tunaweza tukaangalia vizuri, ni namna gani ambavyo tunae-*reform* TMAA ipanuke zaidi, isiwe ni suala la kuangalia migodi peke yake, iangalie pia suala zima la mikataba yetu ya gesi, kwa sababu hatuna chombo ambacho chenyewe kiko *dedicated* kwa ajili ya kuangalia *cost accounting* na makampuni haya yanaingiza gharama nyingi sana kwetu, ili kuweza kupata sehemu kubwa ya mapato baada ya *revenue sharing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuangalie namna gani ambavyo TMAA haitaangalia migodi peke yake, tuipanue iende ikiangalia mpaka kwenye mikataba yetu ya gesi badala ya kuivunja kama jinsi ambavyo Mheshimiwa Dkt. Kafumu anapendekeza. Muhimu ni kufanya *reform* ili kuweza kuifanya kazi yake iwe *more relevant* kuliko kwenda kuiondoa kwa sababu

tunajua kazi kubwa ambayo wameifanya, ukaguzi mkubwa ambao wamefanya na mapato makubwa ya Serikali ambayo yameokolewa kulingana na jambo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa ni suala la mafuta na gesi Zanzibar. Mpaka sasa tunapozungumza bado Katiba inatambua kwamba suala la mafuta na gesi ni suala Muungano. Mpaka sasa tunapozungumza bado TPDC ambayo siyo taasisi ya Muungano inashughulika na mafuta na gesi Zanzibar, kuna haja kubwa, kwa sababu *consensus* tayari ipo, ni vizuri hata kama bado hatujafikia nafasi ya kwenda kwenye *referendum* ya Katiba au kuanza upya mchakato wa Katiba angalau tufanye *amendment* ya kisheria sasa hivi ili suala la mafuta na gesi liweze kutendeka Zanzibar bila kukiuka Katiba, bila kukiuka sheria. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna *consensus*, lakini leo hii kampuni yoyote itakayoingia makubaliano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina madhara ya kupelekwa mahakamani kwa sababu Katiba bado inatambua jambo hili la Muungano na nadhani kwamba halina ubishi. Hakuna mtu ndani ya Bunge hili ambaye atapinga jambo la kuhakikisha kwamba Zanzibar inaweza ika-*manage* mafuta na gesi yenyewe.

Kwa hiyo, naomba na napendekeza kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali tufanye *amendment* hiyo ili tuweze kuondoa tatizo hili la kisheria tuweze kuruhusu ndugu zetu wa Zanzibar waweze ku-*manage resource* hii kwa ajili ya faida yao na kwa ajili ya kuendeleza *blocks* ambazo tayari ziko Zanzibar na tayari zimeshaingizwa kwenye soko tuweze kuhakikisha kwamba na wenyewe hawarudi nyuma katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Zitto, tundaendelea na Mheshimiwa Vedasto Ngombale na Mheshimiwa Othman Omar wamekubaliana dakika tano, tano.

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, lakini nachukua nafasi hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kwa kunichagua kuwa Mwenyekiti wao. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na uzalishaji wa umeme katika kinu cha Somangafungu. Uzalishaji wa umeme katika mtambo huu kwa kweli umekuwa wa kusuasua, umeme unaozalishwa pale unatumika katika Wilaya ya Kilwa na Wilaya ya Rufiji lakini mpaka sasa umeme umekuwa ni wa kukatika katika kila

mara. Tulifanya mazungumzo na Mkurugenzi wa TANESCO alikuja pale akatuambia kwamba tayari vipuli vimepatikana kwa ajili ya kufanya marekebisho ya mitambo pale, lakini mpaka sasa hakuna kinachoendelea alituambia baada ya mwezi mmoja mambo yatatengamaa lakini bado umeme unakatikatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niongelee kuhusiana na suala zima la umeme vijiji. Katika jimbo langu kuna baadhi ya kata na vijiji havijapata umeme kwa mfano kata ya Miteja - kijiji cha Kikotama, kata ya Mingumbi - kijiji cha Nambondo, kijiji cha Chapita, kijiji cha Nampungu, kata ya Namayuni - kijiji cha Nahama, Namakolo, Naliyomanga, kata ya Chumo - kijiji cha Hongwe, Ingirito na Kinywanyu, kata ya Kipatimo - kijiji cha Mtondowa Kimwaga, Nandete, Pondo, Mkarango bado havijapata umeme, kata ya Kibata kata yote kijiji cha Kibata, Hanga, Nakindu, Mwengehi, Namtende vyote havijapata umeme. Kata ya Kandawale - kijiji cha Kandawale, Ngarambi, Namatewa Natipo havijapata umeme. Kata ya Njinjo - kijiji cha Msitu wa Simba, Kipindimbi havijapata umeme, kata ya Miguruwe - kijiji cha Mtepela na Kingombe na Zinga Kibaoni havijapata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika kata ya Kinjumbi kuna vijiji vya Pungutini, Kitope havijapata umeme. Lakini pia katika Jimbo la Kilwa Kusini kwa Mheshimiwa Bwege kuna kata saba yenye vijiji 31 havijapata umeme, kata ya Pande, kata ya Limalyao, kata ya Nanjilinji, kata ya Likawage, kata ya Mandawa, kata ya Kilanjehanje na kata ya Kitole.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo pia la kuunganishiwa umeme katika vijiji ambavyo tayari vimeshapata umeme. Watu wa REA bado wanasumbua, vijiji vimepata umeme lakini kuunganisha umeme majumbani inachukua muda wakati mwingine ni zaidi ya miezi sita toka mwananchi alipie umeme, umeme anakuwa bado hajaunganishiwa. Kwa hiyo, naomba pia Mheshimiwa Waziri hilo pia uliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuwa jana kupitia vyombo vya habari tuliona Mheshimiwa Rais akizungumza na Mabalazi lakini pia alizungumza na Katibu wa SADC akieleza nia ya Serikali ya kujenga kiwanda cha mbolea pale Kilwa Masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza, kukupongeza wewe Mheshimiwa Waziri, nimefurahi sana katika hilo na hata kwenye hotuba yako ukurasa wa 37 umeleza kwamba zimetengwa pesa shilingi bilioni 4.41 kwa ajili ya utengenezaji wa kiwanda hicho, tunashukuru sana. Lakini naomba pia suala hilo liendane sambamba na upanuzi wa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*



**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha...

**MHE. VEDASTO E. NGOMBALE:** Ahsante!

**MWENYEKITI:**...naomba aendelee Mheshimiwa Othman Omar, ameondoka naomba tumalizie na Mheshimiwa Ishengoma.

**MBUNGE FULANI:** Yupo Masjid, aendelee Mheshimiwa Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii, pili namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia nafasi nikaongea kwenye Bunge hili kwa leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Naibu na Wizara nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongelea kuhusu umeme wa REA nampa pongezi Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara nzima kwa upande wa umeme wa REA, kwa sababu umeme wa REA kwa kweli umesambaa kwenye mikao mingi na kwenye vijiji vingi. Umeme wa REA kwanza nashukuru kwa sababu pale ninapokaa nyumbani nashukuru sana Nyakayanja Nyeishonzi tumeweza kupata umeme wa REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo Mheshimiwa Waziri nakuomba sana tena sana, Mkoa wa Morogoro umejaliwa sana kuwa na mito mingi, Mkoa wa Morogoro una vyanzo vya umeme ikiwepo Kihansi pamoja na Kidatu lakini Mheshimiwa Waziri bado kuna vijiji vingi ambavyo havina umeme. Kwa hiyo, *Phase I* ya REA imepita, *Phase II* bado inaendelea, *Phase III* naomba mwezi wa saba ukianza naomba uweze kutupatia umeme kwenye vijiji hivi ambavyo havijapata umeme kwenye Wilaya zote za Mkoa wa Morogoro, Gairo, Kilosa, Mvomero, Morogoro Vijijini, Kilombero pamoja na Mlimba, Ulanga, na Malinyi naomba uwape kipaumbele kwa sababu ndiyo wana vyanzo vikubwa vya umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nishati mbadala, nimeona kuwa utaipa kipaumbele, naomba sana uzidi kuipa kipaumbele kwa nishati mbadala au jadidi, kwa mfano *biogas*. *Biogas* ni rahisi hasa kwa wafugaji, *biogas* ni kitu rahisi ambacho kila mmoja anaweza akatumia, ni *initial costs* ambazo ndiyo kazi. Kwa hiyo, *biomass* pia, umeme wa jua, umeme wa maji, nguvu za maji na upepo kwa mfano Singida pamoja na Makambako ambao tayari ilishaainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana uviangalie na hasa kwa sababu ukichukulia kuwa kutokana na tabia nchi na uharibifu wa mazingira watu



wameanza kukata miti na kutakuwa jangwa. Lakini kama tutatumia hivi vyanzo ambavyo ni rafiki kwa mazingira kwa hiyo watu wataacha kutumia mambo ya mkaa na wataweza kutumia hivi vyanzo vingine. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri naomba aangalie kuhusu bei ya umeme. Najua amesema inateremka lakini naomba iweze kuteremka zaidi. Pia gesi za kutumia nyumbani na zenyewe ni nishati, bei iko juu, naomba pia iweze kuteremka kwa sababu ikizidi kuteremka wananchi wengi wataweza kutumia hiyo gesi na wataweza kuacha kuharibu mazingira kwa kuchoma mkaa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee mapato hasa mimi naongelea kwa upande wa vituo vya mafuta. Nimefanya utafiti mdogo kuhusu vituo vya mafuta, vituo vya mafuta tumeweka mashine, zile unapoweka mafuta zinakata risiti. Nashukuru kuna zile ambazo zinafanya *automatic* hata ukiweka lita moja unapata risiti yako, lakini kuna vituo mbalimbali ambavyo hizo mashine hazifanyi kazi na hao wanaouza mafuta wanafanya makusudi wengine hawazitumii hizo mashine na wengine wanatumia vitabu ambavyo mapato yetu hatuyapati kwa urahisi na wengine watu hawajawa na utaratibu wa kuomba hizo risiti kwa hiyo tunazidi kupoteza mapato. Kwa hiyo, naomba elimu itolewe na ufuatiliaji uweze kufuatiwa kusudi tuweze kupata mapato ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi kwa Waziri wa Nishati na Madini Mheshimiwa Profesa Muhongo ambaye nimeshampa hongera, naomba sana wakati pale unajumuisha ingawaje hujatupatia orodha ya vijiji ambavyo vitapatiwa umeme kwenye mikoa yote wakati wa *Phase III* inayokuja, mimi nakuomba sana uweze kutupatia hiyo orodha ya vijiji ili tuweze kufuatilia na kuona na kuwaambia watu wetu kuwa umeme unakuja kaeni tayari. Hiyo ni nguvu zote na jitihada zote za Serikali ya Chama cha Mapinduzi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachimbaji wadogo wadogo, nilikuwa naongelea kuhusu wachimbaji wadogo wadogo. Nakushuru Mheshimiwa Waziri umesema kuwa umewatengea maeneo. Lakini kumbuka kuwa kila mkoa kwa wastani kuna wachimbaji wadogo wadogo, nilikuwa naleta ombi kwako Mheshimiwa Mwenyekiti kuwa Mheshimiwa Waziri aangalie hawa wachimbaji wadogo wadogo waweze kuwapatia elimu. Naelewa kila mkoa au kila kanda kuna ofisi ya madini, hawa maofisa madini wanaweza wakakaa na hawa wachimbaji wadogo wadogo wakaweza kuwapatia elimu na ninaomba na wenyewe waweze kupatiwa ruzuku pamoja waweze kununua vitendea kazi kwa sababu haya madini ukishika hovy hovy kwa mikono unaweza ukaungua mikono. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa upande wa Mkoa wangu wa Morogoro, Wilaya ya Ulanga ambayo ina madini ambayo hayo madini nashukuru nasikia wanakuja wawekezaji, lakini imeanza mgogoro na hawa wananchi wa Ulanga ambao wanachimba madini yao wanasikia kuwa hawa wawekezaji wataweza kuchukua maeneo yao na hawa wananchi wamekuwa na vitalu vyao vya muda mrefu na wengine ni kurithi.

Kwa hiyo, naomba sana kusudi kukataza hii migogoro isitokee na kuendelea tuweze kuwapa elimu na kuwatengea maeneo yao hao wananchi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Ishengoma nashukuru muda wako umeisha.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Haya, ahsante,

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, naomba mkae nimalize kidogo halafu tutatoa Mwongozo.

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaendelea na wachangiaji wafuatao, naomba niwataje, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Hamidu Bobali, Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Fredy Atupele, Mheshimiwa Edward Mwalongo na Mheshimiwa Josephat Kandege, kwa hiyo, hawa wataanza jioni tukijaaliwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikataa Miongozo kwa Kanuni ya 68(10) na 72 na Kanuni ya 5 kinyume na nilivyozungumza, nilikosea nilisema Kanuni ya 64 lakini ni 68. Kwa hiyo kabla ya kutoa Mwongozo naomba kwanza naomba nitoe Miongozo iliyopita ili tuweze kuendelea.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Kuna Mwongozo wa Spika ulioombwa na Mheshimiwa Ally Saleh Ally, Mbunge wa Jimbo la Malindi kuhusu swali kutojibiwa kikamilifu katika majibu ya Waziri wa Katiba na Sheria kwa swali lililoulizwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Jimbo la Mtambile.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 27 Aprili, 2016 katika Kikao cha Sita cha Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Ally Saleh aliomba Mwongozo wa Spika kwa kupitia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni ya Kudumu za Bunge la Toleo la Januari, 2016 kwamba Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria wakati akijibu swali namba 59 la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Jimbo la Mtambile kuhusu uvunjaji wa haki za binadamu za Mashekhe wa Zanzibar walio katika Gereza la mahabusu ya Segerea. Mheshimiwa Ally Saleh alieleza kuwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria hakujibu swali hilo kikamilifu kwa mujibu wa Kanuni ya 46 ya Kanuni ya Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 hivyo kukiomba kiti kueleza kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi Kikanuni.

Hoja ya msingi katika Mwongozo wa Spika ulioombwa ni kama kweli swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim halikujibiwa kikamilifu na kama halikujibiwa kikamilifu, je, jambo hilo linaruhusiwa?

Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 inaeleza kuwa Mheshimiwa Waziri anayetoa majibu anapaswa kujibu swali lililoulizwa kwa ukamilifu na kanuni hiyo inaeleza; "Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa, isipokuwa kwamba kama jibu linalohusika ni refu au linatakwimu nyingi Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala ya jibu mapema baada ya kikao cha kwanza kabla ya muda wa kujibu swali hilo haujafika."

Katika majibu ya kiti kwa Mheshimiwa Ally Saleh, baada ya kuomba Mwongozo iliamuliwa kwamba kiti kitafanya rejea ya majibu ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria katika Taarifa Rasmi za Bunge yaani *Hansard* na baada ya hapo Mwongozo utatolewa.

Baada ya kupitia *Hansard* nimeridhika kwamba majibu yaliyotolewa yalijitosheleza, Mheshimiwa Waziri alieleza kuwa kazi ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi na kwamba kama yapo malalamiko hayo ya udhalilishaji na ukiukwaji wa haki za binadamu vitendo ambavyo vinaelezwa kuwa mashekhe wanalalamika kuvipata tayari yamepokelewa kwenye Tume. Mheshimiwa Waziri aliendelea kueleza kuwa Tume itayashughulikia malalamiko hayo na itatoa taarifa ya Tume ambayo itawasilishwa Bungeni kwa mujibu wa Ibara ya 131(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Ibara tajwa inaeleza bayana kuwa kila mwaka wa fedha Tume itatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri anayesimamia haki za binadamu taarifa kuhusu; (b) hali ya utelekezaji wa hifadhi ya haki za binadamu katika Jamhuri ya Muungano na Waziri atawasilisha mbele ya Bunge kila taarifa iliyowasilishwa kwake na Tume mapema iwezekanavyo baada ya kuipokea.

Kutokana na majibu hayo ya Mheshimiwa Waziri na kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya Katiba niliyonukuu nimeridhika kuwa swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim lilijibiwa kikamilifu kwa mujibu wa Kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Kama yako malalamiko yoyote ya uvunjaji wa haki za binadamu yaliyofanyika dhidi ya mashekhe waliopo gerezani yatashughulikiwa na Tume kama ilivyoelezwa. Ni vema ikasubiriwa taarifa itakayowasilishwa mbele ya Bunge kwa mujibu wa Katiba na hapo ndipo itajulikana hatua za kuchukua. Huu ndiyo Mwongozo wa suala hilo.

Mwongozo mwingine ni Mwongozo wa Spika kuhusu suala lililolombewa Mwongozo na Mheshimiwa John Wegesa Heche kuhusu usahihi wa majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI wakati alipokuwa akijibu swali namba 64 lililoulizwa na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha Nane, Mkutano wa Tatu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mnamo tarehe 29 Aprili, 2016 Mheshimiwa John Wegesa Heche alisimama na kuomba Mwongozo kwa kutumia Kanuni 68(7) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inayosomeka kama ifuatavyo:-

“Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa hapo hapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa.”

Mwongozo wa Mheshimiwa John Heche ulieleza kuwa wakati Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI anajibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota kuhusiana na posho za Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa alijibu kiujumla bila kueleweka katika mambo ya msingi na bila ya kuangalia utofauti vipato vya Halmashauri.

Mheshimiwa Chikota katika swali la msingi namba 64 aliuliza kuwa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa wana majukumu mengi ikiwemo kuhakikisha kuwa ulinzi na usalama katika maeneo yao je, lini Serikali itanza kuwalipa posho ya mwezi Wenyeviti hao ili kutoa motisha ya kazi yao?

Swali hilo la msingi lilijibiwa na Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa ufupi alieleza kuwa kila Halmashauri inatakiwa

kurejesha katika vijiji na mitaa asilimia 20 ya mapato ya ndani. Sehemu ya fedha hizo inatakiwa kuwalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa.

Baada ya majibu ya swali la msingi Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota aliuliza maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza aliuliza kama ifuatavyo:-

Asilimia 20 ni fedha ndogo inayopelekwa kijijini ikiwa vijiji vitaamua kuwalipa malipo Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa, havitafanya kitu kingine. Serikali haiona sasa ni wakati muafaka wa kubeba jukumu hili na kuwalipa Wenyeviti wa Mitaa?

Mheshimiwa Selemani Jafo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alijibu swali hilo kama ifuatavyo:-

Kwanza ni kweli asilimia 20 ni ndogo na kama Halmashauri itawalipa Wenyeviti wa Vijiji na Mitaa haitatosheleza kufanya kazi nyingine, ndiyo maana Serikali imeweka *specification* katika bajeti ya mwaka huu kwamba kila Halmashauri wakati ikipitia mchakato wa bajeti kuona inakidhi na jinsi gani itahakikisha mapato yake ya ndani kupitia vyanzo vya ndani mbalimbali ili mradi mwisho wa siku ziweze kupeleka fedha na ioneshe ni jinsi gani itakusanya pesa za kutosha. Lengo ni kwamba Wenyeviti wa Vijiji waweze kupata posho na pesa nyingine ziweze kufanya maendeleo ya kijiji.

Swali linalotakiwa kujibiwa katika hoja ya Mheshimiwa John Heche ni kama Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI alitoa majibu ambayo hayakueleweka na hayaridhishi wakati alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota.

Maswali ya Wabunge yanatakiwa kujibiwa kwa ukamilifu kwa mujibu wa Kanuni ya 46(1) inamtaka Waziri aliyeulizwa swali kujibu swali hilo kikamilifu, Kanuni tajwa inaeleza kama ifuatavyo:-

Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kama lilivyoulizwa isipokuwa kwamba kama jibu linalohusika ni refu au linatakwimu nyingi Waziri atampa Mbunge muuliza swali nakala yajibu mapema baada ya kikao kuanza kabla muda wa kujibu swali hilo haujafika.

Aidha, Kanuni ya 45(3) imempa mamlaka Mheshimiwa Spika ya kutathimini swali lililoulizwa kama limejibiwa kikamilifu na kama atajiridhisha kuwa swali hilo halikujibiwa kikamilifu ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge, nanukuu:-

“Iwapo Spika ataridhika kuwa swali la msingi au nyongeza halijpata majibu ya kuridhisha ataagiza lijibiwe kwa ufasaha zaidi katika kikao kingine cha Bunge.”

Kwa mujibu wa kanuni hiyo ni dhahiri kuwa Spika atapima kama majibu yaliyotolewa na Waziri yanaridhisha au hapana, kwa mamlaka hayo baada ya kupitia Taarifa Rasmi za Bunge kama nilivyozirejea mwanzoni mwa Mwongozo huu nimejiridhisha kuwa majibu yaliyotolewa kwa maswali yote, la msingi na la nyongeza yanaridhisha na maswali hayo yalijibiwa kwa ufasaha kama yalivyoulizwa. Hivyo kiti hakioni sababu ya kuchukua hatua yoyote na huo ndiyo Mwongozo uliotolewa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile muda unaenda basi nitatoa Mwongozo kidogo halafu tumalizie, Mheshimiwa.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naomba uniruhusu kwa sababu muda umekwisha nisitaje Kanuni, lakini nilitaka Mwongozo wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la leo namba 205 lilielekezwa kwenye kujua ni kwa namna gani Serikali imejipanga kuboresha nyumba za Askari Magereza, lakini jibu lililotolewa ni uboreshaji wa nyumba za Polisi na jambo hili limezungumzwa karibu bajeti zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Askari Magereza wa nchi hii wanaishi katika hali duni sana, nitoe mfano tu kwenye Jimbo langu la Rombo, wanaishi katika vibanda vya mabazi ambayo kule tunajengea nyumba za nguruwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu ni udhalilishaji mkubwa wa Serikali, ni kwa nini usitolewe Mwongozo kwamba hizi nyumba ambazo zimetajwa katika bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani kwa ajili ya Polisi usiletwe mchanganuo ionekane kwamba Polisi watajengewa kiasi gani na Magereza kiasi gani tena kwenye maeneo yapi ambayo hawa Askari wa Magereza wanaishi kwa kudhalilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, nimepokea Mwongozo na utatolewa baadaye...

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Muda umemalizika tafadhali na kwa vile tumemaliza kazi ya leo mchana huu basi nalisitisha Bunge hadi leo jioni saa kumi.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpaka Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI.**

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha  
2016/2017- Wizara ya Nishati na Madini**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Mwita Waitara.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa hii kuchangia kwenye Wizara hii muhimu sana ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba Wizara hii ndiyo imeshikilia uchumi wa Tanzania, tukisema Tanzania ya viwanda ina maana Wizara hii ndiyo inatakiwa ifanye vema. Tukienda hata kwenye sekta ya afya, tumeshuhudia mikoani hasa katika Wilaya ya Tarime kwenye vituo vya afya ambavyo vipo kando kando ya mji wanawake wakienda kujifungua vituo hivi vinatumia tochi kuwazalisha wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunategemea kwamba Wizara hii iweze kweli kuonesha kama ilivyosema kwenye hotuba yake kwamba asilimia zaidi 98 zimekwenda kwenye fedha za maendeleo na nje ya hizo 98 ambazo ni trilion 1.54; trilion 1.32 zinaenda kwenye nishati. Kwa hiyo, ni matumaini yangu kwamba itaenda kuwatendea haki Watanzania kwa kuwapatia nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende sasa kwenye madini; Halmashauri ya Mji wa Tarime au Wilaya ya Tarime imebarikiwa kuwa na madini pamoja na kwamba Profesa alisema dhahabu siyo kitu siku hizi, lakini bado tunaithamini dhahabu na tukiitumia vizuri inaweza ikatusaidia sana kukuza uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime ina migodi midogo midogo ya Nyabori, Kebaga na Buguti. Hii migodi ya Kebaga, Nyabori



na Buguti; mgodi wa Buguti bado ulikuwa na leseni ya *Acacia* ambao walisema inakwisha Disemba. Kwa hiyo, natumaini kwamba kama itakuwa imekwisha basi watapewa wachimbaji wadogo wadogo ambao tayari wapo *field*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mwanzoni mwa mwaka huu nilimwambia Profesa wakati ameweka ziara ya Tarime atembelee ule mgodi nafikiri nafasi haikumtoshia. Hao wachimbaji wadogo wadogo wanapata changamoto nyingi sana na tukirejea Sera ya Wachimbaji Wadogo ya 2009 ambayo ilielekeza kwamba waweze kupatiwa mitaji kwa maana ya ruzuku ambayo wameonesha kwamba wanaitoa lakini ruzuku hizi ambazo wanazitoa hazifuati utaratibu au utaratibu wake ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, walengwa siyo wale wachimbaji wadogo wadogo, wale ambao tunawa-*target* bali ni wajanja baadhi wanakuja wanajivisha *umbrella* ya wachimbaji wadogo wadogo, wana-*benefit* kwa hizi fedha na wale ambao ni *targeted group* hawapati. Kwa hiyo, ningependa sana utaratibu huu uweze kufuatiliwa vizuri, waweze kupata wale Watanzania ambao kweli ni wachimbaji wadogo wadogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine tuna GST kwa maana ya *Geological Survey of Tanzania* (Mawakala wa Jiolojia) hawaendi kuhakikisha wanasaidiana na hawa wachimbaji wadogo wadogo kujua kwamba sehemu fulani kuna madini. Kwa mfano, sasa hivi wachimbaji wa Buguti na Nyabari ambao nimewaainisha hapa wanachimba kwa kubahatisha; kwanza wanatumia vifaa duni, wanatumia nguvu zaidi kuliko teknolojia ya kisasa; lakini wakifika chini wanakuta hakuna madini wanahama tena wanakwenda kwenye shimo lingine hivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa hii GST ijielekeze kule iwasaidie hawa wachimbaji wadogo wadogo waweze kujua bayana kwamba nikichimba hapa nitakwenda kukutana na madini. Ukizingatia kwa mfano Buguti *water table* ipo juu sana, wanatumia vifaa duni, kutafuta jenereta na kuanza kutoa maji na kuchimba na hakuna umeme maeneo hayo yote ambayo nimeyaainisha, zile Kata hazina umeme kabisa. Hao wachimbaji kwanza hawajaweza ku-*benefit* na hiyo ruzuku wanajikongoja kwa kuchangishana vikundi vile, lakini wakichimba bado hawawezi kupata kinachostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, natambua kwamba huwa kuna Wakaguzi wa Madini ambao wanakagua teknolojia ya uchimbaji. Hawa watu hawawafikii hawa wachimbaji wadogo wadogo kwa kiasi kikubwa. Kwa hiyo, unakuta hawa wachimbaji hawapati ushauri mbadala kutoka kwa hawa wataalam wetu. Ningependa kuelekeza Wizara hii kama tumeamua kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo wadogo tuhakikishe kwamba tunawafikia, tunashauriana

nao, ikiwezekana tunawapatia elimu mbadala na tunawapatia na vifaa ili waweze kuchimba kwa teknolojia ya kisasa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachosikitisha zaidi kupitia uchimbaji mdogo mdogo ule uchenjuaji wa madini *mineral processing* mnaita, unakuta wanachukua yale madini, wanafia *mercury* ili kuweza ku-process na kupata ile dhahabu yenyewe; hii inawaua Watanzania kidogo kidogo, leo hata ukienda kwenye haya maeneo ya dhahabu au madini, utakuta kuna watu vipofu, maana yake haya madini yakiingia kwenye damu yana *affect* zile *chromosome* macho yataharibika. Unakuta watoto wanazaliwa wana vichwa vidogo, unakuta wengine ngozi zao ukizona hazitamalaki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika huu uchimbaji mdogo mdogo tusipowekeza vizuri, tukawapa kinu cha kufanya *direct smelting* mwisho wa siku tunawaua hawa Watanzania, baada ya muda mchache Watanzania wengi wanakufa kwa sababu wanatumia zile *mercury*. Leo ukienda Buguti, ukienda Kebaga, ukienda Nyabori unawakuta akinamama wengine hata ni wajawazito wanashika shika ile *mercury*, inawapa *direct effect* kwa kiumbe aliyepo tumboni, lakini na yeye mwenyewe *after five, ten years* wanafariki dunia. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, fanya *research* kwa wote nenda Geita, nenda Nyamongo, njoo kwenye hii migodi midogo midogo pale na Profesa unajua *mercury effect* yake, lakini wanatumia. Hivyo basi tuwawezeshe, tuwape *modern instruments* za kufanya hiyo *process* ya madini wasitumie mikono yao moja kwa moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Nyamongo kabla sijakwenda kwenye nishati. Nyamongo kwa kweli na naongea hii kama natokea Tarime, tumekuwa tukiongea huku kwa muda mrefu sana ule mgodi siyo neema kwa watu wa Tarime bali ni majonzi kwa watu wa Tarime na hata Watanzania wengine ambao wanafanya shughuli zao pale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba ukienda nchi za wengine kama kuna migodi ni neema, hivi leo kweli ukija Tarime huwezi ukaona *reflection* kwamba kuna mgodi ambao unatoa dhahabu ya kutosha kilometa kadhaa kutoka Tarime Mjini, hatuna barabara za lami, wamejitahidi ndani ya ile Kata ya Matongo pale ndiyo kuna shule wamejenga na kile kituo cha sungusungu, lakini hata ukienda hospitali ile ya mji ambayo mnaisema ambayo ndiyo inatoa huduma hata kwa asilimia kubwa kwa Wilaya nzima ya Tarime haioneshi uhalisia kwamba kuna mgodi upo kwenye hii Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiangalia huduma za jamii maji walikuwa wanatoa kwa kupeleka ile buldoza lidumu la maji lile, ina maana hawajawachimbia kuhakikishia kwamba wanawapa maji ambayo yapo

salama. Kwa hiyo naomba sana kikubwa mwaka 2011 baada ya watu zaidi ya sita kuuawa Nyamongo aliyekuwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Ngeleja, Mama Nagu Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji na Mheshimiwa Wasira walikuja Nyamongo wakawaahidi wale Watanzania kwamba watawapa maeneo mbadala ya kuchimba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile wakaongea na mgodi na wakawaahidi kwamba watachukua yale mawe wawe wanakuja kuwamwagia kwenye maeneo yao, maana wakienda kuokota mawe mnawapiga risasi. Wameshindwa kutimiza yale ambayo waliahidi, kwa sababu naamini Wizara hiyo ni *institution* hata kama ametoka yule Waziri amekuja mwingine, mnabukua *ma-file* mnaona mliahidi nini kwa wale Watanzania mkawatimizie. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la nishati; Jimbo la Tarime Mjini au Wilaya ya Tarime kwa asilimia zaidi ya 70 wananchi wake hawana umeme. Leo tunavyoongea Mheshimiwa Profesa Muhongo, tumeshaleta mapendekezo yetu kupitia REA I pia na hizo njia nyingine za kuweka umeme kwa hawa Watanzania. Kama tunataka kukuza uchumi wetu tuhakikishe tunasaidia, mathalani Tarime Mjini Kata ya Nkende, Nyandoto, Kitale na Kenyamanyoli asilimia zaidi ya 98 hawana umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Nkende kuna soko tunalijenga la Afrika Mashariki hamna umeme, kuna uwanja wa ndege pale, kuna mnada wa Magena, lakini kuna machinjio ya kisasa Nkende na huduma zingine za jamii. Zaidi kwa upande wa pili wa Tarime ni Kenya; wenzetu Kenya ukija usiku ni taa zinawaka tu, ukija usiku upande wa Tanzania ni giza kama vile ni pori. Kwa hiyo, ningependa kuwaomba sana hizi trilioni 1.32 Tarime mtukumbuke, mtuletee hii nishati ya umeme, sisi ni wakulima, sisi ni wafugaji tuweze kusindika mazao yetu, tuweze kukuza uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Watanzania wengine ni wajasiriamali wadogo wadogo wamewekeza, leo mtu mwenye *saloon* kama hana umeme hawezi kumudu kununua jenereta, leo wale wafanyabiashara wadogo wadogo hawawezi kumudu bila umeme. Tukiwaza Tanzania ya viwanda, pia tuwaze Tanzania ya wajasiriamali wadogo wadogo ambao nishati ya umeme ndiyo mbadala wa kuweza kuwakomboa Watanzania. Tuwaze huduma za jamii kama shule, tuwaze huduma za jamii kama hospitali, tuwaze huduma za jamii zinginezo, magereza na vituo vya polisi bila umeme huko vijijini, hata hao wahalifu mnakwenda kuwaweka pamoja na Polisi mnategemea nini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa sana Serikali hii ya CCM kupitia kwa Profesa Muhongo wawekeze na nina imani labda alikaa hawajampunja bajeti yake na akajiridhisha kabisa hii trilioni 1.32 inatoshia kuhakikisha wanaleta

umeme zaidi ya asilimia 70 kwa Watanzania ili tuweze kuondokana na umaskini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote lile lenye nishati mbadala ya umeme utaona uchumi wake utaji-reflect kwa sababu umeme ndiyo kila kitu. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri atuangalie Tarime, Kata nilizozitaja za Kenyamanyoli na mgodi ukiwapelekea umeme hiyo migodi itaenda kufanya kazi bila kutumia jenereta. Apeleke umeme Kitale, Turo, Nyamisangula, Nyandoto na kwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara samahani, ulitajwa kimakosa kwa sababu majina yaliyopo hapa upande wa CHADEMA ukichangia wewe yatakuwa yamezidi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Hamidu Bobali, atafuatiwa na Mheshimiwa Seif Gulamali halafu Mheshimiwa Venance Mwamoto ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nianza kwa kutoa ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati. Kwanza nimpongeze kwa jambo moja anaingia kwenye historia Profesa Muhongo ya kutenga bajeti ya maendeleo ya asilimia 94. Wenzake na Wizara zao tulizozipitisha hapa tumeona Wizara zingine maendeleo asilimia 50, wengine asilimia 40, wengine asilimia 60; yeye ametenga asilimia 94, dhamira ya kuiwasha Tanzania kwa umeme inaonekana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nimshauri Mheshimiwa Muhongo kama Mbunge ninayetokea Mkoa wa Lindi, kuna suala hapa Wabunge wa Mkoa wa Lindi hawajalielewa vizuri na mimi nimwombe kama kuna uwezekano afanye kikao na Wabunge wa Mkoa wa Lindi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna huu mradi mwema sana, mradi wa LNG ambao unakwenda kufanyika pale Likong'o kilometa tatu tu kutoka kwenye Jimbo langu. Wabunge hawajauielewa vizuri na ndiyo maana unaona alipokuwa anachangia hapa Mbunge wa Lindi Mjini alikuwa anasema kiwanda hakijengwi wakati LNG siyo issue ya kiwanda, LNG inakwenda kuchochea viwanda. Sasa nilichokiona hapa kuna tatizo la uelewa kwamba huu uelewa wa Wabunge kwanza ambao ndiyo wawakilishi wa wananchi, fanya kikao na sisi utueleweshe vizuri kabisa. Hii complication unayoiona kwetu Wabunge kwa wananchi huko ndiyo hawaelewi kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku napigiwa simu naambiwa Mheshimiwa Mbunge tunaeleza kwamba sasa Jimbo letu la Mchinga linahamishwa linapelekwa Lindi Mjini. Suala la mradi LNG nawaambia hicho kitu hakipo mbona mimi sijui, sasa mkilhamisha Jimbo la Mchinga kupeleka Lindi Mjini

maana yake mimi Mbunge ndiyo basi! Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo huko chini halieleweki. Sasa naona shida kama na Wabunge na sisi hatulielewi vizuri, naomba Mheshimiwa Waziri atenge muda tu hata nusu saa akutane na Wabunge wa Mkoa wa Lindi, ateleweshe vizuri tuweze kulifahamu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie kuhusu suala la usambazaji wa gesi kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara, dhamira njema naiona kwa Mheshimiwa Waziri. Mradi wa usambazaji wa gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani na kwenye vipuri, nimeona wameelezea Miji mitatu ya Kilwa, Lindi Mjini na Mtwara. Mradi ule unagharimu karibu dola milioni kumi karibu shilingi bilioni 22 lakini kwa mwaka huu wametenga shilingi milioni 700, nataka tu kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri hizi milioni 700 walizozitenga mwaka huu za nini? Kwenda kufanya *impact assessment* au kufanya *evaluation* maana hizo ndiyo *terminologies* tulizozioea, hizi milioni 700 ni za nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu hapa aniambie, huu mradi wameuandika vizuri kabisa hapa na kwa takwimu kama mwenzangu alivyotangulia kusema Profesa yupo vizuri sana kwenye takwimu, kwa hiyo, ameanisha vizuri kwamba mradi utagharimu shilingi bilioni 22, lakini mwaka huu wametenga milioni 700 za nini hizi milioni 700? Kwa hiyo, naomba majibu katika hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimboni kwangu kumbakia vijiji 15 kupata umeme; umeme wa *REA phase I* na *phase II* umebakisha vijiji 15, kwa Lindi na Mtwara kubaki na vijiji 15 siyo *privilege* kwa sababu tuna umeme mwingi unapotea tu, bado ni suala la usambazaji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, karibu *megawatt* 30 Waziri unajua zinapotea kila siku kwamba hazitumiki, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri mradi wa *REA phase III* animalizie vijiji vilivyobakia katika Jimbo la Mchinga vyote vipate umeme kwa sababu ametengeneza fitna kubwa kuonekana vijiji vingine vina umeme na vijiji vingine havina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Kijiji cha Dimba, Ruvu, Namtamba, Mputwa, Kiwawa, Luchemi, Luhoma, Micheye, Mihandara, Lihimilo na Mkongo, vijiji hivi naomba sana vipatiwe umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine iliyopo Mheshimiwa Waziri hivi sasa ninapoongea kuna vijiji vimepata mradi wa *REA phase II*. Jambo la ajabu ni kwamba unakuta nguzo zilizopo pale kijijini ni nguzo tatu nne; kijiji kikubwa ambacho vijiji vingine ni Makao Makuu ya Kata, Makao Makuu ya Tarafa, unakuta wanapewa nguzo tatu au nne ndiyo za usambazaji! Kuna shida kubwa sana, unakuta kijiji kizima chenye wakazi karibu 3,000 au 4000

wanapewa nguzo tatu nne, nani atapata umeme? Kwa hiyo, jambo hilo linaleta changamoto kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo kubwa pale Kitomanga, tatizo kubwa Lutamba, Milola, Mvuleni kuna tatizo kubwa, wamepeleka umeme sawa upo lakini wananchi wanautazama tu, kwa sababu kuna nguzo tatu tu ambazo zimepelekwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ni kwamba hivi sasa ninapoongea nina wananchi kule karibu 200 wamekamilisha taratibu zote za kuingiziwa umeme mpaka sasa huu karibu mwezi wa tatu umeme hawajapata. Nimewahi kuuliza changamoto ni nini? Nguzo ipo karibu wamelipia wamemaliza, wamefanya *wiring*, kuna shida kubwa watu karibu 200 Mvuleni, Lutamba, Milola, Mchinga, Maloo na Kilolambwani watu wamelipia wanasubiri umeme, umeme hawapati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atueleze tatizo ni nini, mita zimekwisha au LUKU hizo ndiyo shida, tatizo ni nini? Watu wamelipia na wamekamilisha taratibu zote lakini umeme hawapati. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo kwa kweli limenipa shida sana ni kuhusu Mchinga. Mchinga ambapo ndiyo Makao Makuu ya Jimbo pale palipata umeme kabla ya hizi *program* za REA, ndiyo kilikuwa Kijiji pekee, Mchinga na Vijiji viwili. Vijiji pekee vya pale katika Jimbo zima vilikuwa na umeme kabla ya kuingia *program* ya REA, ilipokuja kwenye *program* ya REA Mchinga haikuwa *included*. Kilichokuja kutokea ni kwamba ule umeme ambao ulikuwa nguzo tatu, nne pale za awali REA ilikwenda imeiacha kabisa Mchinga hivyo watu wa Mchinga leo hawanufaiki na REA na badala yake kuna madai makubwa ya watu kupatiwa umeme na Mchinga ni sehemu kubwa ina vivutio vingi vya uwekezaji lakini shida ni kwamba umeme hakuna. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na suala la madini ya *gypsum*, naomba tu Mheshimiwa Waziri anisikilize, Mheshimiwa Waziri hapo anayemsemesha Waziri kidogo namwomba dakika moja tu Waziri anisikilize. (Makofi/ Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuomba kuna suala la *gypsum*, Jimbo la Mchinga ni miongoni mwa Majimbo au maeneo ambayo yana *gypsum quality*. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri aliniunganisha na watendaji wake, nilimletea *sample* ikapimwa ikaonekana *the best gypsum* inatoka pale Mchinga, ipo na majibu yapo pale Wizarani kwamba ile *gypsum* ambayo nimeipeleka *one among the best gypsum in Tanzania*, ipo pale. Shida iliyokuwepo ni kwamba hivi sasa ninavyoongea kuna maeneo ya vitalu



ambavyo tayari vimeshasajiliwa watu zaidi ya 200 wamesajili mimi siwajui, wananchi wenyewe hawawajui. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mkurugenzi wa Madini wa Kanda ya Kusini Ndugu Mtwampaka, kwa sababu niliunganishwa naye, aliniletea orodha ya watu ambao wana *certificates* karibu 200 za kumili ile migodi. Nilipokwenda kuwahoji wanakijiji hakuna hata mgodi mmoja ambao wananchi wanajua. Hawa watu wenyewe hawajulikani, wako kwenye maandishi tu. Nataka kujua Mheshimiwa Waziri, kuna taratibu gani zinafuatwa ili mtu kupata *certificate* ya kumiliki eneo la uchimbaji wa madini ama hii migodi ya *gypsum*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shida kubwa Mchinga, nikwambie Mheshimiwa Waziri, kama hili litaendelea hawa waliochukua *certificates* wajue tu kwa Mchinga ni *nullified*, yaani mimi nikiongea kule kazi imekwisha. Kwa hiyo, kama wataendelea kujificha, Mbunge siwajui, Mkurugenzi wa Halmashauri hawajui, wananchi hawawajui, wajue hizo *certificates* zao ni za mfukoni, hazita-*function* Mchinga. Nahitaji watu wote ambao wana *certificates* za kumiliki maeneo ya uchimbaji waje tuwaone, wasijifiche, waje tuwaone.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna shida ya watu kutoka *TPDC*, hili nilishakueleza Mheshimiwa Waziri, wanakwenda Mchinga kuchukua maeneo, wanakwenda ku-*lease* wanakatia hati za ardhi kwa sababu tu Mchinga kunaonekana kuna *potentiality* ya gesi na *gypsum*. Hili namhakikishia Mheshimiwa Waziri hakuna mtu kutoka *TPDC* atakayepata eneo Mchinga, ninayeongea ndiye Mbunge wa Jimbo la Mchinga, ndiyo mwisho, ndiyo *final say* pale. Hakuna mtu ambaye atakwenda kuwadhulumu watu wa Mchinga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Seif Gulamali, Mheshimiwa Gulamali ni kama nilipata taarifa kuna mtu unagawana naye dakika ama siyo wewe?

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapana, nafikiri ulipata *wrong information*.

**NAIBU SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Gulamali akimaliza atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kutumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Manonga kwa kutuomba dua familia yetu na hatimaye jana



kuweza kufanikiwa kupata mtoto wa kiume, nashukuru sana. Hiyo ni taarifa nawaambia wananchi wa Manonga nimepata mtoto wa kiume ambaye sasa atajulikana kwa jina la Salim, ni mtoto wangu wa kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nijielekeze kwenye hoja husika katika Wizara hii ya Nishati na Madini, kwanza nimpongeze Waziri aliyepata nafasi ya kuteuliwa na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Sospeter Muhongo pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Medard Kalemani. Ni viongozi imara, shupavu, wanawajibika na wanafanya kazi kweli. Nawaunga mkono kwa sababu natambua juhudi wanazoendelea kuzifanya na natambua vita kubwa ambayo wanapambana nayo ndani na nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hayo yote nipende kuchangia katika sehemu moja inayohusu vinasaba. Niishauri Wizara ama tushauriane, katika sehemu hii jana liliibuka suala hili la vinasaba katika ajenda zetu humu ndani. Limezungumzwa na kuna mtu mmoja ambaye ame-*declare interest* kwamba yeye ni mfanyabiashara na masuala haya ya vinasaba yanahusika kwake na ameeleza faida na hasara. Siku ya leo tumepata *document* inatembea humu ndani ikieleza faida ya vinasaba. Sasa mimi hapa nimepata walakini kidogo, inawezekana, maana kuna Wabunge sasa kama wanafundishwa kusifia na wengine wanafundishwa kukataa, mivutano imekuwa mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tujadili kwa maslahi ya nchi yetu, tusijadili kwa maslahi ya mfanyabiashara au ya Serikali au ya kukandamiza watu au watu wapate mlungula, kwa sababu inaonekana kuna watu humu wanajadili huku hata *document* yenyewe tunayoisoma mpaka tuisome, ueleweshwe, uanze kuja kusifia, hii *document* inatoka wapi ya kufundisha watu jinsi gani ya kuzungumza humu ndani?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwa sababu yeye ni makini sana *document* hii inazungumzia faida ya vinasaba, umepatikana msukumo kutoka wapi kuja kuwafundisha Wabunge kuzungumza faida ya vinasaba? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe sasa Wizara hii husika, Mheshimiwa Sospeter Muhongo ni mtu makini, isije kuwa hapa kuna watu wanapokea hela kuja kusifia ama kuja kuponda. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, Wizara yake iende ikayafanyie kazi, ajue kwenye vinasaba kumejificha nini? Inawezekana tunapata faida lakini kuna watu wanapata faida kwa kupokea rushwa. Haiwezekani hapa watu wanazungumzia vinasaba, wengine hata biashara hawajui wala hawajawahi kuifanya!

Mheshimiwa Naibu Spika, tuombe Mheshimiwa Waziri, hili suala la vinasaba, nimepata wasiwasi kuona *document* hii imekuja humu, Wabunge

wanafundishwa jinsi ya kuchangia, hii hapa ninayo. Kwa hiyo, naomba nimwambie Mheshimiwa Waziri waende wakaliangalie vizuri hili suala zima. Inawezekana tunawakandamiza wafanyabiashara ama tunawa-favour wafanyabiashara. Kwa hiyo tukaangalie, tusije tukawa tunawaumiza.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati mwingine hata hii EWURA sijaiielewa vizuri, hizi Kanuni za uanzishwaji wa *petrol stations* sheria ziko Dar es Salaam, zinatakiwa zisambazwe kwenye Halmashauri zetu kule. Maana unakuta wafanyabiashara wana vituo vyao vya mafuta wanaambiwa hana hiki, hana hiki, ukiuliza sheria hana sheria, sheria ziko wapi, wanazo ofisini kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Sheria hizi zisambazwe ili wananchi wawe wanafahamu, wawe na uelewa wa jinsi gani ya kuendesha biashara hizi kuliko kukaa tunawabambikiza kesi milioni tano faini, tunawaumiza. Lazima tuangalie pande zote mbili, upande wa Serikali lakini pia tuangalie upande wa wafanyabiashara.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

#### TAARIFA

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gulamali naomba ukae, Mheshimiwa Ester Bulaya taarifa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, amesimama *Chief Whip* wa upande wa pili, inabidi uskilize, sawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, sijui kwa nini mdogo wangu ame-panic nilivyosimama, kwa nia njema tu! ameshika *document* na tunajua *document* zinavyogawiwa kwenye Bunge zinakuwa na utaratibu. Sasa huku wengine hatujapata hizo *documents*. Kwa hiyo, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji, labda hiyo *document* yeye ameipataje? Inazungumzia nini na hiyo rushwa ikoje? Je, yeye kashawishiwa au la? Ili tujue, kwa sababu upande huu sisi hatujapata hiyo *document* na inazungumzia vinasaba na suala la vinasaba kama alivyosema linahitajika tulifahamu kwa kina. Tumelielewa juu, sasa mpaka imefikia masuala ya kutolewa *document*, sijui kama ni jambo la kulinyamazia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hilo tu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya uliomba kumpa taarifa, nadhani badala ya taarifa umemuuliza maswali. Nadhani hiyo *document* haijaja kiofisi, kwa hiyo pengine wamepewa watu ili wazungumzie kama yeye alivyozungumza. Kwa hiyo, nadhani na sisi hatutai-treat kama *official*, yeye

amalize mchango wake kwa kadri alivyoshawishiwa namna ya kuongea. Mheshimiwa Gulamali! (Makofi/Kicheko)

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru, dakika zangu zilindwe. Nafikiri hapo sasa Wizara itaangalia jinsi gani ya ku-handle hiki kitu, kwa sababu tayari imeshaanza kuingia migongano ya mawazo, kuna wengine wanasifia na wengine wanaponda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze pia katika matatizo ambayo nilikuwa nazungumzia EWURA kusambaza hizi sheria katika Halmashauri zote nchini ili wananchi wanaotaka kufungua hivi vituo vya mafuta watambue ili kuweza kuhakikisha kwamba wanafanya biashara zao wakiwa salama badala ya baadaye kuwatwisha mizigo na kuleta hasara kwa wananchi hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo niombe Wizara hii ya Nishati ikae chini iangalie kwa kina, fedha za mafuta zinakusanywa na EWURA, Wizara ya Nishati na madini haiwezi ikajitengenezea utaratibu au tukatengeneza sheria hapa ambayo itawasukuma wao ingawa chombo hiki kiko chini yao. Maana EWURA wanasimamia maji, sijui mafuta, na vitu vingine vya kupanga bei. Sasa niombe Wizara ili iangalie kwa kina jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuchangia hayo nijielekeze kwenye Jimbo langu la Manonga. Nipende kumpongeza Naibu Waziri wa Nishati na Madini, alikuja Jimboni kwetu akaangalia maeneo yetu, tuna maeneo ya uchimbaji wa dhahabu. Pamoja na kuona changamoto mbalimbali alijionea mwenyewe jinsi gani tuna vijiji karibu 40 havina umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji vya Mwatinja, Mwashiku, kuna Kata ya Ngulu, Kata ya Ntobo, Kata ya Igoweko, Kata ya Uswaya, Kata ya Utambarale, Kata ya Mwamala, Kata ya Sungwizi, Kata ya Kitangiri, maeneo yote hayo hayana umeme. Naiomba Wizara iangalie, inapogawanya mpango wa REA phase III, basi tuwekwe kwenye program hii tupate umeme. Tunahitaji umeme kama vile ambavyo maeneo mengine yanavyohitaji kupewa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo alikuja Naibu Waziri, Mheshimiwa Kalemuni alizungumzia ufutaji wa leseni kwa baadhi ya waliomiliki maeneo makubwa ya ardhi ambayo yana rasilimali ndani yake hayaendelezwi kwa miaka mingi sana. Akatoa tamko akasema kuanzia leo nimefuta leseni ya haya maeneo na aliitaja kampuni moja ya Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachoshangaza mpaka leo wale wananchi aliowapa maelekezo waende wakafuatilie wapate haki ya kumiliki ardhi ili waweze kufanya kazi ya uchimbaji mdogo mdogo pale, walikwenda pale ofisini Tabora, wakaambiwa process hii bado, hatujapata tamko kutoka Wizarani,

hatujapewa maandiko, hao wahusika alikuwa nao, mgongano huu wa kauli mbili tofauti umetoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Wizara yake iangalie vizuri ili kuangalia huu mgongano wa kimaslahi usiweze kujitokeza. Leo tunaambiwa kwamba huyu aliyepewa lile eneo la ardhi leseni yake itakwisha mwezi wa tisa, lakini hapo hapo siku ile alifuta ile leseni yake, hapa mgongano unatokea wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri wachukue hatua, kama wamefuta leseni maana yake wamefuta *from the sport* na hapo wanaanza kutoa maeneo kwa wadau wa maeneo husika, mwisho wa siku itakuja tarehe hiyo ya kufuta watatuambia ameomba Mwekezaji mwingine kutoka nje ya maeneo yetu. Naomba sana Wizara iliangalie hili la mgawanyo wa rasilimali hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutatua mgogoro alikuja Kamishna wa Madini, alikutana na watu kutoka Nzega wakizungumzia mgogoro wa *Resolute*. Likatoka agizo, amemwondoa yule mtu aliyekuwa kwenye lile eneo la *Resolute*, aliyekuwa Mwekezaji amekaa kinyume na utaratibu. Akasema *from the sport* aondoke, lakini mpaka tunavyoongea dakika hii yule bwana anaendelea kufanya kazi zake katika lile eneo la *Resolute* Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba hii Wizara ya Nishati, haya matamko yetu ambayo yanatoka Wizarani hawa walioko chini wanayachukuliaje na wanayafuatilia kwa namna gani, ili tunapotengeneza mazingira tutengeneze mazingira ya uaminifu. Siyo tu uaminifu kwa Wabunge, tutengeneze uaminifu pia kwa Serikali yetu ili tuaminiwe. Serikali iaminiwe, Wabunge waaminiwe na wananchi wafanye kazi zao kwa usalama. Hizi kauli mbili zitapelekea kuleta mgongano wa kimaslahi kati ya yule mwekezaji na wananchi ambao wanataka kuwekeza katika lile eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondoa mgogoro ambao utakuja kujitokeza katika eneo la *Resolute* Nzega, tulitatie haraka iwezekanavyo kutokana na kauli ambayo Mheshimiwa Waziri alishaitoa ya kwamba hawa watu waondoke, wawaachie hawa wananchi na waweze kujipatia kipato chao cha chini, waweze kuhangaikia kupata vitu viwili vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimezungumza kuhusiana na matatizo haya ya umeme, hayapo tu katika Jimbo la Manonga, yapo pia katika eneo letu la Wilaya yetu ya Igunga. Mgogoro upo wa madini katika Kata ya Nanga. Kuna mwekezaji Mchina alikuja pale, akasema anataka lile eneo, akataka kuingia *contract* ya kulimiliki eneo lile, akawaambia shilingi

ngapi wakakubaliana milioni mia tano. Wale wananchi wakakubali wakaandikishana mikataba, wakapewa milioni mia mbili za kianzio.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha ajabu baadaye tena anakuja anataka sasa awe mbia, waendeleo na yeye kama mzawa. Ukienda ukifuatilia Mchina yule amepewa sijui kibali cha uraia cha muda gani. Niombe hata watu wa Uhamiaji wanapotoa vibali vya uraia waangalie, mtu anakaa, ameshaanza kutengeneza mazingira ya mwezi mmoja, miezi miwili, anakwenda *Immigration* anaomba uraia, anapewa uraia anaanza kuja na *documents* za kusema nipewe sasa kama mzawa. Wizara hizi ziangaliwe kwa umakini. Tuna mgogoro pale Nanga kati ya Mwekezaji huyo ambaye ni Mchina ili tuutatue.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naunga mkono hoja. Ahsante.  
(Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi ambaye muda wake atagawana na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote kwa kutenga bajeti kubwa ambayo haijawahi kutokea, asilimia alizotenga tuna uhakika kwamba umeme sasa utakuwa umefika sehemu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba leo mnachozungumzia hapa ni suala la umeme. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda yuko pale bila ya umeme hatofanya chochote, lakini hamuelewi huo umeme mnaozungumza ni umeme gani. Umeme tunaazungumza sasa hivi ni ule ambao unatokana na nguvu za kule Kidatu, Kihansi na ule mwingine unaotoka kwenye bwawa la Mtera, yale maji yanatoka katika Wilaya ya Kilolo. Vyanzo vitano vya maji ambavyo vinajaza Kihansi vinaanza kwenye vyanzo ambavyo vinatoka kwenye Wilaya ya Kilolo, sehemu ya Muhu na Mkasi. Maji yanayojaza bwawa la Mtera yanatoka kwenye vyanzo vikuu ambavyo ni Mto wa Lukosi na Mto Mtitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishaongea na Mheshimiwa Waziri nikamwomba kwamba ni vema sasa tukaenda kule akatembea aone uhalisia. Kwamba wale wanaopika chakula kizuri wenyewe hawali. Mpaka hivi ninavyomwambia kuna Kata ya Kimala, Idete, Ukwega, Udekwa, Kising'a, Nyanzwa na Mahenge wanausikia tu umeme kwenye bomba, wakati wakijua kabisa kwamba chanzo kikuu ni Wilaya ya Kilolo. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa alishaniahidi kufika kule, naomba afike ili aangalie ni jinsi gani atanifikiria tuweze kupata umeme vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nishauri tu, kwamba kwa kuwa mwaka wa juji, mwaka wa jana tulikuwa kwenye kujenga maabara, maabara zile hazitakuwa maabara kama hakutakuwa na umeme, kwa kuwa sasa wananchi wenyewe hali zao si nzuri sana niombe Serikali, Wizara ya Elimu ikishirikiana na Wizara hii tuweze kuhakikisha kwamba kwenye shule zote za sekondari ambako tumejenga maabara waweze kuingiziwa umeme, hilo atakuwa ametatua na ametusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine *na-declare interest*, nilikuwa Mkuu wa Wilaya, nikiwa Mkuu wa Wilaya nililetewa kesi hizi zinazohusiana na vinasaba, bahati nzuri nitazungumza yale ambayo ni ya ukweli na Mungu ananiona. Mfanyabiashara yule baada ya kukamatwa alikuja ofisini kwangu, baada ya kuja ofisini kwangu nikaomba watu wa EWURA waje, walipokuja walituelimisha jinsi gani watu wanavyotorosha mafuta. Baadaye alikubali kweli mafuta yale yalikuwa ni ya *transit* na alikuwa anakwepa kodi.

Baada ya kufanya utafiti ikaonekana kwamba zaidi ya wafanyabiashara 316,000 walikuwa wanakwepa kodi. Wafanyabiashara wa mafuta siyo mchezo ni *ma-giant*. Kwa hiyo, unaweza ukakuta kelele yote hii ambayo inapigwa hapa ni kwa sababu wale nao wana uwezo wao. Hivi jiulize, kama EWURA wasingeweza kudhibiti mafuta bei hii ambayo ipo sasa hivi ingekuwapo? Tulishafikia mpaka shilingi 3,000 kwa lita, leo tunanunua mpaka Shilingi 1,200 yanashuka, ni kwa sababu ya udhibiti mzuri wa EWURA.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi EWURA wasikatishwe tamaa. Kwa sababu juji nilisikia hapa kwamba hata tenda za kupata mtu wa kutoa vinasaba hazikutangazwa, kitu ambacho siyo kweli, zilitangazwa kwenye magazeti na kwenye tovuti na ushahidi upo, kwa nini tuseme uwongo? Naomba, badala ya kuwakatisha tamaa tuwape nguvu kitu gani tufanye ili mafuta yadhhibitiwe, wananchi wetu bei zikipungua waweze kusafirisha mazao yao, waweze kusafiri, kwa sababu bila kudhibiti hiyo nawahakikishieni mifumuko ya bei haitapungua, itaongezeka. Nawaomba wasikate tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana watu wa EWURA, endeleeni na kazi hiyo, ongezeeni nguvu. Hawa ambao wanapambana nao wapo wengi wameshawakamata. Mtu anayekamatwa siku zote anakuwa na ugomvi na Polisi, akishaona Polisi anaona huyu mtu hafai. Tumuongezee. Mimi najua watu wameshaambiwa maneno hapa kama alivyosema yule bwana mdogo, siwezi kuwavunja, wana *interest* zao. Kama mtu ana *interest a-declare interest* hapa. Mheshimiwa Waziri asikate tamaa, moto ni ule ule, hapa kazi tu, kanyaga twende. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ni kuhusu viwanda. Kama tunakwenda kwenye viwanda, tumeamua Serikali yetu kuwekeza kwenye viwanda, umeme



lazima uwe wa uhakika. Kuna sehemu ambazo tumeweka maeneo kwa ajili ya EPZA, ziangaliwe zile ili *Processing Zone* zile tuweze ku-process mazao na kuyapa thamani ili kuweza kuuza na kupata bei zinazofaa. Mheshimiwa Waziri wa viwanda apige kelele atakavyoweza, kama umeme hautafika itakuwa haina maana yoyote. Washirikiane vizuri na Waziri wa Kilimo kwa sababu viwanda vyake pia kama hakutakuwa na mageuzi ya kilimo hatafanya chochote! Kama wasambazaji wa pembejeo wataendelea kuwa wababaishaji hatafanya chochote, ubora wake utabakia kwenye vitabu na maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulanzi unatengenezwa pale Iringa, tunashindwa kwa sababu ya umeme, hebu Mheshimiwa Waziri aje atembelee, wenzetu Kenya wanasema ni bamboo *juicy*, lakini ndiyo ulanzi huo huo. Ulanzi siku ya kwanza unakuwa ni togwa, togwa ni *juicy*, siku ya pili unakuwa mkangafu, mkangafu ndiyo unanza kuwa pombe, siku ya tatu unakuwa mdindifu, mdindifu ndiyo unalewa, yeye alisoma Tosamaganga najua alikuwa anapiga ule! (*Kicheko/ Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri wa Mambo ya Ndani alisoma shule ya Tosamaganga na Naibu Waziri wa Maliasili alisoma Tosamaganga na wenyewe wanatoka Tosamaganga, kwa hiyo asiposaidia wakajenga viwanda atakuwa hajafanya kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nafikiri ni kengele yangu ya mwisho au bado?

**NAIBU SPIKA:** Bado Mheshimiwa.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningeomba kwa kweli tufanye hivyo na kuna mambo mengi, kuna sehemu nyingi, kuna viwanda kwa mfano hata kule Busega hawana umeme, wangepata umeme wangeweza pia angalau wakachinja hata wale ng'ombe badala ya kuleta ng'ombe Dar es Salaam kwenye malori wangeleta nyama.

**MBUNGE FULANI:** Sawa kabisa.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hawawezi kuleta nyama kama hamna umeme, Eeh! hakuna mabarafu yale zitaoza zile. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ili tupate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja! (*Makofi*)



**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Kapufi, dakika tano, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, ajiandae dakika tano, halafu Mheshimiwa Ruth Mollel ajiandae!

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku-*declare interest*, mimi ni mchimbaji mdogo wa madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme tunapomzungumzia mchimbaji mdogo haina tafsiri ya kuturudisha nyuma kwa mchimbaji aliyekuwa akitumia *excel*, akitumia Kinu na nyundo kuponda mawe. Bado mchimbaji mdogo anaweza akaja kwenye uchimbaji kwa kutumia *crushers* za sasa hivi akatumia teknolojia ya sasa hivi. Kwa hiyo, tukimwongelea mchimbaji mdogo, naomba kwanza tupate sura hiyo, ili tupate picha ya huyu mchimbaji mdogo ni lazima awezeshwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchimbaji mdogo akiwezesha tutamtoa ambaye jabari analipasua pasua na kuligeuza unga kwa kutuma nyundo na nguvu zake 'kwa kutumia *muscles*' hao wengi kwa sasa hivi ninavyoongea na wengi walishapoteza maisha! Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tuwaangalie hawa wachimbaji wadogo kwa maana ya kuwawezesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mpanda niwaelezeni tu, kuna maeneo ya Dirifu, Idindi, Katisunga, maeneo haya wanapatikana wachimbaji wadogo, lakini kuna leseni kubwa imewaataamia wachimbaji hawa! Nilichokuwa nakiomba kwake Mheshimiwa Waziri, kama alivyotenga katika maeneo mengine naomba na wachimbaji hawa wadogo wa eneo la Mpanda waweze kupatiwa leseni. Tukifanya hilo tutakuwa tumewasaidia watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye gari kuna kitu kinaitwa *shock absorber*. Wachimbaji wadogo tukiwapatia maeneo nao ni *shock absorber* ya namna yake katika kupunguza suala la ajira. Katika eneo moja unaweza ukakuta kuna wananchi zaidi ya 500, mchimbaji mmoja mdogo tunapopiga kelele ya kwamba tunataka tuwainue bodaboda, machinga, mchimbaji mmoja mdogo aliyewezeshwa vizuri ana uwezo wa yeye pia kumiliki bodaboda, naye anaisaidia Serikali hii kwenye kufanya shughuli nyingine za namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *system* ilivyokuwa huko nyuma tulikuwa tukiona wachimbaji wadogo wanashindana kwenye kunywa na kufanya vitu vingine, sasa hivi wamebadilika. Wachimbaji wadogo hawa wamekuwa wakijenga majumba mazuri, wachimbaji wadogo hawa wamekuwa wakiwekeza hata kwenye kilimo! Kwa hiyo, tukiweza kuwa-*support* maana yake tuna-*support* na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimweleze Mheshimiwa Waziri, ni kweli ule Mji kwa mfano, ukienda Johansburg ule mji umejengwa kwa dhahabu ya pale. Kwa hiyo, tukiwawezesha watu hawa wataijenga Mwanza, wataijenga Chunya, wataijenga Mpanda, naliomba sana hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpanda ina shida nyingine ya umeme, tunazungumzia habari ya kupewa *power plant*, lakini eneo lile Mkandarasi ni mmoja ambaye tunaambiwa ana maeneo mengi ya kufanya kazi. Naomba namna yoyote ifanyike kuhakikisha eneo hilo linafanyiwa kazi mapema kwa sababu vinginevyo mji ule tutaendelea kupata umeme wa mgao.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru ndugu yangu mmoja, Mheshimiwa Ally Saleh, wakati akichangia aliongea kitu kimoja nilikipenda sana. Alisema, tunaweza tukafanya vizuri zaidi kwa sababu tuna utulivu wa kutosha, ile *point* niliisikia asubuhi aliongea hapa, nami niendeleo kuamini kwa utulivu huu tulionao kama nchi, tuna nafasi kubwa ya kufanya mambo makubwa. Nimtie moyo tu Mheshimiwa Waziri kwamba sasa safari hiyo bado tunayo na ni nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye eneo la *tanzanite*; Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Waziri, niseme kitu kimoja, tunaomba tujiulize, mtu mmoja aliniambia hivi; ukilifahamu swali ni sehemu ya kujibu mtihani. Kama hujajua swali linataka nini huo mtihani umefeli. Kwa nini tusijiulize hawa watu wanakwenda kuuza *tanzanite* nje kwa sababu gani, shida ni nini mpaka wakauze nje? Tukishajuliza swali hilo tuna nafasi kubwa ya kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku nimekwenda South Africa, nakuta *tanzanite*, niliona *tanzanite* nikachekelea nikijua hapa naenda kusikiliza habari ya nchi yangu Tanzania, lakini wale watu katika kibao, anakwambia kutana na *tanzanite* ambayo Mama Afrika ameizawadia Afrika, haijatajwa Tanzania! Hivi tunafanyaje ku-*promote* mambo haya kwa sababu tunaweza tukawa tunalaumu tu *tanzanite* hazitoki, hazitoki! Je, eneo la *promotion* likoje? Pale South Africa mtu mwingine akifikiri *tanzanite* ni jina tu, lakini hajui kwamba kuna neno Tanzania pale. Tumefanyaje katika eneo hilo, naomba nalo hilo lizingatiwe sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuongelea suala la vinasaba, binafsi bila kushawishiwa na mtu yeyote, sababu za msingi zilizopelekea mpaka tukapata hii kitu, hizo hizo ziendeleo kuimarishwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, dakika tano.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kupata fursa hii kuweza kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo mawili, jambo la kwanza ningependa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo. Nampongeza kwa kazi aliyoifanya yeye na Watalaam wake ambao waliwezesha kupata *tender* ya kutoa mafuta kutoka kule *Lake Albert* Uganda mpaka Tanga bandarini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa dhati kabisa, najua ilikuwa ni kazi kubwa, lakini mwishowe tumeipata! Pia nataka kusema tu kwamba Mheshimiwa Waziri tumepata hiyo kazi tunataka kujua kwamba tutafaidika vipi na hili bomba ambalo litapita kwenye Wilaya yangu na litaishia kwenye bandari yetu ya Tanga. Nafikiria kwamba ni vizuri wakajipanga na Waziri wa Uchukuzi kuona namna gani ambavyo wataweza kupanua bandari ya Tanga. Kuweka vitu vya kisasa kwenye bandari ya Tanga, kuhakikisha kwamba mafuta hayo basi, tunaweza kuyakidhi na kuyahudumia jinsi inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningefurahi sana kama Mheshimiwa Waziri angeitisha kikao ili tuone kwamba tutafaidika vipi, tu-*sensitize* na wananchi wetu tuweze kuona tunaweza kuongeza *value* gani kwenye hilo bomba na tunaweza kufaidika nini kwenye hilo bomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, pia napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kutokana na mradi wa *REA*. *REA* imetusaidia sana, *REA* imetusaidia kupata Majimbo haya na mpango huu ni mpango ambao unatakiwa uendelezwe hata kwenye Idara nyingine ambapo tutakuja kuchangia kwenye mada zinazofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Jimbo langu nafikiri linaweza kuwa ni Jimbo moja kubwa kuliko Majimbo yote hapa! Jimbo langu lina Kata 37, Vijiji 135, Vitongoji karibu 550, lakini mgao ambao umefanyika kwa *REA* awamu ya kwanza na awamu ya pili, vijiji ambavyo nimepata katika Jimbo la Muheza ni vichache sana! Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie kwa dhati kabisa aone kwamba hii awamu ya tatu, Jimbo la Muheza linaweza kufaidika namna gani. Nafikiri hatujazidi hata asilimia 40 kwenye mgao ambao tumepata! Vijiji vingi kwenye kila Tarafa, Jimbo lina Tarafa nne na kila Tarafa ina matatizo, kuna vijiji ambavyo havijapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri aangalie, akitilia maanani pia Hale *power station* tunatoa karibu *megawatts* inaweza kuwa 20, pia ukijumlisha na Pangani tunatoa karibu *megawatts* 60. Kuna vijiji ambavyo viko karibu na *power stations* hizo, lakini usiku wao wanaangalia umeme kwa mbali tu. Kuna Vijiji vya Makole, Mhamba, Kwafungo na Songa vyote hivyo

vinaangalia umeme usiku kwa mbali. Ningeomba aangalie kabisa aone ataweza kutusaidiaje!

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu alipoteuliwa tu, ziara yake ya kwanza ilikuwa ni Hale na naamini aliweza kuwaona hao wanavijiji ingawaje Hale haiko kwenye Jimbo langu iko kwenye Jimbo la Korogwe. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ningeshukuru na ningefurahi kama angeweza kuliangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine sasa hivi Muheza tuna matatizo makubwa ya *transformer*, tunayo *transformer* ndogo na ambayo ni chakavu. Sasa Serikali inapata lawama kubwa sana ya umeme kuzimika zimika! Tungeomba Waziri atutafutie *transformer* kubwa, kwa sababu tunataka tufaidike na hilo bomba, tunataka tuifanye Muheza kiwe kituo cha matunda. Sasa kama hatutapata umeme wa uhakika ina maana kwamba hata hivyo viwanda ambavyo tunategemea kuvijenga Muheza vitakuwa ni matatizo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tungeomba sana ajaribu kuliangalia suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni Mkandarasi, nilishawahi kumwambia Waziri kwamba Mkandarasi Sengerema ana kazi nyingi sana! *Speed* anayokwenda nayo ni ndogo sana! Sasa nafikiri ni muhimu akampunguzia kazi ili tuweze kupata Mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana! (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ruth Mollel, atafuatiwa na Mheshimiwa Othman Omar Haji kwa dakika tano, Mheshimiwa Ruth Mollel, dakika 10.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, Ahsante! Napenda ku-*declare interest* kwamba, nilishafanya kazi katika ofisi inayohusika na mazingira na najaribu kuangalia uhusiano wa uchimbaji wa madini na mazingira. (*Makofi*)

Natambua kwamba uchimbaji wa madini au madini yenyewe unajenga uchumi wa nchi yetu na una faida kubwa katika nchi yetu, hilo halina ubishi. Hata hivyo, ni ukweli pia kwamba uchimbaji madini unaharibu mazingira kama usipodhibitiwa na kusimamiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo migodi mikubwa na najua kwamba kabla hawajapata leseni lazima huwa inafanywa tathmini ya athari kwa mazingira ambayo tunaita *Environment Impact Assessment (EIA)* - tathmini ya athari kwa mazingira na baada ya hapo leseni zinatolewa, baada ya kutoa ile *EIA* inakuwa kwamba tunasahau kabisa kwamba kuna jambo sasa la kufuatilia kwa karibu ile migodi mikubwa inavyofanya shughuli zake na kuweza kuona jinsi gani wanavyoharibu mazingira kwa namna ya maji yenye sumu, namna ya

afya ya wale wafanyakazi na mara nyingi tunakuwa *reactive* jambo limeshatokea ndiyo tunakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba leseni zinapotolewa pamoja na kwamba *EIA* inafanywa na Wizara nyingine, lakini kunakuwa hakuna uhusiano wa karibu sana na *sector Ministry*. Mapendekezo yangu ni kwamba *EIA* inavyotolewa na *certificate* inapotolewa, hizi Wizara ziweze kuzungumza ili kusudi hata wakati wa kwenda kufanya ukaguzi tupate wale wadau wakubwa wote ambao wanahusika na migodi na wale wanaohusika na mambo ya mazingira pamoja na Wilaya zile zenye madini yenyewe. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumesikia Wabunge wengi wakichangia wanasema kwamba, watu wanapata leseni wanakwenda kwenye maeneo yao wao wenyewe wenye Wilaya zao hawana habari. Ina maana kwamba, Serikali inafanya kazi mkono mmoja haujui mfuko mwingine unafanya kitu gani! Kwa hiyo, tunahitaji tuwe na timu ambayo anayetoa leseni, anayefanya *EIA* na yule mwenye eneo lake ambalo migodi ipo wote wafahamu ni kitu gani kinachoendelea katika lile eneo kwa ajili ya kudhibiti na kuhakikisha mazingira yanakuwa salama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona katika *speech* ya Mheshimiwa Waziri kwamba kuna maeneo mwaka jana 2015/2016 walitenga heka 7,731 kwa ajili ya wachimbaji wadogo na mwaka 2016/2017 wametenga hekta 12, 000 ni jambo jema. Nashauri kwamba, wachimbaji wadogo nao pia wanaharibu mazingira sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepita Mererani, nilishapita wakati mwingine sehemu za kule kwenye *diamond* - Mwadui, wanachimba wanaacha mashimo, ile ardhi inakuwa tupu hakuna miti ni mashimo! Kwa hiyo, kuna umuhimu mkubwa sana kwa ajili ya kudhibiti na kuangalia kwamba mazingira yanarejeshwa katika hali yake ya asili. Najua wachimbaji wadogo wadogo wanakuwa na *Environment Management Plans*, lakini nani anawasimamia? Hakuna mtu anayewasimamia, wanachimba wanaacha!

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba Wizara inayohusika ya Nishati na Madini, Wizara inayohusika na Mazingira na yale maeneo ambayo ile migodi inachimbwa, ile midogo midogo, watafute jinsi ya *kuya-incentivised* wale wachimbaji wadogo kusudi wahakikishe kwamba lile eneo lililochimbwa na kuharibiwa linarudishwa katika hali yake ya asili ya miti na majani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeangalia pia katika taarifa ya *Audit* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu alivyozungumzia kuhusu *petroleum exploration* na pia nimeona kwamba Ofisi ya Rais Mazingira wamefanya *inspection* tatu tu katika miradi karibu 71 na inaelekea kwamba hakuna uwezo mkubwa sana. Hili ni

eneo pia ambalo ningependa Mheshimiwa Waziri alizungumzie ni jinsi gani *inspections* ya haya maeneo itaimarishwa ili kuhakikisha kwamba tunachunga mazingira yetu. Napendekeza pia hizi *teams* ziendeele kufanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala la umeme, najua kwamba mimi mwenyewe nilishavuta umeme nikaweka nguzo kama mbili, tatu na tunalipia gharama kubwa na naamini kuna wengi pia wanafanya hivyo na hizo nguzo baadaye ni za TANESCO pamoja na kwamba ni sisi ndiyo tumezilipia pamoja na LUKU tumezilipia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri anapomalizia hoja yake atuambie ni kwa jinsi gani watu ambao wameweka hizo nguzo za umeme kwa gharama zao na hizo nguzo ni za TANESCO ni kwa namna gani wanaweza ku- *compensate*? Je, inawezekana ku- *compensate* kwa kupitia *bill* za umeme kwamba wewe umeweka nguzo tatu, bei ni kadhaa na kwamba labda *bill* ya umeme uwe unalipa kiasi fulani na ufidie kwa ile miti ya TANESCO ambayo umeweka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru Mheshimiwa Waziri akitujibu hilo suala tuweze kujua ni jinsi gani TANESCO wanaweza kutu-*compensate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi sana wamezungumzia suala la Nyamongo na mimi nasikitishwa kwamba, nilikuwemo suala la Nyamongo lilikuwepo, nimetoka sasa sijui karibu miaka mingapi suala la Nyamongo bado linaendelea. Mheshimiwa Waziri, hii Nyamongo ina shida gani, kwa nini hii *issue* haiishi? Maana yake imekuwa ya muda mrefu sana na miaka mingi, pengine labda kuna kitu Waheshimiwa Wabunge hatujui, labda kuna tatizo fulani, tunaomba Mheshimiwa Waziri anapomaliza hoja yake, atueleze kuna shida gani na hili suala la Nyamongo ambalo tumelizungumza miaka nenda miaka rudi!

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Othman Omar Haji kwa dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete halafu Mheshimiwa Edward Mwalongo ajiandae.

**MHE. OTHMAN OMAR HAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakwenda moja kwa moja kuhusu mafuta na gesi. Hapa naanza na TPDC, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania. Kwa makala chungu nzima nilizosoma nimegundua kwamba TPDC siyo shirika la Muungano, lakini shirika hili lilipewa kazi ya kushughulikia sekta ya mafuta



Tanzania nzima. TPDC katika miaka ya karibuni lilikuwa likitoa vibali na kuingia mikataba na mashirika tofauti ya Kimataifa, moja kati ya mashirika hayo lilikuwa Shirika la Shell la Uholanzi. Shirika la Shell lilifanya utafiti wa mafuta katika vitalu vilivyoko Zanzibar, ikiwepo kitalu namba Tisa, namba 10, namba 11 na namba 12, vitalu hivi vyote vinaonekana katika maeneo ya Zanzibar. Namuuliza Waziri mwenye dhamana, TPDC ilikuwa na uhalali kiasi gani kuingia katika maeneo ya Zanzibar na kutafuta mafuta bila ya idhini ya watu wa Zanzibar! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha TPDC kuingia katika maeneo ya Zanzibar na kutafuta mafuta ni sawasawa na kuwadharau watu wa Zanzibar. Tunaomba tu wenzetu waache kijicho juu ya Zanzibar kwa sababu Wazanzibari kuna rasilimali nyingi sana Tanzania Bara wao hawana habari nazo, wametoshaka na umaskini wao. Tanzania Bara kuna madini ya aina chungu nzima, Tanzania Bara kuna gesi, lakini hujamsikia Mzanzibari hata mmoja kudadisi masuala ya madini, masuala ya gesi yaliyoko bara. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Sheria ya Mafuta iliyoungwa mwaka jana (*The Petroleum Act 2015*), Sheria Na. 2 ambayo imezipa nafasi pande hizi mbili kushughulikia mafuta kila mmoja upande wake, lakini kutokana na hali ya Zanzibar ilivyo, Serikali dhalimu iliyopo, sisi hatuna imani kwamba wanaweza wakawatendea haki Wazanzibari wakaweza kudhibiti mafuta yale bila ya kuyatorosha kuyapeleka Tanzania Bara. Kwa sababu Serikali iliyopo kule ni dhalimu, ni Serikali imewekwa na Tanzania Bara na wanaketi kama ni mawakala wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sisi siyo Serikali ya Wazanzibari, kwa hiyo hawana uwezo, jambo lolote lile mtakalowaambia, wakiambiwa wa-pump mafuta walete Tanzania Bara wataleta, hawana uwezo wa kuyazuia mafuta. Kwa maana hiyo, hatutegemei kwamba kwa wakati huu inaweza ikaja kampuni kuchimba mafuta kule kwa muda huu. Mafuta yale yaliyoko Zanzibar, na yapo, yatakaa vilevile mpaka pale ambapo watu wa Zanzibar watakuwa na Serikali yao wenyewe waliyoichagua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie katika maeneo ya madini. Wachangiaji wengi sana hapa wamezungumzia kuhusu madini. Moja katika madini ambayo yameonekana Tanzania hii ni madini ya *uranium*. Pamoja na umuhimu wa madini haya ambao ni pamoja na kuzalisha umeme, kama wanavyofanya wenzetu Afrika Kusini kule, pamoja na kutengeneza silaha za nyuklia, madini haya yanatoa mionzi hatari ambayo ni hatari kwa maisha ya watu. Kuna maeneo mengi ambayo madini haya yameonekana, kama maeneo ya Bahi yaliyopo Dodoma hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, namuuliza Naibu Waziri...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)



**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa. Tunaendelea, Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Edward Mwalongo, Mheshimiwa Cecil David Mwambe ajiandae.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu sana katika uchumi wa nchi yetu, Wizara ya Nishati na Madini. Nakushukuru wewe kwa kazi nzuri unayoifanya, pia nimshukuru Mungu kwa kutupa nafasi hata kufika mahali hapa siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mungu zaidi kwa jinsi ambavyo alimwongoza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumchagua Profesa Sopeter Muhongo katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Profesa hakika unaitendea haki sana Wizara hii. Pia niwashukuru wale wote ambao ni Watendaji Wakuu, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa REA Tanzania, Dkt. Lutengano Mwakahesya, Mkurugenzi wa *Geothermal* Tanzania na Watendaji wengine wote katika nishati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo mchango wangu nielekeze zaidi nikianza na umeme wa vijijini (*REA*). Mpango huu wa umeme vijijini hakika mwaka jana wengi wetu tumeokoka sana katika mpango huu wa *REA*. Tumeokoka kwa sababu pamoja na kwamba siyo vijiji vyote vimepata, naamini katika awamu hii ya III vijiji vingi vitapata umeme huu. Nikija katika Jimbo langu la Busokelo, Busokelo ni miongoni mwa Majimbo ambayo tumenufaika na mpango mzima wa *REA*. Pamoja na kwamba kuna changamoto za hapa na pale, kuna baadhi ya maeneo kama Lupata, ukienda Isoko, ukienda Mpata, ukienda na maeneo mengine ya Kilimansanga bado umeme huu haujafika lakini tuna imani kwamba vijiji 30 vilivyosalia, tunaamini katika mpango huu wa awamu ya III vitapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala zima la mpango wa umeme vijijini, kwa vile vijiji ambavyo vilikuwa awamu ya pili, tunaomba watendaji pamoja na wahusika wote vikamilike kabla ya Juni ili wananchi wale kwa sababu tulishawaaminisha kwamba watapata umeme, na walituamini, tunaomba kabla ya Juni kwisha waweze kupatiwa huo umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la madini. Mkoa wa Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo imebarikiwa sana katika nchi yetu ya Tanzania. Tuna madini ya aina nyingi sana, ukienda kule Chunya utakuta kuna *gold*, ukienda huku Ileje utakuta kuna madini, ukienda Kyela makaa ya mawe, ukija Busokelo, kwa hiyo tuna madini ya aina mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na madini aina ya *calcium* yanayopatikana pale Mlima wa *Panda Hill*. Mheshimiwa Waziri katika kitabu

chake haya madini sijayaona hapa, lakini naamini kwamba atatuma timu yake waweze kufanya *exploration* na *extraction* kule, basi wananchi wale watafaidi sana haya madini kwa sababu tunaamini hata utengenezaji wa mbolea aina ya *NPK* inatokana na madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hivyo tu, nikisoma kitabu cha hotuba na Waziri ameandika vizuri sana, *very technical*, ukurasa wa 62 kuna madini aina ya *niobium*, madini haya pia Mbeya yanapatikana na kazi kubwa ni kutengeneza vifaa vya elektroniki ikiwemo pamoja na *engine* za ndege tunaita *jet*, lakini pamoja na kutengenezea vitu mbalimbali, mambo kama kompyuta na simu. Kwa hiyo, tunaomba kama yataweza kuendelezwa, pamoja na kwamba upembuzi yakinifu ulishafanyika na utafiti umefanyika, sasa kazi kubwa iliyobaki ni kwamba yaanze kufanyiwa kazi kwa maana ya kuchimbwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujumuisha hotuba yake hapa atuambie kwamba ni lini hasa rasmi wananchi wa Mbeya, katika maeneo ya *Panda Hill*, Mbeya na Tanzania kwa ujumla watanufaika na haya madini ili waweze kuinua uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika suala la *geothermal* (jotoardhi). *Geothermal* ni umeme ambao unatokana na nguvu ama joto lililoko ardhini na Busokelo tumebahatika kuwa na sehemu inayopatikana hiyo *geothermal*. Kwa hiyo naomba nimshukuru Waziri kwanza kwa sababu nakumbuka siku ile alikuja, alifika katika eneo hili la Mto Mbaka na alituhidi kwamba mara tu baada ya uchunguzi ama baada ya utafiti kukamilika mwezi wa Septemba wataanza kuchoronga visima vya huko, kwa hiyo tunaomba asitusahau.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba pamoja na timu yake ya wataalam waje katika eneo hili kwa sababu wananchi wakati tunahimiza kwamba wasifanye maendeleo yoyote kwa sababu hili eneo litakuwa ni sehemu mojawapo ya kuzalisha umeme na sisi tutakuwa tunauza maeneo mengine, walisikiliza ile kauli kwa sasa hivi wanasubiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo *geothermal* pekee tu, katika Jimbo la Busokelo pia tuna gesi aina ya *carbondioxide*. Hii gesi imeanza kuchimbwa tangu mwaka 1984, lakini kwa bahati mbaya hata hivi sasa ninavyoongea tuna viwanda viwili, kimoja kipo Kanyebele na hii gesi inatoka Kijiji cha Mpata, lakini pia kuna kiwanda kingine karibu na Tukuyu Mjini kwa ajili ya gesi hii na gesi hii inatumika zaidi katika masuala mazima ya kwenye soda, kwenye bia na maeneo mengine ambayo yanasababisha vitu visioze wala visiharibike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya, kwa makampuni ambayo yamewekeza kule, kuna kitu tunaita *social responsibility* kwa maana ya jamii inayozunguka, huwa hawafaidiki na gesi hii. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, kwa

nguvu zako zote pamoja na watendaji wako wote kuisimamia vizuri gesi hii aina ya *carbondioxide* kwa sababu wananchi wanaona yanakwenda magari na kurudi kuchukua, lakini hawaoni wananufaikaje na hii gesi. Hii ni changamoto kubwa sana, kwa sababu nakumbuka kipindi tunaomba kura ni miongoni mwa mambo ambayo yalitusababisha tupate wakati mgumu sana. Kwa hiyo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri alizingatie hilo atakapokuwa anajumuisha hotuba yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala hilo, ukienda Kata ya Lufilyo kuna madini ambayo yanapatikana kule kwa ajili ya kutengenezea marumaru na ukiangalia Tanzania nzima hii, mara nyingi sana tuna-rely kwenye marumaru za ku-*import* kutoka China lakini kule kuna madini ya kufanya hivyo. Katika Kijiji hiki cha Kikuba, Kata ya Lufilyo, kuna maji ama maporomoko ambayo yanaweza yakasababisha umeme wa *Hydro Electric Power* kwa maana ya umeme wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo basi, tunaomba wataalam ama watafiti waanze kuja kuchungulia kule kwa ajili ya kuleta wataalam ili waweze kutuambia ni kitu gani pengine baada ya hapo kitafuata ili wale wananchi wasiangalie tu yale maji yanakwisha pasipo faida yoyote, naamini tukiwekeza katika umeme itatusaidia sana kama nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala zima la matumizi ya umeme. Mara nyingi sana tunasema umeme; naishauri Serikali tuanze kutoa elimu kwa jamii kwamba umeme huu siyo kwa ajili ya kuwasha taa, siyo kwa ajili ya kupiga pasi tu, siyo kwa ajili ya kuangalia TV ama runinga, tufikiri katika uwanja mpana hasa kwa maana ya kuleta viwanda vidogovidogo, vile vya kuchakata hata kwa mikono yao. Nafikiri umeme utakuwa na faida sana na REA hii itakuwa na faida sana kwa wananchi kama tutaanza kutoa elimu ya namna hiyo. Maana wengi wetu wanafikiri kwamba umeme ni kwa ajili ya kuwasha taa na pengine kuangalia vitu vingine, lakini kumbe umeme ni zaidi ya matumizi hayo. Nafikiri elimu hii ikiwafikia na kama Wizara watakuwa na mipango ya kutoa elimu hiyo kwa jamii itapendeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nizungumzie suala zima la Serikali kuhusika asilimia mia moja katika kuwekeza kwa maana ya nishati ya umeme. Umeme ni gharama kubwa sana, tunaomba Serikali kwa jinsi ambavyo wameshaanza kutafuta wadau wengine waendeleo hivyo hivyo. Hakuna Taifa lolote duniani ambalo kwa nguvu zao wenyewe wanaweza wakajitosheleza katika nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati nzuri nilipata nafasi ya kutembea Mataifa mengine duniani, kama Ujerumani, utakuta nyumba moja ya familia moja inakuwa na vyanzo vitano vya nishati ya umeme; utakuta kuna maji,

utakuta kuna *solar*, utakuta kuna umeme wa upepo utakuta kuna umeme wa *biogas*, *geothermal* na kadhalika, hata ukatika umeme wa aina moja, basi umeme wa aina nyingine ule una-*take up*, hivyo katika nchi yetu pia tuanze kufikiri katika mfumo huo, tusi-*rely* tu katika vyanzo vya umeme wa aina moja, kwa maana kwamba kuna gesi halafu pia kuna umeme wa maji, lakini pia tuanze kufikiri zile *energy* ambazo ni *renewable* kwa maana ya kwa mfano *geothermal*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *geothermal is an energy* ambayo inakuwa *renewable*, inaweza ikazalisha umeme na kuzalisha na kuzalisha, lakini tuki-*rely* katika umeme wa maji, sisi wote ni mashahidi hapa, kwa sababu wakati mwingine, kama kipindi cha miaka miwili iliyopita nchi yetu ilikuwa katika janga kubwa, kwa hiyo umeme ama mabwawa ambayo tunategemea yalikuwa hayatoi maji sawasawa kama vile ambavyo tulitegemea. Pia tukija katika gesi, gesi ile ukisha-*extract* hatutegemei tena kwamba itaendelea kuwepo vilevile kwa miaka na miaka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niunge mkono Wizara hii na hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Natumaini Mheshimiwa Waziri amelitilia maanani hilo hasa gesi ya Tukuyu. Tunaendelea, Mheshimiwa Edward Mwalongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil David Mwambe. (Kicheko)

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafsi nami niweze kuchangia hoja hii ya Wizara ya Nishati iliyopo mbele yetu. Kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na baada ya hapo nijielekeze kwenye suala la umeme vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Njombe Mjini tuna masikitiko makubwa sana, wengi wamesifia REA lakini Njombe Mjini tunasikitika kwa sababu hata kijiji kimoja hakijapata umeme wa REA. Utaratibu wanasema Njombe tunatakiwa kupata umeme kutokana na Mkandarasi anayetengeneza umeme kutoka gridi ya Taifa kwenda Songea. Mkandarasi yule anakumbwa na matatizo mengi tu, mara hana fedha, mara nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii hali inaleta sintofahamu sana kwa wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini na inasababisha hali ya siasa kuwa ngumu, lakini vilevile morali inapungua sana kwa wananchi wakisikiliza habari ya TANESCO na habari ya REA, wanaingwiwa na kasumba kwamba kwa sababu lile Jimbo linaitwa Jimbo la Njombe Mjini na umeme wa REA ni wa vijijini, kwa hiyo Njombe haimo. Kwa hiyo, naomba sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuwa

anakuja kufunga hotuba yake atuambie, Njombe tutapata lini umeme wa REA. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana TANESCO na REA kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa ajili ya umeme wa kupeleka kwenye kwanda kipya tunachotaka kukijenga pale Lwangu, Kiwanda cha Chai. Naomba sasa Wizara na TANESCO wasaidie, msimamo ambao tumekubaliana kwamba kazi ile inaanza mwezi wa Sita kweli ianze, kwa sababu tumeshapata mwekezaji kwa ajili ya chai, chai ile wakulima wale wameshalima haina kiwanda. Kwa hiyo, naomba sana Kijiji cha Lwangu kipelekewe umeme kutoka Kilocha ili chai ile ianze kusindikwa pale kwenye Kijiji hicho cha Lwangu na wananchi waanze kupata fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia kwa Jimbo la Njombe na kwa maana ya Mkoa wa Njombe ni Mchuchuma na Liganga. Kwa kweli Wanamkoa wa Njombe tunasikitika sana kwa sababu Mchuchuma na Liganga ni hadithi ya miaka mingi sana, juzi nimesema na leo narudia, kwamba kwa kweli *if we are serious* na maendeleo ya nchi hii, Ujerumani imeendelea kwa chuma, chuma ndicho kilichoendeleza nchi, sasa chuma cha Liganga ni hadithi tu miaka yote, chuma Liganga, chuma Liganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, wamefanya kazi ya kuchepusha madaraja wakisema madaraja yaliyopo ni madogo, mitambo haitaweza kupitia, madaraja yale safari hii yamesababisha matatizo, maji yamejaa yameshindwa kupita, kisa ni kwamba wamechepusha madaraja ili wapitishie mitambo, hakuna cha mitambo, majani yameota. Wale Waheshimiwa waliokwenda kule kwenye migodi inasemekana kwamba wamegundua kuna madini mengine, wameanza kuchenjua hayo, habari ya chuma wameachana nayo. Sasa tuambiwe na Wizara, Mchuchuma ipo ama haipo! (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine cha kusikitisha, Mchuchuma amepewa NDC. Watu wote humu ndani tunajua NDC ilivyo, hivi afya ya NDC ikoje jamani? NDC anaweza akachimba chuma! NDC haiwezi kuchimba chuma leo, uchumi wa NDC uko chini sana. Niwaombe sana Serikali muwe na maamuzi na kama mmesema kwamba Mashirika ya Hifadhi ya Jamii yaingie kwenye biashara inayoajiri watu wengi, migodi ile ya Mchuchuma na Liganga inatarajiwa kuajiri watu 30,000. Hayo Mashirika ya Hifadhi ya Jamii yapelekwe huko wafanye hizo kazi za kuchimba makaa kule Mchuchuma na chuma pale Liganga. Kwa hiyo, niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hotuba yake aseme chochote juu ya Mchuchuma na Liganga ili tujue msimamo ukoje. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu TANESCO Njombe. TANESCO Njombe wana shida kubwa sana. Wapo vijana wachapakazi sana pale, wanajitahidi lakini ukatikaji wa umeme kutokana na hali ya hewa ya Njombe, mvua nyingi na miti mingi, mara nyingi sana miti inaangukia nyaya, hawana gari za kutosha, wana gari moja TANESCO Njombe. Wasafiri kilometa 70 upande mwingine wa Jimbo la Lupembe kwenda kuangalia tatizo la umeme, wakitoka huko warudi Jimbo la Njombe Mjini waende mpaka Luponde tena kuangalia umeme, unaweza ukakuta siku mbili Kiwanda kama cha Chai Luponde kinakosa umeme kisa TANESCO hawana gari ya kuwafikia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini na wakubwa wa TANESCO watakuwa wanasikia maneno haya. Naomba wawasaidie wale wachapakazi vijana pale Njombe ili wapate gari lingine la kufanya service kwenye lane za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la viwanda. Sisi Njombe tuna viwanda, moja ya kiwanda tulichonacho ni Kiwanda cha Nguzo (TANWAT). TANWAT wameingia kwenye tenda ya kuomba ku-supply nguzo TANESCO, wamekosa. Ni jambo la kusikitisha sana! Masharti ambayo wameweka TANESCO na utaratibu waliouweka unasikitisha sana. Wametoa tenda hii South Africa tena ku-supply nguzo za umeme wakati Njombe kuna nguzo za umeme. Ni kweli inawezekana kiwango ambacho kinatakiwa ni kikubwa sana, ndiyo uwape South Africa shilingi bilioni 60 ku-supply nguzo TANESCO, halafu wazawa wananyimwa kwa kuwalambisha tu unawapa Sao Hill nguzo za shilingi bilioni 24!

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, kwa hili nitakwenda ofisini kwake tukae tuongee tuliangalie. Haiwezekani kabisa, kwa sababu nguzo hizi hawa Makaburu wata-supply kwa miaka mitatu, ina maana viwanda vyetu vile sasa havitakuwa na kazi. Nasi kama Watanzania tunasema tunataka nchi iwe ya viwanda, ni lazima tuanze ku-favour viwanda vya ndani. Kama haiwezekani hiyo, basi hata viwanda haitakaa iwezekane. Maana yake watakuja watu wa viatu, wataatengeneza viatu, tutasema viatu vya Tanzania vina udhaifu moja, mbili, tatu, havinunuliwi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, kama nguzo hizi kiwanda kile kimekaguliwa, ubora wa nguzo umekaguliwa, imeonekana kwamba ubora ni sahihi, kinachodaiwa ni kwamba hawana fedha, basi wangewapa hata kidogo tu ili wajijenge kiuchumi kesho waweze kuwa suppliers wazuri zaidi. Kwa suala la nguzo naomba niseme hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala haya yanayohusiana na suala la madini. Kule katika Jimbo la Njombe Mjini kuna mgodi wa madini katika Kijiji cha Uliwa. Mgodi ule ulisababisha ugomvi sana na wananchi kwa sababu tu leseni zilitolewa kwa watu wawili, wote wafanye utafiti katika eneo moja. Naomba sasa, kama utaratibu ndivyo unavyoruhusu, basi urekebishwe kwamba kama ni



leseni inatolewa kwa mtu mmoja na idara hii inayohusika na leseni iwe inatoa kwa utaratibu mzuri ili kusaidia wananchi wale wasiingie kwenye mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana, yuko mwekezaji mmoja yuko tayari pale kuchimba yale madini ya copper, basi mwekezaji yule apewe kibali aendelee na kazi kwa sababu anazunguka siku nzima, miaka inakwenda kazi haifanyiki; na wananchi wale hawajapata elimu ya kutosha kwamba je, ni utaratibu gani unatakiwa ufanyike ili waweze kupewa kitu kinachotakiwa, kama ni mrabaha wa kijiji au ni wa Halmashauri au wa nini. Matokeo yake ni kwamba wananchi wale wamesimama pale wanasema mwekezaji haingii na mwekezaji anasema nina leseni; na upande mwingine kuna sehemu kuna mwekezaji mwingine anasema naye ana leseni. Kwa hiyo, naomba sana Wizara isaidie uchimbaji wa yale madini katika Kijiji cha Uliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niseme nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecil David Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Kandege na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Nishati na Madini. Moja kwa moja nielekeze kwanza mchango wangu katika Shirika la Umeme la TANESCO. Mpaka sasa hivi tunafahamu TANESCO wana deni kubwa sana kutoka kwa wazabuni, lakini pia kutoka kwa watu mbalimbali. Namwomba Mheshimiwa Waziri watakapokuwa wanaleta majumuisho yao watueleze wazi wazi, kama kuna mpango wowote wa kukiongezea nguvu Kitengo cha Masoko cha Shirika la Umeme Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wale wamekuwa wakifanya kazi kwa mazoea. Nafikiri kama wanaamua kufanya kazi kibiashara, basi angalau wangukuwa wanazungukia kwenye maeneo ambako kuna ujenzi mpya unaendelea na wao kutafuta wateja badala ya wateja kuanza kuhangaika kwenda kwenye Ofisi za TANESCO kuomba wakaandikishwe. Hata hivyo, watu hao wanaokwenda Ofisi za TANESCO wakishalipa pesa yao kwa ajili ya gharama za kuunganishia umeme, hili zoezi linakuwa refu sana, wamekuwa wenye urasimu mkubwa sana watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii tunaiona zaidi katika maeneo yetu, ukifika maeneo ya Masasi, ukifika maeneo ya Ndanda, hasa zaidi maeneo ya sokoni, kuna watu wengi sana wamejiandikisha pale kupata huduma ya umeme, lakini sasa hivi ni miezi mitatu, miezi minne watu wale wanashindwa kupelekewa umeme ambao tayari wameshaulipia. Sasa TANESCO watueleze kama walikuwa tu wanatumia kiujanja ujanja kutaka kukopa pesa kwa hawa watu



wanaotaka kuunganishiwa umeme na hawawekewi umeme kwa muda, wakati masharti ni kuwapelekea. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia niseme, kwenye biashara ya mafuta, EWURA pamoja na tozo mbalimbali zilizopo kwenye biashara ya mafuta. Mfanyabiashara wa mafuta ni mtu amekuwa wa kuonewa sana kwa kipindi kirefu. Ukiangalia gharama za mafuta sasa hivi japokuwa zimeshuka kufikia sh. 1,600/=, lakini nyingi katika hii pesa inakwenda kwenye upande wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo za mafuta zinakadiriwa kufikia sh. 500/= mpaka sasa hivi na mfanyabiashara wa mafuta anapata tu pale sh. 200/=. Kwa hiyo, sh. 900/= ni gharama halisi ya mafuta. Kwa nini Serikali isione kuna haja ya kupunguza kodi mbalimbali zilizoko kule ndani ya mafuta hasa zaidi hizi tozo ili mwananchi aweze kununua mafuta kwa gharama nafuu zaidi tofauti na gharama iliyopo sasa hivi? Naamini kwa sababu umekuwa ukipata sifa nyingi na hili jambo unaweza kulichukulia hatua. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kusikitika kabisa niwaambie kwamba, katika eneo letu la Wilaya ya Masasi, suala la kukatikiwa umeme sasa hivi limekuwa kama *fashion*. Haipiti siku mbili, siku tatu, lazima umeme utakatika. Ukipiga simu TANESCO kutaka kufahamu kwa nini imekuwa hivyo, hata wenyewe wakati mwingine wanashindwa kujua sababu za msingi. Mara utaambiwa mikorosho imedondokea nguzo, mara utaambiwa miundombinu duni katika eneo hili kwa sababu iliwekwa kwenye miaka ya 1990.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa tufahamu wazi kabisa Serikali ina mpango gani kuweza kutubadilishia miundombinu katika eneo letu la Wilaya ya Masasi ili tuweze kupata umeme wa uhakika kwa sababu umeme huu unazalishwa katika maeneo yetu ya Mtwara na tumeambiwa kwamba unatumia umeme wa gesi lakini tuseme kweli, sisi hatufaidi umeme ule kwa sababu tunaupata kwa matatizo makubwa sana katika Wilaya zote zinazozunguka maeneo ya Masasi ikiwa ni pamoja na Nanyumbu na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Ndanda ndiyo kuna vichekesho, kwa sababu katika maeneo haya ndiko unakopita umeme unaokwenda kutumika maeneo ya Masasi, maeneo ya Nachingwea na maeneo mengine. Hata huko Ruangwa maeneo ya kwa Waziri Mkuu umeme wake unakatiza katika maeneo ya Jimbo langu. Wazee na vijana, watu mbalimbali katika maeneo yale walishawishiwa wadondoshe mikorosho yao, wengine wakate miembe ili zipite pale nguzo kwa ajili ya kuwaletea wao huduma za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimejaribu kumweleza mara nyingi tu hapo Mheshimiwa Waziri katika suala hili, lakini ni ajabu kabisa mpaka sasa hivi tunaingia katika hili Bunge la Bajeti, hakuna hatua zilizochukuliwa za moja kwa moja katika vijiji ambako nguzo za umeme zinapita katika maeneo hayo. Tunaomba tupewe taarifa ya vijiji vile. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Vijiji vya Chipite, Mkwera, Nanganga na maeneo mengine, umeme unapita juu ya vichwa vyao, lakini pale chini watu wale hawana umeme. Kuna wakati ulifika katika Kijiji cha Liputu, Mzee wangu mmoja pale alikuwa haoni umuhimu wa kuwa na zile nguzo shambani kwake, aliamua kuchoma nguzo moja moto. Bahati nzuri wakati huo alifikishwa Polisi, wakati ule Mheshimiwa Mkuu wa Kituo ana busara, kabla hajaamua kujiingiza kwenye siasa, walimaliza lile jambo *amicably* lakini yule mzee alikuwa haoni umuhimu wa kuwa na nguzo inayopita shambani kwake. Yeye alikuwa anatamani lile eneo alitumie kwa ajili ya kilimo na siyo kupitisha nguzo ambazo zinakwenda kunufaisha watu mwishoni mwa lile eneo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuweza kupunguza gharama, nafikiri wakati mwingine TANESCO ifikirie kuwa na njia mbadala. Kusingekuwa na haja ya kupitisha umeme maporini, badala ya umeme ule kuupitisha kwenye vijiji ambako wanakaa watu, vikakona vikaenda kule. Sisi tumeamua sasa hivi kufuata njia kuu moja kwa moja. Kusingekuwa na haja ya kupitisha umeme katika Kijiji cha Chigulungulu ambapo umeme ule sasa hivi unatakiwa uzunguke Namalembo ili kufika mpaka Msikisi wakati tayari kulikuwa kuna *shortcut* inayopitia katika Vijiji vya Chiroro na vijiji vingine katika Kata ya Msikisi ili kuweza kupata umeme katika maeneo yale. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashindwa pia kuelewa, pale TANESCO wanapokuja kutaka kuunganishia umeme nyumbani kwako, wao walikuwa na jukumu la awali la kuweka miundombinu iwakaribie watu katika maeneo yao ambako ujenzi unaendelea. Sasa hivi kunaonekana kuna mtindo wa TANESCO kuweka nguzo tu katika maeneo ya barabara. Utakapotaka wewe kuomba umeme ambaye ujenzi wako umemaliza, kiwanja cha tano kwenye mtaa wako, unaambiwa ulipie zile nguzo zote ambazo ziko pale barabarani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaomba kupata jibu, nguzo hizi mwishoni zinakuwa mali ya nani? Gharama zile nilizolipia mimi kuwekeza kwenye nguzo zile mwanzoni: Je, naweza nikarudishiwa na hili shirika baadaye watu wa hapa katikati ili kufika nyumbani kwangu wakishakuwa wamejenga katika maeneo yao? Tunaomba hili tupate jibu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilitoa taarifa katika Kijiji cha Chikundi, kuna Zahanati pale inatoa huduma nzuri sana kwa ajili ya akinamama kujifungua ili kuweza kupunguza mzigo wa akinamama wanaokwenda kujifungulia katika

Hospitali ya Rufaa ya Ndanda. Sasa hivi wana miaka mitatu, miaka minne inakadiriwa panatakiwa kupatikana nguzo kama kumi, kumi na moja; lakini wale Wamisionari wa Ndanda wamepelekewa *quotation* ya shilingi milioni 11 ili kuweza kuweka umeme katika ile Zahanati ya Chikundi ambako yule mama pale, Mkunga anajitahidi kuwasaidia akinamama kujifungua akiwamulika kwa tochi. Tunaomba sasa hapa tupate majibu moja kwa moja, mnaweza mkatusaidia vipi katika maeneo yale? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kinachochekesha zaidi, mimi napakana na Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Jimbo lake na baadhi ya maeneo fulani. Wanakijiji wengine wanatoka vijijini ambako ni mbali kabisa kufika kule kwa Waziri Mkuu, wanategemea kupata umeme kutokea katika upande wa Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji vya Chinongwe, Mandanga, Likwachu pamoja na Vijiji vya Mbecha, wale watu siku za Jumamosi wanafanya maandamano ya kuja upande wa Ndanda kununua *ice cream*, kwa sababu kule kwao wanakosa hata *ice cream*. Tumwonee Mheshimiwa huruma, tuhakikishe tunapeleka umeme katika haya maeneo ili watu waweze kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Ngamadani, pale pana gereza kubwa sana, lakini nako penyewe umeme unapita juu ya vichwa vyao. Pana wafungwa pale, pana Askari Magereza pale, siku wakija kupotea msiwalaumu lakini wanaishi kwenye mazingira magumu! Wanashindwa kuvuta maji kwa ajili ya kupeleka kwa matumizi ya wale Maafisa Magereza pamoja na wafungwa wao waliopo katika eneo lile kwa sababu ule mkusanyiko ni mkubwa sana. Tunaomba mtusaidie katika maeneo yetu, hatufahamu sisi tumewakosea nini nyinyi, lakini tunasema. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Chingulungulu na kwenyewe umeme unakatiza juu ya vichwa vya watu. Mnashindwa tu kupeleka *transformer* ndogo ikashusha umeme kwa ajili ya kuhudumia watu pale. Tungepata angalau *transformers* chache za KV 50 zingeweza kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea na Meneja wa TANESCO siyo muda mrefu, aliniambia makadirio ya nguzo 1,200, pamoja na *transformer* 30 litaweza kumaliza tatizo la umeme katika eneo letu; lakini mimi nishushe zaidi, hata mkitupa nusu ya hii tutawaelekeza sisi *alternative route* za kuweza kuwafikia watu kwa kutumia *transformer* moja katika vijiji viwili au vijiji vitatu ikiwezekana kwa sababu njia za mikato za kuelekea hayo maeneo sisi tunazitambua. Tulikuwa tukifanya kampeni katika hayo maeneo, kwa hiyo, tunajua vizuri. Hii pia itasaidia TANESCO kuweza kupunguza gharama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kata ya Chigugu, Vijiji vya Mbemba pale kuna zahanati kubwa sana, iko pale toka enzi za ukoloni, lakini mpaka sasa hivi hawana umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante. Nasubiri majibu ya Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwambe nilidhani unaunga mkono hoja. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Josephat Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratias Ngalawa.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ili nami nisije nikamaliza kama Mheshimiwa Mwambe bila kuunga mkono, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu, afya na uwezo wa kusimama jioni ya leo, niungane na Watanzania wenzangu na Wabunge wenzangu ili kuishauri Serikali katika kuhakikisha kwamba kasi ya maendeleo na hasa umeme inaenda kutendeka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kushauri kwa kuisaidia Serikali na hasa nimesikia hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri, akiwa anaelezea jinsi ambavyo bajeti imeongezeka kwa kiasi cha asilimia 50. Naomba nimkumbushe, hiyo asilimia 50 atakuwa amesahau shilingi bilioni 79, kwa hiyo, inapaswa iongezeke kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 50. Hiyo shilingi bilioni 79 iko wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma katika Sheria ya Bajeti na hasa katika uanzishaji wa Mfuko wa REA, fungu lile ni *ring fenced*. Maana yake ni nini? Pesa hiyo haiwezi kwenda kutumika kwa shughuli nyingine yoyote. Kwa mujibu wa sheria inatakiwa iende upande wa REA. Sasa nini kilichotokea? Serikali inawezekana walijikopesha kiasi cha shilingi bilioni 79 ambacho wana wajibu wa kuhakikisha kwamba kinarudi na kinaenda REA, kwa sababu lengo lake ni kupeleka umeme vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika kile ambacho ametaja kwamba ni ongezeko la asilimia 50, ukichukua na hii bakaa unayovuka nayo, naomba urekebishe vitabu vyako visome kwamba kuna shilingi bilioni 79 ambayo inapaswa iongezeke katika bajeti yako. Najua Serikali wamejikopesha na muungwana akikopa ana kawaida ya kulipa na Serikali hii inayoongozwa na CCM italipa ili dhana ya kuhakikisha kwamba umeme unafika kila vijiji Tanzania inaenda kufikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ambayo napenda kuchangia ni kuhusiana na suala zima la uzalishaji wa umeme. Ukimsikiliza Mheshimiwa Waziri, tunajipongeza tumezalisha umeme wa kutosha, lakini ukitazama *projection* tuliyokuwa nayo na nini ambacho tulitarajia kuzalisha, bado kasi yetu haitoshi. Tulisema kwamba tungezalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe pale Kiwira, ilikuwa tuzalisha umeme pale Mchuchuma, lakini haya yote hatujaweza kufanya. Ni vizuri Mheshimiwa Waziri anapokuja kumaliza hotuba yake, atuambie baada ya miradi hii kutofanya kazi, tunajielekeza wapi kwenye vyanzo vingine vya uhakika ili kasi ya kupata umeme wa kutosha kwa ajili ya kutosheleza Watanzania na kuuza kwa nchi jirani tunakwenda kuifikia? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimwongeze vyanzo vingine vya umeme, ukienda Mkoa wa Rukwa pale, kuna makaa ya mawe maeneo ya Namwere pale. Wachunguzi wanasema kwamba makaa yale yanafaa kwa kuzalisha umeme. Namwomba Mheshimiwa Waziri aelekeze nguvu kule. Kama haitoshi, maporomoko ya Kalambo, maporomoko ya pili Afrika baada ya *Victoria Falls* ambayo hayajatumika vizuri na Wizara ya Maliasili na Utalii, hebu tutumie chanzo hiki kwa ajili ya kuzalisha umeme na kazi ni ndogo tu. Kama imewezekana kuwa na mahusiano mazuri tukaanza kuzalisha umeme kule Rusumo, ni rahisi kabisa kwenda kwa majirani zetu Zambia kwa sababu yale maanguko yako mpakani mwa Tanzania na Zambia. Hebu tufanye utafiti, maanguko yale tutumie kwa ajili ya kuzalisha umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijielekeze upande wa REA. Tumeambiwa tunaenda REA Awamu ya Tatu, ni jambo jema. Hata hivyo, ni lazima tujitathmini; katika hii Awamu ya Pili tumenufaika sawa? Haiwezekani maeneo kama Wilaya ya Kalambo ilikuwa na umeme sifuri, halafu unaposema tunaenda Awamu ya Tatu bila kutazama huyu ambaye alikuwa na sifuri amepata nini? Naomba kuwe na *exception* katika mtazamo kabla hatujakwenda REA Awamu ya Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri na maeneo mengine ambayo umeme ulikuwa haujafika, barua nimepeleka ofisini kwake, kwa uchache tu nimtajie vijiji ambavyo vimetajwa kwenye barua niliyopeleka kwake, ni pamoja na Kijiji cha Mwazye ambako anazaliwa Muadhama Polycarp Pengo, hakuna umeme pale. Pia Kijiji cha Kazila, Kijiji cha Kamawe, Tatanda, Sopa, Ninga, Kanyezi, Musoma na vyote hivyo viko kwenye barua. Alikuwa Makamu wa Rais Mstaafu, akawaahidi wananchi; amekuja Mheshimiwa Rais, akatoa ahadi, naomba aende kutekeleza kabla hatujaenda hiyo awamu ya tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee suala la TPDC. Ukitaka kushiriki vizuri, lazima uwekeze ili katika mnyororo wa uzalishaji na utafutaji wa mafuta na gesi, Shirika letu la TPDC ambalo ni kwa ajili ya Watanzania wote liwe

na nguvu, linatakiwa liwekeze kwa maana ya mtaji. Ukisoma ile sheria, imeeleza kabisa kwamba ili uweze kushiriki, lazima uwekeze kiasi cha pesa ambacho kinatakiwa. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa kupitia Wizara yake tutazame kwa jicho la huruma, jicho la maslahi mapana kwa ajili ya Watanzania wote tuhakikishe kwamba tunawekeza vya kutosha TPDC. Hii itaondoa hii dhana ambayo watu wengine wamekuwa wakisema eti wagawane wao lakini Watanzania kwa ujumla wetu tusiwe na shirika letu ambalo ndiyo kwa ajili yetu sisi sote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, itasaidia sana, itaondoa kelele ambayo imekuwa ikijengeka kwamba eti mzawa ni kumjali mmoja mmoja. Hebu tujaliwe kwa ujumla wetu tuwekeze katika kampuni yetu kama ambavyo Mataifa mengine wamefanya. *Statoil*, lile ni shirika la Kiserikali, *Petrol Brass* ni shirika ambalo *part* ni Serikali na watu binafsi. Kwa hiyo, ni vizuri tuhakikishe nguvu hii tunapelekea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini haya machache ambayo nimeyaongea yamechukuliwa kwa uzito na yatafanyiwa kazi. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Mhagama, dakika tano na Mheshimiwa Goodluck Mlinga dakika tano.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuongea tena katika Bunge lako la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hoja zangu zinajikita katika maeneo machache sana kama mawili hivi au matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza kabisa ni juu ya *flagship project*, makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga. Kwa hiyo, tunapozungumza ni *flagship project* maana yake ni *project* ambazo zinatiliwa mkazo kwa kiasi kikubwa ili kuweza kuifanya nchi isonge mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, najikita kwanza kwenye fidia. Mradi hauwezi ukaanza kabla fidia haijalipwa na katika *valuation* ya ulipaji wa fidia, tunaona ripoti inasema wananchi wale wa Ludewa kwa maana ya Chuma na Liganga wanatakiwa walipwe shilingi bilioni 14. Hapo hapo nikijaribu kuangalia bajeti iliyokuwa imepangwa na Wizara hasa Wizara ya Viwanda inaonyesha ni shilingi bilioni 10.

Sasa nakuja kujiuliza swali la msingi, hii shilingi bilioni nne iko wapi? Kwa sababu katika majibu ya awali ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, pindi nilipokuwa nimeuliza swali tarehe 19 Aprili, tuliambiwa kwamba fidia inalipwa mwezi Juni, mwaka 2016. Kwa sasa tumebakiwa na muda mchache



sana kuifikia Juni. Tumbakiwa na kama siku kumi au kumi na moja Juni hiyo ifike.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa sababu tulishawaaminisha Wanaludewa kwamba tunalipa hiyo fidia na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri akasema miradi hiyo itaanza mwezi Machi, 2017, nikiwa namaanisha kwamba fidia hizo zitakuwa tayari zimeshalipwa, lakini bado napata utata mmoja, kwenye *strategic plan*. Kwa sababu naamini nilivyokuwa nimejibiwa kwamba hizi fidia zitalipwa mwezi Juni na mradi ule unaanza 2017 mwezi Machi, naamini kwamba ningeona kwenye ripoti. Ripoti ingesema kwamba mradi huu unaanza Machi, 2017 ili kutengeneza *assurance*. Tusipozungumza hivyo, bado mwakani tutakuja na hadithi hizi. Hatutaweza kum-pin Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala langu ni moja tu, tunapozungumzia *project, project* ina *time frame*. Kwa hiyo, mwisho wa siku ni lazima utueleze mkakati wako na namna utakavyoanza na maadam umeshatu-assure kwamba mwezi Juni, 2016 unalipa fidia, watu wa Liganga na Mchuchuma na Mradi unaanza mwezi Machi, 2017, kwa hiyo, ipo kwenye *plan* yako. Hiyo *plan* inapaswa na sisi tuifahamu. Bila hivyo, nasi inatupa matatizo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili la Mchuchuma, kwa mujibu wa wataalam na Wizara unatarajia kutupa umeme wa *megawatt* 600, kwa maana ya hii Mchuchuma coal. Kwa hiyo, naamini kuna haja sasa ya kutengeneza nguvu ya kutosha, huu umeme tuufanyie kazi ili uweze kuongeza kwenye pato la nchi, ili twende kwenye uchumi wa viwanda ambao tunataka.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachojua, kwenye *flagship project* kama hii, kuna maeneo mtambuka; kuna suala la VETA. Suala hili la VETA lilizungumzwa sana na hata kipindi hicho Hayati mtangulizi wangu, Marehemu Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mungu amweke mahali pema peponi, alilizungumza kwa kasi, aliliuliza ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano na majibu nakumbuka yalitolewa na Mheshimiwa Mhagama kwamba *feasibility study* ilishafanyika, michoro ilishakuwa tayari, hati ipo na inatakiwa kuanza kujengwa. Kwa maana ya kuwaandaa vijana kushiriki kwenye mazoezi maalum kwa maana ya kazi na mambo mengineyo ambayo yatakuwepo katika hiyo miradi ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijaribu kuangalia *documents* zetu ambazo sisi Wabunge tumepewa, hiki Chuo sasa hakipo kabisa. Kwa hiyo, inamaanisha kwamba hatuna maandalizi ya kutosha kwa sababu ile VETA ilivyokuwa imewekwa pale, ilikuwa ni kuwaandaa watu katika kazi za ufundi ili ku-support *operations* ambazo zinakwenda kufanyika ndani ya miradi hii mikubwa inayokuja.



Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu hii shughuli ni mtambuka na inashirikisha vitu vingi, naiomba Wizara ya Madini, Viwanda na hata na Wizara ya Elimu ambayo inashughulika na mambo ya ufundi, tukae pamoja kuhakikisha kwamba miradi hii wakati inaanza, basi tuanze vile vile maandalizi ya ujenzi wa VETA. Kwa sababu ni kitu cha muhimu na bahati nzuri Bunge lako Tukufu lilishaelezwa kwamba kile chuo kitajengwa. Kama hakitajengwa, lazima tupewe sababu za msingi, zimeyeyukia wapi? Kwa nini hakijengwi? Kwa sababu tulishawaaminisha watu VETA ilishaenda mpaka Shaurimoyo kwa ajili ya kutayarisha eneo; eneo walipata limepimwa hati ipo, michoro ipo na BOQ zote zipo, kwa nini hiki chuo kisijengwe? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hilo, kwa kweli tunapaswa tulifuatilie na madamu kwa sababu Serikali ilishasema na sababu za kujengwa zilikuwepo, naamini zile sababu hazijakwisha, bado zipo, kwa hiyo, kijengwe ili tuweze kutoa mafunzo kwa wanafunzi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala la Maganga Matitu Resources. Suala hili la Maganga Matitu Resources, hawa wako kwenye partnership na NCD.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE: DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, dakika tano; Mheshimiwa Goodluck Mlinga, dakika tano; atafuatiwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, dakika tano.

**MHE. KIZITO M. JOSEPH:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia muda niliopewa niende moja kwa moja, kwanza kutoa salamu za shukurani kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, ambaye majira ya jioni kuelekea saa moja, mvua zinanyesha, amechoka, amefanya kazi kutwa nzima Ludewa, anarudi anakwenda Songea Mjini, alikubali kuendesha mkutano Madaba. Wananchi wa Jimbo la Madaba hawataisahau ile taswira.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ile Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, alitoa majibu ya moja kwa moja ya tatizo kubwa la umeme la wananchi wa Madaba. Wananchi wa Madaba wanamshukuru na wapo pamoja naye katika safari hii ya kutekeleza majukumu aliyopewa na Mheshimiwa Rais. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna changamoto katika utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Waziri, lakini changamoto hizi zinahusisha zaidi

muundo wa utaratibu huo wa utekelezaji. Kwa utaratibu ambao Mheshimiwa Muhongo ameuweka, ni kwamba Madaba ifikapo Desemba tutapata umeme, lakini katika kipindi hiki cha miaka miwili Madaba Mjini patakuwa *hub* ya umeme unaotoka Makambako kuelekea Songea, lakini pia *hub* ya umeme unaotoka Mchuchuma na Liganga kuelekea maeneo mengine ya Taifa letu. Maana yake nini? Maana yake Madaba inakwenda kupitia *transformation* kubwa sana ya uchumi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto inayotupata kwa sasa ni kwamba Serikali bado ina ugumu kidogo wa kuchangia gharama kuweza ku-meet gharama za wafadhili kwenye hilo jukumu na kikwazo kinaonekana kipo Hazina. Naomba watu wa Hazina wasikalie pesa kama zipo. Kama pesa zipo na zimepangwa kwa matumizi hayo, basi zitolewe zikafanye hizo kazi ili hizi Wizara husika ziweze kujibu matatizo ya wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kwenye hili tu kwa sababu linanigusa na wananchi wa Madaba lina wagusa sana. Ndani ya Jimbo langu la Madaba ni kijiji kimoja tu cha Lilondo kina umeme na umeme huu ni wa wananchi. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Mwijage, ambao kwa namna moja au nyingine wamesaidia sana kupatikana ule umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo yote ya Jimbo la Madaba, Vituo vyote vya Afya, saa hizi mimi Mbunge kwa kutegemea posho ninazopata hapa Bungeni, naweka *solar*. Hata ukiangalia gari ninayoitembelea ni ya kawaida sana ili niweze kubana matumizi ya kupata *solar* kwa ajili ya Vituo vyote vya Afya. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na wananchi wa Jimbo la Madaba wanaomba sana kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Sospeter Muhongo, kwamba yale ambayo ameyapanga wanamwomba Mwenyezi Mungu amjalie nguvu ili ifikapo Desemba na kuendelea changamoto hii iwe imekwisha. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo miradi ya kielelezo ya kiuchumi. Ndugu yangu...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. KIZITO M. JOSEPH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga dakika tano, Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae na Mheshimiwa Ester Bulaya dakika tano.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. UKAWA naona mnashusha pumzi, kuweni na amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Waheshimiwa Wabunge, Jimbo langu la Ulanga na Wilaya nzima imebarikiwa kuwa na madini ya kila aina kasoro *tanzanite*. Isipokuwa shida kubwa tunayoipata, wanasema mbega aliponzwa na uzuri wake, ndiyo shida kubwa tunayoipata Jimbo la Ulanga. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini, imejitenga kabisa na wananchi wa Tanzania. Wao wamekuwa madalali. Wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na Madini wanatembea na ramani za madini ya nchi hii makwapani, kazi yao kubwa ni kutafuta wawekezaji, wanawapa leseni, hawajali pale wanaishi watu; hawajali wale watu wanatakiwa wafidiwe na kama hata ni kufidiwa ni shilingi ngapi? (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, mtakubaliana na mimi, nendeni sehemu zote ambazo kuna uchimbaji mkubwa wa madini, watu wa pale wanaishi maisha duni sana, malalamiko makubwa sana yamejaa pale. Mheshimiwa Waziri nakuamini, Profesa maana yake ni mtu wa *research*, fanya *research*, haya yanatokana na nini? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeongea hivyo Mheshimiwa Muhongo, anajua namaanisha nini? Katika hotuba yake ame-specify kuna miradi mikubwa ya madini ambayo inatakiwa ianze; madini ya *graphite* ambayo katika Tanzania yako sehemu mbili; Ulanga na Ruangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo wale wawekezaji waliowapa leseni wameshakuja kule wanataka kuwahamisha watu. Mheshimiwa Waziri ametuma watu wake waje kule waangalie: Je, kuna umuhimu wa wananchi kuhamishwa au la? Wananchi wamelalamika, watu aliowatumia wamesema wamempa ripoti, wamesema watu hawatakiwi wahamishwe, Mheshimiwa Profesa Muhongo suala hilo limekwenda kwake, lakini bado ana kigugumizi. Kwa nini anashindwa kutoa kauli? Kuna nini katikati hapa? Wananchi wangu hawana amani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie, hii Wizara ya Nishati na Madini mwaka 2010 ilitoa hadi leseni ya Waziri mwenzao ilimpa mbia afanye uchimbaji wa madini kwenye nyumba ya Waziri mwenzao, Marehemu Mama Kombani. Hii Wizara ya Nishati na Madini ilitoa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ikampa mwekezaji achimbe madini; ilitoa Mahakama ya Wilaya; ilitoa eneo la wakazi zaidi ya

15,000, imempa mwekezaji achimbe; yaani hawajali, wanapotoa hawaangalii kama kuna watu wanaishi. Mheshimiwa Muhongo naomba alifanyie kazi. Wale wawekezaji aliowapa leseni, hawawezi kuchimba *graphite*, labda wakachimbe Jimboni kwake, lakini siyo Ulanga. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, napenda kuongelea suala la umeme. Umeme unazalishwa Kidatu tangu mwaka 1970. Kutoka Kidatu kwenda Ulanga ni kilomita 150. Imechukua miaka 20 Ulanga kupata umeme. Hata sasa hivi, umeme upo, kwa wiki unawaka mara moja. Mheshimiwa Profesa Muhongo, nilimwambia akatoe zile fito, aweke nguzo za kupitishia umeme. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu, Waheshimiwa Wabunge kuna jipu. Mheshimiwa Profesa Muhongo nimeshamwambia zaidi ya mara mbili, kuna hii sheria iliyopitishwa mwaka 2015 ya uagizaji mafuta kwa pamoja. Hiyo sheria inampa mamlaka Waziri ku-*declare* mafuta ya *on transit* yatumike nchini.

Hebu Waheshimiwa Wabunge fikirieni, imepaki meli pale ina mafuta lita laki tano; Waziri anaidhinisha yatumike nchini. Yale mafuta huwa hayalipiwi kodi, halafu sheria inampa nguvu Waziri kusema yeye ndio ataamua, yaani *emergency condition* ambazo yeye ata-*declare*. Sasa hiyo *emergency condition* hawajasema kuna sheria, yaani Waziri kichwani mwake siku hiyo kaamka kasema *emergency condition* leo ni hii, ana-*declare*. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Muhongo asisubiri aje aongee Mheshimiwa Zito hapa, asisubiri aje aongee Mheshimiwa Godless Lema, ni mimi Mlinga nafagia nyumbani, sawa! Naomba wakati anahitimisha aseme, la kwanza, kiasi gani cha mafuta ambacho amesha-*declare* cha *on transit* kitumike Tanzania? Kiasi gani cha kodi ambacho kimeshalipwa na ni lini analeta sheria hii tuifanyie marekebisho; hatuwezi tukamwamini. Dhamana yetu hatuwezi tukampa yeye. Mheshimiwa Profesa Muhongo, mimi leo sina mengi, ni hayo tu yanamtosha. (Kicheko/Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya dakika tano na Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae dakika tano.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nashukuru sana kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu liko mpakani kabisa mwa Zambia na Tanzania. Ni Jimbo ambalo ni lango kuu la nchi za Kusini na kati mwa Afrika. Jimbo la Tunduma linakuwa na wageni wengi sana ambao wanatoka nchi mbalimbali; *South Africa*, Botswana, Zimbabwe, Congo, Malawi na Zambia. Cha kushangaza katika Serikali yetu hii huwezi kuamini, Mji wa Tunduma hauna

umeme wa kutosha kabisa. Wageni wengi katika Mji wa Tunduma sasa hivi wanakwenda kulala Zambia kwa sababu ya kuhofia usalama wao kutokana na giza kubwa linalokuwepo katika Mji wa Tunduma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimshauri tu Mheshimiwa Waziri wakati anakuja hapa atuambie, ni lini Tunduma tutapata umeme wa kutosha ambao utasaidia kuwavutia wawekezaji na watu wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ili waweze kutumia gesti zilizoko Tunduma na kuweza kukaa katika nyumba ambazo tumezijinga katika Mji wetu wa Tunduma kuliko kuwa na giza katika mpaka wetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa sana kwa nchi kama Tanzania ambayo sasa mpaka wa Tunduma ni mkubwa unaoingiza fedha nyingi. Miezi sita tu ulikuwa umeingiza karibuni shilingi bilioni 22 kwenye mpaka wetu wa Tunduma. Huwezi kuamini, hata maji Tunduma pale, imefika mahali mashine zetu za kuvutia maji kila siku zinakufa kwa sababu ya umeme kuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka Mheshimiwa Waziri atuambie leo, kwamba ni lini atahakikisha umeme wa pale utakuwa vizuri? Kama wameshindwa kuleta umeme Tunduma, tuna *transforma* pale upande wa Zambia, miaka ya nyuma tulikuwa tunatumia umeme wa Zambia. Tunaomba watuunganishe na umeme wa Zambia ili wananchi wetu wa Mji wa Tunduma waweze kuwa na umeme masaa 24. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mitaa mingi sana kwenye Mji wangu wa Tunduma haina umeme. Mitaa hiyo ni Namole, Msambatuu, Chiwezi na Mtaa wa Niumba, hawana umeme kabisa. Tunavyozungumzia mitaa, ina maana ni maeneo ambayo yako mjini, lakini huwezi kuamini, hakuna umeme kabisa. Wananchi wanalima vizuri, wanazalisha, lakini wanashindwa kupata huduma muhimu za umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, atuambie, ni lini atahakikisha kwamba wananchi hawa, maeneo ambayo nimeyataja wanahakikisha kwamba wanapata umeme kwa kipindi hiki ambacho tunacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia imekuwa ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu, kwamba katika Wilaya zetu ambamo wamepelekwa Mameneja wa Wilaya, wamekuwa wanalalamikiwa sana na wananchi katika maeneo yale, kuna mambo ya msingi sana ambayo ilitakiwa Wizara ifanye, lakini imefika mahali wanashindwa kufanya kwa sababu fedha ambazo zinakuwa zimepangwa kwenye bajeti kwa ajili ya kuweka umeme, unakuta fedha zile hazifiki. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sana, tunapotengeneza bajeti hapa Bungeni na tunapitisha, tunaomba hizi fedha ziende katika maeneo hayo ili zikawatumikie wananchi, waweze kupata huduma ya umeme. Kitendo cha kutengeneza bajeti hapa halafu baadaye bajeti zile zinashindwa kuwafikia wananchi kama tulivyokuwa tumepanga, ni kurudisha maendeleo nyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukubaliane kabisa, hakuna nchi yoyote inaweza kupiga hatua kama nguvu ya umeme katika nchi hii itakuwa chini kiasi hiki. Wananchi wengi sana wamejiajiri, hasa vijana, wamejiajiri, wanachomelea, wana viwanda vidogo vidogo, lakini vile viwanda sasa hivi vimeanza kufa na wameshindwa kufanya kazi hizo kwa sababu ya kukosa umeme katika nchi hii. Tunaomba nchi hii iachane na mazoea ya kutoa ahadi ambazo hazitekelezeki; wawe na muda mzuri wa kutekeleza na kufanya mambo ambayo yanaweza yakawasaidia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Tunduma nimeshamwambia Waziri wa Uchukuzi, Waziri wa Maji na sasa namwambia Waziri Profesa Muhongo, wahakikishe kwamba wanaleta umeme na huduma zote za kijamii kwenye Mji wa Tunduma kwa Wizara zote, zinapatikana pale kwa sababu sisi ndio tunaolinda Bandari ya Dar es Salaam. Bandari ya Dar es Salaam asilimia 60 ya mzigo unapitia kwenye mpaka wa Tunduma. Kwa hiyo, tuna....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, dakika tano.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii nami kwa dakika chache niweze kuchangia Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa, ningependa Mheshimiwa Waziri atupe *status* ya umeme nchini ikoje? Kumekuwa na tatizo la umeme kukatika mara kwa mara. Tuliambiwa hakuna mgao, je, mgao umerudi kinyemela? Hapa Dodoma peke yake umeme ulikuwa unakatika kila Jumapili kuanzia asubuhi unarudi saa 12.00. Siku hizi unarudi saa 9.00 kwa sababu Wabunge tupo Dodoma. Tunaomba hilo utuambie. Pia atujibu, kwenye fedha hizi za umeme, kiasi gani kinaenda katika kumalizia viporo? Kiasi gani kinaenda kwenye miradi mipya? Hilo pia tunaomba atufafanulie, siyo hivi tu kama ilivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wale asilimia 30 tuliorudi humu ndani, mwaka 2015 nilipokuwa nikichangia Wizara ya Fedha,



nilisema fedha zilizopaswa kwenda REA zimeenda kutumika kwenye matumizi mengine. Nilisema, Waziri kama huyo anaweza aka-survive kwenye nchi yetu. Kavunja Katiba, kavunja Sheria ya Bajeti, kavunja kanuni za nchi! Leo athari tunaiona hapa, miradi ya REA Awamu ya Pili haijatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti anasema, shilingi bilioni 70 ilikopwa, Serikali yetu sijui nini! Imevunja taratibu, hapa hakuna kutafuna maneno, wamekwenda kutumia fedha zilizokuwa kwenye *ring fence*. Maana ya kuwa kwenye *ring fence*, hazipaswi kutumika kwenye matumizi mengine. Leo tutamnyooshea kidole Mheshimiwa Muhongo wakati hatukumpa hela, watu wamekwenda kunywa chai na maandazi huko ofisini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliyasema haya mwaka 2015 nikiwa Chama cha Mapinduzi. Leo Makamu Mwenyekiti wa Bajeti ameyasema. Tunapozungumzia haya jamani, kwenye mambo ya muhimu ya kuondoa Taifa letu kwenye giza, kweli tumeshindwa kuchukua maeneo mengine, tunaenda kuchukua fedha zilizowekewa uzio? Leo hapa kila mtu akisimama, vijiji vyangu vya Awamu ya Pili havijakamilika. Hakupewa hela. Pesa zimekwenda kutumika kwenye matumizi mengine. (Makofi)

Nawahakikishia Waheshimiwa Wabunge ambao mmeingia sasa hivi, kama tusipoibana Serikali, huu utaratibu ukiendelea, Bunge lako Tukufu linapitisha fedha, Serikali inaenda kutumia kwenye matumizi mengine, hatuwatendei haki wananchi. Tukatae Bunge hili kuwa *rubber stamp*, tuseme mwisho, tuazimie pesa za REA, ile trilioni moja tunayoipitisha hapa iende, mwakani tuzungumzie mambo mengine tena, siyo umeme vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya hayana Chama! Wabunge wengi nyie tunatoka vijijini huko, tunajua hali halisi ikoje. Mimi Jimbo langu la Bunda Mjini, baba yangu alikata Kata saba vijijini alijua zitamsaidia na ndiyo nimemchapa. Kata saba ziko vijijini kule, nataka umeme uwake. Kaleta Kata saba Jimbo la mjini, nimemkunguta huko ndiyo nimemshinda vibaya hajaambulia hata Kata moja! Ndiyo nasema hizo zote ziwake umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Babu yangu, hapa hakuna cha viwanda kama hakuna umeme. Halafu tunazungumza mambo kama haya, Waziri wa Fedha hayupo! Hayupo! Lazima awepo! Mambo ya msingi kama haya, mwenzake alikula, hakupeleka fedha. Tunahitaji fedha hizi tunazotenga kwa mambo yanayogusa maisha ya Watanzania. Leo Vijiji vyangu kule vya Kangetutya, Kamkenga, Guta, Nyamatoke, Miale kote huko kuwe na umeme. Sasa leo shilingi bilioni 70 zile hazikwenda, halafu tunaongea lugha nyepesi eti Serikali umekopa hela iliyokuwa kwenye *ring fence*! *This is the shame*. Mpeni pesa Mheshimiwa Muhongo tumalize biashara ya kusambaza umeme vijijini. Sasa tunakula bila



kunawa halafu tunakuja kufanya kazi tena ya kupitisha kumaliza viporo hapa! Bunge letu lazima liwe kali kwa maslahi ya Taifa. Hii tabia iwe mwisho! *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri kingine, Jimboni kwangu Kata ya Kabasa Kung'ombe kuna mgodi pale. Naomba tutembelee ule mgodi, wanafanya kazi katika mazingira hatarishi. Kwanza hauwanufaishi wananchi wa Kata ya Kung'ombe lakini mazingira yale siyo mazuri, hawafuati taratibu, kemikali zinawaumiza wananchi wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine pale kwenye Kata ya Mjini, umeme kwa wananchi ni shida, gharama kubwa, wananchi wa Bunda masikini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Tunaendelea. Mheshimiwa Richard Philip Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Boniventura Bunda.

Waheshimiwa Wabunge, Waziri asipokuwepo humu ndani ni kwamba yupo kwenye majukumu mengine. Waziri wa Bajeti anatarisha bajeti ambayo ataisoma wiki mbili zijazo. Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupata nafasi hii. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kuweza kuandaa bajeti na kusimamia Wizara kiujumla. Kwa sababu dakika ni tano, naomba kwa ufupi tu niseme kwanza suala la wachimbaji wadogo wa madini ambao wapo katika Jimbo langu la Nsimbo, Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya kuna watu wanaopewa leseni ambazo ni ndogo *(Primary Mining License)*, wamekuwa wakishirikiana vizuri na wananchi katika uchimbaji wa madini, lakini pale inapotokea mtu anapopanda daraja anaenda leseni kubwa, *(Mining License - ML)* anakuwa sasa na masharti magumu ya kushirikiana na wananchi katika uchimbaji wa madini. Hii imepelekea kuwa na mgogoro mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mfano mzuri, mwaka huu imetokea Kampuni ya Sambaru, imeweza kuingia kwenye mgogoro na wananchi wa Kijiji cha Ibindi mpaka ikahatarisha amani. Sasa ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri; tuna takriban vijiji 10 ambavyo wananchi hawa ndipo wanapata kipato. Tunaomba maeneo haya yawe ni kwa ajili ya wachimbaji wadogo tu na tusiweke uchimbaji mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunasema hivi? Maeneo haya yapo kilometa 15 mpaka 20 kutokea mjini na ndiko ambako inapatikana dhahabu.

Watu wanachimba na uchimbaji wao mdogo mdogo na wanaweza kukidhi maisha yao ya kila siku; kulipa ada na vitu mbalimbali katika maisha. Sasa tukiwekea namna hii, itakuwa inapelekea mgogoro na kuhatarisha amani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile katika mlolongo mzima wa kazi za Wizara, tumewahi kupata taarifa, kuna ule ufadhili wa *World Bank* kwenye kusaidia wachimbaji wadogo wadogo tu, ufadhili takriban Dola milioni nne. Sasa katika vile vituo saba vya mfano, namwomba Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo, maeneo ya Jimbo la Nsimbo yawe ni moja ya Kituo cha mfano katika hivyo vituo saba ambavyo vitapata msaada wa Benki ya Dunia katika huo ufadhili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile wachimbaji wadogo wana malalamiko kuhusiana na gharama za upande wa Wizara ya Maliasili na Utalii. Gharama kwa hekta moja ni takriban sh. 1,500,000/= kwa mtu ambaye ameingia kufanya machimbo maeneo ya hifadhi ya misitu. Wakati huo huo, kwa hekta moja kwa upande wa madini, analipia sh. 80,000/=. Sasa imekuwa inawawia ngumu kuweza kukidhi hizi gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba Wizara hizi mbili zikae kwa pamoja ziweze kuona namna gani hizi gharama zinapunguzwa ziendane na uhalisia wa uharibifu unaotokana na uchimbaji. Ni mara kumi zaidi watu wachajiwe kulingana na miti ambayo imeharibika kuliko kuchukua tu eneo wakati watu wengine wanachimba hata miti mingi anakuwa hajaikata. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa awamu ya II ya REA. Nashukuru Jimbo langu Kata nne zimeweza kupata umeme, lakini bado Kata nane. Kwa hiyo, naomba katika hii Awamu ya Tatu, ule upembuzi yakinifu ambao tayari umeshafanyika, wasiruke vijiji. Maana kuna vijiji vingine wamepitisha umeme lakini hawakuweka zile *transformer* na wenyewe waweze kufaidika na umeme huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura, halafu Mheshimiwa Mendrad Kigola ajiandae. Kama hayupo, Mheshimiwa Mendrad Kigola, tutamalizia na Mheshimiwa Bashe.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru sana kwa kunipa nafasi nichangie. Nami natoa pongezi sana kwa Waziri Muhongo kwa kazi nzuri aliyoifanya mwaka uliopita. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba tena amerudi kwenye Wizara hii muhimu. Wabunge wengi

sana wakisimama wanaomba umeme vijijini na tuna matumaini makubwa sana kwenye Awamu hii ya Tatu vijiji vile ambavyo vilikuwa vimebaki kwamba vitapewa umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kutoa ile *service charge* kwa sababu ilikuwa ina-discourage sana wananchi, lakini Serikali ilitangaza kwamba imetoa *service charge* kwa hiyo, wananchi saa hizi nadhani hata bei ya umeme imeshuka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, nashukuru sana kwa kupunguza gharama za umeme hasa kwenye *installation* kwenye nyumba zetu. Hii italetu nafuu sana wananchi waweze kuingiza umeme kwa urahisi kwenye nyumba zao. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni masuala ya gesi. Naiomba Serikali, gesi isiwe mijini tu, hata watu wa vijijini wanahitaji kutumia gesi. Hata mwaka 2015 niliongea kwamba inabidi elimu itolewe kwa wananchi kuhusu matumizi ya gesi. Sasa na gharama kubwa sana; ukienda kununua au kubadilisha mtungi wa gesi unakuwa na gharama kubwa sana. Naomba Serikali ifikirie masuala ya gharama ya gesi. Tunasema kwamba wananchi wasitumie mkaa, mbadala wake watumie gesi, lakini gesi bado vijijini haijafika. Naiomba Serikali iweze kupeleka gesi vijijini. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine, kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini kuna vijiji vingi havijapata umeme. Ni asilimia 37 tu ambavyo vimepata umeme. Naomba kwenye Kata ya Mtambula, Idunda, Kiyowela, Luhunga, Mninga, Kata zile zote pamoja na vijiji vyake; kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini nina vijiji 88. Kati ya vijiji hivyo kuna vijiji 50 havijapata umeme.

Sasa tunapopeleka umeme vijijini, naiomba Serikali kuwaambia wale Makandarasi, umeme unapelekwa kwenye kaya za watu, siyo kwenye barabara. Unaweza kuona umeme upelekwa lakini bado haujaenda kwenye Vitongoji. Kwa mfano, mimi kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini, nina vitongoji 365. Kati ya vitongoji hivyo kuna vitongoji karibu 200 havijapata umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, umeme upelekwe kwenye vitongoji ili wananchi waweze kupata umeme. Kwa mfano, pale Malangali nashukuru kwanza REA wamepeleka umeme, lakini mpaka leo haujawaka na *transformer* wameshaweka tayari. Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani nilikwambia, kwamba wananchi wa Malangali hata sasa hivi wamenandikia *message*; Kata ya Malangali, Mbalamaziwa na Kwatwanga kule Kata ya lhohanza, umeme haujawaka lakini nyaya zipo pale. Kwa hiyo, watu wameangalia nyaya tu, umeme upo pale. Namwomba Naibu Waziri hili alichukulie kiundani zaidi, awashe umeme pale wananchi waanze kufaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kuna vijiji vingine wanaangalia nguzo za umeme zilipitishwa miaka ya nyuma, kwa mfano Kijiji cha Lugolofu, nyaya zimepita tu juu pale, kwa hiyo, ina-discourage sana, wananchi wanalinda nguzo. Siku moja waliniambia tutashangaa wamekata nguzo zile zimedondoka chini, sasa itakuwa imeleta tatizo kubwa. Kwa hiyo, naiomba Serikali, vile vijiji ambavyo vinalinda nyaya, hebu muwapatie umeme basi na wenyewe wafaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine katika Jimbo langu la Mufindi Kusini, kuna Mto Nyalawa, tulifanya *research*, kuna maporomoko makubwa sana pale. Tungepata umeme kutoka katika Mto Nyalawa halafu tungeweza kupeleka kwenye vijiji vingi sana kwenye Jimbo langu la Mufindi Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, kwa sababu muda ni mdogo, naunga mkono hoja. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, dakika tano; na Mheshimiwa Waziri Mwijage ujiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Jambo langu la kwanza kabisa, kwa dhati namshukuru Waziri wa Nishati na Madini. Namshukuru kwa kuonesha nia ya kushughulikia tatizo lililoko Katika Jimbo la Nzega la wachimbaji wadogo na chuo cha MRI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri na naomba AG ampe nafasi ili aweze kusikia hili tatizo Mheshimiwa Waziri, kwamba agizo alilolitoa Mheshimiwa Waziri la kumtaka mchimbaji aliyeingia kinyume na utaratibu, aliyeingizwa na MRI katika eneo la *Resolute* na mwezi mmoja aliopewa, pamoja na Waziri kupeleka *delegation* kubwa akiwepo Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Kamishna wa Madini, yule mtu mpaka leo anaendelea na uchimbaji ndani ya eneo la Mgodi wa *Resolute*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niliongea na Naibu Waziri Kalemani na tulishauriana juu ya *solution* ya jambo hili. Nataka niitahadharishe Serikali, *tension* iliyoko katika eneo lile, ni *tension* kubwa. Kwa hiyo, nashauri Waziri awaagize wataalam wake, yule mtu atoke ndani ya lile eneo kwa sababu *perception* ya wananchi juu ya lile eneo siyo jambo zuri sana. Hilo ni jambo la kwanza. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, Mheshimiwa Waziri anafahamu, nami nashukuru amenipa *commitment*, miradi ya umeme iliyokuwa inafadhiliwa na MCC katika Jimbo la Nzega kwa maana ya mradi wa umeme wa kutoa umeme Nzega Mjini kupeleka Kitangili, kutoka Kitangili kwenda Migua; kutoka Migua kwenda katika Kata ya Mwanzoli, Kijiji cha Kitengwe. Naomba

tuhakikishiwe wananchi wa Nzega kwamba mradi hii iliyokuwa inafadhiliwa na MCC itaingia kwenye REA Phase III, kwa sababu kuna upungufu mwingi katika miradi ya REA Phase II katika Jimbo la Nzega. Kwa hiyo, naomba Serikali itoe *commitment* katika jambo hili. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka niseme katika hotuba ya Waziri, wazo la *East African Countries* kununua *share* kwa ajili ya kushiriki katika mchakato *refinery* kwenye *project* ya uzalishaji wa mafuta katika nchi ya Uganda, mradi huu ni jambo muhimu sana. *Strategically* ni muhimu kwa sababu maisha ya Watanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki, gharama za mafuta zitashuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Muhongo ni jambo la kuisukuma Serikali na sisi Wabunge tumsaidie ili Serikali ya Tanzania iweze *play part* yake ili tuweze kupata *shares* zetu katika mradi huu na Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sababu *economically* litatusaidia sana jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, Waheshimiwa Wabunge, nimesoma hotuba ya ndugu yangu Mheshimiwa John Mnyika, kwa heshima Kabisa, tunajua suala la *ESCROW* mna hoja ya kumhusisha Waziri Muhongo, ni kutaka kumfanya kondoo wa kafara katika jambo hili. Naomba Bunge hili lisifanye makosa ya Mabunge yaliyopita kushughulika na watu dhaifu na kuacha msingi wa matatizo. *We all know* katika mioyo yetu suala la *ESCROW* kama *beneficiaries* wakubwa wa *ESCROW* wapo, wanajulikana. *If we real want to deal with it*, tuwafuate hao, lakini tumwache Mheshimiwa Profesa Muhongo atimize wajibu wake. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja ahsante. (Makofi)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Bashe.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ALLY S. UGANDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kumpongeza Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo na Naibu wake Waziri Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Kalemani na Katibu Mkuu wa Wizara Profesa James Pallangyo Justin William Ntalikwa kwa kazi nzuri ya kuhakikisha wanawapatia Watanzania umeme kwa kuzima kibatari majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, sina budi kushukuru katika Jimbo langu la Kibiti vipo baadhi ya vijiji tumeshapata umeme kwenye *phase I* ambapo ni 18 kati ya 40. Vijiji hivyo ni Kibiti, Nyamisati, Mchukwi, Mlanzi, Mahenge, Bungu, Songa na vinginevyo lakini umeme wake bado unasumbua wakati wote. Naomba Serikali yangu sikivu ya Chama Tawala kuliangalia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji ambavyo umeme umefika lakini bado haujawaka. Vijiji hivyo ni Mwangia, Mngaru, Kimbuga, Miwaga, Ngulakula, Uponda Uchembe na Jaribu Mpakani. Vijiji hivi miundombinu ya umeme imekamilika lakini bado kuwashwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji ambavyo havifanyi vizuri katika suala zima la ukandarasi na miundombinu yake haiendi kwa kasi. Wakandarasi katika maeneo haya kazi zao zimesimama kwa muda mrefu. Naomba wananchi wa Jimbo la Kibiti tuelezwe tatizo ni nini. Vijiji hivyo ni Nyamatanga, Rungungu, Ruaruke Kikale, Mtunda na Muyuyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, fidia ya mradi wa umeme wa kilowati 400 toka Somanga - Dar es Salaam – Kinyerezi. Lipo tatizo la fidia katika mradi huu kwani cha ajabu yapo maeneo wameshalipwa lakini katika Jimbo langu la Kibiti bado kabisa. Naomba majibu kutoka kwa Waziri mwenye dhamana fidia hii tutalipwa lini na tutalipwa kwa kiwango kile au tutafanyiwa tena *valuation* mpya kwani umeshapita muda mrefu. Maeneo ambayo wameshafanyiwa malipo ni Dar es Salaam, Kipunguni Kivule.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme maeneo ya delta. Maeneo haya yote ya delta ambayo yana Kata tano za Salale, Msala, Kiongoroni, Maparoni na Mbuchi. Kata hizi zipo kwenye mazingira magumu pembezoni mwa Bahari ya Hindi ambapo vipo jumla ya vijiji 16 sawa na vitongoji 67.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Kibiti vijiji ambavyo havina umeme vipo 40. Naomba Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi katika *phase III* Jimbo langu la Kibiti tupewe umeme. Vijiji hivyo ni Kinyanya, Mkupuka, Nyamwimbe, Bumba Msoro, Pagae, Makima Motomoto, Mjawa, Zumbwini na Tomoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya gesi majumbani ni muhimu sana. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu sikivu gesi iondolewe vikwazo kama vipo kwani nishati hii ina mchango mkubwa katika kutunza mazingira kwani itapunguza matumizi ya mkaa, kuni, umeme na mafuta ya taa katika matumizi ya siku majumbani na wananchi wapewe elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya gesi na faida zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika letu la Umeme TANESCO Rufiji lina changamoto kubwa kama ifuatavyo:-

- (i) Vifaa vya kisasa vya kufanyia kazi;
- (ii) Usafiri;

(iii) Posho za saa za ziada;

(iv) Posho za likizo;

(v) Ukarabati na majengo ya ofisi na nyumba; na

(vi) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusu miradi ya REA kwamba haina fidia.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sheria za udhibiti katika tasnia ya uchimbaji madini. Mwezi Julai, 2015, Bunge hili lilipitisha kibabe Miswada mitatu ya sheria za udhibiti katika tasnia ya uchimbaji. Miswada hiyo ilikuwa ni ya Sheria ya Petroli, Sheria ya Usimamizi wa Mapato ya Mafuta na Gesi ya mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika tasnia ya uchimbaji Tanzania ya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wote wa upinzani hatukuunga mkono namna Miswada hiyo ilivyoletwa Bungeni na namna ambavyo mijadala ya Miswada hiyo ilivyokuwa ikiendeshwa. Kwanza, Miswada yote mitatu ililetwa kwa hati ya dharura na pili mijadala yake iliendeshwa kwa pamoja na uamuzi wake ulifanyika kwa pamoja kinyume kabisa na kanuni na taratibu za kibunge za utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za Wabunge wa Upinzani kwa wakati huo na mpaka sasa ni kwamba kulikuwa na uharaka gani wa kuleta Miswada hiyo katika hati ya dharura na kuendesha mjadala wa Miswada hiyo haraka bila Wabunge kupata nafasi ya kutosha ya kupitia na kuelewa maudhui ya vifungu vya Miswada hiyo? Ni nini kilikuwa kinafichwa katika Miswada hiyo hadi kufanya mambo haraka haraka namna hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi na Wabunge wote wa Upinzani hatukuridhishwa na namna Miswada hiyo ilivyopitishwa. Hii ni kwa sababu sheria nzuri inapatikana ikiwa kuna maridhiano miongoni mwa Wabunge katika kupitisha Miswada mbalimbali ya sheria. Kwa maoni yangu, kitendo cha Serikali kutumia jeuri ya wingi wa Wabunge wa CCM kupitisha sheria mbovu kwanza ni kuudhalilisha mhimili wa Bunge lakini pia kunaiondolea Serikali sifa ya utawala bora kwa maana ya utawala wa sheria kwa kuwa sheria hizo zinakuwa mbovu na au za kulinda maslahi ya mafisadi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ilivyokuwa wakati ule presha ilikuwa kubwa sana kwa sababu Serikali ya Awamu ya Nne ilikuwa inamaliza muda wake na inasemekana kuwa ilikuwa imeshaingia mikataba na makampuni makubwa ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta na kwa hiyo ilitaka



kutunga sheria haraka haraka ya kuwalinda kabla haijaondoka madarakani ili isije ikaingia Serikali nyingine halafu ikatengua mikataba hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu kubwa ilikuwa ni uwezekano wa chama cha upinzani kushinda uchaguzi mkuu wa 2015 na kufuta mikataba yote ya kinyonyaji ambayo Serikali ya CCM iliingia na makampuni makubwa ya utafutaji na uchimbaji wa gesi na mafuta. Kwa kuwa Rais John Pombe Magufuli ameonekana dhahiri kuwa hapendi ufisadi wala mikataba ya kinyonyaji inayolikosesha Taifa letu mapato, atumie madaraka yake na kuagiza iletwe Miswada mingine ya sheria ya kuifuta ile iliyopitishwa kibabe ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kuipitia na kuiridhia kwa maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bei ya umeme na gesi. Baada ya ugunduzi wa gesi katika nchi yetu, wananchi walitegemea kuwa bei ya umeme na gesi kwa matumizi ya majumbani ingeshuka kwa kiasi kikubwa ambapo wananchi wengi wenye kipato cha chini wangeweza kumudu gharama ili waweze kunufaika na huduma hiyo. Bei ya mtungi wa gesi wa kilogramu 15 ni Sh. 45,000/=. Bei hii ni kubwa kwa wananchi wa kipato cha chini kiasi kwamba hawawezi kununua gesi kwa matumizi ya nyumbani na kwa maana hiyo wanaendelea kumaliza misitu yetu kwa ajili ya kutafuta nishati ya kuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali ipunguze bei ya gesi hadi kufikia angalau Sh. 20,000 kwa mtungi wa gesi wa kilogramu 15 ili wananchi wa kipato cha chini waweze kununua. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tumewavutia wananchi wengi kutumia nishati mbadala na hivyo kuhifadhi misitu yetu ambayo ina maana kubwa sana katika utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika kwenye umeme. Ikiwa gesi yetu inazalisha umeme, Serikali iagize *TANESCO unit* moja ya umeme iuzwe Sh.50 ili Watanzania wanufaike na hii rasilimali ya gesi asili iliyogunduliwa katika nchi yetu.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukarabati jengo la Ofisi ya Madini Tunduru. Tunapongeza na kuishukuru Serikali kwa ukarabati huu. Tunaomba jengo hili liwe chanzo cha uwepo wa wataalam na vifaa stahiki kwa uboreshaji wa sekta ya madini hasa wachimbaji wadogo katika Kata za Ngapa, Muhuwesi na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, uboreshaji huduma ya upatikanaji wa umeme Wilaya ya Tunduru. *REA phase II*, vijiji 33 vinaendelea kwa usambazaji. Tunaomba kasi ya mkandarasi iongezeke, yuko taratibu sana. *REA phase III* vijiji 52 nilivyowasilishwa Ofisi ya REA na *TANESCO* Mkoa wa Ruvuma, naomba vijiji hivi viwe miongoni mwa vijiji kipaumbele vipate umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujua *transformer* iliyopata matatizo ya kiufundi matengenezo yake yamefikia wapi? Naomba changamoto zilizojitokeza kuhusiana na *transformer* hiyo iliyopatikana kutoka TANESCO zitatuliwe ili miradi iliyopangwa kutumia *transformer* hiyo ikamilishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tunduma iko kati ya Songea na Mtwara. Umeme wa njia kuu (*national grid*) kutokea mradi wa SIDA kupitia Makambako, Songea unaishia Namtumbo pia umeme wa gesi na kadhakika. Kwa njia kuu kutokea Mtwara bado hatujaona wazi mpango wa umeme huu kwenda Tunduru. Naomba Tunduru iingizwe katika mipango ya usambazaji wa umeme kupitia *national grid*. Wakati tunasubiri mpango wa *national grid* Tunduru ipatiwe/iongezewe *generators (DGs)* zenye uwezo na ufanisi. Pia kutengeneza zilizopo na/au kuongeza nyingine kutoka maeneo mengine au mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunaendelea na mipango yote, tufikiriwe pia kutumia/kupatiwa umeme wa nishati mbadala kwa kadiriri itakavyofaa kitaalam. Zikitumika njia za *biogas* au ile ya kutokana na mabaki ya mazao (*biofuel*), basi njia hizo zinufaishe vikundi vya wananchi hasa akinamama kwani Tunduru ni mashuhuri kwa uzalishaji mazao ya kilimo.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nishukuru kwa kunipa nafasi kupitia uchangiaji wa njia ya maandishi ili niweze kuwasilisha mambo machache yanayohusu utekelezaji wa miradi mbalimbali ya umeme hususani katika Jimbo la Iramba Mashariki, Wilaya ya Mkalama na Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kitabu cha hotuba ya Waziri, ukurasa wa 20 imeelezwa kuwa katika awamu ya III ya REA vijiji vyote ambavyo havikupata umeme vitapatiwa nishati hiyo. Hata hivyo, utekelezaji wa mradi wa REA unaoendelea umeacha maswali mengi kwa Mbunge na wananchi wa Mkalama kwa misingi ifuatayo:-

- (i) Vijiji vingi viliachwa yaani havimo katika orodha ya kupata umeme.
- (ii) Vijiji vichache vilivyopitiwa na mradi huo nguzo zimepita barabarani na hazijaingia mitaani zilipo huduma za zahanati, shule na huduma zingine za jamii ikiwemo makazi ya wananchi. Mfano ni vijiji vya Kinyangiri, Gumanga, Lambi na Iguguno.
- (iii) Vijiji vingi na vikubwa ambavyo baadhi havimo katika mradi huo ni hivi vifuatavyo:-
  - (a) Kirumi (hospitali na zahanati) Kata ya Matongo;
  - (b) Mwangeza, Dominiki;

- (c) Mwanga, Kidarafa, Kidigida, Msiu;
- (d) Kata yote ya Miganga (Miganga, Ipuli)
- (e) Mtamba, Kinandili;
- (f) Senene, Iguguno Shamba, Mpako;
- (g) Yulansoni;
- (h) Nyahaa, Mkiwa, Igengu;
- (i) Kikhonda, Kinampundu, Mdilika; na
- (j) Gumanga kilipo kisima cha maji kilometa 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina ushauri ufuatao:-

- (i) Mradi wa REA upanuliwe ili uweze kufika katika maeneo niliyotaja;
- (ii) Nguzo ziongezwe na zifike zilipo huduma muhimu siyo kuishia barabarani;
- (iii) Wananchi wanaopitiwa na mradi wa umeme walipwe fidia kwa wakati, mfano wananchi wa Kijiji cha Tamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyojaa matumaini ya Watanzania kujitoa kwenye vibatari hadi kuwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu la Lushoto tunakushukuru baadhi ya vijiji vimepata umeme. Pia ametuma timu yake imeenda kupima maeneo yote ambayo yamekosa umeme wa REA II na kuwahakikishia wananchi wangu kuwa Jimbo la Lushoto litapata umeme kwa yale maeneo yote yaliyobaki. Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wananchi wangu wameshakuwa na matumaini makubwa juu ya suala zima la umeme, niendeleo kumwomba kwa Mwenyezi Mungu ili aweze kutimiza ahadi yake hiyo ili ifikapo 2020 wananchi wangu waendeleo kuamini Serikali yao ya Chama cha Mapinduzi. Pia napenda kuorodhesha maeneo ambayo hayajapata umeme pamoja na kwamba maeneo mengine ya kata na vitongoji yameshapata umeme. Kata ambazo hazina umeme pamoja na vijiji vyake ni kama ifuatavyo:-

- (i) Makanya yote;
- (ii) Ngwelo baadhi ya vijiji;
- (iii) Kilole baadhi ya vijiji;
- (iv) Kwekanga baadhi ya vijiji;

- (v) Gare baadhi ya vijiji;
- (vi) Kwemashai baadhi ya vijiji;
- (vii) Ubiri baadhi ya vijiji;
- (viii) Magamba baadhi ya vijiji;
- (ix) Kwai baadhi ya vijiji;
- (x) Mgambo baadhi ya vijiji;
- (xi) Mbwei baadhi ya vijiji;
- (xii) Malimbwi baadhi ya vijiji;
- (xiii) Lushoto baadhi ya vijiji;
- (xiv) Mlola baadhi ya vijiji; na
- (xv) Ngulwi baadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu umeme katika visiwa vidogo na vikubwa vilivyopo Ukerewe. Pamoja na sera ya Serikali kusambaza umeme vijijini bado kuna tatizo la nishati ya umeme katika visiwa mbalimbali vilivyopo katika Jimbo la Ukerewe. Nashauri Wizara itoe kauli ya matumaini juu ya upatikanaji wa umeme katika visiwa hivi kwa sababu nishati hii ni kichocheo cha maendeleo kwenye visiwa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo *line* kubwa za umeme zimepita basi vijiji hivyo vipatiwe nishati mbadala ya kushuhudia tu nyaya zimepita kwenye maeneo yao. Pia pale ambapo tayari kupitia REA umeme umefika kwenye eneo basi wananchi wanaohitaji nishati hii wapewe haraka badala ya kuzungushwa hadi wanakata tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kisiwa cha Ukara umeme wa jua kupitia kampuni binafsi ya JUMEME umewekwa lakini gharama za nishati hii ni kubwa mno kiasi kwamba wananchi wanashindwa kuimiliki. Naomba Wizara iingilie na kuhakikisha kuwa gharama zinakuwa nafuu.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba hii kwa maandishi. Matatizo ya REA *phase II* katika Jimbo langu na nchi nzima ni umeme kutofika kwenye taasisi nyingi katika maeneo ambayo umeme umepita na *transformer* kuharibika kwa muda mfupi baada ya kufungwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni ombi la upatikanaji wa umeme wa REA *phase III* katika maeneo ya Kata ya Monduli Juu, Mfereji, Moita, Naalarami, Migungani, Majengo, Esilalei, Mswakini, Makuyuni na Lashaine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni ubovu wa Sheria za Madini ambapo katika maeneo yenye mchanga na kokoto, watu wanaenda kukata

leseni ya madini ofisi za madini bila kupitia vijijini. Kuna uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uchimbaji wa kokoto katika Kata ya Nanja.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha aniambie ni lini umeme wa joto ardhi (*geothermal*) utanza kuchimbwa uliopo Kata ya Ntaba. Je, wananchi wa maeneo hayo watanufaikaje na mradi huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna vijiji ambavyo vilikuwa kwenye awamu ya pili ya REA ila hadi sasa vijiji hivyo havijapata umeme. Tunaomba vijiji hivyo vipate umeme vilivyopo ndani ya Jimbo la Busokelo visivyopungua 30.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Waziri wa Wizara ya Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri yenye kuleta matumaini makubwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Kuna tatizo kubwa la umiliki wa maeneo yenye udongo unaoashiria kuwa na madini. Maeneo hayo yapo chini ya Serikali za Vijiji na Halmashauri. Hawa watu wanaopewa leseni za umiliki wa maeneo haya bila hata Serikali ya Kijiji wala Halmashauri kujua ni kutengeneza migogoro na wenye maeneo yao na kuiona Serikali yao haiwatendei haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aniambie ni utaratibu upi unatumika wa utoaji wa leseni hizi za umiliki wa maeneo haya yenye udongo wa madini? Leseni zinazotolewa zinadumu kwa kipindi gani? Katika tozo zinazotowwa mwenye eneo lake anafaidikaje? Halmashauri husika inapata nini kutokana na uharibifu mkubwa unaofanyika?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe majibu.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri kwa juhudi zake za kuhakikisha zabuni ya bomba la mafuta kutoka Ziwa Albert- Uganda hadi Bandari ya Tanga inafanikiwa. Namwomba aangalie uwezekano wa kusaidia vyombo mbalimbali bandari Tanga kwa sababu ni chakavu ili tupate vyombo vya kisasa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza Waziri kwa mradi wa REA. Mradi huu ni moja ya sababu zilizotufanya tuingie Bungeni. Binafsi nina eneo la Jimbo kubwa kuliko Majimbo yote hapa Bungeni. Nina kata 37 na vijiji 135. Vijiji ambavyo nimefanikiwa kupata umeme ni asilimia ndogo sana ambayo haizidi

asilimia 50. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri REA III nipate mgao mkubwa. Nimetuma orodha ya vijiji 100 kwa kuanzia. Aidha, naomba anitatulie tatizo la *transformer* Mjini Muheza, kila siku umeme unakatika sababu ni uchakavu na ni dogo, limeelemewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi Sengerema apunguziwe kazi. Kasi anayokwenda nayo kwenye mradi wa REA hairidhishi, anafanya taratibu sana. Aidha, utaratibu wa kuwekewa umeme usiruke kijiji kupunguza malalamiko ya vijiji vinavyorukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la madini, ni kwa nini Serikali isianze mipango maalum ya kujenga kiwanda kikubwa cha kuanza kusafisha madini yetu hapahapa nchini. Mipango hii imekwishaanza nchi nyingine kama Zimbabwe, Botswana na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ni lazima iangalie uwezekano wa kuweka maeneo maalum ya madini ambapo wawekezaji wakija wanaweza kuonyeshwa moja kwa moja badala ya wawekezaji kuzungushwa. Aidha, wale walioshika maeneo bila ya kuyaendeleza wanyang'anywe.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini kuna mabonde yenye mchanga ambapo siku za awali (nyuma) umiliki huo ulikuwa chini ya vijiji husika na kuwezesha vijiji hivyo kupata mapato.

Hata hivyo, katika miaka ya hivi karibuni, Wizara ya Nishati na Madini imebadili utaratibu huo na kukabidhi mabonde hayo kwa mawakala mbalimbali ambao wamekuwa wakitoza tozo tofauti kwa kila eneo na wakati mwingine mawakala hawa hutoza tozo hizi katika barabara kuu kwa kuweka *road blocks* kwa kushirikiana na askari wa barabarani. Kwa kuwa utaratibu wa tozo hizo ni chanzo cha mapato ya Halmashauri za Vijiji na wameweka katika *by laws* zao; na kwa kuwa utaratibu huo mpya haujawashirikisha vijiji husika, je, Serikali haioni upo umuhimu wa kupitia upya utaratibu huu kwa manufaa ya Serikali za Vijiji hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karatu ni mji wa utalii kwa kuwa ni lango kuu la kuingilia Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro. Tukitambua mchango mkubwa wa sekta ya utalii katika nchi yetu lakini baadhi ya vijiji katika Wilaya ya Karatu havina umeme. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji vya Buger, Gongali, Endamanghang, Kansay na baadhi ya vijiji katika Mji wa Karatu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza viongozi wote wa Wizara ya Nishati na Madini kwa:-

- (i) Kupunguza urasimu wa wateja na kutembelea wahitaji wa umeme;
- (ii) Kusambaza nguzo kwa sehemu kubwa; na
- (iii) Kutenga 94% bajeti ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja juu ya mradi wa Kinyerezi II. Mradi huu unagusa mitaa 40 lakini hadi sasa ni mitaa nane tu imefanyiwa tathmini na mitatu tu ndiyo wamepewa *cheque* ambazo hadi sasa hakuna pesa kwa wananchi. Fidia kwa wananchi hawa imechukua zaidi ya miaka mitano (5) sasa na hivyo hata malipo yake hayatakuwa halisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mitaa inapewa pesa za kulinda mabomba ya gesi. Naomba pesa za ulinzi ziingaliwe upya ili kuboresha malipo haya kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa Kinyerezi II unapitia Kata za Kivule, Kipunguni, Gongo la Mboti, Majohe na Kinyerezi. Hata hivyo, Jimbo la Ukonga lina ukosefu wa umeme katika Kata za Pugu, Buyuni, Chanika, Msongola na Zingiziwa. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini pamoja na kupeleka umeme mijini na vijijini, ni muhimu kipaumbele kiwe kwenye maeneo ya shule, vituo vya polisi, zahanati na visima vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ukonga lina changamoto ya kuhudumiwa na sehemu mbili yaani Kituo cha Gongo la Mboti na Kisarawe. Suala hili linasumbua wananchi, naomba uwekwe utaratibu wa kupunguza hiyo kero.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana aangalie kwenye migodi hasa huduma za jamii kwa wanaozunguka mgodi na mrahaba wa 0.3% namna unavyokokotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LEONIDAS T. GAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea kuhusu usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka machimbo ya Ngaka – Mbinga kupitia Songea Mjini. Makaa ya mawe ni moja ya madini yanayochimbwa katika eneo la Ngaka lililopo Wilayani Mbinga. Uchimbaji wa madini haya ni muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi yetu. Uchimbaji huu unasababisha makaa yasafirishwe kwa njia ya magari makubwa aina ya malori.



Malori haya ni mengi sana na yanasafirisha makaa haya kupitia Mji wa Songea, matokeo ya malori haya kwa Songea Mjini ni:-

(i) Uharibifu wa miundombinu ya barabara ambayo unafanya mazingira kuwa mabovu na mabaya hasa katika maeneo ya Lilambo, Ruhuwiko, Lizaboni, Mjini, Mfaranyaki, Bombambili, Msamala, Mshangano na Shule ya Tanga.

(ii) Magari haya yanapopita huangusha makaa na hata yanapopata ajali. Hali hii inaharibu mazingira ya kiafya ya wananchi wa Songea. Hii ni athari ya kiafya ya wananchi wangu wa Songea Mjini.

(iii) Magari haya yanasababisha msongamano mkubwa wa magari Mjini Songea na makelele kwa mingurumo mikubwa ya malori haya ambayo ni kero kwa wananchi wangu.

(iv) Songea Mjini hakuna eneo maalum la kuegesha magari haya ama yakiwa yamebeba makaa ya mawe au yakiwa yanajiandaa kwenda kubeba makaa ya mawe. Madereva hulazimika kuegesha kwenye maeneo yasiyostahili kama kwenye vituo vya mafuta na kadhalika na hivyo kusababisha kero kwa wananchi wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya, je, Manispaa ya Songea ambayo ndiyo inayofanya kazi zote za marekebicho ya matatizo yanayosababishwa na malori haya inanufaika vipi na machimbo haya ya makaa ya mawe?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali iamue kujenga njia ya mchepuko ili kuepusha madhara hayo kwa kupita nje ya Mji wa Songea. Zipo barabara za asili zinazotoka eneo la Peramiho na kuunganisha na barabara kuu ya Songea – Dar es Salaam kupitia Njombe ambazo ni barabara ya Peramiho – Shule ya Tanga na barabara ya Peramiho – Madaba. Aidha, ufumbuzi wa kudumu ni mpango wa utengenezaji wa reli ya Mtwara – Mbambabay kupitia Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. COSATO D.CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, napenda kuongelea kuhusu nguzo za umeme kutoka nje. Viwanda vya *Sao Hill* (Mafinga) na *TANWAT* (Njombe) waungwe mkono katika suala la tenda ya nguzo hasa kwa ajili ya *REA phase III* na *TANESCO*. Nguzo kutoka nje zinapata msamaha wa *import duty* na pia malipo yanafanyika kwa wakati. Pia Serikali (*TANESCO*) inawasaidia kwa mfumo wa *Letter of Credit (LC)*. *Favour* hii inayotolewa kwa kampuni za nje haitolewi kwa wazalishaji wakubwa kama *Sao Hill* na *TANWAT*.

Viwanda nilivyovitaja vina uwezo kwa sababu vina misitu, lakini pia hata wananchi wamepanda miti ya kutosha. Nashauri tuunge mkono wazalishaji wa nguzo wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni REA. Pongezi zangu kwa watendaji wa REA, hiki ni chombo cha kupigiwa mfano siyo kwa sababu wanapewa fedha la hasha, bali utendaji bora wa watumishi wote wa REA. Tumeona taasisi ngapi za Serikali zinapewa fedha lakini bado hakuna tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri mkubwa kuhusu REA, Serikali ione uwezekano kupitia TAMISEMI/Wizara ya Fedha kuzisaidia Halmashauri gharama za *wiring* kwenye maeneo ya huduma (shule na zahanati) ambazo REA wamefikisha umeme lakini wananchi (vijijini) wameshindwa kuingiza kwenye shule, mabweni na zahanati kwa kuwa hawana uwezo. Nafahamu ni jukumu la REA kufikisha umeme na siyo kugharamia kuingiza ndani, hata hivyo Serikali kwa pamoja mnaweza kuona tunawasaidiaje.

Tatu, katika Jimbo langu Mafinga Mjini kuna kijiji kinaitwa *Sao Hill* huko ambako nguzo za umeme zinazalishwa. Kijiji hicho naomba tukiwekee umeme kuenzi japo mchango wa kijiji hiki katika suala zima la nguzo. Tuwaonee imani yaani wao nguzo zitoke kwao lakini umeme wausikie. Pia vijiji vya Mtule, Matanana, Kisada, Bumilayinga, Ulole, Itimbo, Maduma na Kikombo na pia maeneo ya pembezoni mwa Mji wa Mafinga, nashauri TANESCO wafunge *sub-station* maana matumizi yameongezeka kutokana na kuongezeka kwa viwanda vya kuchana mbao na kukua kwa mji.

Nne ni kuhusu mafuta na gesi. Pamoja na wafanyabiashara kupiga vita EWURA, nashauri Wizara iwe makini na wafanyabiashara wanjanja wanaojenga hoja dhaifu za kuondoa “*marker*” ili kudhibiti wanaokwepa kodi. Pia tumejipanga vipi kuhakikisha haturudii makosa ya kwenye madini katika suala zima la kuhakikisha kuwa tunanufaika na sekta ya mafuta na gesi?

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Kamati na viongozi mbalimbali na watumishi wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya bajeti. Naipongeza Serikali kwa kuwa na mradi huu adhimu wa umeme vijijini. Faida nyingi zimepatikana na uchumi wetu umeboreshwa na mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika REA II, Jimbo la Bagamoyo lilipata miradi 10 tu na miradi hii ilitegemewa kukamilishwa Juni 2015. Ingawa miradi hiyo ni michache lakini utekelezaji wake umesuasua sana na uko nyuma ya ratiba, hadi leo miradi minne (4) kati ya hiyo 10 haijakamilika kama ifuatavyo:-

- (i) Kijiji cha Buma, nyaya hazijafungwa katika nguzo;
- (ii) Kijiji cha Kongo, hivi karibuni tu ndiyo nyaya zimepelekwa;
- (iii) Kijiji cha Kondo, mradi haujaanza;

(iv) Kijiji cha Matimbwa, nguzo 20 hazijafungwa nyaya. Zahanati mpya ya Kijiji ilijengwa kwa ufadhili wa NGO ya Korea ipo katika eneo hili ambalo halijafikiwa na umeme; na

(v) Kijiji cha Pande, mradi umehamishwa kwa sababu wananchi wanapisha ujenzi wa bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atuthibitishie kuwa miradi hii itapewa kipaumbele kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu REA III, katika Jimbo la Bagamoyo tumewasilisha miradi 29 tu. Ni matumaini yetu kuwa utekelezaji REA III Bagamoyo utakuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo linaathiri maendeleo ya uchumi na ya kijamii kwa wana Bagamoyo ni kukatika kwa umeme mara nyingi Bagamoyo Mjini na katika Kata za Magomeni na Dunda. Serikali isimamie upatikanaji wa umeme kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ugunduzi wa gesi asilia Bagamoyo na Chalinze, tumeshuhudia utafutaji ukifanywa na fununu za kupatikana gesi Bagamoyo na Chalinze. Tatizo ni kuwa hakuna taarifa za kugundulika gesi katika majimbo tajwa. Waziri atujulishe kama kweli gesi imegunduliwa Bagamoyo na Chalinze.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia hotuba hii kwa kumshukuru Mungu kwa kunijalia kuwa miongoni mwa Wabunge wa Bunge hili lako Tukufu.

Pili, nachukua fursa hii kwa kuwapongeza wananchi wangu wa Jimbo la Tumbatu kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wa Bunge hili. Natambua imani kubwa waliyonayo kwangu na naahidi sitawaangusha.

Tatu, napenda kumpongea kwa dhati Mheshimiwa Rais, Dkt. Magufuli kwa kuonesha imani na uwezo mkubwa wa kuongoza nchi yetu. Aidha,

napenda kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa pamoja na Baraza lake la Mawaziri kwa uimara wao katika kuongoza Wizara zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo la KUA katika Kisiwa cha Zanzibar. Kwanza napenda kutoa masikitiko yangu makubwa kuona kwamba katika hotuba yote ya Mheshimiwa Waziri Zanzibar haikutajwa hata kidogo pamoja na kwamba ni miongoni mwa wateja wakubwa wa TANESCO.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namwomba Waziri anieleweshe, kwa nini Zanzibar inatozwa bei kubwa ukilinganisha na wateja wengine? Kwa mfano, KUA moja inatozwa sh. 16,550/= kwa Zanzibar lakini kwa wateja wengine KUA moja (KUA) inatozwa sh. 13,200/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi inayochukuwa katika kuwapelekea wananchi huduma hii katika vijiji vyao. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri haikuzungumza vijini na maeneo yaliyosambaziwa umeme. Naomba Mheshimiwa Waziri aoneshe maeneo hayo (*locations*) na kiwango cha usambazaji (*Kms*) uliofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hali ya ujenzi wa *line* hizo haioneshi kama zimejengwa kwa wataalam wa mambo ya umeme. Inaonekana kuwa hakuna *design* yoyote iliyofanyika kabla ya kujengwa *line* hizo. Ni vyema, Makandarasi kwa usimamizi wa TANESCO wakalazimishwa kuwa na *design* pamoja na *profiles* ya kazi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida *lifetime* ya nguzo za umeme huwa ni zaidi ya miaka 20 lakini nguzo ambazo zinatumiwa katika kazi hii hasa za REA hazioneshi umadhubuti halisi kwa kazi hii. Hivyo nakuomba Mheshimiwa Waziri anieleze *lifetime* ya nguzo hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. BUNGARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini awali ya yote, napenda kukupongeza kwa kuchaguliwa tena kuwa Waziri wa Nishati na Madini, Wizara nyeti na muhimu katika Tanzania yetu. Mwenyezi Mungu akuzidishie busara na hekima.

Pia napenda kukupongeza kwa katika hotuba yako ukurasa wa 36 mpaka 37 kwa kuturejeshia mradi wa ujenzi wa kiwanda cha mbolea, mradi utakaogharimu Dola za Kimarekani bilioni 1.98 sawa na shilingi za Kitanzania

bilioni 411.24. Natoa shukrani kwa Serikali kwa kutupatia mradi huu mkubwa kwa maendeleo ya Kilwa na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote hayo, Jimbo la Kilwa Kusini, pamoja na gesi inatoka katika Jimbo la Kilwa Kusini lakini katika mradi wa umeme vijiji REA, kwenye Jimbo la Kilwa Kusini ni Kijiji kimoja tu cha Matanda ndicho kimepata umeme katika mradi wa REA. Mheshimiwa Waziri naomba vijiji vifuatavyo vipate umeme wa REA: Pande, Mtilimita, Namwando, Nakimwera, Nangao Malalani (Kata ya Pande), Rushungi, Kisongo, Ruyaya, Lilimalya Kaskazini na Kusini, Namakongoro (Kata ya Linimalyao), Makangaga, Nakia, Nanjilinji 'A' na 'B' (Kata ya Nanjilinji), Likawange, Mirawi, Nainokwe (Kata ya Likawaga) Kilole, Ruatwe, Kisangi, Kimbarambara (Kata ya Kikole).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wilaya ya Kilwa Jimbo la Kilwa Kusini ndilo Jimbo litowalo gesi asili kwa heshima na taadhima lipewe kipaumbele katika mradi wa umeme vijijini. Natanguliza shukrani. Ahsante.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wetu kuanzia kwa Mheshimiwa Rais wetu mpendwa John Pombe Magufuli. Nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Majaliwa na Baraza zima la Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuwapongeza viongozi wetu wa Bunge letu kuanzia kwa Mheshimiwa Spika, kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Wasaidizi wote wa Bunge. Naendelea kumwomba Mungu aijalie nchi yetu amani, mshikamano na utulivu; kwake yeye yote yawezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali ya Awamu ya Nne kwa mpango wake wa Wakala wa Umeme Vijijini. Kwa kweli kazi iliyofanyika ni nzuri sana na inatia moyo. Nachukua nafasi hii kumpongeza sana Profesa Sospeter Muhongo kwa moyo wake wa kujituma kwa nia njema ya kuwa mzalendo na moyo wa kupenda kuifanya nchi yetu kuwa ya umeme hadi 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii pia kuwaombea wafanyakazi wa Wizara ya Nishati na Madini kuanzia Taifa mpaka ngazi ya chini. Mungu awape uzima na maisha marefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Mbulu katika mpango wa REA Awamu ya Kwanza na ya pili, imebahatika kupata umeme katika Majimbo yote mawili, vijiji 18 kati ya 123. Hivyo naomba sana Wizara hii iwatendee haki wananchi wa Mbulu. Maombi yangu ya kumwomba Mheshimiwa Waziri afanye ziara Wilayani Mbulu kutembelea miradi ya REA Awamu ya Kwanza na pili ili kujiridhisha na hali mbaya ya miradi hiyo hususan Vijiji vya Jaranjar Kata ya Tlawi na Guneneda Kata ya Tlawi na Kata ya Ayamohe.

Mheshimiwa Naibu Spika, barua yangu yenye dodoso la vijiji 33 niliyotuma kwa Mheshimiwa Waziri mwezi Februari, 2016 ifanyiwe kazi kwa kuwa Mbulu tumepunjika sana. Kwa Wilaya ya Mbulu imepata vijiji 18, naomba nijibiwe kwa barua ni lini Mheshimiwa Waziri atafanya ziara Wilayani Mbulu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri elimu itolewe na ngazi zote za TANESCO katika maeneo ambayo umeme unatarajiwa kutolewa au kupelekwa kwa wadau/wananchi wa maeneo husika. Wizara itoe elimu kwa wachimbaji wadodo wadogo wa madini ya dhahabu katika Kata za Nahasena, Aehandu ili kuondoa mgogoro katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria za kupata mrabaha katika machimbo kati ya HLW na wachimbaji itazamwe. Elimu itolewe kwa watumiaji wadogo wa umeme majumbani kwa kuondolewa kwa VAT na *Service Charge* ili kuleta hamasa ya matumizi makubwa ya umeme. Pia, watendaji wachache waliopo katika ngazi za Wilaya wadhibitiwe wanaotumia urasimu, ubabaishaji kwa wateja wanaohitaji kuunganishwa na umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira mazuri ya Tanzania katika kutumia umeme wa gesi yaandaliwe kwa kufanya tafiti za kitaalam ili umeme huu wa gesi uwe na tija kwa uchumi wa nchi yetu. Watazania wahamasishwe kutumia gesi kwa matumizi ya majumbani ili kupunguza matumizi makubwa ya mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri EWURA iwe na sekta mbili; moja, isimamie maji na nyingine isimamie mafuta na nishati ili kuleta tija.

Pia, utafiti ufanyike haraka kama Tanzania tumenufaika na asilimia nzuri ya mrahaba katika upatikanaji wa madini nchini. Pia, Sekta ya Mafuta itazamwe upya ili VAT irudishwe katika mafuta kuongeza mapato ya Serikali kwa kuwa mwenye kuhitaji mafuta ana uwezo, kwa hiyo, anastahili kulipa kodi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kama ilivyowasilishwa leo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Madini nchini bado haijaleweka hasa kwa wananchi wengi wa vijijini, jambo linalowafanya wananchi wengi kunyanyasika hasa pale ardhi yao inapogundulika kuna madini na wao kutakiwa kuhama pengine bila ya hata kujua stahiki zao, zaidi ya kuambulia mashimo. Sambamba na hilo, hata utaratibu wa upatikanaji wa leseni kwa wachimbaji wadogo, hauko wazi hasa kwa watu waishio vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale katika Kijiji cha Lilombe kuna machimbo ya madini ya dhahabu na *sapphire*, lakini wachimbaji wadogo

wanapotaka leseni, hulazimika kwenda Tunduru Mkoani Ruvuma ambako ndiko kuna Ofisi ya Kanda.

Vile vile soko la madini wanayoyapata hulazimika kwenda kuyauzia Tunduru, hivyo Halmashauri ya Liwale haina mapato yoyote yatokanayo na machimbo hayo. Maeneo ya machimbo hayo ni ardhi inayomilikiwa na Kijiji cha Lilombe, lakini inapotolewa leseni wananchi hawa hawashirikishwi katika lolote. Hivyo kuweka mgogoro kati ya wachimbaji hao na Halmashauri ya Kijiji. Nini kauli ya Serikali juu ya mgogoro huu? Kwa nini kusifunguliwe Ofisi ya Madini Liwale? Kwa nini wachimbaji wasilipe ushuru kijijini ili kijiji kipate mapato yatokanayo na ardhi yao badala ya kuachiwa mashimo na mapato yaende mkoa mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Liwale iko kilometa 120 toka Wilaya ya Nachingwea ambako kuna umeme wa gesi asilia, lakini kwa masikitiko makubwa hadi leo Liwale inategemea umeme wa mafuta (*generator*) ambao kutokana na ukosefu wa barabara kuna wakati Liwale hubaki gizani kutokana na kukosa mafuta. Vile vile *generator* hilo kwa sasa limezidiwa na watumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mradi huu wa REA kwa Wilaya ya Liwale ni wa kusuasua sana hasa baada ya kukosekana kwa umeme wa uhakika. Wilaya yenye vijiji 76 ni vijiji vitano tu vyenye umeme wa REA. Njia kuu ya umeme kutoka Nachingwea hadi Liwale ujenzi wake haujapewa msukumo unaostahili. Kumekuwepo na visingizio vingi, haijulikani kikwazo ni nini na nani kati ya Mkandarasi, TANESCO au Serikali. Namwomba Waziri mwenye dhamana kuhakikisha mradi huu unakamilika ili kusukuma maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa kiwanda cha kuchakata gesi (*LNG – LINDI*) ni bora ukaharakishwa sambamba na kulipa fidia kwa wale waathirika wa ujenzi huo. Vile vile ni jambo la kuzingatia kuwa vijiji vyote vinavyopitiwa na bomba hili la gesi ni lazima vipatiwe umeme sambamba na kuwalipa fidia watu wote ambako bomba hili limepita. Hakuna dhambi kubwa itakayofanywa na Serikali hii kama mtawanyima umeme wanavijiji Mkoa ya Lindi na Mtwara. Naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Moja kwa moja nianze mchango wangu nikiuelekeza kwenye kilio cha muda mrefu cha wananchi wa Kata ya Malolo ambao wapo kwenye Jimbo la Mikumi wakilalamikia fidia yao ya uharibifu mkubwa sana wa mazao na mashamba yao uliosababishwa na kupasuka kwa bomba kubwa la mafuta ya TAZAMA Pipeline.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu mwaka 2011 bomba la TAZAMA lilipasuka na kusababisha hasara kubwa sana siyo tu kwa mazao bali zaidi kwenye afya



za wananchi wa Kata hiyo ya Malolo hasa kwenye Vijiji vya Mgogozi, Chabi, Malolo 'A', Malolo 'B' na maeneo mengine yaliyozungukwa na bomba hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na wataalam walikuja kufanya tathmini ya uharibifu uliotokea na walikubaliana na wananchi wa Kata ya Malolo kuwa watalipwa fidia ya sh. 320,000,000/= kwa madhara hayo. Tofauti na walivyokubaliana, wananchi wakaambiwa na Halmashauri ya Kilosa kuwa watalipwa sh. 50,000,000/=. Sasa wananchi wa Malolo wanataka kujua ni lini watalipwa sh. 320,000,000/= zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Kata ya Malolo kwa masikitiko makubwa sana wanaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi iwape majibu, ni lini itawafuta machozi yao kwa kuwalipa haki yao hii muhimu ya fidia hii ambayo hawajalipwa tangu mwaka 2011?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, napenda sana kuchangia kuhusu mradi huu wa REA. Inasikitisha sana kuona Jimbo la Mikumi halijaguswa kabisa kwenye mradi wa REA I na REA II na sasa tunaingia kwenye REA III tukiwa na sintofahamu kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mikumi limebatizwa jina na sasa kuitwa Jimbo la giza kwa sababu ya vijiji vingi sana vya Jimboni Mikumi kukosa umeme. Nilishaandika na kuipeleka barua kwa Mkurugenzi wa REA na kumwelezea hali halisi ya Jimbo langu la Mikumi lakini pia baada ya kuuliza swali la nyongeza kwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini ambaye naye alinijibu kwamba atahakikisha mradi wa REA III vijiji vyangu vya Jimbo la Mikumi vyote vitaingizwa kwenye mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda Mheshimiwa Waziri akija kwenye majumuisho yake atuambie ni lini vijiji vifuatavyo vya kwenye Jimbo langu la Mikumi vitapata umeme?

- (1) Kata ya Maloo – Vijiji vya Mgogozi, Malolo A & B, Chabi, Itipi;
- (2) Kata ya Vidunda – Vijiji vya Vidunda, Udungu na Chonwe, Itembe;
- (3) Kata ya Uleling'ombe – Vijiji vya Uleling'ombe, Mlunga, Lengewaha;
- (4) Vijiji vya Mhenda – Vijiji vya Mhenda, Kitundueta, Ilakala, Maili 30;
5. Kata ya Masanze – Vijiji vya Munisagara, Chabima, Dodoma Isanga;

6. Kata ya Tindiga – Vijiji vya Malui, Tindiga, Kwalukwambe, Malangali;
7. Kata ya Ulaya – Vijiji vya Nyameni, Mbuyuni, Kibaoni, Ng'ole, Nyalanda;
8. Kata ya Kilangali – Vijiji vya Mbamba, Kiduhi;
9. Kata ya Mikumi – Vijiji vya Ihombwe, Tambuka Reli, Msimba;
10. Kata ya Zombo – Vijiji vya Kigunga, Madudunizi, Nyali, Zombo; na
11. Kata ya Ruhembe – Kijiji cha Kielezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Sospeter Muhongo, Mbunge na Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Naibu Waziri wake Dkt. Kalemari, Mbunge, kwa kazi kubwa mnayoifanya. Pia nawapongeza watumishi na wafanyakazi waliopo kwenye Kamati hii chini ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Nyasa na mimi mwenyewe kwa kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya, Mbamba Bay/Kilosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilimwandikia Mheshimiwa Waziri kwenye barua yangu, kimsingi nafahamu jitihada zinazoendelea katika kufikisha umeme kwenye Vijiji vyote 82 vya Jimbo langu kupitia REA III kama ambavyo nilifahamishwa. Natarajia kupitia dhamira hiyo, uwezo wake Mheshimiwa Waziri na ahadi ya Chama cha Mapinduzi iliyonadiwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais siku ya tarehe 8/9/2016 – Tingi, suala hilo litakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *line* kuu ya umeme wa *Kilowatt* 33 Mbinga – Mbamba Bay inapita kwenye msitu lakini pia katika milima na mabonde makali kiasi wakati mwingine kusababisha *short* na hivyo kukosesha umeme Mbamba Bay.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwa kuwa mpango pia ni kuendelea kusambaza *line* hiyo katika vijiji vingine vya Ziwa Nyasa hadi Lituhi, ni vyema kutengeneza *T-off* eneo la Kihegere ili kuunganisha *line* hiyo na ile iliyoishia eneo la Kipape – Chemeni, kiasi cha kusaidia endapo umeme wa upande mmoja kukatika. Kipande hicho ni kama Kilometa 15 – 20 tu. Pia naomba kuweka

*transformer* katika Kijiji cha Mkalole na Makunguru kabla ya kufika Mbamba Bay. Jimbo letu la Nyasa ni changa kimaendeleo naomba lisaidiwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuwashukuru na kuwapongeza REA kwa jitihada zao katika kutekeleza majukumu yao. Tunawaomba mwendelee kupokea simu zetu bila kuchoka. Natanguliza shukrani zangu za dhati.

**MHE. SALIM M. BAWAZIR:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa kazi nzuri wanazofanya, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wote wa Mashirika yaliyopo Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaelekeza mchango wangu kwa REA. Naomba Serikali iangalie jinsi ya kusambaza umeme katika Vijiji vya Kata zifuatazo – Kata ya Magubike ‘A’ na ‘B,’ Kidefe, Lumuma, Madoto, Kitete, Lumbiji, Mambaya, Kitonge 1 na 2. Muandi, Chaombele, Ifunde, Mwasu, Kitati, Mzaganza, Mkundi, Dumila Juu, Mkundi Matogolo. Msowero Shule ya Sekondari, Mayambaa Kitongoji cha Mkobwa, Sukutari, Kichangani, Majengo, Mfulu, Madudu, Mbigili, Mabawa, Mateteni, Peapea, Buyuni na Mabatini Unone.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vyote hivyo havijapata umeme wa REA. Naomba Mheshimiwa Waziri utusaidie kupata umeme kwani wananchi wa maeneo hayo wana shida sana. Sambamba na wananchi, umeme pia ni muhimu ufike kwenye shule ya Sekondari ya Msowero. Umeme utasaidia wanafunzi kujisomea nyakati za usiku.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinasaba viliwekwa kwa kuwa bei ya mafuta ya taa yalikuwa bei ya chini. Wafanyabiashara wakawa wanachakachua mafuta, lakini sasa bei ya mafuta ya taa iko juu kuliko *diesel*. Sasa vinasaba vya nini tena? Tunapoteza fedha za Watanzania ambazo zingeweza kutumika kwa kununua madawa na madawati kwa wanafunzi mashuleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lingine ni leseni za mafuta. Upatikanaji wake unasumbua sana wafanyabiashara, masharti ni mengi mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwa maeneo yanayohusu Jimbo langu la Bunda Vijijini. Jimbo la Bunda lina Vijiji 39. Matatizo ya umeme ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, REA / vijiji vilivyopata umeme ni Kyandegge, Migeta, Mariwanda, Salama ‘A’ na Hunyuri

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo umeme wa *REA Phase I* uliwekwa katika maeneo ya *center* (Barabara kuu). Aidha, maeneo yote ya Taasisi; Mashuleni, Hospitali, Ofisi) hakuna umeme. Aidha, katika Vijiji vya Mariwanda, Hunyari, umeme uliwekwa katika *volt* ndogo (muhimu). TANESCO Bunda wanajua.

*REA II*: Vijiji vilivyopata umeme ni Kiloreli, Kambubu, Nyamuswa, Marambeka, Salama Kati, Kurusanga, Mikomariro na Mibingo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo vijiji vya *REA II* nilivyovitaja kuanzia cha 1 – 6 umeme umewaka katika maeneo ya *center* tu. Taasisi zote za Umma hakuna umeme. Wizara imetoa agizo kupitia Mheshimiwa Muhongo (Waziri) kuwa Taasisi zote za Umma zipate umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, *REA III*; vijiji ambavyo vinahitaji umeme ni Manchimaro, Tingirima, Nyangiranga, Rakana, Tiringati, Bigegu, Nyaburundu, Mahanga, Mmagunga, Nyariswori, Sarakwa, Majengo, Nyangere, Nyabuzame, Mmuruwaro, Nyang'ombe, Nyanungu, Rubimaha na Bukoba,

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yangu kuwa maeneo yote hayo yatapewa umeme wa *REA Phase III* kama ilivyoahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni.

N.B. Vijiji vya Bukoba na Samata vimewekewa *transformer*, tunahitaji umeme uwake. Mungu ibariki Wizara, Mungu ibariki Tanzania.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Ushetu halikubahatika kujengewa miundombinu ya umeme. Tumepata vijiji viwili tu. Tunao uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na misitu na tunahitaji kuchakata mazao yetu ili tuinue uchumi wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumehamia Makao Mapya ya Halmashari ya Ushetu ambayo yako katika Kata ya Nyamilangano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu Mheshimiwa Waziri, tupelekewe umeme kwa haraka Makao Makuu ya Halmashari yetu ya Ushetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, tujengewe miundombinu ya umeme kwenye vijiji vyote *REA II* ili tuweze kuchangia katika kukuza viwanda na uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa ushirikiano wako na nia yako thabiti kutusaidia wana Ushetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mawaziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote wa Wizara hii. Napenda kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Buhigwe Makao Makuu tunashukuru umeme umefika na baadhi ya vijiji umeme umefika. Tatizo ni kwamba kati ya vijiji 48 tumefikisha umeme vijiji tisa tu. Tunaomba kipaumbele kwani Mkoa wa Kigoma tumeachwa sana na mikoa na wilaya nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, REA III, tunaomba vijiji vyangu vya Wilaya ya Buhigwe vipate kuwekewa umeme kwani imeanza kuwa kero na siasa kupamba moto kwamba CCM hawawapendi. Kata ambazo hazijapata umeme Buhigwe ni Muhinda, Janda, Munzeze, Mkatanga, Kibwigwa, Kibande, Munyegera, Kilelema, Kajana, Mugeru, Bukuba, Kinazi na Rusaba

Mheshimiwa Naibu Spika, jamani tuoneeni huruma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawakumbusha kuwa vijiji vyetu ni vikubwa sana na wananchi ni wengi, tunaomba *transformer* za kutosha kwani vijiji vilivyopata vitongoji, wengine wanalalamika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Wizara kwa uamuzi wa kuzalisha umeme pale Mto Malagarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nawatakia ufanisi bora wa kazi zenu.

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri wanayoifanya wakiongozwa na Mheshimiwa Profesa Muhongo, Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini na watalaam wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ya Nishati na Madini, katika Jimbo langu la Itilima, Makao Makuu ya Wiliya, REA *phase two*, haikuweza kuweka umeme katika maeneo ya nyumba za viongozi wa Wilaya ikiwemo nyumba ya Mkurugenzi na nyumba ambayo Viongozi wa Kitaifa hufikia pamoja na kituo cha mafuta kilichojengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naombe Wizara ya Nishati na Madini ione umuhimu kwenye REA *phase three* iweze kuzambaza umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo ya Makao Makuu ya Tarafa ipo miradi ya maji ya Serikali iliyowekezwa inahitaji umeme. Mfano Tarafa ya Kinamweli Kijiji cha Nzezei tunao mradi wa maji ambao uko tayari, unafanya

kazi kwa kutumia jenereta ambayo inaleta gharama kubwa kwa wananchi pamoja na kituo cha afya cha Zagayu ambacho kinatoa huduma ya afya katika Vijiji 18 pamoja na Wilaya jirani ya Maswa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Kanadi katika Kijiji cha Migato ni center kubwa ambayo inaweza kuongeza mapato makubwa kwenye nchi yetu pamoja na ajira kwa vijana; inahitaji umeme. Kuna baadhi ya Vijiji ambavyo havina umeme katika Jimbo langu la Itilima kama ifuatavyo:-

Tarafa ya Kinang'weli, Kijiji cha Nhobola, Sunzara, Kidula, Ngwamnemha, Sawida, Isegwe, Mahembe, Kinang'weli, Isegwa, Lulung'ombe, Kabale, Sasago, Mlimani, Kashishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Itilima, Gambasuga, Dasina, Musoma, Ng'wabagwa, Ng'wangwita, Ikangalipu, Tagaswa, Nseme, Magazo, Nkololo, Mwalushu, Ng'wamanhu, Ng'wagwita, Dasina B, Banamhala, Bugani, Isakang'wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarafa ya Kanadi ambavyo havina umeme ni kama ifuatavyo; Chimwamiti, Shishasi, Ng'wakatale, Mtobo, Mwabalah, Pijulu, Nkuyu, Ngailo, Migoto, Simiyu, Lali, Madilana, Mhunze, Ngwabulugu, Ngailo, Lali, Nyatugu, Senani Ng'waogama, Ng'wangutugu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hoja yetu niliyosema, Mheshimiwa Waziri aweze kutupatia hitaji hilo muhimu kwenye eneo langu la Jimbo la Itilima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukuwe nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini Profesa Muhongo kwa weledi wake na uchapa kazi katika Wizara hii ambayo anaimudu sana. Sina shaka na uchapa kazi wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo machache, naomba uweze kutusaidia sisi Wananchi wa Jimbo la Rufiji wenye wimbi kubwa la umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rufiji ina ardhi yenye rutuba na bonde zuri katika kilimo. Serikali haijawahi kufikiria uwekezaji wa namna yoyote katika bonde hili toka Adam na Hawa mpaka sasa. Hali hii imepelekea uchumi wetu kuwa na hali mbaya. Ukosefu wa maji, hakuna shule za sekondari (Kidato cha Tano) japo kuwa Rufiji ni kubwa kuliko Mkoa mmoja wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wamepata chuki sana dhidi ya Serikali na hili ni dhahiri na matokeo ya uchaguzi uliopita uliokuwa na ushindani

mkubwa. Tumesahulika mpaka tunahisi ni mpango maalum wa Serikali kutukwamisha kila kitu ili tuendeleo kubaki katika maisha ya ujima ya karne ya 19. Rufiji mtandao hakuna, tunalazimika kupanda kwenye miti kuwasiliana na ndugu zetu na hata Benki hakuna, tunasafiri zaidi ya kilometa 100 kufuata huduma ya benki, lakini Rufiji ni kilometa 170 tu kufika Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee, nimwombe Mheshimiwa Waziri yeye sasa awe mkombozi wetu kwa kusaidia kutatua kero za Wizara yake katika Jimbo la Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya kata 13 za Rufiji, ni kata tano, tu zenye umeme, lakini ni zaidi ya vijiji 40 kati ya 56 ambavyo hakuna umeme na hata maeneo yenye umeme, basi unawaka mara moja au mbili kwa wiki. Kwa mwezi umeme unawaka mara nne au tano, hii ni kero kubwa. Namwomba atume tume yake kufuatilia suala hili na kubwa zaidi nimwombe afike Rufiji ajionee.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutaja Vijiji vichache, Tawi, Kikobo, Kitapi, Nyakipanda, Chumbi A' B, hizi ziko katika Kata ya Mbwala na Chumbi. Kata ya Ngarambe, Namakano, Ngarambe, Kingurila na vijiji vingine hakuna umeme. Maeneo yote ya Kata ya Mkongo, vijiji vyote vya Kata za Mwasemi, Ngorongo na Kipujila.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo haya yote hayana umeme na maisha ya maeneo hapa ni maisha ya zamani sana. Hakuna umeme, hakuna mitandao, wananchi hawajui kinachoendelea katika nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini uwezo wa Mheshimiwa Waziri, na yeye ndiyo pekee wa kutusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa, namwomba Mheshimiwa Waziri ashughulikie suala la malipo ya fidia katika mradi wa Kilwa Energy, ambapo wananchi wanadai fidia. Pia wapo watu wengine ambao si wenyeji wa maeneo hayo wamejumuishwa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo ya kurudia kufanywa *Evaluation* ya malipo hayo. Wananchi wa maeneo hayo ni pamoja na Umwe Kusini, Kata ya Umwe, Mtanange, Kata ya Muholo, Kijiji cha Kiwanga, Shella na maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja kwa asilimia zote.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa usambazaji umeme vijiji unaotekelezwa na REA katika Awamu ya Pili uligusa vijiji vichache sana katika Wilaya ya Karatu. Serikali inatamka kuwa Awamu ya Tatu itaelekezwa katika vijiji vyote vilivyobakia nchini .



Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ni habari njema kwa ananchi wote. Nimwombe Mheshimiwa Waziri agawe orodha ya vijiji kwa kila Wilaya ili sisi Wabunge tuweze kufuatilia utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Karatu inavyo visima virefu 13 vya maji ambavyo vinaendeshwa kwa mashine za Diesel.

Mheshimiwa Naibu Spika, uendeshaji wa visima kutumia Diesel Engine ni gharama kubwa unafanya wanachi kushindwa kuendesha miradi hii. Nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii apeleke umeme katika miradi hii ya visima vilivyoko Vijiji vya Basodamsh (2), Emaranek (3), Kiviwasu (2), Rhotia Kainan (1), Endabash (1), Gilambo (1), Gendaa (1), Getamoa (1), Kambi Faru (1).

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifikisha umeme katika visima hivi pia kwa vijiji ambavyo visima vipo vitanufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini. Serikali imeteua mawakala kukusanya kodi au tozo ya madini ya ujenzi Example mchanga, kokoto, mawe, moram na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili limeleta vurugu na mkanganyiko mkubwa. Kwa muda wote wa nyuma madini hayo yamekuwa chini ya Halmashauri za Vijiji kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya. Mfano, huko nyuma tozo zilizokuwepo ni; kijiji sh. 5,000/=, Halmashauri sh. 5,000/= na wapakiaji Sh. 10,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakala huyo aliyeletwa sasa naye anachukua sh. 5, 000/= na Serikali Kuu sh. 3, 000/=. Jambo hili limeongeza gharama ya kupata mchanga. Lori tani saba kutoka Sh. 20, 000/= hadi Sh. 28, 000/=. huyu Wakala anapata sh. 5, 000/= kwa kila tani saba kwa sababu gani? Hivi Halmashauri zetu haziwezi kukusanya mapato?.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu bwana hachangii matengenezo ya barabara, jambo hili halikubaliki kabisa na litaleta mgogoro mkubwa. Tunaomba Waziri amuondoe wakala huyu na ushuru huo ukusanywe na Halmashauri ya Wilaya.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kuhusu vijiji vya Chipite, Chikindi zahanati, Mbamba, Mbaju, Rahaho, Nanajani pamoja na Mlingura. Vijiji hivi vimepitiwa na waya wa umeme za KVA 33, kuelekea maeneo ya mbele. Nini mpango wa Serikali katika kuhakikisha vijiji hivi vinashushiwa

umeme wakati wananchi waliharibu mazao yao mikorosho, miembe na mengineyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia katika Kijiji cha Chikindi kuna zahanati pale umeme umepita karibu wanaambiwa walete nguzo kwa shilingi milioni moja. Serikali haioni kama ni muhimu sana kuweka umeme katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Kijiji cha Nanajani kuna gereza pale, hadi leo wanafuata maji mbali kwa ajili tu ya kukosa umeme. Mitambo ya umeme katika eneo la Masasi ni duni sana. Ningeomba kufahamu mipango ya Serikali katika eneo hilo.

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwelekeo wa usambazaji umeme Wilayani Kongwa kwa TANESCO na REA kama ifuatavyo:-

(a) Vijiji ambavyo havina umeme kama Pembamoto, Mbagilwa, Bangibanyi, Makole, Nguji, Muungano, Mkoko, Kiteto, Masinyeti nakadhalika.

(b) Vijiji vyote ambavyo bado huduma ya umeme haujafika kwenye sekondari, zahanati, visima vya maji, makanisa, misikiti, vitongoji vilivyochwa.

(c) Miji midogo inahitaji umeme sana Kibaigwa, Kongwa, Mlali, Mkoka, Sagara, Mbande, Songambebe, Pandambili.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hotuba iliyopo mbele yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wake kwa kazi kubwa na umahiri wa hali ya juu katika Wizara hii nyeti kwa jinsi wanavayojitua kulitumikia Taifa hasa katika kusimamia huduma ya umeme kwenye maeneo yote ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, naomba kuchangia katika huduma ya umeme vijijini (REA). Huduma hii ni nyeti na imelenga kusambaza umeme kote nchini, lakini zipo changamoto kwa baadhi ya maeneo nchini. Mfano, katika Jimbo langu la Kilindi lenye ukubwa wa sm<sup>2</sup> za mraba 6,125 vijiji 102 na kata 21 ni vijiji 24 tu ambavyo vimepata umeme, tena ni maeneo ya Bura. Je, Waziri na Wizara kwa ujumla, ni lini vijiji vilivyobaki vitapata umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa yapo maeneo yenye huduma za kijamii hatuna umeme, mfano zahanati, shule za sekondari na shule za msingi. Ni imani yangu Serikali italitazama suala hili katika awamu ya tatu ili maeneo nyeti yaliyobaki yapate umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika Wilaya ya Kilindi kuna tatizo la kukatika kwa umeme mara kwa mara, hali hii imetokana na umeme mdogo, miundombinu chakavu na ukosefu wa *transformer*. Umeme uliopo ulilenga kutoa huduma kwa wananchi wachache na wakazi 300,000. Nishauri hatua za haraka za dhati zichukuliwe ili wananchi wapate huduma hii kwa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia juu ya sheria ya utoaji wa leseni kwa wachimbaji wa madini. Sheria hii imesababisha migogoro ya mara kwa mara kwa kuwa Sheria hii ya Madini na Sheria ya Ardhi zinafautiana. Mwenye leseni anapotaka kuchimba madini ni lazima akubaliane na mwananchi aliye katika eneo husika kwa ajili ya fidia. Sasa, inakuwa vigumu mwananchi kuondoka eneo hilo pale anapojua dhahabu au aina nyingine ya madini yamegundulika eneo hilo, hususani pale inapotokea fidia inayotolewa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile kuna changamoto kwa Ofisi ya Madini ya Handeni inayohudumia Wilaya ya Kilindi kutoa leseni kwa watu waliopo nje ya Kilindi na kuwaacha wazawa wa wilaya husika. Hali hii imechangia migogoro ya mara kwa mara. Naishauri wizara isogeze huduma ya ofisi wilayani Kilindi, naomba jibu kwa Wizara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepitia kitabu chote cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijaona sehemu ya hotuba yake inayoonesha dhamira ya Serikali katika kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo katika Jimbo la Kilindi. Naomba majibu ya kuridhisha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Aidha, kama Serikali ikitoa ruzuku basi fedha hizo hazifiki kwa walengwa. Nashauri kila Mbunge anayetoka kwenye eneo lenye madini ahusishwe katika kusimamia zoezi hili ili walengwa wanufaike na nia nzuri ya Serikali katika kuwasaidia wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kuchangia hotuba hii juu ya kutokuwa na ofisi yenye hadhi ya wilaya, kwa maana ofisi ya TANESCO. Watumishi wa TANESCO kiukweli ni wachache, hawana vitendea kazi vya kutosha kuweza kuwafikia wananchi wenye jiografia ngumu. Naomba Waziri ashirikiane na Shirika la Umeme tupate ofisi bora na watumishi wa kutosha wa kuwahudumia wananchi wa wilaya hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa jitihada kubwa alizofanya za kufanikisha upatikanaji wa mkataba wa kujenga bomba la mafuta kutoka Uganda hadi Tanga litakalosaidia kukuza uchumi wa Mkoa wa Tanga na Taifa kwa ujumla; ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa ajira wakati wa ujenzi na baada ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu lina ofisi ndogo ya TANESCO ambayo inahudumia kutoka Itigi hadi Mitundu, kilometa 70; na REA II umeme unakwenda hadi Mwamagembe, kilometa 63 toka Mitundu. Ofisi hii pia inahudumia toka Mkiwa hadi Itigi kilometa 30. Kwa maana hiyo ukianzia kilometa 30 ongeza 70 ongeza 63; na ukiongeza REA III mtandao unaongezeka. Jimbo langu kwa sasa lina Halmashauri ya Wilaya ya Itigi kwa maana karibuni kutakuwa na Wilaya ya Itigi, hivyo noamba ofisi yenye hadhi ya Wilaya ili kuendana na mtandao mzuri wa Wizara hii ambayo nami naipongeza. Ahsante.

**MHE. CHARLES J. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali na hususani Wizara ya Nishati na Madini kwa kuja na mpango wa bajeti itakayowezesha Taifa letu kuwa na umeme wa uhakika. Sekta ya Nishati ni muhimu katika kutekeleza dhamira ya Taifa ya kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri juu ya utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini chini ya REA na TANESCO. Tofauti na mipango ya REA katika kusambaza umeme Mkoa wa Kagera una upekee wake kutokana na ujenzi wa nyumba za makazi sehemu za vijijini. Wananchi wa Kagera kila familia hujenga mbali na familia nyingine katika familia ambazo hazijabanana. Kaya moja inaweza kuwa mita 100 – 200 kati ya nyumba moja mpaka nyumba nyingine. Hali hii inapeleka mgao wa kilomita mbili na nusu kila kijiji waishio sehemu ndogo tu ya kijiji. Changamoto hii wananchi na viongozi tumeiwakilisha kwenye ngazi mbalimbali za REA, TANESCO na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani kwa kazi nzuri iliyofanyika niombe na kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na vijiji kuwa vikubwa sana na aina ya makazi, tathmini ifanyike na waongezewe wigo wa usambazaji. Usambazaji wa umeme kwenye Jimbo la Muleba Kaskazini utoe kipaumbele kwa Kijiji cha Kahumuko, Kata ya Katoke na Omurunazi, Kata ya Mushabego kutokana na uwepo wa mashine za kusukuma maji ambazo zinatumia *diesel*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Nyakatanga, Kijiji cha Bihija hakikutajwa, khusishwe. Kata ya Rutoro nashauri Kijiji cha Misambya khusishwe na izingatiwe kuwa kijiji kimoja kimeandikwa mara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri pia Kata ya Bumbiile ni eneo kubwa sana, kwa hiyo *solar min grid* ziongezwe ili kufikia vijiji vingi hasa wananchi wakazi. Kata ya Boziba, Kisiwa maarufu kwa shughuli za uvuvi na biashara ya samaki kisiwa hiki kiongezwe *solar min grid* ya umeme wenye uwezo wa kuhimili shughuli za kibiashara kadri ya mahitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii ili Wizara hii itekeleze miradi iliyopanga pamoja na kujibu hoja zangu ambazo naziwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Profesa Muhongo na timu yake yote ya Wizara kwa utendaji uliotukuka kwenye utekelezaji wa *REA Phase II*. Wilaya ya Wanging'ombe kuna vijiji vinahitaji *transformer* tu na *LV line* ya kilomita moja mpaka mbili ili wananchi wapate huduma ya umeme. Niliwahi kumwandikia Waziri lakini hadi leo hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Vijiji hivyo ni Lusisi, Ihanja, Idindilimunyo, Luduga sekondari, Igelehedza, Mpuhilu, Igelango na Ipunda. Majibu niliyopewa toka *REA* ni kuwa *quantities* za mkataba wa *REA phase II* zimekwisha. Sasa swali langu, je, mradi mlioanzisha *REA* kutoa umeme kupeleka Kijiji cha Itengelo ambacho hakikuwepo kwenye mpango wa *REA II* zimetoka wapi na kwa nini *REA* wanaanzisha miradi bila kuhusisha uongozi wa Serikali ya Wilaya pamoja na Bunge?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri atekeleze ombi hili la wananchi wa Wilaya ya Wanging'ombe.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nashauri ni kwamba, *TANESCO* wasipokee mradi huu mpaka wajiridhishe pasipo shaka kuwa umekamilika kufuatana na mkataba. Yapo maeneo mengi kama Imalinyi, Kanani, Ludinga nguzo zimewekwa lakini hakuna waya. Pia yapo maeneo zilifungwa *transformer* za size 50 ambazo zimekuwa zikiungua mara kabla ya kutumika. Zaidi ya *transformer* 40 kwa Mkoa wa Njombe zimebadilishwa baada ya kuungua. *Specifications* ziangaliwe upya kama ndizo sahihi kwani zimekuwa zinaungua hasa wakati wa mvua na radi. Sasa hivi ni kiangazi tatizo hili halipo, lakini mvua zitakaporudi linaweza kujirudia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Wanging'ombe ina vijiji 106. Katika mpango wa *REA phase II* na *phase I* ni vijiji 42 tu ndivyo vina umeme. Naomba mpango wa *REA phase III* Serikali ipeleke umeme kwenye vijiji vilivyobaki ambavyo ni takribani vijiji 64.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuhakikisha nishati ya umeme inapatikana. Nawapongeza Makatibu Wakuu wa Wizara na Wakurugenzi wa taasisi zote zilizopo ndani ya Wizara kwa jinsi wanavyojituma kuhakikisha nchi yetu inaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuwekea jiwe la msingi mradi wa Kinyerezi ambao utakapokamilika utakuwa msaa kwa wananchi wa Tanzania. Pia nipongeze Serikali kwa kupata fursa ya ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Uganda kwenda Tanga. Ni jambo jema na lenye tija kubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza EWURA kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha wananchi wanapata huduma mbalimbali. Hata hivyo, kila panapo mazuri hapakosi changamoto zake. Kwa kweli kumekuwa na lawama nyingine ambazo haziwahusu EWURA, lakini kwa kuwa EWURA ndiyo wanaotoa leseni za mafuta basi lawama zote zitawaendea wao na lazima wazipokee, kwa mfano, ukaguzi wa mazingira. NEMC ni tatizo kubwa kwa wafanyabiashara wa mafuta. Gharama ni kubwa sana kwa watu wa mkoani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kukaa pamoja na NEMC kuona utaratibu gani mzuri ambao utafaa kwa kuwasaidia wafanyabiashara. Nami naweka maslahi yangu wazi kuwa ni mdau wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa mafuta ni jambo jema sana, naipongeza EWURA kwa kuwa makini na kazi yao. Kwa uzoefu wangu wa sekta ya mafuta sijaona wakipokea rushwa na hawana mazungumzo na mtu yeyote. Bado nawashauri, EWURA wamezidi kuwa kama mapolisi wapunguze misimamo, watoe elimu kwa wafanyabiashara, tukielimika tutafuata sheria za nchi na mambo yatakwenda vizuri tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa TPDC nitazungumzia juu ya mauzo ya gas. Tumekuwa tukitumia gesi kama chanzo cha umeme peke yake, ni vyema tukaongeze vyanzo vingine vya umeme kama mkaa wa mawe na maji tupate kuuza gesi yetu nchi za nje. Gesi inatakiwa na nchi nyingi za Afrika Mashariki, tungeweza kuiuza nchi ingepata pesa za kigeni zingesaidia kuuza uchumi wetu. Tumepata bomba la mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga, basi bomba hilo lingekwenda sambamba na bomba la gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, REA. Nawapongeza sana kwa kazi nzuri ya kusambaza umeme vijijini. Naomba katika Mkoa wa Dar es Salaam wakamilishe umeme maeneo ya Mianzini, Vikunai, Vijibweni na Kisarawe II.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuweke *transformer* katika maeneo ambayo umeme mkubwa wa kutoka Kigamboni kwenda Pemba Mnazi umepita juu kwa baadhi ya vijiji na wananchi wanaangalia kwa kuwa hakuna *transformer*.

Mheshimiwa Naibu Spika, TANESCO. Nawapongeza sana kwa kuwa tatizo la kukatika umeme mara kwa mara limepungua kwa kiasi kikubwa sana. Endeeleni hivyo. Mameneja wa TANESCO Wilaya ya Temeke wanafanya kazi

nzuri sana na ni wepesi kujibu pale panapotokea hitilafu za umeme. Nampongeza Mkurugenzi na timu yake yote wanajitahidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. RISALA S. KABONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekua na tatizo kubwa la ukataji wa miti na kuvamia mapori kwa ajili ya uchomaji wa mkaa baada ya ujangili wa wanyama sasa ni ujangili wa misitu. Namtaka Waziri atoe majibu ni namna gani Serikali hii kupitia Wizara hii imejipanga kuzuia au kupunguza matumizi ya mkaa hasa mijini ambako kuna nishati mbadala ya gesi na soko kubwa la mkaa limeelekezwa huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukataji wa miti kwenye mapori umeendelea kusababisha mabadiliko ya tabianchi ambayo yanasababisha mafuriko sehemu kubwa nchini. Mafuriko haya yanatokana na ukataji wa miti ambayo huzuia kingo za mito na hivyo kusababisha mafuriko makubwa. Namtaka Waziri atoe majibu ya kina ni namna gani amejipanga kuokoa misitu kwa kwa faida ya kizazi cha sasa na kizazi kijacho.

Mheshimiwa Naibu Spika, namtaka Waziri atoe majibu ni kwa namna gani Serikali imeweka mkakati wa kudhibiti wachakachuaji wa mafuta ya magari ili kuondokana na adha ya uharibifu wa magari.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashuhudia matumizi ya *solar* kama umeme mbadala maeneo mengi nchini na hasa mijini. Namtaka Waziri anipe majibu ni kwa namna gani zinaweza kusaidia wananchi wa vijijini ili watumie nishati hii kwa wingi kwa kuuza *solar* kwa bei nafuu kwenye maduka ya Serikali ili wananchi wengi wafaidike na nishati hii. Naomba Waziri anipatie majibu haya kwa faida ya wananchi wetu wa vijijini.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu, uzima na afya njema ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka Waziri wa Nishati na Madini afahamu kuwa mwaka 2012 Mtwara na viunga vyake kulitokea vuguvugu la gesi na wananchi wakidai haki ya ajira kupitia sekta hii muhimu, lakini kwa makusudi kabisa Serikali ilitumia nguvu kubwa kuwapiga wana Mtwara na hata kuwaua kwa risasi akiwemo mama mjamzito eneo la Mkanaled. Wapo waliovunjwa viungo vya miili yao na wapo waliochomewa nyumba moto na wapo waliopoteza mali na rasilimali ambako kulifanywa na vyombo vya dola.



Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali baadaye iliunda tume ya kuchunguza athari za vurugu hizo ambayo iliongozwa na Chara Mwijage, lakini cha ajabu mpaka leo hawajaleta mrejesho na wananchi pamoja na askari kadhaa pia wameathirika sana. Je, ni lini Serikali italipa athari hizi kama ilivyoahidi?

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa kutumia gesi majumbani ambao utaanza Dar es Salaam, Mwanza, Tanga na maeneo mengine, tayari mchakato wake umekamilika maeneo hayo isipokuwa Lindi na Mtwara ambako gesi yenyewe inatoka, wanasema watafanya upembuzi yakinifu. Ni jambo la ajabu sana Bomba la gesi limejengwa kwa miezi 18 tu limekamilika ila kuleta maendeleo Kusini Serikali inaleta kigugumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri aseme ni tarehe ngapi huo upembuzi umefanyika maana mimi ni Mbunge wa Jimbo sina taarifa yoyote Mtwara? Je, ni lini gesi itasambazwa majumbani Mtwara na Lindi na ni kwa nini Waziri asianze Mtwara na Lindi ambako gesi inatoka na ipo karibu?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara mjini kuna mitaa mingi sana kama vile Chipuputa, Kihoro, Komoro, Mbawala Chini, Lwelu, Dimbuzi, Kata ya Mtawanya, Likombe, Mitengo na Naliendele maeneo mengi nguzo za umeme hazijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unatoka Mtwara mjini ambapo kuna *plant* ya kufua umeme, Makao Makuu ya TANESCO Mkoa umeme hakuna. Wananchi wanauziwa nguzo kwa pesa nyingi ambayo hawana uwezo kutokana na hali ngumu kiuchumi kwa kuwa fursa za ajira hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara kwa niaba ya wananchi wa Mtwara, kupeleka nguzo kata zote za Mtwara mjini na wasiwape wananchi mzigo wa kulipia nguzo kwa kuwa wanatakiwa kunufaika na rasilimali ya gesi ikizingatiwa ndiyo waangalizi wa miradi yote ya gesi ambayo ni muhimu kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pesa ya kuunganisha umeme hii iliyosemwa imepunguzwa hadi 99,000, bado ni nyingi, wananchi wengi hali zao ni mbaya kiuchumi, hivyo wanashindwa kumudu gharama hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba gharama hii ya 99,000 iondolewe kwa wananchi wa Mtwara na Lindi kwa kuwa rasilimali hii muhimu inalindwa na wananchi hawa, hivyo ni vyema wakalipa gharama za umeme na siyo kupewa mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba la gesi liko nje sana, mimi kama Mbunge nimekuwa nawaasa wananchi walinde rasilimali hii muhimu kila siku, hivyo Wizara ihakikishe inafunika Bomba hili na hasa maeneo yaliyoathirika na

mvua. Nimeeleza hili kwenye Kamati (TPDC) na leo naiomba Wizara bomba lipo nje sana Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msimbati inakotoka gesi yenyewe Serikali inashindwa kujenga barabara ya lami ya kutoka mjini. Ni jambo la ajabu sana hakuna kituo cha afya, maana ni kata kwa mujibu wa maeneo ya kiutawala, kwa nini Serikali isijenge kituo cha afya? Jengeni tafadhali.

Sambamba na hilo, Mtwara nzima hakuna hata shule moja au hospitali ambayo imejengwa kwa rasilimali hii inayotoka mkoani humo. Hivi naomba kuuliza, wananchi wa Mtwara wakidai haki hii ni dhambi?

Mheshimiwa Naibu Spika, namsihi sana Waziri katika hotuba yake kueleza asilimia 94 ni maendeleo, basi aiangalie Mtwara kwa namna ya kipekee kabisa ili malalamiko yaweze kwisha na Watanzania wanufaike na rasilimali hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mrabaha ni muhimu sana kwa wana Mtwara, mwekezaji wa kiwanda cha Mbolea anaomba gesi kwa kununua Msanga Mkuu apewe ili wana Mtwara wapate ajira, Dangote apewe gesi maana anaagiza makaa ya mawe Afrika Kusini. Pia Wizara ijenge shule ya gesi Mtwara ili kuondoa malalamiko.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kuunga mkono hotuba ya Waziri. Pia naipongeza Serikali kwa mipango yake mizuri ya kusambaza umeme nchi nzima hata huko vijijini ili kuchochea maendeleo kwa wananchi na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Nyang'hardware lina kata 15 na vijiji 62 hadi leo hii ni kata mbili zimefikwa na umeme, nazo ni Kata ya Khalumwa na Nyang'hardware. Hata hivyo, Kata ya Khalumwa ndipo yalipo Makao Makuu, ni Kijiji kimoja tu ndiyo kina umeme. Pia Kata ya Nyang'hardware ni kijiji kimoja tu ndiyo umeme umefika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Busolwa tayari *line* imeshafika, lakini umeme haujawaka. Pia Kata ya Nyijunau nyaya za umeme zimepita juu kuelekea Kata ya Nyang'hardware ila Nyijundu haina umeme. Kata ambazo hazina kabisa umeme ni hizi: -

- Kata ya Bukwimba na vijiji vyake;
- Kata ya Nundu na vijiji vyake;
- Kata ya Izunya na vijiji vyake;
- Kata ya Kafita na vijiji vyake;
- Kata ya Kakora na vijiji vyake;
- Kata ya Nyijundu na vijiji vyake;

- Kata ya Busolwa na vijiji vyake;
- Kata ya Kaboha na vijiji vyake;
- Kata ya Shabaka na vijiji vyake;
- Kata ya Mwingiro na vijiji vyake;
- Kata ya Nyaburanda na vijiji vyake; na
- Kata ya Nyamtukuza na vijiji vyake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, tukiipitisha bajeti hii umeme upelekwe kwenye kata hizo, nitashukuru sana.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kwanza kabisa kuunga mkono hutuba ya Waziri wa Nishati na Madini asilimia mia moja. Nishati na Madini ni sekta muhimu sana katika kuchangia Pato la Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ni kichocheo kikubwa katika kuleta mapinduzi na mageuzi ya uchumi kutoka uchumi duni na tegemezi na kuwa uchumi wa kisasa na wa kujitegemea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwenyezi Mungu ameijalia nchi yetu vyanzo vingi kama siyo vyote vya nishati kama vile maji, jua, upepo, makaa ya mawe, gesi, joto ardhi na hata nishati kutokana na madini ya *Urani*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na neema hii kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia katika nchi yetu, kinachotakiwa hapa hivi sasa ni kuwekeza zaidi katika nyanja za uzalishaji, usafirishaji na usambazaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kupitia Shirika la Usambazaji Umeme nchini *TANESCO* na kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*) imetekeleza miradi mingi mikubwa na midogo mbalimbali nchini naipongeza sana Serikali na hasa baada ya kugunduliwa kwa kiasi kikubwa cha gesi hapa nchini kumepelekea kuzalishwa kwa umeme wa gesi katika miradi ya Kinyerezi I na II na kuondokana na utegemezi wa uzalishaji wa umeme na maji na mafuta mazito. Uzalishaji huu wa gesi nchini ni chachu ya kuzalisha umeme kwa wateja na hasa wale wa vijijini na wa kipato cha chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini kwa jitihada zake kupitia Shirika la Umeme nchini na Wakala wa Nishati Vijijini *REA* kwa utekelezaji wa miradi ya *Electricity V* na ile ya Wakala wa umeme Vijijini katika maeneo kadhaa ndani ya Wilaya ya Mbogwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali maeneo yaliyopelekewa huduma; Mbogwe, Ngemo, Nanda, Ilolangula, Isebya, Ikobe, Ikuguigazi, Lulembela, Nyakapera, Bukandwe, Masumbwe, Iponya, Nhomolwa na Lugunga. Hata hivyo zipo Kata mbili za Nyasalo na Bungonzi bado

hazijapatiwa huduma hii muhimu ya umeme na inayo matumani makubwa kwa Serikali kupitia mpango wake kabambe wa *REA Phase III*. Vijiji vyote na Kata zote zitapata huduma hii muhimu ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini nchini imekuwa na mchango mkubwa katika ukuzaji wa Pato la Taifa. Wilaya yetu ya Mbogwe wamejali kuwa na madini ya dhahabu na zipo leseni za utafiti muda mrefu. Hata hivyo, zipo changamoto nyingi katika eneo hili la leseni za utafiti hasa utafiti wenyewe kuchukua muda mrefu.

Kampuni ya Mabangu inayo leseni ya muda mrefu wa utafiti katika maeneo ya Kata za Nyakafura, Lugunganya na Bukandwe. Utafiti katika eneo la leseni ya Mabangu *Resolute* umechukua muda mrefu sana na kupelekea malalamiko yasiyokuwa ya lazima kutoka kwa wananchi hasa wenye nia ya kushiriki katika shughuli za uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yametolewa mara kwa mara kwa Wizara kuitaka Kampuni ya Mabangu na mshirika wake *Resolute* wafungue mgodi na wakishindwa kufungua mgodi ni vyema wakaliachia eneo hilo wakapewa wachimbaji wadogo wadogo. Tunaikumbusha Wizara kuitaka Mabangu na *Resolute* wafungue mgodi kwa maslahi ya Wilaya yetu ya Mbogwe. Nawasilisha.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, kwanza kabisa nakupongeza kwa hotuba yako nzuri. Pili, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii naomba nichangie maeneo yafuatayo:-

(i) Sekta ya Umeme, suala la kukatikakatika kwa huduma ya umeme Wilaya za Mpwapwa, Kongwa, Gairo; je, ni sababu gani zinazofanya umeme kukatikakatika katika Wilaya hizo na kusababisha vitu vingi kuungua. Mheshimiwa Waziri ana maelezo gani kwa wananchi wa maeneo hayo kwa kuwa ni kero kubwa sana.

(ii) Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipatia umeme Vijiji vya Makutupa, Bumila, Mbori, Inzomvu, Tambi, Mlembule, Mwenzele, Nana, Mafuto, Majani, Mugoma, Mzogole, Kisisi, Sazima, Igoji Kusini (Isalaza), Chamanda, Kiboriani, Makanana, Chibwengele, Pandambili (Jimbo la Mpwapwa) Makawila, Chimaligo, Kazania, Kiegea na Ngalamilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Madini, kwa kuwa Wilaya ya Mpwapwa kuna Wachimbaji wadogo wadogo Vijiji vya Winza (wanachimba

rubi), Tambi, Mlembule (wanachimba copper) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo wa Wilaya ya Mpwawa ili waboreshe hali ya uchimbaji wa madini kuliko hivi sasa wanatumia vifaa duni. Je, Mheshimiwa Waziri au Naibu watatembelea lini Wilaya ya Mpwapwa ili kukutana na wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja hoja hii na kumtakia Mheshimiwa Waziri kila la heri, bajeti yake ipitishwe na Bunge hili Tukufu.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, shukurani kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam wa Wizara kwa hotuba nzuri yenye kuleta matuamini kwa Watanzania. Mradi wa umeme wa REA kwa Kisiwa cha Mafia umebakiza vijiji na maeneo 10 kukamilika, navyo ni vijiji vya Gonge, Jojo, Mariam, Bani, Jibundu, Juani, Chole, Dongo na Maeneo ya Tumbuju, Bwejuu na Tongani. Ombi langu kwa Wizara ni vijiji na maeneo husika viingizwe kwenye mradi wa REA Phase III.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni uzalishaji wa umeme kwa sababu umeme Mafia unatokana na chanzo cha mafuta yanayoendesha majenereta yaliyopo. Kutokana na gharama kubwa ya ununuzi wa mafuta na matatizo ya usafiri wa mafuta hayo kwa njia ya bahari, ombi letu wananchi wa Mafia ni kwamba, Serikali sasa iunganishe na umeme wa SONGAS kupitia kupitishwa kwa *submarine cable* kutokea Nyamisati kwenda Kilindini takriban kilomita 50 ili kuondokana na adha ya kusafirisha mafuta mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utafiti wa mafuta na gesi, katika Kisiwa cha Mafia ni jambo linalofanywa mara kwa mara. Kwa habati mbaya sana wananchi wa Mafia wamekuwa hawapewi taarifa tunaomba Wizara na Waziri wakati atakapokuwa anajibu awaeleze wananchi wa Mafia kama mafuta au gesi vimegundulika Mafia au hapana ili kuondoa hali ya sintofahamu kwa wananchi wa Mafia.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine kwenye ugunduzi wa gesi hasa maeneo ya kina kirefu cha bahari yaani *off share* maeneo ya Kusini mwa Tanzania. Mpakani mwa Wilaya ya Kilwa na Mafia, katikati ya bahari kuna visima viwili ambavyo kimpaka kimo katika Wilaya ya Mafia, lakini kutokana na matatizo ya usafiri shughuli za uchimbaji na utafiti zimekuwa zikifanyika kutokea Wilaya ya Kilwa.

Swali je, wananchi wa Mafia wananufaika vipi na visima hivi ambavyo kimpaka vipo Mafia lakini shughuli za uchimbaji zinafanyika Kilwa?

Suala lingine ni bomba jipya la gesi kutoka Kusini kuja Dar es Salaam, ujenzi umekamilika kwa asilimia 100. Swali, je, ni lini bomba litaanza kusafirisha gesi kutoka Kusini kwa matumizi ya kibiashara? Swali lingine, ni lini umeme ghafi utachakatwa na kuweza kutumika kwa matumizi ya majumbani?

Mheshimiwa Naibu Spika, natanguliza shukurani na naunga mkono hoja.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza Sekta ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jumuiya ya Ulaya inatekeleza sera ya malighafi (mkakati wa malighafi) kwa lengo la kukabiliana na upungufu wa madini muhimu kwa maendeleo ya nchi za Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati huo wa malighafi wa jumuiya kuna madini zaidi ya 26 ambayo Jumuiya ya Ulaya imeyawekea mkakati wa kuyatafuta na kuyapata kwa gharama yoyote, mahali popote yalipo. Nashauri Wizara itambue uwepo wa mkakati huo na ijipange vizuri kuwezesha Tanzania kunufaika na madini yaliyo katika kundi hilo la madini muhimu kwa kuzingatia mtazamo wa Nchi za Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mkakati huo wa Jumuiya ya Ulaya wa malighafi *raw material strategy*. Jumuiya ya Ulaya inaelekeza nia yake kusaidia Mataifa mbalimbali katika jitihada zake za kutafiti upatikanaji na madini mbalimbali na kuweka kumbukumbu za uwepo madini hayo hasa madini muhimu. Nashauri Serikali ijipange vizuri kunufaika na mpango huo wa Jumuiya ya Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tunajipanga kuwa nchi ya viwanda pamoja na jitihada nzuri zinazofanyika kusambaza umeme vijijini kuna changamoto ya umeme unaosambazwa maeneno mbalimbali kuwa wa *low voltage*. Nashauri jitihada ziongezwe za kuwekeza miundombinu ya kuongeza nguvu za umeme na hivyo kuondokana na tatizo la umeme wa *low voltage*. Kwa kufanya hivyo, itasaidia sana kupatikana umeme wa uhakika utakaosaidia mapinduzi ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kielelezo namba nne katika ukurasa wa 83, kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini hadi Aprili, 2016 ni asilimia 1.9 iliyoendelezwa. linaonekana kama nchi tuna kazi kubwa ya kufanya hasa kuendeleza kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na kuwahimiza kuendeleza visima vya gesi ambayo imeshagundulika. Kama nchi lazima

tujiulize kwa nini inachukua muda mrefu kuendeleza visima vya gesi asilia na tunatakiwa kufanya nini kuendeleza kwa haraka visima vya gesi asilia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uzima na kuniwezesha kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi. Hivyo, naanza kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wananchi haturidhishwi na mwenendo wa utolewaji wa fedha za bajeti zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa REA. Takwimu zinaonyesha kwamba, katika miaka mitatu ya fedha iliyopita 2013/2014 hadi Aprili, 2015/2016, wastani wa REA umekuwa kwa asilimia 60 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, wananchi hawaridhishwi na uwekezaji wa vinasaba katika mafuta. Ili hali, TRA wana vituo njiani vya ukaguaji wa mafuta ni kupoteza pesa za walipa kodi wa Tanzania, ni kuwanyanyasa walipa kodi na kutajirisha mtu binafsi anayetengeneza vinasaba. Hivyo, Waziri atueleze ni kwa nini wanaona tabu kuondosha vinasaba kwani havisaidii?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, mgodi wa makaa ya mawe, Kiwira, utaanza uzalishaji utaongeza umeme na uzalishaji huu utaboresha sana upatikanaji wa umeme wa kufikia malengo tunayotarajia kuliko kutofanya. Aidha, kudharau au kujali maoni ya wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kupeleka fedha, zinazoidhinishwa kwa wakati na kupelekwa kama vile zilivoidhinishwa badala ya kupeleka pungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, Serikali itueleze kuhusu madini ya *Tanzanite*, inakuwaje yanauzwa India, Kenya na Afrika Kusini kwa wingi zaidi ya Tanzania na Tanzania, inachukua nafasi ya nne na India nafasi ya kwanza ilihali, madini hayo yanapatikana Tanzania peke yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hatuoni kama ni uharamia unaofanywa na wawekezaji na hata wachimbaji wadogo kuuza holela madini haya? Serikali haina udhibiti wa kutosha kwani Serikali haioni umuhimu wa kufunga mgodi mpaka ijipange kuliko kumalizika kwa madini bila Tanzania kupata faida yoyote na badala yake kuambulia aibu na kukosa Pato la Taifa na kuwapa umaarufu nchi nyingine na Tanzania kuendelea kuwa maskini na kutajirisha nchi nyingine ili hali madini yale yanatoka Tanzania pekee.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa kuwa, Serikali haina dhamira ya dhati ya kudhibiti madini yanayotoroshwa, ambayo ni ghafi kwani haitoi kauli yoyote. Hivyo, tunaomba, na tunaishauri Serikali, usimamizi wa migodi hii,



uangaliwe na Taifa letu lipate pato la kutosha kuliko kunufaisha Mataifa mengine ambayo hayazalishi madini haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la gesi ni muhimu na litasaidia Tanzania kupata umeme mwingi na kusaidia viwanda kuimarika. Vile vile iuzwe, itumike majumbani katika shughuli mbalimbali kuliko kuendelea kununua kwa makampuni mengine ya kuuza wakati, Tanzania tunayo gesi ya kutosha. Pia, Serikali iandae mpango mkakati utakaoweza kusimamia vizuri gesi asilia pamoja na kutafuta masoko madhubuti na ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali iwekeze katika miundombinu na utalaam wa madini ya vito ili kuwezesha ukataji na uuzaji wa Tanzanite kufanyika hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, Serikali isimamie kwa umakini wa hali ya juu ukamilishwaji wa miradi na vipaumbele vya uzalishaji vya umeme ili kutuwezesha kupata umeme wa kutosha hapa nchini ili tuwe na viwanda vya kutosha vyenye kukidhi mahitaji ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa Serikali ijipange kutekeleza haya kwa moyo wa dhati na sio kuwarubuni Watanzania. Tunapenda kuona Tanzania inaneemeka na rasilimali zake na kuipata Tanzania tuitakayo, iliyoimarika na kupiga hatua za maendeleo mbele zaidi na siyo kila siku tukawa watu wa kurudi nyuma tu na ku-enjoy mafanikio ya wengine tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia nawatakiwa kila la kheri Serikali na naiombea iwe na moyo wa dhati na kutekeleza yale tunayowaelekeza na kuyafanyia kazi kwa wepesi zaidi ili kuleta maendeleo ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha maoni ya wananchi wangu. Ahsante sana.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwapongeze viongozi wote wa Wizara ya Nishati na Madini katika kufanikisha uandaaji mzuri wa hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini ni muhimu katika mpango wa Serikali wa maendeleo na kufanikisha nchi yetu kuwa ya viwanda, kwa kuwa nishati ni kiungo muhimu katika viwanda vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, REA; kwanza naomba Waziri aendelee kuwa imara katika Wizara hii na kuwezesha umeme vijijini kufikia malengo. Katika Jimbo la Nsimbo Mkoani Katavi, jimbo lina kata 12, lakini kata nne tu ndiyo zilizopata umeme wa REA. Sambamba na hilo, umeme umepita Kijiji cha

Kapalala bila kuwekewa *transformer*. Tunashauri Wizara ikamilishe umeme katika kijiji hicho tukizingatia kuna wananchi wahitaji. Vile vile, tunahitaji, majibu ya Waziri ni lini kata zilizobaki nane zitakamilika kupata umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, gridi ya Taifa; Mkoa wa Katavi ni moja ya mikoa hapa Tanzania, ambayo haina umeme wa uhakika, yaani wa gridi ya Taifa. Hivyo, tunatumia umeme wa jenereta ambazo zilitolewa Shinyanga na tayari ni chakavu hazifanyi kazi kulingana na uwezo. Hivyo basi, tunahitaji Serikali ikague umeme uliopo Wilaya jirani ya Kaliua kwa kuwa ni jirani sana na Jimbo la Nsimbo. Hivyo, tunahitaji kauli ya Serikali ni lini itafanya upembuzi yakinifu wa kuleta umeme Jimbo la Nsimbo kupitia Kata ya Ugala?

Mheshimiwa Naibu Spika, madini; mradi wa wachimbaji wadogo wa Benki ya Dunia, Jimbo la Nsimbo ni mojawapo lina vijiji 11 ndani ya kata sita zina wachimbaji wadogo. Hivyo, tunaomba Serikali kuchagua maeneo ya mfano kati ya hayo saba. Naomba na Jimbo la Nsimbo tuna sehemu mbalimbali. Kwa mantiki hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko la Nsimbo kuwa kati ya vituo saba vya mfano.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la wachimbaji wadogo; wachimbaji wadogo, ambao wana uwezo wa kuwa na leseni, waweze kupata leseni kwa mujibu wa Sheria (*Primary Licence*) na waweze kurahisisha wananchi wasio na leseni kuchimba katika maeneo yao na kuweza kuuza dhahabu na kupata mapato kuwasaidia kujikimu wao na familia zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara ikitoa leseni kubwa *mining licence (ML)* wenye uhalali huo wanakataza wananchi kuchimba. Mfano mzuri ni kampuni ya SAMBARU, Kata ya Ibindi iliingia katika mgogoro na wananchi na hali siyo shwari. Pia, eneo la Dirifu, Kata ya Magamba nako kulitokea vurugu Januari, 2016. Kwa mantiki hiyo, tunahitaji Serikali kutoa tamko vijiji vifuatavyo viwe kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Jimbo la Nsimbo, Kata ya Machimbi, Kijiji cha Katisunga na Kapanda; Kata ya Ibindi, Kijiji cha Ibindi, Kapandamu na Kasherami; Kata ya Sitalike, Kijiji cha Mtisi; Kata ya Urwira, Kijiji cha Urwira, Usense; na Kata ya Itenka, Kijiji cha Msangama. Jimbo la Mpanda Mjini, Kata ya Magamba, Kijiji cha Dirifu *Society*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana maeneo ya vijiji hivyo kuwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo kwa kuwa eneo la awali ni Wilaya ya Tanganyika, eneo la Kipalamsenga, ambako kuna madini zaidi ya aina ya shaba. (*Copper*)

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za maliasili kwa wachimbaji madini utafutaji wa madini kuna wakati wananchi au kampuni huingia katika hifadhi za

misitu. Wananchi hutozwa gharama za uharibifu wa misitu. Tatizo lililopo ni tozo zipo kwa ukubwa wa eneo badala ya kuangalia idadi ya miti na kupelekea watu wengi kushindwa kumudu gharama hizo. Hivyo, tunaomba, Wizara hizi mbili zikae pamoja na kuangalia gharama hizo, zipitiwe upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa mafuta Lake Tanganyika kwa kuzingatia maendeleo ya nchi tunahitaji Serikali kupitia Wizara isaidie utafiti wa mafuta katika eneo la Ziwa Tanganyika. Hivyo, taarifa ni muhimu nasi wananchi kujua maendeleo ya utafiti huo na vyema kuwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maelezo hayo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. SEIF H. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwasilisha maombi makuu mawili. Moja, ni kuomba Wizara kuweka msukumo wa malipo ya fidia kutoka TANESCO kwenda kwa wananchi wa Kata ya Simbo, Chabutwa na Mwisi kwani kwenye ziara ya Naibu Waziri Mheshimiwa Merdard Kalemami alikuja Jimboni na Meneja wa TANESCO Mkoa wa Tabora aliahidi mbele yake kuwa pesa za fidia zipo na hivyo wanasubiri wamalize tathmini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo naomba Wizara ipeleke msukumo kwa Meneja wa TANESCO ili kuweza kuwalipa wananchi wa Kata hizo husika ili kuondoa misugvano isiyo ya lazima, hizi ni fedha ambazo walipaswa walipwe toka mwaka 2010 mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Wizara ya Ujenzi na Nishati na Madini, napenda kuwasilisha mawazo yangu juu ya kuongeza *substation* nyingine ndani ya Wilaya ya Igunga tofauti na ile iliyopo Wilaya ya Nzega katika Mji wa Nzega Ndogo toka pale Nzega Ndogo kwenda Choma ni karibu kilomita 30 na kutoka Choma kwenda Ziba kwenda Igunga ni kilomita 50, jumla umeme umesafiri kilomita 110 bila kuwa na *substation*. Naomba pale Ziba tuwe na *substation*, iunganishwe umeme/waya toka Nzega kwenda Ziba ili kupunguza kukatika kwa maana njia ya Nzega Ndogo kwenda Choma nguzo zinapita kwenye majumba hivyo tukipata *substation* Ziba na *network* tokea Nzega, Ziba itarahisisha kupunguza tatizo la umeme Wilayani Igunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo tu nawasilisha.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Wizara hii kwa hotuba nzuri iliyojieleza vizuri kwa maslahi ya Watanzania kwa ujumla, pamoja na yote naomba Serikali iweke makazi katika suala lifuatalo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana hasa katika maeneo yanayozunguka migodi yetu. Suala hili

limesababisha mauaji ya vijana hawa wanaparamia migodi kuweza kupata chochote kama tunavyosikia mara kwa mara kwenye mgodi wa Nyamongo, Mkoani Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali yangu sikivu, Serikali inayotekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi inayoahidi kupanua wigo wa ajira kwa vijana, iweke mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba, migodi mikubwa kama Nyamongo inauza mchanga ambao hauhitajiki na mgodi kwa wananchi ili nao waende kusafisha na kupata japo kidogo katika rasilimali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini suala hili linawezekana na naamini kwamba, Serikali hii, haitashindwa kuweka utaratibu huu wa wananchi kupata mchanga huo kutoka migodini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha kwa Waziri wa Nishati na Madini vijiji ambavyo havipo kabisa kwenye mpango wa umeme wa REA Jimbo la Mbozi. Vijiji hivi ni pamoja na:-

Ikonga, Maninga, Iporoto, Twinzi, Halambo, Shasya, Mbuga, Rungwa, Hamwelo, Insani, Itentula, Mboji, Iyenga, Nsega, Ileya, Igaya, Magamba, Mtunduru, Naulongo, Iwalanje, Nambala, Mbulu, Myovizi, Ivufula, Isenzanya na Manyara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niaba ya wananchi wa Mbozi naomba Mheshimiwa Waziri awasaidie ili waingizwe katika REA phase III.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia makaa ya mawe yanayochimbwa Kijiji cha Magamba na Kampuni ya Wagamba Coal Company katika Jimbo la Mbozi kuna changamoto zinajitokeza. Kampuni hii haijawahi kulipa service levy katika Halmashauri ya Mbozi tangu uchimbaji wa makaa ya mawe uanzishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kampuni hii iagizwe kulipa service levy katika Halmashauri ya Mbozi ili kuchochea maendeleo. Pia kampuni hii ielekezwe kutengeneza barabara ya kutoka Magamba-Isansa-Shiwinga-Mlowo katika Jimbo la Mbozi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa katika mipango ya uanzaji wa miradi ya Mchuchuma wa makaa ya mawe na Liganga chuma. Wizara ya Nishati na Madini tarehe 19/4/2016 ilijibu kuwa fidia ya kulipa wananchi itafanywa mwezi Juni, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe fidia hii ilipaswa kulipwa mwezi Februari 2016. Wizara ya Viwanda na Biashara imetenga sh. 5,000,000,000 Liganga na kwa Mchuchuma sh. 5,000,000,000 kiasi kilichopangwa ni sh. 10,000,000,000 ambacho ni kidogo ukilinganisha na fidia ya sh. 14,000,000,000. Naomba maelezo pesa nyingine ambazo ni pungufu zitapatikanaje ili ziweze kulipwa katika kipindi kifupi kilichobaki cha Juni, 2016.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya Wizara ya Nishati na Madini kwa kazi nzuri hasa ya usambazaji wa umeme Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali izingatie mipango ya umeme Vijijini (REA) ili itekeleze mipango mizuri ya kusambaza umeme ambao ni muhimu kwa uchumi wa viwanda. Naomba Serikali izingatie utekelezaji wa miradi ya Halmashauri ya Mbeya ambayo wananchi waliahidiwa na kusesitiza kuwa bajeti ya kusambaza umeme katika Vijiji vya Halmashauri ya Mbeya umetengewa shilingi bilioni 52.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara na Serikali kwa michakato ya miradi mikubwa ya madini ikiwemo *niobium* ya milima ya Panda Hill.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 62 hotuba inaonesha haya madini ya *niobium* yanapatikana Wilaya ya Songwe. Naomba isahihishwe kuwa haya madini ya *niobium* yanapatikana katika milima ya Panda Hill (Songwe) Wilaya ya Mbeya na siyo Wilaya ya Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na madini ya *niobium*, milima ya Panda Hill yamegunduliwa madini ya *calcium* ambayo yanatumika kutengeneza mbolea ya NPK. Naomba Serikali iweke mkakati wa haraka kufufua mradi huu na kuwanufaisha wananchi wa Wilaya ya Mbeya, kuongeza uchumi na pia uzalishaji wa mbolea za NPK hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kupongeza shirika la TANESCO kwa kazi nzuri licha ya changamoto mbalimbali. Napendekeza, Serikali ichukue hatua za makusudi kupunguza mzigo mkubwa wa madeni ya TANESCO hasa yale ya fedha za kigeni. Kuna uwezekano mkubwa wa *restructuring* ya hii mikopo iwe ya shilingi badala ya *forex*. Pia hatua za makusudi zichukuliwe, kuondokana na kununua umeme kwa fedha za kigeni, kutoka kwa wazabuni wa TANESCO - ikiwemo Songas.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza Serikali iweke kipaumbele cha umeme wa joto ardhi ambao gharama iko chini na upatikanaji wake ni wa uhakika na hauna madhara kwa mazingira. Serikali ihakikishe mradi wa joto ardhi wa ziwa ngozi uanze na kukamilika haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua za kuimarisha rasilimali watu katika shirika la TANESCO ili iendane na usambazaji wa REA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mungu kwa neema za kutujalia sote uhai. Kipekee nampongeza Mheshimiwa Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Dkt. Merdad Matogolo Kalemuni, Naibu Waziri wa Nishati na Madini pamoja na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kero yangu kubwa ni kuhusu gharama kubwa ya biogas kwa kuwa maeneo ya vijijini ni wafugaji hususan wanawake wa Kilimanjaro. Naomba iwepo namna ya kupunguza gharama ya kujenga na kuunganisha nishati na madini ya biogas majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, michango mikubwa watumiaji wanayotozwa kwa ajili ya EWURA hainiingii akilini na wala haipendezi kwa watumiaji wa maji na umeme wanavyotozwa na EWURA katika ankara tofauti, bahati mbaya EWURA yenyewe hairejeshi chochote kwa wananchi kama CSR, natumaini kuona wakitoa mchango wa kuwaelimisha wanawake kwenye ujasiriamali na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wengi wa umeme vijijini ni kwa ajili ya taa na baadhi luinga na kuchaji simu. Namwomba Mheshimiwa Waziri awaagize Mameneja wa Mikoa wateremshe tozo za vijijini ili familia nyingi zinufaike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tozo la umeme kwenye shule na vyuo; kumekuwepo na malalamiko makubwa sana kwa wamiliki wa maeneo tajwa. Namwomba Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kurekebisha tatizo hili, mfano, Kibosho School of Nursing, Chuo hiki kiko Moshi Vijijini katika Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo. naunga mkono hoja.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Profesa Muhongo pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba na kazi nzuri wanayoendelea kufanya. Kwa bahati mbaya sitapata nafasi ya kuchangia, yangu ni machache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Karagwe Vijijini ina vijiji 110 na kila kimoja bado kinahitaji huduma ya REA III. Orodha ya vijiji tayari tumeshawasilisha Wizarani, naomba sana Karagwe ipate REA III kuanzia Julai, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, Upinzani wamekuwa *objective* na ushauri wao naomba tuuzingatie hasa:-

- (a) Mapitio ya mikataba ya umeme wa *emergency*;
- (b) *Energy Mix Policy or National Energy Policy* isisahau *hydro-power* bado ni *potential* na *environmentally friendly* tuipe *weighting* ya kutosha;
- (c) Hoja za wachimbaji wadogo zina mashiko;
- (d) Dira ya *STAMICO* tuiangalie na tuizingatie *whether* kupewa *tail- end production segment* ni *economical* kwa *STAMICO*;
- (e) Mfuko wa *abandonment cost and environmental rehabilitation* haupo wazi, ni vema Serikali ikatoa maelezo ya uendeshaji wake; na
- (f) Sheria ya Watumishi iweke katazo kwa Watumishi wanapostaafu kujiunga na kampuni za nishati na madini kwani kwa hali ilivyo sasa ina-*attract rent seeking behavior*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeme wa *REA* katika Jimbo langu lenye vijiji 87 na mitaa tisa mradi wa *REA* II umehusisha vijiji vitatu tu. Hii inakuwa ngumu kujibu maswali ya wananchi. Nashauri kuwa *phase III* ihusishe vijiji vyote kama Mheshimiwa Waziri alivyoahidi wakati nimempelekea hoja hii kwa mapendekezo ya vijiji vitakavyohusika kwenye *REA phase III* vijiji au mitaa ifuatayo haijawekwa.

Mitaa ya Nanyamba Mjini, Natoto, Chitondela, Chikwaya, Mibabo, Vijiji Miule, Mtimbwilimbwi, Shaba, Mbambakofi, Hinju Mtiniko, Maili, Maranje, Ngorongoro, Misufini, Kiromba, Kiyanga, Mayembe Juu, Mayembe Chini na Mchanje.

Mradi wa *REA* Mtwara Manispaa eneo la Ufukoni, Mbaye na Mji mwema ambao *phase II* ulitakiwa kukamilika mwezi Juni unasukasua, hivyo usimamiwe ili ukamilike kwa wakati.

**MHE. RASHIDI M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri ya kusambaza na kusimamia nishati ya umeme. Hata hivyo, naomba ufafanuzi Mheshimiwa Waziri atakapofanya majumuisho katika maeneo yafuatayo:-



Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa chanzo cha nishati ya umeme wa gesi katika Mkoa wa Mtwara, hali ya usambazaji wa umeme hairidhishi. Pale ambapo umeme umefika hali ya kukatikakatika kwa umeme inaendelea kuwakatisha tamaa wananchi wa Mikoa ya Kusini hususani Wilaya ya Masasi. Kwa kweli ikiwa nishati ya mwanga wa kibitari inayoweza kuzimika kwa upepo wakati wowote inapaswa iwe tofauti na ile ya umeme. Kwa sisi watu wa Masasi inatuwia vigumu kutofautisha kutokana na kukatikakatika kila wakati bila ya taarifa yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atueleze hali hii itakwisha lini? Je, Serikali haioni sababu ya kuwa na njia mbadala ya umeme ambayo kwa sasa umeme unaokuja Masasi unapitia Tandahimba, Newala - Masasi kuelekea Nanyumbu? Matatizo yoyote ya umeme katika maeneo hayo yanatuathiri mara kwa mara wananchi wa Masasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunalo tatizo kubwa la kutofanyiwa marekebisho au matengenezo ya nyumba za wafanyakazi wa TANESCO zilizopo katika Kata ya Migongo, Jimbo la Masasi. Nyumba hizi zinageuka kuwa magofu wakati watumishi wanahangaika mahali pa kukaa. Naomba nijue mkakati wa Serikali kuhusu nyumba hizi ?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuwateua Mheshimiwa Profesa Muhongo na Naibu wake Dkt. Kalemani, tuna imani nao na tunawaomba pia tutawapa ushirikiano. Pamoja na pongezi hizo pia tunawapongeza sana Viongozi Wakuu wa Wizara hii, Katibu Mkuu na Watendaji wote wanayoyafanya katika kutekeleza majukumu yao vizuri sana, hongereni sana na naunga mkono hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nina mambo mawili ya kuomba:-

(i) Mradi wa umeme wa upepo Singida tafadhali tunaomba sana mradi huo uanze, tuna makampuni mengi yanayotaka kuwekeza huko na mengine yalishafanya tathmini ya fidia kwa wananchi na wananchi wanasubiri kulipwa fidia. Hii itasaidia sana kutuliza maswali.

(ii) Wachimbaji wadogo wa Sekerike, Hondo na Samsaru wanaomba wapatiwe umeme, pia kuna wawekezaji ambao ni ASHANTA wamezuia maeneo ambayo hawayafanyii kazi yoyote, hivyo inaleta mtafaruku sana kwa wachimbaji wadogo. Naomba Wizara iliangalie ili itende haki ya kuwapa wananchi walio tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu ya kumpongeza Waziri Profesa Sospeter Muhongo na Naibu wake Mheshimiwa Kalemani kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha nchi yetu inapata umeme. Aidha, nawapongeza kwa usimamizi mzuri wa Sekta ya Madini, nawatakiya kila la kheri chapeni kazi bila wasiwasi kwani Wabunge tuko nyuma yenu kuhakikisha mnakuwa katika mazingira rafiki ya kufanya kazi. Pia nawapongeza kwa kuwasilisha bajeti nzuri yenye kuleta matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali juu ya mpango wa umeme vijijini unaotekelezwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA). Yapo maeneo hapa nchini ambayo yana changamoto kubwa sana katika usambazaji wa umeme. Maeneo hayo ni yale ya visiwa vingi ambavyo viko katika maziwa na bahari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba ili kupunguza gharama za kutumia *marine cable* kupeleka umeme katika visiwa, basi REA wasambaze umeme huo kwa njia ya *solar* (umeme jua) Jimboni kwangu nina visiwa katika Ziwa Victoria vya Nafuba, Sozia, Namuguma, Machwela, Rwiga, Buyanza, Kwigali, Bwenyi na Nyakalango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa shughuli kubwa za kiuchumi katika visiwa hivi ni uvuvi, umeme huu utasaidia sana kuhifadhi mazao ya samaki pamoja na viwanda vidogovidogo vya kuchakata samaki na kutengenezea boti na mitumbwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kunipa afya ya kuweza kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya umeme ni nusu ya maisha ya binadamu hasa kwa wanawake kwa sababu mwanamke ni mdau mkubwa ndani ya nyumba; ikiwa umeme hamna au gesi basi kwake ni mtihani, itabidi afunge safari kutafuta kuni ili familia waweze kupata chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazingira ya ukataji wa miti kwa ajili ya kuchoma mkaa ili aweze kupikia au kufanya biashara. Miti inakwisha na nchi inakuwa na ukame kwa sababu ukataji wa miti unaharibu vyanzo vya maji na wafugaji wanahangaika kutafuta maji kwa ajili ya kuharibika kwa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini, wachimbaji wadogo wadogo: Watanzania wengi ni wachimbaji wadogo wadogo ndiyo ambao wana mchango mkubwa katika kulipatia Taifa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hutoa ruzuku kwa wachimbaji wadogo ili waweze kujiimarisha katika kazi zao, lakini la kusikitisha ruzuku hizi haziwafikii walengwa na kuanza kutoa malalamiko, mfano maeneo ya Mwanza, Geita na kadhalika. Naishauri Serikali iunde Kamati ya kusimamia jambo hili, ikibainika wahusika washughulikiwe, hayo ndiyo majipu ya kushughulikiwa kutumbuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishati ya mafuta ni muhimu sana katika maisha ya binadamu kama ilivyokuwa maji ni muhimu katika maisha ya binadamu na mafuta ni hali kadhalika, kwa sababu mafuta tunaendeshea magari, meli, ndege na pia kuendesha mitambo, kama hakuna umeme yanatumika kwenye jenereta. Hivyo, nishati ya mafuta inaleta uchumi katika Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha nchi hii haina *formula* ya bei maalum. Ukienda Dar es Salaam bei nyingine, Unguja bei nyingine, Ukienda Mtwara bei ni nyingine na nchi nzima bei hazilingani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaiomba Serikali ipange mpango maalum kwa kupanga bei ambayo inalingana ili wafanyabiashara wasiwanyonye wananchi, wengine ni wanyonge katika nchi hii wanahitaji kuangaliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa mchango huu, naomba kuwasilisha.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia REA inafanya kazi ya kusambaza umeme vijijini, pamoja na kufanya kazi hiyo katika Mkoa wa Iringa, Wilaya ya Iringa Vijijini kuna *substation* iliyopo katika Kijiji cha Tagamenda ambapo umeme umeanza kusambazwa kwenda mikoa mbalimbali ikiwemo Shinyanga na mingine

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu cha kushangaza, wanakijiji wanaofanya kazi ya kulinda umeme huo, hawajapata umeme hata huo wa REA. Swali kwa Wizara, hivi hawaoni kuwa hawawatendei haki wananchi wa Vijiji vya Tagamenda, Wangama, Ikuvilo na vingine ambao huishi karibu na kituo hicho *substation* kuunganisha umeme huo au hata wakapata umeme wa REA na wasiwe walenzi tu wa kituo na nyaya hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, anapohitimisha naomba kupata majibu ili tuweze kuondokana na adha hii kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia katika Wizara hii ya Madini mambo yafuatayo:-

Katika Mkoa wa Njombe Vijiji vingi havina umeme, mfano, katika Halmashauri ya Njombe Mjini, Kata tatu tu ambazo ziko mjini, wakati Kata kumi ni za vijijini hata kama vijiji hivi vina hadhi ya mji. Hivyo, naiomba Serikali ione ni namna gani inasaidia hizo kata kumi ambazo hazina mradi wa REA kwa sababu zina hadhi ya mji wakati kata hizo ziko vijijini, mradi wa REA ni wa vijijini tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ukataji wa miti huharibu mazingira, ili kuzuia ukataji wa miti bei ya gesi ipungue ili watu wengi watumie gesi kuliko kutumia kuni na mkaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa kuwa kuna vyanzo vingi vya kupata nishati, basi Serikali ifanye utafiti maeneo mbalimbali kwa kuzingatia rasilimali zilizopo kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kutengeneza nishati. Mfano, maeneo yenye mifugo mingi basi Serikali ione namna ya kupeleka program ya kutengeneza umeme au nishati ya gesi kutokana na kinyesi cha wanyama. Hali kadhalika maeneo yenye maji mengi au takataka nyingi kama maeneo ya mijini basi takataka hizo zitumike kutengeneza gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Njombe hasa Njombe mjini, inazalisha takataka nyingi basi takataka hizo zitumike kwa ajili ya kutengeneza gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Ludewa ina madini mengi ikiwemo chuma, makaa ya mawe na mengine. Naomba Serikali ihakikishe inasimamia uchimbaji wa madini ambayo yatatuongezea kipato. Wawekezaji wanaofika kwenye migodi hiyo ya Liganga na Mchuchuma wahakikishe wanapeleka huduma za jamii katika maeneo hayo ya Mchuchuma na Liganga pamoja na Wilaya yote ya Ludewa. Huduma hizo kama Umeme, Maji, huduma za afya na barabara za lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni kitu muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na ajira kwa wananchi wetu. Bado naendelea kuzungumza kuhusu Mikoa ya Pembezoni kwa kuchelewa kupata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa tunao umeme wa jenereta unaosaidiana na umeme kutoka Zambia ambao una changamoto zake,

naomba Serikali kuona umuhimu wa kutuunganisha na *grid* ya Taifa kutokea Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la usambazaji wa umeme vijijini huu wa REA, tukaongeze kasi kwa mikakati maalum kuharakisha vijiji vya mipakani kupata umeme huo, Kata zifuatazo Kabwe, Mirando, Kipili, Wampembe, Kala, Kasanga, Wampambwe, Sopa, Katete, Mambwenkoswe. Vilevile vijiji vya Bonde la Rukwa ukizingatia ni wakulima wazuri wa mpunga na alizeti wanahitaji kuwa na mashine za kukoboa mchele na kusindika alizeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kuwa bajeti ya nishati haikidhi mahitaji kwa Mkoa wa Rukwa, baada ya kukamilika kwa barabara ya Tunduma, Sumbawanga ambayo ni mwanzo wa kufunguka Mkoa wa Rukwa. Naomba Serikali kuangalia Mkoa huu kwani unahitaji kupiga hatua kwa maendeleo ya wananchi wake.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya ya kutatua kero na changamoto nyingi zilizopo katika Sekta ya Nishati na Madini nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo namwomba Mheshimiwa Waziri au nimkumbushe ahadi yake ya kuvipatia umeme vijiji vifuatavyo vilivyopo katika Jimbo la Mchinga ambavyo ni:-

Vijiji vya Dimba, Ruvu, Namtamba, Ruchemi, Michee, Kiware, Mputwa, Lihimilo, Namkongo Matapwa na Mnyangara. Mheshimiwa Waziri vijiji hivi ni miongoni mwa vijiji vilivyopo Jimboni ambavyo havijapata umeme kupitia mradi wa umeme vijijini REA. Nakumbuka hoja hii kwakuwa tayari tulishawahi kuzungumza na Mheshimiwa Waziri kuhusu suala hili la umeme mara kadhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ni kuhusu suala la madini, Mheshimiwa Waziri kwanza nimpongeze kwa juhudi zake mahsusi za kunisaidia juu ya suala la wanakijiji wenyewe kuunda vikundi ili waombe hati za wachimbaji wa madini *gypsum* na kupeleka sokoni kama vile katika kiwanda cha *cement* Dangote. Mheshimiwa Waziri pamoja na msaada wake huo kwangu bado kuna haja ya Wizara yake kufanya juhudi za maksudi kuhakikisha kuwa maeneo yote yaliyopo Jimboni yanayohusishwa na upatikanaji wa gesi, mafuta na madini yamepimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na uvamizi mkubwa wa watu kutoka maeneo mbalimbali kuja kurubuni wapiga kura wangu kwa kununua maeneo yenye madini kwa kiasi kidogo cha fedha. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri Wizara yake ifanye mkakati maalum na kukutana na wananchi wa Jimbo hili ili kuhakikisha kuwa maeneo yote yanayotiliwa

mashaka kuwa yamo madini yapimwe ili kuwaokoa wananchi kutokana na kasi kubwa ya watu kutoka mbali kuja kuchukua maeneo haya kwa kuwapa fedha kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia TANESCO ihakikishe zoezi la upatikanaji wa mita za LUKU na kuunganishiwa kwa umeme kwa wananchi ambao wapo vijijini, wameshakidhi vigezo vya kupatiwa umeme. Jimboni kwangu kuna kaya zaidi ya 200 ambazo zimekamilisha taratibu zote za kuingiza umeme lakini kumekuwa na *delay* kubwa kwa TANESCO Lindi kuwaingizia umeme wananchi hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu kwenye maeneo makuu mawili, yaani nishati na madini. Naomba nianze na Sekta ya Madini ambayo tunajua kuwa, kuna Watanzania wamejajiri kwenye sekta hii, lakini pia, kuna wawekezaji toka nje wamewekeza kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo langu la Tarime Mjini limebahatika kuwa na migodi midogo kwenye Kata ya Kenyamanyori na Turwa. Wilaya ya Tarime tumebarikiwa kuwa na Mgodi wa *North Mara* ambao ni mkubwa na muwekezaji wa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya uwekezaji wananchi walikuwa wakifanya uchimbaji mdogomdogo, lakini baada ya uwekezaji ule wamepata adha kubwa sana, hawana maeneo yaliyotengwa dhahiri kwa ajili ya kuwapa maeneo ya kuchimba bali wameendelea kuuawa pale wanapokuwa wameenda kuona chochote kwenye mabaki (vifusi).

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na mgodi iliahidi ndani ya Bunge hili Tukufu wakati nilipotaka mkakati wa Serikali kutatua wimbi la mauaji ya Watanzania kwenye huo mgodi 2011, waliahidi kutenga maeneo pamoja na kumwaga vifusi vile kwenye maeneo ya wananchi, pamoja na ku-support vikundi mbalimbali ili vijishughulishe na ujasiriamali kuweza kukukuza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yalisemwa na kurudiwa na Mheshimiwa Nagu, aliyekuwa Waziri wa Uwekezaji, Mheshimiwa Wasira aliyekuwa Waziri wa Mahusiano na Uratibu na Mheshimiwa Ngeleja aliyekuwa Waziri wa Nishati na Madini. Ni vyema sasa Serikali ikatimiza haya kwa wananchi na Wilaya ya Tarime na Watanzania waishio Nyamongo na maeneo jirani na *North Mara*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime kuna migodi ambayo wachimbaji wadogo wadogo wanashughulika na uchimbaji wa

madini. Maeneo hayo ni Nyabhozi na Kebaga, Kata ya Kenyamanani na Mgozi mwingine ni ule wa Bajeti ambao upo mpakani mwa Turwa na Kenyamanani. Kwa ajili ya kuboresha au kutatua changamoto zinazowakabili wachimbaji hawa wadogo ni muda muafaka Serikali kuhakikisha hizi ruzuku za zaidi ya bilioni 500 zinawanufaisha walengwa na sio matajiri wachache wanaojivisha joho la uchimbaji mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto zinazowakabili wachimbaji wadogo wadogo ambazo naomba Serikali kujitahidi ndani ya bajeti ya mwaka huu waweze kupatiwa ruzuku, sambamba na vifaa muhimu vya kurahisisha uchimbaji. Changamoto ya kwanza ni juu ya teknolojia inayotumika kuchimba madini, ni ya kienyeji ambayo ni hatarishi sana kwa maisha yao; mfano kuchoronga miamba inabidi watumie nguvu nyingi badala ya *morden equipments*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni changamoto ya maji. Aina ya uchimbaji ni *underground* ambapo unakuta *water table* ipo juu sana, hivyo inawawia vigumu kufanya shughuli za uchimbaji sababu ya maji na ikizingatiwa vitendea kazi vyao ni duni sana. Ni rai yangu sasa, Serikali itambue maeneo haya na kutoa ufadhili wake kwenye mashine za kuvutia maji kama vile *motor, generator* na waweze kutoa kwenye vikundi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto nyingine ni miundombinu mibovu ya barabara kuelekea kwenye migodi hii. Nashauri Waziri akae na Wizara husika kuweza kushawishi ujenzi wa barabara angalau kwa ngazi ya changarawe ukizingatia migodi hii inachangia kwenye pato la Serikali kupitia leseni za uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine lenye changamoto kubwa ni juu ya kuweza kupata mitambo ambayo hupima udongo na miamba, ili kujua upatikanaji wa dhahabu au madini mengine. Maana kwa sasa wachimbaji wadogo wadogo wanajichimbia kienyeji na kwa kubahatisha tu na hivyo kujikuta wanapoteza nguvu kazi nyingi sana na haina ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Wilaya ya Tarime tumekuwa hatupatiwi sehemu ya mrahaba toka ACCACIA, kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwa kutoa kiasi cha fedha ambacho hutumika kuleta maendeleo ya kijamii. Baadhi ya maeneo ya huduma za jamii ambazo ACCACIA wanapata ndani ya Mji wa Tarime ni Hospitali ya Mji, soko, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Uhamiaji, Stendi, Mahakama, hivyo kwa kuwa wafanyakazi wa ACCACIA wanapata huduma tajwa hapo juu ni dhahiri kuwa ACCACIA wana wajibu wa kuhakikisha Halmashauri yetu ya Mji wa Tarime inapata huduma muhimu za kijamii pamoja na mrabaha toka mgodi wa *North Mara*. Mji wa Tarime una ukosefu wa maji na barabara za mitaa ni mbovu mno.



Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mchana huu nichangie katika Sekta ya Nishati ya Umeme; Halmashauri ya Mji wa Tarime kwa asilimia zaidi ya 70 hawana nishati ya umeme. Halmashauri ya Mji wa Tarime ina mitaa 88, ambapo kiuhalisia kuna kata nne ambazo zipo na vijiji na hamna nishati ya umeme kabisa. Kata hizi ni Ketare, Kenyamanyori, Nandoto, Nkende na baadhi ya maeneo ya Kata ya Turwa na Kata ya Nyamisangura.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishapeleka barua kuelekeza maeneo yenye uhitaji mkubwa wa umeme, hivyo naomba kujua kama *REA Phase III* imeyafanyia kazi na ukizingatia Kata ya Kataer, Nyandoto na Kenyamanyori wanajihusisha sana na kilimo ambacho kitasaidia kwenye dhana nzima ya Tanzania ya Viwanda, tuweze kusindika mazao yetu, kufungua viwanda vidogo vidogo. Kata ya Nkende ndio yenye soko la Kimataifa ambalo linajengwa pale, pia kuna uwanja wa ndege ambao unatumiwa na watalii waendao Nyamongo na hata Viongozi wa Serikali na kisiasa, hivyo taa ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia Kata ya Nkende ndiyo yenye Mnada wa Magera ambao Serikali imeahidi kuufufua. Pili, ni katika Kata hii ya Nkende ndiyo tuna machinjio ya kisasa, ofisi ya Uhamiaji inajengwa karibu na *Mgena Airport* na *Remague East Africa Market*, lakini pia wajasiriamali wadogo wadogo wanategemea nishati hii ya umeme ili kuendesha shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ijulikane kuwa mahitaji muhimu ya kijamii, kama shule za sekondari na msingi, hospitali, vituo vya afya, zahanati, vituo vya polisi, viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao; hivyo, naomba sana Wizara hii itoe kipaumbele katika Halmashauri ya Mji wa Tarime ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya ya Tarime. Hivyo nishati ya umeme ni ya muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho naomba Wizara hii ichukue hatua ya kuhakikisha hakuna ukatikaji wa umeme mara kwa mara bila kutoa taarifa kwa mteja/wateja kitu ambacho husababisha uharibifu wa vifaa vinavyotumia umeme na kusababisha hasara kwa mlaji. Utolewe Waraka toka ngazi ya Wizara ukiamrisha uboreshaji wa utoaji wa nishati ya umeme bila kuleta madhara kwa mlaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha kwa kutoa ushauri kwa Serikali kuhakikisha fedha za maendeleo zilizotengwa zitumike kwa ajili ya bajeti iliyotengwa ikiwa ni pamoja na kutoa elimu mbadala kwa wachimbaji wadogo wadogo, ili wapate elimu mbadala kwa uchimbaji wenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawasilisha.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, umeme kukatiza maeneo machache tu ya mjini (REA) huku vijiji vingi vikibaki bila umeme.

Mheshimiwa Spika, nguzo za REA/umeme zimewekwawekwa tu bila kufuata barabara na mara nyingi zinakatiza katika viwanja vya watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *fluctuation* ya umeme kitu kinachoshusha *rate/quality* za uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nguvu ndogo na bajeti ndogo kuwekwa katika joto ardhi, nishati inayoonekana ni ya gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa mapendekezo kwa Serikali juu ya hitaji la msingi la kutumia *transformer* za TANELEC kwa lengo la kupunguza gharama ambazo Serikali inaingia kwa kununua *transformer* za China/India wakati Tanzania ina hisa kwenye hiyo kampuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pesa nyingi imetoka kwa mwaka 2015/2016, lakini bado changamoto za umeme ziko dhahiri. Hivyo, ama usimamizi ni mbovu au miundombinu hii haiwagusi watu moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekuzi kushushwa nishati ya gesi kwa lengo la kuleta unafuu wa maisha kwa wananchi wanaoitumia.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Muhongo kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni mambo muhimu kuhusiana na nishati na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza kwa kupewa/kutengewa bajeti kubwa kwa lengo la kuboresha mambo ya nishati ambayo ni muhimu sana katika kuipeleka nchi yetu kwenye uchumi wa kati. Naomba nimwombe Mheshimiwa Waziri kwamba, wajitahidi kuhakikisha mipango inakwenda kama ilivyopangwa kwa faida ya wananchi wote wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri yafuatayo katika Jimbo langu la Chilonwa:-

Umeme wa *REA Phase II* ulikuwa ufike hadi Kata ya Zajilwa, Kijiji cha Zajilwa, lakini haujafika, naomba sasa ufike.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba umeme katika *REA Phase III* uende pia, maeneo yafuatayo:-

Vijiji vya Gwandi Bwawani na Magungu vilivyo Kata ya Zajilwa; Vijiji vya Izava, Umoja, Segala, vilivyo Kata ya Segala; Vijiji vya Ikombo, Solou na Itiso vilivyo Kata ya Itiso; Vijiji vya Manyemba, Chiwondo, Igamba, Nayu, vilivyo Kata ya Dabalo; Vijiji vya Chitabuli, Mlimwa, vilivyo Kata ya Membe; Vijiji vya Bwawani na Chalinze B vilivyo Kata ya Manchali; Vijiji vya Mlebe, Msamalo, vilivyo Kata ya Msamalo; Vijiji vya Makoja, Butiama, Ikowa, vilivyo Kata ya Ikowa; Kijiji cha Humekwa, kilicho Kata ya Haneti na Kijiji cha Kawawa kilicho Kata ya Msanga.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Jimbo la Mufindi Kusini tunaomba umeme katika Kata za Mtambula, Maduma, Idunda, Kiyowela, Magunguli, Itandula, Idete na Mninga. Pia, naomba umeme upelekwe kwenye Vituo vya Afya Kihanga, Mninga, Mtwango na Udumuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kwenye taasisi ni muhimu sana kupata umeme naomba sana shule za msingi, sekondari na taasisi za kidini kupelekwa umeme. Jimbo la Mufindi Kusini tuna tatizo kubwa la umeme, tunaomba Serikali ipeleke umeme katika Jimbo la Mufindi Kusini; vijiji vingine nyaya zimepita juu kwenye nyumba za watu, tunaomba Serikali kuangalia kwa huruma vijiji hivi, kwa mfano Kijiji cha Rugolofu, Kitasengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naipongeza Serikali kwa kufuta *Service Charge* na kupunguza gharama za uingizaji wa umeme katika nyumba.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri binafsi, Naibu Waziri na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba katika REA III vijiji 23 vifuatavyo vipatiwe umeme, ili waweze kwenda na kasi ya maendeleo sawa na maeneo mengine:-

Vijiji vya Lutongo, Kabusungu, Kilabela, Kilino, Isanzu, Igogwe, Shibula, Bulyanhulu, Ilalila, Chabakirua, Masemele, Igombe A, Igombe B, Mhonze A, Buganda, Zenze A, Zenze B, Iseni, Ilekako, Igalagale, Kasamwa, Imalang'ombe na Ilesa. Kazi mnayoifanya ni nzuri sana na inatia moyo, endeleeni kuchapa kazi msikatishwe tamaa na watu wasioitakia mema nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeambatanisha Shule za Sekondari zisizo na umeme. Naomba zipatiwe umeme maana ziko nje au vijijini; Mwinuko, Nundu, Kilimani, Shibula, Kirumba, Kabuhoro, Kangaye, Ibinza, Lukobe, Mihama na Sangabuye.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa Wizara hii ya Nishati na Madini na kutokana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika Wizara hii hasa katika Mkoa wa Rukwa, napenda kuchangia mambo yafuatayo:-

Suala la TANESCO kuwadai wananchi pesa za nguzo. Suala hili limekuwa likileta shida kwa wananchi wetu hasa pale wanapohitaji huduma hii muhimu ya nishati katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, elimu kwa watu walio karibu na nguzo. Suala hili limekuwa na changamoto nyingi, hasa katika Mkoa wangu wa Rukwa. Naishauri Serikali kutoa elimu kwa wananchi wetu wajue athari zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukatika kwa umeme bila taarifa. Suala la kukatika kwa umeme katika Manispaa ya Sumbawanga limekuwa likiwaathiri sana wafanyabiashara, hasa pale wanapokosa taarifa ya kukatika kwa umeme na kuleta athari kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la maeneo mengi kukosa umeme. Katika Mkoa wa Rukwa na Wilaya zake kuna shida kubwa ya kukosa umeme mpaka leo. Je, Serikali au Wizara ina mkakati gani wa haraka wa kupeleka umeme katika Wilaya ya Nkasi, Wilaya ya Kalambo na Sumbawanga Vijijini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vigezo gani vinatumika katika kufikisha umeme vijijini, REA III? Kutokana na kutambua kuwa Mkoa wa Rukwa uko Tanzania, lakini ni maeneo mengi katika mkoa huu wananchi wengi hawajafikiwa wala kuwa na dalili zozote za kupelekewa umeme!

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama halisi za mtu kuvuta umeme. Kumekuwa na hali ya manung'uniko kwa wananchi wanapokuwa wanahitaji kuingiza umeme katika nyumba zao, wamekuwa wakiambiwa bei tofauti tofauti. Je, ni kiasi gani wananchi wanapaswa kutoa?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kukatika kwa umeme mara kwa mara katika Manispaa za Sumbawanga na Nkasi. Hali hii imekuwa ikijitokeza mara kwa mara, je, Wizara inatambua suala hilo na je, kuna utaratibu wowote wa kumaliza tatizo hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la madini yanayopatikana Sumbawanga. Napenda kujua kama Wizara inajua kuwa kuna madini yanapatikana Manispaa ya Sumbawanga? Kama ndivyo, wameweka mkakati gani? Kwani mpaka sasa mambo yanayofanyika ni kinyume kabisa na umiliki wa vitalu na madini yetu yanakwisha.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru, ila nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Profesa Sospeter Muhongo pamoja na timu yake kwa kazi nzuri na uwajibikaji uliotukuka katika kuwatumikia wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nijielekeze kuchangia katika Usambazaji wa Umeme Vijijini (REA) katika hotuba iliyokuwepo mbele yetu. Nchi yetu ina malengo ya kuwa nchi ya viwanda na kufikia katika azma ya uchumi wa kati. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali, lakini ukweli ni kwamba, tuna changamoto kubwa ya vikwazo vya uchumi kimojawapo ni kukosekana kwa nishati ya uhakika ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaoishi vijijini wanakosa huduma hii muhimu ya nishati ya umeme ambao ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya watu wetu. Niiombe Serikali iongeze kasi ya usambazaji na kuiongezea fedha za kutosha Wizara ya Nishati kuhakikisha inasambaza umeme kwenye vijiji vingi na kwa wakati muafaka pia, kukamilisha miradi ya umeme ambayo haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisambaza umeme vijijini tutawezesha wakulima kuongeza thamani ya mazao kwa kufungua viwanda vidogo vidogo, tukisambaza umeme vijijini wavuvi watahifadhi samaki; pia, itawawezesha wafugaji kuhifadhi nyama kwa muda mrefu, sambamba na kuongeza ajira kwa vijana kwa kuanzisha shughuli mbalimbali za kijasiriamali; mfano saluni za kike na za kiume, uuzaji wa vinywaji baridi, viwanda vya kuchomea vyuma na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri katika bajeti hii ahakikishe vijiji vifuatavyo katika Jimbo la Pangani vinapatiwa umeme huu wa REA; Kigurumba Misufini, Mivumoni, Matakani, Kidutani, Jaira, Kikokwe, Langoni, Mtango, Mtonga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumaliza, tunaomba Wizara iwe na mkakati maalum wa kuunganisha umeme katika shule za sekondari za kata, zahanati na vituo vya afya, ili kuimarisha huduma za jamii za wananchi wetu.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya ya kupata nguvu ya kutoa

mchango wangu katika Wizara hii muhimu ya Nishati na Madini. Pia, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dokta John Pombe Joseph Magufuli, kwa hekima kubwa ya kumteua Profesa Muhongo katika nafasi ya Uwaziri wa Wizara hii. Ni kweli ametundendea haki Watanzania kwa maana upele umempata mwenye kucha katika Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Profesa Muhongo, Naibu wake, Katibu Mkuu wa Wizara na Timu nzima ya Wataalam Wizarani kwa mipango yao na mwanzo mzuri wa utendaji katika Wizara hasa kuleta umeme wa uhakika kwa sisi wa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishauri Serikali kuhusu leseni kwa makampuni ya uchimbaji wa madini; wakati wa kuitoa kwa wawekezaji hao (leseni) ni vizuri kuwashirikisha wananchi wa eneo husika kupitia viongozi wao, kwa maana ya wawakilishi katika vijiji, kata, jimbo na wilaya, ili kuondoa migogoro ya wananchi na wawekezaji katika meneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ni vema ifahamike faida na manufaa ya uchimbaji huo kwa jamii na Taifa kwa ujumla, badala ya hali ya sasa mwekezaji anapata leseni Dar-es-Salaam na akifika maeneo husika halipi fidia wala *service levies* katika Halmashauri husika kwa kisingizio cha madini sio mali ya mtu na wao wameshalipia Serikalini kwa wamiliki wa madini hayo. Nashauri, kabla ya kutoa leseni, Wizara ni vizuri kufanya utafiti katika maeneo husika, ili kufahamu hali halisi ya eneo hilo la uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, machimbo ya *marble* katika Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki, katika Halmashauri ya Morogoro, katika Vijiji vya Kivuma, Kata ya Kibuko, Tarafa ya Mkuyuni na Kijiji cha Masiyu, Kata ya Gwata. Wawekezaji hawajalipa fidia kwa wananchi na pia, kutolipia ushuru wa huduma katika halmashauri kwa miaka zaidi ya ya sita tangu waanze uchimbaji, Kampuni ya *Zhong Fa!*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sababu hii imekosesha mapato stahiki kwa Serikali, kwa sababu mrabaha wanalipa katika mkoa uliosajili *TIN* zao, ambao uko mbali na machimbo husika, ambao hawajui kiasi halisi kinachopatikana. Nashauri katika suala la mrabaha washirikishwe *TRA* Wilaya na Mkoa husika wenye machimbo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, naomba kupatiwa umeme katika Kata ya Mkulazi vijiji vinne, Kata ya Mafuli vijiji vinne, Kata ya Kidugalo vijiji saba, Kata ya Ngerengere vijiji viwili, Kata ya Kiloka kijiji kimoja, Kata ya Gwata vijiji viwili, Kata ya Mkambarani vijiji viwili, Kata ya Mkuyuni vijiji viwili, Kata ya Kinole vijiji vinne, Kata ya Tegetero vijiji vinne na Kata ya Kibuko vijiji vyote vinne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya vijiji 64 ni vijiji 16 tu ndivyo vyenye umeme, naomba katika REA III tupatiwe umeme katika vijiji hivi na kata hizi kwa ujumla, kwani hata huko tunakotaka kwenda katika uchumi wa viwanda, hasa Kata ya Mkulazi kwenye mradi mkubwa *flagship* wa *Mkulazi Village* afya na Bwawa la Kidunda ambalo vijiji vyake vina umbali zaidi ya kilometa 50 toka kijiji kimoja kwenda kingine; mfano Usungwa, Mkulazi, Usangara mpaka Kidunda. Naomba tupatiwe umeme ili katika REA nasi tufanane na Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hatuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia mia moja. Tatizo kubwa la umeme Kiteto ni umeme wa REA katika Kata ya Kijungu, Kata ya Songambe, Kata ya Magungu, Kata ya Dongo na Kata ya Sunya. Kata hizi zote zilikuwa za REA II, sasa tunaomba majibu ni lini Kata hizi zitapatiwa umeme, maana sasa tumeingia REA Awamu ya III haya maeneo yakiwa bado?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na kunipa uwezo wa kuchangia leo. Naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa na imani kubwa kwa kumteua Mheshimiwa Profesa Muhongo kuwa Waziri na Mheshimiwa Dkt. Matogolo kuwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, uamuzi wa kupeleka asilimia 40 kwenye maendeleo kwa Wizara ya Nishati na Madini; napongeza kwa juhudi kubwa katika sekta zote za nishati na madini. Naomba nianze na suala la nishati; kwanza nishukuru kwa mradi wa REA, katika Wilaya ya Babati maeneo yanayotarajiwa kupata nishati hii tayari wananchi wameanza kujipanga kutumia kwa maendeleo. Katika REA II maeneo mengi yameachwa, tunaomba na nashauri, katika Mpango wa REA III hayo maeneo na taasisi muhimu yapatiwe umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Wizara kupitia TANESCO itusaidie kupitisha *design* ya nguzo za *cement* za umeme ili tuweze kuanza kuzalisha. REA III itahitaji nguzo nyingi sana, tukiruhusiwa sasa uzalishaji baada ya *design* kukubalika itatusaidia kufanya matayarisho mapema.



Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba Wizara isaidie kufuta (*charges*) gharama ya kutotumia umeme katika mradi wa kilimo na viwanda vya kuongeza thamani ya mazao yetu ambayo viwanda hivyo hufanya kazi kwa miezi miwili au mmoja tu pamoja na umwagiliaji. Tozo hiyo inaua viwanda na sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iangalie namna ya kuongeza tozo kwenye mafuta, napendekeza iongezwe sh. 200/= kutokana na bei ya mafuta ya dunia imeshuka sana. Hakuna nauli, usafiri au bidhaa iliyoshuka, hawana kodi iliyoongelea kutoka kwa wafanyabiashara, ikiongezwa sh. 200/= kwa lita, sh. 70/= iende REA, Umeme Vijijini, sh. 70/=; Maji Vijijini, sh. 40/= iende Mfuko wa Utafiti na sh. 10/= Mazingira. Bei ya mafuta ikipanda duniani, basi tozo hii ipungue kidogo kidogo. Tunaweza kupata takribani shilingi bilioni 330 kwa miezi sita. Kwa hiyo, wastani wa shilingi bilioni 110 kwa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, nashauri Serikali iondoe Kodi ya VAT kwenye vito na vidani (*germstone and jewelry*) vinavyouzwa ndani ya nchi (*local sale*). Kama bei ya dunia ya dhahabu inajulikana na vito kuweka VAT inafanya sekta isikue. Nashauri kituo cha Arusha cha Mafunzo kiboreshwe na mafunzo ya kuchonga vito na kutengeneza vidani (*jewelry and lapidary*) ianze mapema. Napongeza juhudi za Wizara kwa sasa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Sasa tunaanza na Waheshimiwa Mawaziri, tunaanza na Mheshimiwa Mwijage Charles!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, Sekta ambayo nimeitumikia kwa miaka 31 nikiwa fundi bomba wa kupaka grease mpaka nilipokuwa Naibu Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Bajeti na *speech* nzuri, Naibu Waziri ambaye amevaa viatu vyangu, yaani kama vya kwako kabisa, lakini na Watendaji wote ambao nimeishi nao kwa miaka 31 ambao naamini wanaifanyia vizuri nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijajibu hoja zilizojitokeza kutoka Wizara ya Nishati, nichukue fursa hii kuishukuru Serikali kupitia Wizara hii kwa namna walivyosambaza umeme kwenye Jimbo langu la Muleba ya Kaskazini. Nifikishe ujumbe wa Wanamuleba Kaskazini, asilimia 16 wanaoishi visiwani, Mheshimiwa Profesa Muhongo wanamtegemea kwamba kwa kurudi kwake, Visiwa vya Goziba, Makibwa, Bumbire na Kerebe vitapata umeme, sina wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge zilizojitokeza kwenye bajeti hii ya Nishati na Madini. Suala la EPZ Simanjiro,

*Tanzanite*; tumeshatoa EPZ, tumeshatoa eneo tumefidia. Sasa hivi tunatafuta wawekezaji watakaoweza kutengeneza Tanzania Minerals Business Center. Nikiwaonesha picha yake kama ndoto ikiwa kweli, suala la *Tanzanite* litakuja kubadilika na kuwa ndoto ya mambo ya zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini, mpango wao ni kutengeneza kituo kimoja cha madini na EPZ ilianzishwa nyakati zile kwa misingi hiyo. Kwa hiyo, hilo suala halina tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe na Ofisi ya Bunge kwa kuitanguliza bajeti yangu na Wizara ya Nishati ikaja baadaye. Wako waliokuwa wanasema viwanda haviwezekani, sasa angalieni, kuna *power generation* inaendelea kutokea, kuna *power transmission* inaonekana, kuna *power distribution*. Kama nilivyozungumza, tumieni umeme huo mpaka vijijini kwa kuanzisha viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, muwe na imani, *think positive*, muione *glass* ya maji iliyoko nusu kwamba imejaa nusu, msione kwamba iko tupu nusu. Huu umeme unakuja, maneno anayoyasema Mheshimiwa Profesa Muhongo, nina imani naye, ni mambo ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala ambalo limechukua hisia za watu wengi la Mchuchuma na Liganga. Mchuchuma na Liganga, Waraka la Baraza la Mawaziri wa mwaka 96, Waraka Na. 6 ndiyo ulisukuma suala la Mchuchuma na Liganga. Sasa hivi tuko wapi? Nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kama kuna mtu yeyote anajua makandokando yanayokwamisha Mchuchuma na Liganga aje aniambie mimi. Mheshimiwa Deo, Mzee wa Njombe njooni wote mnione.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Mchuchuma na Liganga Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati alijibu swali hapa akasema anaanza kulipa mwezi wa Sita na anayewajibika kulipa ni Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; yaani mimi ndiyo Waziri mwenye dhamana, niwahakikishie kwamba Tanzania sasa ziko pesa za kutosha za kuweza kulipa hao wananchi. Ninachoomba ni ushirikiano wa Wabunge. Hii sitamwachia mtu, nitashughulika mimi mwenyewe na Makatibu Wakuu na Madiwani wote tuhakikishe watu wanakuwa *compensated*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kama kuna mtu anaelewa makandokando yoyote kuhusu mradi huu, anieleze. Hakuna kurudi nyuma, tunakwenda mbele. Tunakwenda na mwekezaji huyo aliyepo, aje alipe. Kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, mradi huu katika kuujenga tutaajiri watu 3,000, lakini utakapokuwa umeanza, utajiri watu 6,000 wa moja

kwa moja. Huu mradi utakuwa na *indirect employment* watu 24,000, lakini utachangamsha maeneo yote ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze, wananchi wote wataelimishwa namna ya kushiriki. Tuna uhakika sasa amekuja huyu mwekezaji ambaye ni Mbia wa NDC, tumekaa naye na bahati nzuri Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge, Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu alikuwa nami, tumekaa nao, nimewauliza, wakanionesha nyaraka, hii ni ukweli. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tujiweke tayari, tu-*think positive* huu mradi uweze kuendelea. Kwa hiyo, haki za watu zitalipwa. Nilichozungumza na walioliona kwenye vyombo vya habari, tunachotaka, ni lazima VETA iwepo, iwafundishe Watanzania. Nimesema mbele ya Bunge Tukufu, Watanzania watashiriki kwenye ngazi zote za utendaji kuanzia ngazi za chini mpaka ngazi za juu. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge, nimepata faida ya kushiriki kwenye mchakato mzima wa kampuni. Nimewaeleza nilipoajiriwa TPDC, nilikuwa *pipeline operator* nikifungua *valve*, lakini nimepanda mpaka nikawa *international trader* wa *Chevron*, nikapanda mpaka Naibu Waziri wa Nishati. Kwa hiyo, nami napenda vijana wa Kitanzania wakachakate chuma watengeneze vyuma. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie ndugu zangu wa Kilimanjaro; *Kilimanjaro Machine Tools* inapoanza Mchuchuma na Liganga na yenyewe itaanza kazi. Kwa hiyo, suala la Mchuchuma na Liganga zile historia na hadithi zimefikia mwisho, tunakwenda kwenye *reality* na mwekezaji, pesa zimeshaingia nchini. Ule mradi utajengwa kwa gharama ya Dola bilioni tatu na Tanzania tunashiriki kikamilifu katika mradi huo. Tutakapokuwa tumefikia kikomo, tutakuwa na hisa asilimia 49.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mtu anafahamu makandokando yoyote, asiache kuja kuniambia Mwijage ulikosea, aje twende wote. Mchuchuma na Liganga ni mradi kielelezi, kwa sababu wenyewe utachochea viwanda vingine. Badala ya kuagiza chuma ambacho ni bidhaa nzito kutoka huko Amerika na sehemu za Uchina tutakuwa na chuma hapa nyumbani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mradi wa Mchuchuma na Liganga kutakuwepo mtambo mwingine wa kuchenjua madini yanayopatikana ndani ya mtambo huo wa *titadium* na *vanadium* yanayoendana na chuma. Ndiyo maana mradi wa Mchuchuma na Liganga ulichelewa. Chuma chake siyo cha kuchukua na kuchakata, kina taratibu zake na huyu mwekezaji amefanya *research* na amejihakikishia. Kwa hiyo, ndiyo maana ilani ya Chama changu

inasema huu ni mradi kielelezi, ndiyo maana mpango wa miaka mitano unaitwa mradi kielelezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka nilifafanue hilo, kwa hiyo, Mchuchuma na Liganga *is a reality*, lakini umeme unakuja. Watu wengine wanafanya mahesabu kwamba imechukua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba umalize. Naomba umalize!

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa muda wa kuchangia bajeti hii. Niwahakikishie kwa kumaliza kwamba, umeme upo wa kutosha. Kauli za kwamba hatuna umeme wa kutosha zinawakimbiza wawekezaji lakini wawekezaji wanaijua Tanzania ndiyo maana sasa kutoka Mtwara kwenda mpaka Dar es Salaam, ukanda mzima wa gesi wa uwekezaji ndiyo sehemu ya *preference* ya kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ndugu zangu tuzungumze vizuri, tuipe imani hii bajeti kusudi wawekezaji waweze kuja, nami niweze kutengeneza viwanda, *score card* yangu iboreke na tajiri namba moja anione nafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono bajeti ya Mheshimiwa Profesa Muhongo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Kalemani!

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami naomba pia leo kwa mara ya kwanza kabisa nihutubie Bunge lako Tukufu kwa niaba ya Watanzania wote, nikiwakilisha Jimbo la Chato. Nianze sasa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai mkubwa na kupata fursa ya kuongea na kuunga mkono hoja hii ya Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa nguvu kubwa kabisa nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuchaguliwa na kuaminika kwa Watanzania wote kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Makamu wa Rais, mama yetu Mheshimiwa Suluhu Hassan, kwa mara ya kwanza kupata Makamu wa Rais kwa akinamama hapa Tanzania. Ni historia kubwa, Watanzania wote

tunajivunia na hasa akinamama wenzetu. Tunawapongeza sana akinamama kwa kuwakilishwa na Makamu wa Rais wa akinamama. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee pia kumpongeza Waziri Mkuu. Nampongeza Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa kwa kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kadhalika kwa aina ya pekee kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein kuchaguliwa kuwa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa aina ya pekee nimpongeze sana Profesa Sospeter Muhongo, Waziri wangu anavyonisimamia na kuniongoza katika kusimamia majukumu makubwa ya Wizara ya nishati na madini. Nawashukuru sasa kwa nafasi ya pekee wananchi wangu wapendwa, wananchi wa Chato walivyonichagua kwa kura nyingi na wananchi wote kuwakilisha kama Mbunge wao, naamini wataendelea kunirejesha mpaka uzee wangu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa aina ya pekee sasa, niishukuru sana familia yangu, wazazi wangu walivyovumilia kwa kipindi chote katika kutekeleza majukumu yangu ya Wizara ya Nishati na Madini, nawapongeza sana Mwenyezi Mungu awajaalie uhai na uzima. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, sasa nijielekeze kwenye kuunga mkono hoja. Kabla sijasahau, niseme naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, waliochangia ni wengi, zaidi ya Wabunge 109, lakini naweza nisijibu hoja zao zote, nitakachofanya, tuombe sana Bunge lako Tukufu kwa ridhaa ya Kanuni za Bunge, itambue ushiriki wa Waheshimiwa Wabunge hawa 109 kwa sababu sitaweza kuwataja, lakini waingie kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nianze sasa na kujielekeza kwenye hoja za msingi. Kambi ya Upinzani Bungeni imetoa hoja za msingi sana katika kuonesha kuwa na wasiwasi kana kwamba tutaweza kupata kweli nishati ya umeme ya kuweza kutufikisha kwenye uchumi wa viwanda? Wamekuwa na wasiwasi kwamba, sasa hivi tuna takriban *megawatts* wanasema 2,780 ndiyo ilikuwa *maximum*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mnyika kwamba hizo *megawatts* 2,780 ambazo tulikusudia kuzifikisha, sasa nimhakikishie miaka mitano ijayo tutakuwa na zaidi ya *megawatts* 3,000; lakini kuja kufikia mwaka 2025 tutakuwa na zaidi ya *megawatts* 10,000. Ili kumthibithishia sasa, nimweleze tu kwa upande wa nishati ya gesi, sasa hivi tuna *installed capacity* nyingi za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyofahamu, pale Kinyerezi tuna *megawatts* 150 ambazo tayari tunazo. Tunaendelea kupanua *megawatts* 185, tutakuwa nazo; Kinyerezi II pia tutakuwa na *megawatts* 240, unatambua Mheshimiwa Rais alizindua hivi karibuni. Tunaendelea na kuwekeza kwenye nishati hiyo hiyo; tutaendelea kuwa na Kinyerezi III ambayo itakuwa na *megawatts* 300; lakini bado upo uwezekano mkubwa kuwa na Kinyerezi IV *megawatts* 320. Bado tuna Somanga Fungu, tuna *megawatts* 350; bado tuna Kilwa Energy, *megawatts* 320 na kadhalika. Huo ni umeme wa gesi na tuna uhakika kwamba umeme utakuwa mwingi zaidi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleee tu kusema, tutakuwa na umeme mwingi wa uhakika sana hasa kwenye nishati ya maporomoko ya maji. Tunatarajia kuwa na *megawatts* 80 za kutoka Rusumo ambazo tutazigawanya *megawatts* 26.7 kila nchi. Hizo ni nguvu kubwa, itasaidia sana kwa wananchi wa Ngara na maeneo ya jirani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tuna umeme wa Kakono wa maji, sasa hivi tunatumia umeme wa kutoka Uganda kwa wenzetu wa Kagera. Sasa tutaachana na umeme wa Kagera kwa kutoa Uganda, tutaanza kutengeneza umeme wetu. Pale Kakono tutakuwa na *megawatts* 87 na tutausafirisha kwa kilomita 38.8 kutoka Kakono mpaka kwenda Kyaka. Huo ni umeme wa uhakika, nataka niwahakikishie wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunazo nguvu nyingi za umeme, tunapozungumza tutaachana na matatizo ya umeme, tuna uhakika na hizo ni takwimu za kisayansi. Niendeleee sasa kusema tu, kuwa na nguvu ya umeme na bila kusafirisha bado haisaidii, niwahakikishie sana Watanzania kwamba sasa nguvu kubwa ya umeme tutakayokuwa nayo kama tulivyoeleza kwenye taarifa yetu ya bajeti, tunaanza sasa kuusafirisha umeme huo ambao utatatua tatizo kubwa la kukatika kwa umeme. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tatizo la kukatika kwa umeme wananchi naomba niwaeleze, ni kwa sababu ya mambo yafuatayo: kwanza, umeme tulionao ni kweli una *low voltage*. Ili kuondokana na *low voltage*, sasa tunakuja na umeme mkubwa wa Kilovoti 400 na huu umeme utatapakaa nchi nzima. Nianze kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutakuwa na umeme wa kilovoti 400 tunaosafirisha kutoka Mbeya unapita Sumbawanga, unaenda Kigoma, unaenda Mpanda mpaka Nyakanazi. Huo urefu mkubwa sana, ni kilomita 1,148. Umeme huo huo tutausafirisha kutoka Nyakanazi mpaka Geita, kilomita 133; umeme huo huo tunautoa Nyakanazi na tutautoa Geita mpaka Bulyankhulu, kilomita 50. Ukanda huo utakuwa na umeme wa uhakika. (Makofi)



Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo tutaanza kuzalisha umeme wa Malagarasi. Umeme wa Malagarasi ndiyo utakuwa mkombozi wa umeme mkubwa kwa wananchi wa Kigoma na maeneo ya jirani kama Ngara. Huo umeme tunaanza kuutekeleza kuanzia mwakani na utakamilika 2019. Kwa hiyo, niwahikikishie wananchi wa Kigoma na eneo la jirani kwamba tunapozungumza eneo la umeme, kwa sasa hivi tumejifunga mkanda, ni suala la kufa na kupona, Watanzania wote watapata umeme wa uhakika ifikapo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendeleo kuzungumzia suala hilo hilo la umeme. Tutausafirisha umeme mwingine; nataka niwaeleze mwone jinsi Tanzania nzima itapata umeme wa kutosha. Tutakuwa na umeme wa kutoka *North East Grid* na huo umeme tutaanza sasa kuutoa Kinyerezi kwa upande wa mashariki. Utatoka Kinyerezi utaenda Chalinze, utaenda Tanga mpaka Arusha mpaka Namanga kilomita 664. Kwa hiyo, Watanzania wa maeneo yale watakuwa wana uhakika wa umeme ambao haukatikikatiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la kusafirisha umeme mkubwa ni kuhakikisha kwamba umeme uliopo sasa ni mkubwa, unatoshwa kwa matumizi ya viwandani, matumizi ya nyumbani na biashara ndogo ndogo pamoja na biashara kubwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wananchi na Waheshimiwa Wabunge, nataka tena niwahakikishie, tunao mradi ninaousema wa *backbone*. Huu mradi ni wa umeme mkubwa. Ni umeme ambao unatoka Iringa unapita Dodoma unakwenda Singida mpaka Shinyanga na unatumika kwa maeneo yote ya Kanda ya Ziwa na ndiyo umeme wa uhakika mkubwa tunaouzungumzia, siyo umeme wa kutakatikakatika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, suala la kukatika kwa umeme, baada ya miradi hii kukamilika mwaka 2018/2019 yatapungua kwa kiasi kikubwa sana. Sasa hivi niseme tu, siyo kwamba sasa hivi tuna mgao wa umeme. Hatuna mgawo, isipokuwa kuna kukatikakatika kwa umeme kutokana na sababu nilizozitaja hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie hilo kwamba tunaposema kutakuwa na nguvu kubwa ya umeme, ni umeme wa nguvu kubwa utakaofaa viwandani. Naelewa Mheshimiwa Matiko anajua kwamba, kuna mgao wa umeme na dada yangu naomba uridhike kuwa tatizo hilo litapungua sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie REA na ninapokuwa najibu haya, najibu kwa ujumla wake kwa sababu maswali ni mengi sana. Nizungumzie REA. Ni kweli kabisa REA, awamu ya pili imekwenda maeneo yote tuliyopeleka awamu hiyo, lakini umeme unaishia kwenye vituo tu vya vijiji na siyo kwa



wananchi. Lengo kubwa la mradi wa REA, awamu ya pili lilikuwa ni kusafirisha miundombinu ya umeme ili kufikisha vituo vikubwa na baadaye usambazaji kwenda kwa wananchi katika vitongoji uendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa awamu inayokuja, wananchi wengi wameuliza, Waheshimiwa Wabunge mmeuliza kwamba umeme unapita kwenye nyuso za watu. Sasa unakuja mradi unaoitwa *underground distribution transformer*. Mradi huu unaanza kutekelezwa kuanzia Januari mwakani na utakamilika miezi 18 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la mradi wa *distribution* hiyo ninayosema ni ya *underground*, siyo chini ya ardhi Mheshimiwa Matiko kama unavyosema. Lengo lake, ni kupita kila mahali ambapo *transformer* na miradi mikubwa ya umeme ambapo Kilovoti 33 imepita, itakuwa sasa inatandaza umeme kutoka kwenye vituo hivyo kwenda kwenye miji ya wananchi. Kwa hiyo, umeme huo utafika kwenye kaya za wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niwahakikishie suala kwamba kuna maeneo yameachwa, yatazibwa pengo pamoja na mradi tunaosema wa *underground distribution transformer*. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mradi mwingine huo huo ambao sasa utapita kwenye njia zilizopitisha umeme wa kilovoti 33, kutandaza umeme kutoka kwenye vituo hivyo umbali wa kilomita 10. Huo unaitwa *European Union Distribution Grid* na utasaidia sana kueneza umeme kwenye maeneo yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, huo mradi pia unagharamiwa takriban shilingi bilioni 58.4 na mradi ule utakapokuwa unapita, maeneo yote ambayo hayakufikiwa na umeme kwa umbali wa kilomita 10 kutoka kwenye nguzo kubwa, sasa utapatiwa umeme wa uhakika na baadaye utapitisha umeme huo huo wa kilovoti 400.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nataka tu kueleza maelezo ya kina kabisa kabisa kuhakikisha kwamba umeme unaokuja ni mkubwa na utaingia kwenye Vijiji vyetu na wananchi wote watapata umeme wa uhakika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie sasa kuzungumzia kwenye suala la umeme kuhusiana na kuunganisha Vijiji kwa Vijiji. REA awamu ya tatu ni kweli kabisa, kama tunavyosema REA ya awamu ya pili inakamilika mwezi Juni mwaka huu. Tunachofanya sasa hivi ni kukamilisha uhakiki kutambua vijiji ambavyo havijapata umeme hadi leo, lakini vilikuwa kwenye scope ya REA II, lakini kadhalika ni kuainisha vijiji vyote ambavyo havijapata umeme ama

vilikuwa kwenye scope ama havikuwepo kwa sababu lengo kubwa ni kupelekea umeme katika vijiji vyote vilivyosalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge wala wasiwe na wasiwasi kwamba wanahitaji kuona orodha ama kijiji chako kitasahaulika REA ya awamu ya tatu itapeleka umeme kwenye vijiji vyenu vyote. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hili tatizo la akinamama kujifungua kwa kutumia tochi, hili tatizo la akinamama kuonekana na macho mekundu na wakadhaniwa ni wachawi, kwenye hii awamu ya tano miaka mitano hadi kumi ijayo litatokomea kabisa. Tunataka akinamama badala ya kupuliza moto wa mkaa waanze sasa kukandamiza na kuona mwanga mweupe wakati wa usiku. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwa sababu Serikali imejipanga, ina uhakika wa kuwapatia umeme wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie bei ya umeme. Umeme unapokuwa mwingi na umeme unapokuwa wa uhakika, kwa kawaida gharama za umeme zinashuka bei. Kwa sasa kwa sababu tunatumia kwa kiwango kikubwa umeme wa gesi na kiwango kikubwa sana pia umeme wa maji, tunataka sasa kuachana na umeme wa mafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua tulizochukua kuachana na umeme wa mafuta ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, mikataba yote iliyokuwa inatumia umeme wa mafuta inapokwisha sasa hatuiendelezi. Huo ni uamuzi wa Serikali. Kwa hiyo, tumeachana na umeme wa Aggreko, tumeachana na umeme wa Symbion kwenye mikataba ya dharura. Sasa hiyo ni kuonesha kwamba Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba umeme tunaoutumia ni wa gharama nafuu na unaondoa gharama kubwa kwa Serikali na wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, gharama za umeme kwa sasa kama mnavyojua, sasa hivi ili uunganishe umeme kwa wananchi wa Vijijini, ni sh. 27,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hapo, Mheshimiwa Waziri wangu wakati anawasilisha bajeti yake alieleza kwa kina sana, kwanza tumepunguza gharama zote za kuunganisha na kuomba umeme, lakini kadhalika tunatarajia wananchi watakapoanza kutumia umeme mwingi wa gesi, gharama huenda zikapungua zaidi. Kwa sasa tumeanzia kuondoa gharama za umeme wanapoomba leseni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tumeanzia na kuondoa gharama za umeme wananchi wanapoomba leseni. Kwa hiyo, wananchi wetu sasa hivi, twende tuwaeleze huko kijijini hawatakiwi kuwasilisha ombi kwa kulilipia, anakwenda anajaza fomu, anaipeleka, anapata umeme, kimsingi ni bure, ukiondoa ile gharama ya kodi ya VAT 28,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini akiunganishiwa umeme pia, ataendelea kuutumia umeme huo, TANESCO akija kufanya service halipii kitu chochote na penyewe ni bure. Kwa hiyo, tuwatangazie wananchi wajue sera za Serikali, lakini ili kusema kwamba tuna bei ya chini, tunajilinganisha na nani? Sisi tunaeleza mambo ya kisayansi. Kwa sasa hivi sisi tunazalisha Megawatts kwa ujumla wake 1,554.12 kwa sasa kwa ujumla wake. Kwenye taarifa yetu tumesema 1,461 zipo kwenye grid lakini ukijumlisha na ule ambao haupo kwenye grid ni 1,554.12.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya, kwa Afrika Mashariki ndiyo wanaoongoza peke yao wana megawatts 2,357, lakini nchi nyingine zote ziko chini yetu. Waganda kwa sasa wana megawatts 849, sasa hivi watu wa Burundi wenyewe wana megawatts 49 na wenzetu wa Rwanda wana megawatts 185.9, kwa hiyo, sisi ukiji-rank bado tupo juu kwa maana ya kuzalisha umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niwaeleze, maana yake Waheshimiwa Wabunge tunapozungumza masuala ya umeme kwa sababu tunazungumza uchumi lazima tuzungumze kwa takwimu. Sasa tunajilinganisha vipi kwa bei...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri naomba umalizie. Naomba uwe unamalizia, kengele ya pili tayari.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijazungumzia madini, nataka nizungumzie kwenye madini, nikimbie basi niende kwenye madini nizungumze kidogo. Pamoja na kwamba nimejieleza sana kwenye masuala ya umeme, lakini pia nizungumze kidogo kwenye tasnia ya madini.

**NAIBU SPIKA:** Dakika moja tu Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, niombe tu kusema, kwa sasa Wizara yetu inatenga maeneo mengi kwa ajili ya kuwagawia wananchi. Tumesema ni kilometa 12,000 tunatenga maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo. Maeneo yatakayotengewa sasa leseni na utafiti unaoendelea yako ya Kasubuya hekta 498, Malengwa hekta 682, yako pia ya Geita takribani hekta 2001 na mpaka kule Chato-Msasa hekta 12,28 na kadhalika na kadhalika. Nyamongo tunaendelea kufanya utafiti kugundua maeneo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba muda umekwisha, napenda sana nipatiwe muda niendeleo kusema zaidi kwa sababu ni nafasi ya pekee lakini kwa sababu muda umekwenda sana...

**NAIBU SPIKA:** Wakati mwingine Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Muhongo, Waziri wa Nishati na Madini.

**MBUNGE FULANI:** Kandamiza kweli kweli.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitoe shukurani nyingi kwa Wabunge wote kwa sababu maswali yalikuwa ni mengi sana mliyoyauliza kwa kuongea na maswali mengi sana mmeyauliza kwa maandishi na ikifika saa mbili usiku leo, tutakuwa yote tumeyajibu na tumeya-bind kama hivi, mpaka wale waliouliza kabla hatujakwenda mapumziko tayari tumeshayajibu. Kwa hiyo, niombe kwa ruhusa yako jibu la kila mtu tutaliweka kwa maandishi na tutawasambazia Wabunge wote kupitia ofisi ya Bunge. Hiyo inaonesha jinsi ambavyo ufanisi ulivyo mkubwa kwenye Wizara ya Nishati na Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kutoa shukurani kwamba yote mliyoyasema tumeyazingatia na tutayafanyia kazi kwa sababu maswali yanafanana fanana na ushauri unafanana fanana, ni vizuri nijibu kwa pamoja na ili mpatemwelekeo wa Taifa linakwenda wapi. Kwanza nianze na suala la Zanzibar, ndugu zangu wa Zanzibar hakuna suala lingine tena kwa sababu sheria imeshawaruhusu mnaweza mkatafuta mafuta wenyewe na mkayaendeleza nyie wenyewe. Hakuna anayewagandamiza, lakini niwaeleze mambo sasa ya kitaalam kuhusiana na hayo mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala ambalo itabidi mkae na majirani zenu na ndiyo maana inabidi utafiti ufanyike, ijulikane mna gesi kiasi gani, mna mafuta kiasi gani na yako wapi. Hilo swali hilo, yako wapi? Huku upande wa Msumbiji na Tanzania itabidi Tanzania na Msumbiji tukae chini kwa sababu gesi ile na mafuta haikuheshimu mpaka wa Ruvuma. Ziwa Tanganyika itabidi tukae pamoja na Kongo kwa sababu mafuta na gesi iliyomo pale haijaheshimu ule mpaka wa katikati ya ziwa. Kwa hiyo, ni vizuri ndugu zangu kama nchi moja ni lazima kwanza tujue mafuta hayo na gesi iko wapi, *geographic location*, halafu tukitoka pale tunakwenda kwa wataalam wanaojua, kuna *the law of the sea* ambayo ina *define continental shelf* na *margin* ya kila nchi. Kwa hiyo niwaachie hapo, inabidi bado tushirikiane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niye upande wa umeme, Naibu Waziri ameongelea, watu wanasema tuwe na vyanzo vingi. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na Watanzania ni kwamba Wizara inavijua, imeshavipigia mahesabu na hiyo ndiyo inaitwa *energy mix* au *energy matrix*. Tunakuwa na uhakika wa umeme kupatikana kwa sababu tutazalisha umeme kutoka kwenye gesi asilia, kwenye makaa ya mawe na kwenye maporomoko. Tutazalisha umeme kutoka kwenye jua, kwenye upepo, kwenye joto ardhi, kwenye *bio-energies* yaani *biomass* na *biogas*. Umeme wa joto ardhi, tumetengeneza ramani Tanzania tunajua joto ardhi iko wapi na ndiyo maana tunataka kuanza kuchoronga pale Ziwa Ngozi, Mbeya. Tunachotafuta sasa hivi ni kujua ukubwa wa *volume* ya ile *steam* inaweza ikazungusha *turbine* ya ukubwa gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaambie kwamba, vyanzo vipo, vinatosha na tunavifahamu. Hata *speed* ya upepo wa Singida tumeshapiga mahesabu, *speed* yake ni kali, ni mita tisa kwa sekunde moja ambayo inaruhusu kuweka mitambo ya kuzalisha umeme wa upepo na upande wa jua vile vile tumetengeneza ramani tunajua sehemu ambazo tunaweza tukapata umeme mwingi sehemu za Singida, Shinyanga na Dodoma. Kwa hiyo, kitaalam tuko vizuri tunajua kwamba umeme utapatikana wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niye kwenye suala la tunakokwenda. Haya mahesabu tukienda hatuendi kwa kubahatisha. Wizara hii ya Nishati na Madini ni lazima uchanganye sayansi, uchanganye na uchumi ndiyo utakwenda vizuri. Tumeshasema tuna maendeleo tunataka kuwa nchi ya kipato cha kati. Kuingia kwenye kipato cha kati kinaanzia dola 1,045, sisi tumesema tunataka kuanzia dola 3,000. Kwa hiyo, mwaka 2015 kama tutakuwa na *GDP per capita* ya dola 3,000 na sasa hivi *GDP* yetu ni karibu dola bilioni 50, iko inayumba yumba kidogo pale na tukichukulia kwamba tunazaliana kwa kiwango cha asilimia nne, kwa hiyo kufika mwaka 2025 huenda tutakuwa kati ya watu milioni 65 au milioni 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mahesabu tunachukulia milioni 70 ukipiga mahesabu ya *GDP per capita* 3,000 ni lazima *GDP* yetu iwe na bilioni zaidi ya 200, ndiyo linakuja suala la umeme sasa. Kuendesha huo uchumi unahitaji umeme mwingi na ndiyo maana unaona bajeti ya hii Wizara imejiwekeza kupatikana umeme mwingi, kwa hiyo ndugu zangu hivi vitu vinakwenda kwa mahesabu siyo kwa nadharia na ndiyo maana *speech* yangu ilikuwa imejaa takwimu, haikujaa malalamiko na matusi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu kwenye dunia ya sasa ni lazima tufanye biashara ya umeme. Ndiyo maana tunajenga huu msongo wa *kilovolt* 400 kutoka kwenye mpaka wa Zambia na kwenye mpaka wa Kenya. Tunataka kuuziana umeme, hakuna sababu wewe kununua umeme wa bei mbaya hapa wakati Ethiopia wana umeme wa bei nafuu, huko ndiko tunakokwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ethiopia na nchi za Afrika Mashariki, nchi 11 tumeshawekeana mkataba tutatumia umeme wa maji ambao ni senti saba kwa *unit* moja. Kwa hiyo, suala la kutumia umeme wa mafuta tena ni historia kwa hii nchi. Kwa nini mtu atuuzie umeme wa bei mbaya wakati *transmission line* tunatoa umeme Ethiopia kuja huku. Kwa hiyo, ndiyo maana ya kuweka hizi na ndiyo maana kila Jumapili umeme unakatika kwa sababu tunajenga msongo mkubwa wa kusafirisha umeme, ni heri uumie sasa upate faraja baadaye. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kuendesha haya yote tunaitaka TANESCO mpya. Wengine wanasema TANESCO igawanywe imekuwa kubwa sana. Ndugu zangu kwenye dunia ya nishati, TANESCO ni kitu kidogo kabisa hamna kitu. Kwa sababu kama alivyosema Naibu Waziri, uwezo wetu wote wa umeme ni *megawatts* 1,500. Kampuni moja India inazalisha umeme na kuuza zaidi ya *megawatts* 100,000, sasa wewe utagawa kampuni yenye *megawatts* 1,500 unakuwa unagawana umaskini tu pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, watu wanaopata huduma ya TANESCO bado ni wachache. Kwa hiyo, mabadiliko ya TANESCO ni kwamba inakwenda yenyewe inajibadilisha na sehemu zingine za TANESCO zinazikwa, zinakufa, ndiyo maana sasa hivi uzalishaji wa umeme uko wazi, kuwa mtu yeyote anaweza kuzalisha umeme na anaweza akamuuzia mtu yoyote bila kupitia TANESCO.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia ule mradi tunavyokwenda kufika mwaka 2025, kama ulivyo na simu ya *tigo*, ya *voda*, ya nini, TANESCO ya mwaka 2025 itakuwa ni hiyo hiyo. Unachagua nani akuuzie umeme kama ilivyo nchi zingine duniani na wote wamekwenda huko na wengine bahati nzuri wamekulia huko, kwa hiyo TANESCO inabadilika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji mpya nakiri kwamba kuna mikataba mibovu, sasa dawa yake tunatengeneza vigezo vya kuwekeza kuleta ushindani. Tarehe 30 hii *document* itakuwa tayari, itasambazwa dunia nzima na tutawaambia kwamba tunataka Lindi tunataka *megawatt* 300, je, wewe Kampuni hii unatupatia ofa ipi? Tunataka makampuni yashindane na hii itatoa haya mambo ya rushwa na mambo ya kupata mikataba mibaya. Kwa hiyo, ndugu zangu ngojeni tarehe 30 na kuonyesha kwamba sisi tuko wazi kabisa, *World Bank*, *African Development Bank* wote wamehusishwa kutengeneza hii *document*, ushindani. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, usafirishaji ameshauzeleza, usambazaji vile vile tunakokwenda ikiwa hawa wakandarasi wa REA wanasambaza umeme vijijini, kwa nini watu binafsi wasisambaze umeme badala ya kutegemea tu TANESCO? Ndiyo hiyo nasema mabadiliko TANESCO vile vile haitakuwa inasambaza



umeme peke yake. Ndiyo mabadiliko hayo yanakuja na hii *document* siyo vitu vya kichwani tumeshaitayarisha, imeshapitishwa kwenye *Cabinet*.

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la *TANESCO*, nakiri kwamba deni ni kubwa na upande mmoja ni mikataba mibovu, kuna wizi, kuna rushwa na uongozi dhaifu. Ndugu zangu Watanzania niwaeleze, mtu asije akaueleza ubora wa kampuni yoyote ambayo inauzia *TANESCO* umeme sasa hivi, haipo. Labda kama awe ametumwa kuishabikia lakini tukisema ukweli mbele ya Mwenyezi Mungu mikataba yote siyo mizuri. Sasa nimechukua hapa mifano, utasikia mwingine anaimba *SONGAS*, *SYMBION*. *SONGAS capacity charge* kwa mwezi tulikuwa tunawalipa dola za Marekani milioni nne nukta sita, *SYMBION* milioni mbili nukta nne, *IPTL* milioni mbili nukta sita, *AGGREKO* milioni mbili, hakuna ambayo ina manufaa makubwa kwetu. Kwa hiyo, ndugu zangu ninachowaomba Wabunge msitumiwe, msishabikie mkaja hapa kutetea Kampuni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uongozi wa *TANESCO* sasa hivi unabadilika, kila baada ya miezi mitatu tunafanya tathmini. Ukitaka kubaki Meneja wa *TANESCO* ni lazima kila baada ya miezi mitatu tukutathmini. Umekusanya fedha kiasi gani za Shirika? Umeunganisha wateja wapya kiasi gani? Umekuwa na ubunifu wa kutatua matatizo ya umeme kwenye eneo gani na kwa kiasi gani?. Tathmini ya pili inakuja tarehe 1 Juni, moja ilishafanyika watu wakaanguka, mwezi wa Sita tarehe moja inafanyika, tarehe 1 Septemba inafanyika. Kwa hiyo, kila miezi mitatu. Kwa hiyo, ukitaka kuwa Meneja *TANESCO* inabidi ujitume kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nguzo. Ni kweli kwamba nguzo tumesema *TANESCO* haipaswi kum-charge mtu. Ni tatizo la ukosefu wa fedha, tunakubali hilo lakini ni suala la mpito, huko tunakokwenda *TANESCO* ni lazima iwafuate wateja. Huwa nawaeleza ni mfano kama wa mtu anayenunua daladala kufanya biashara ya kusafirisha watu, halafu anakwenda kumwomba yule mtu atakayetumia daladala nipatie hela niongeze ninunue daladala, maana yake ndiyo hiyo ya *TANESCO* kuomba nguzo. Kwa hiyo, hiki ni kitu cha mpito ndugu zangu, yatakwisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nguzo za ndugu zangu wa Iringa, nimekwenda Iringa nimewatembelea, twendeni na vigezo. Kama mtu ana kiwanda cha nguzo aende *TANESCO*, ni lazima viwango vya *TANESCO* tuvikidhi. Hatuwezi kununua nguzo tu kwa kusema kwamba, haya mambo ya ubora hayana uzalendo, kwa sababu mambo yakiharibika mtawageuka tena *TANESCO*. Kwa hiyo, kama kuna mtu ana uwezo wa kuuza nguzo aje nguzo zake zifanyiwe tathmini na nguzo hizo tutanunua hapa. (*Makofi*)



Mheshimiwa Naibu Spika, umeme vijijini, REA Awamu ya II hadi sasa hivi ndugu zangu, jana Hazina imeweka bilioni 80.2. Hadi jana Serikali imeshatoa asilimia 80 ya fedha za REA Awamu ya II. Kwa hiyo, huko kwenu mtaona mabadiliko wakandarasi watakavyokwenda kasi, hamna kisingizio na nimemuuliza REA MD anasema hizo akizipata, Wakandarasi wanalipwa na nia yetu ni kazi za REA awamu ya II zote zikamilike ikifika Juni mwaka huu. Awamu ya III, mmeona tumeongeza. Sasa ndugu zangu, tuna shilingi bilioni 534.4 na Hazina kwa kuwa makusanyo yetu yamekuwa mazuri, nina uhakika fedha zote hizo zitapatikana. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali ya hiyo wengine hawakujua kwamba mbali ya hizi fedha, mnazopitisha humu Wizara nayo tunasumbuka, tunazunguka duniani kutafuta fedha. Msidhani ni za bajeti tu! Ndiyo maana Jumatatu msiponiona hapa nitakuwa nimekimbia kwenda kuwatafutia fedha. Mambo yakienda vizuri na tunajejadiliana naye mwingine anataka kumwaga milioni 200 REA, dola sio shilingi! Huko huwa tuna majadiliano kwenye dola tu sio shilingi tena. Kwa hiyo, akimwaga hizo 200 jamani mtakuwa wapi? Sasa tatizo kama hutaki bajeti hii ipite, basi sasa hata hiyo 200 usahau. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, solar kwa watu wa visiwani, nataka kuwahakikishia watu wa visiwani tumeshafanya uamuzi na REA, REA wameshaleta kwangu kwa maandishi kwamba visiwa vyote vilivyoko ndani ya mipaka ya Tanzania vitapata umeme wa jua – solar uzuri wa hii, hii tunaongea tayari tuna pesa, unajua huku Nishati na Madini tunaongea kitu cha uhakika. Tuna hela, wala hatulalamiki ooh! fulani katunyima hela ah ah! Tuna hela! Sasa uzuri wa hizi solar vijijini tunaomba Wabunge mtusaidie vijana waliosoma VETA wanaweza kwenda pale REA waone namna wanavyoweza kuwatumia. Wale vijana wenye utaalum, kuna fedha wanaweza wakapewa pale. Nendeni REA vijana wajikite kwenye huu umeme, tutatoa ajira, tutatoa na fedha na REA huwa inatoa fedha kuwawezesha watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakandarasi nimekaa nao vikao karibu viwili, wale wabovu wote hawatapata miradi tena niseme transformer za TANELEC mimi mwenyewe nilienda pale siyo kwamba waliosema hapa ndiyo wamegundua hilo, ni mimi nilienda pale. Ila wengine tuna kawaida ya kukaa kimya tunafanya vitu kimya kimya, kwa hiyo aliyeongea mambo ya TANELEC hapa siyo yeye wa kwanza, wa kwanza ni mimi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimewaeleza TANESCO na REA kwamba REA Awamu ya III tujitahidi kutumia transformer zetu kwa sababu wenye share kwenye TANELEC ni TANESCO na NDC nao wana share. Hata hivyo, ndugu zangu tatizo ni Sheria yetu ya Manunuzi, kwa hiyo tunaomba Sheria ya Manunuzi iweke sehemu kwamba ni lazima vitu vya ndani vitumike. Kibaya cha Sheria ya Manunuzi hata kama mtu anataka kula rushwa,

kudanganya anakimbilia hiyo sheria na nyie ndiyo mliipitisha humu mliokuwemo, mimi sikuwepo hapa wakati huo. Kwa nini mlipitisha hii sheria? (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja mafuta, wengi wamelalamika, lakini Waheshimiwa Wabunge na Watanzania tulisema usimamizi ni mbovu. Sasa hivi TPDC tumeitoa kwenye shughuli ya kufanya biashara, kutafuta mafuta na gesi, wakati huo huo inasimamia makampuni mengine. Kwa hiyo, tumeanzisha PURA (*Petroleum Upstream Regulatory Agency*). Hii ndiyo itasimamia mikataba yote, kila kitu hata TPDC yenyewe itasimamiwa, itapitia mikataba, itaweka ma-auditor, kwa hiyo, nadhani hapo tutakuwa tumepiga hatua na udhaifu huo utakuwa umetoweka. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, uagizwaji wa mafuta, vilevile tumeanzisha *Petroleum Bulk Procurement Agency*, huko nyuma ni waagizaji mafuta walikuwa wamejiweka pamoja wenyewe wanaji-regulate wenyewe, sasa tuna chombo cha Serikali na chenyewe kinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa mafuta wengi sana mmeongea EWURA, unajua Waheshimiwa Wabunge kuna mihimili mitatu, unashangaa mtu anayetaka kulazimisha mhimili wake ndiyo uwe na sauti kubwa kuliko mihimili mingine. Mlishatoa pendekezo kwamba EWURA iko Maji, iko Nishati inayumbayumba sasa nyie mmetoa ushauri kwa Executive, kwa hiyo ushauri wenu tunauchukua, tunakwenda kuufanyia kazi, lakini tusije hapa tena unasema tulisema, hapana! Mnashauri nyie, sisi tuna shauri Bunge, sasa ushauri unaweza ukachukuliwa au ukakataliwa. Hiyo ni muhimu sana, ushauri unaweza ukakubaliwa au ukakataliwa! Kwa hiyo, tutalichukua hili kama Serikali tutalifanyia kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la vinasaba limekuwa kubwa, mmeliongelea kwa hisia, hatuwezi kuamua hapa. Naitisha na nimeongea na wengine Jumanne kwa sababu nitakuwa nimepewa kazi zingine na wakubwa zangu, lakini Jumanne tarehe 24 yaani Jumanne ya wiki ijayo, saa nne asubuhi nataka nianze kikao cha kutatua hili tatizo la EWURA na vinasaba. Hatuwezi kulitolea uamuzi hapa, tukitoa hapa litakuwa la kisiasa maana sisi wote hapa wanasiasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeita wale wanaohifadhi mafuta, naomba watoe wawakilishi wanne wanaohifadhi mafuta, wawakilishi wanne wanaosafirisha mafuta, wawakilishi wanne wanaofanya biashara ya mafuta, waje pale Wizarani na mimi mwenyewe ndiyo nitakuwa Mwenyekiti, saa nne asubuhi Jumanne tarehe 24, tuyaongee yote waziwazi na EWURA ikae pale ijibu mapigo. Baada ya hapo ndiyo tutaona tunakwendaje, lakini suala la vinasaba hatuwezi kulifanyia uamuzi hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi asilia, LNG fidia italipwa, mmeomba tusomeshe vijana, ndugu zangu fuateni mambo tuliyoyafanya tumesomesha vijana wa Lindi na Mtwara wengi sana VETA. Tumewalipia kuja mpaka hapa chuo chetu. Wakati tunaenda mimi mwenyewe nimeomba *scholarships* China, wamenipatia *scholar* 25 kila mwaka kwa miaka mitano. Tunatafuta watu wa Lindi na Mtwara, kwa hiyo watu wa Lindi na Mtwara kusema tuwasomeshe tunajitahidi, ndugu yangu hawa wengine wa China wameshachaguliwa. Kwa hiyo, kama mna vijana muwalete halafu hii LNG biashara yake sio tu ya *oil and gas* unataka watu ma-*chemist* wazuri, ma-*physicist* na wengineo. Kwa hiyo, bado hao tunaotaka kuwasomesha lazima wapambane na mambo ya sayansi. Unajua mambo ya sayansi tena hayana mambo ya mkoa. (Makofi/Vicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge sawa mmesema tutawaita, tutakaa chini, tutaongea na watu wengi wa Lindi na Mtwara, tunaongea sana labda tu hii semina niwaite tena tukae chini, ni bahati mbaya wenzenu tuliwapeleka mpaka Norway, tumewapeleka Malaysia, tumejitahidi sana. Sasa mngewabakiza wale unajua! Haya! Gesi asilia inatumika viwandani sasa hivi tunavyosema kuna viwanda 37 Dar es Salaam vinatumia gesi na vinataka gesi zaidi. Kwa hiyo, ndugu zangu tusidhani kwamba gesi haijatumika, inatumika. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, gesi majumbani, tumefanya majaribio, bomba la kilometa 6.3 kutoka Ubungo mpaka Mikocheni nyumba za TPDC wale ndani ya nyumba wana mabomba mawili; bomba la maji na bomba la gesi. Tanzania ya Mheshimiwa Magufuli anayosema ya viwanda ndiyo hiyo hata nyie Wabunge tutaanza na nyie muwe na mabomba mawili la gesi na la maji. Hawa wa TPDC wananiambia kwamba kwa mwezi wanalipa shilingi 25,000 elfu kutumia gesi kupikia, chini kuliko hata mkaa. Kwa hiyo, huko ndiyo Tanzania mpya inayokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Lindi na Mtwara mnajua tumeshaanza kufanya *feasibility studies* na huenda tutazipata hizo fedha. Mimi mwenyewe nazisimamia kuzitafuta tutapata hizo fedha, ndiyo maana mwingine akisoma kwenye bajeti anasema mbona hapa mmeweka kidogo lakini hizi fedha ni nyingi, hapana! Sisi tunategemea fedha nyingi nje siyo hii. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna Lindi na Mtwara mtapata. Nyie wenyewe Waheshimiwa kwa kuwa ni Madiwani nyumba mjenge zimekaa kwenye foleni vizuri, mahali ambapo bomba litapita maana bomba kulipitisha kwenye *squatters* ni *problem* kweli kweli. Kwa hiyo, huo umeme unakuja Lindi na Mtwara na Dar es Salaam ndiyo tumeombea fedha kusambaza gesi majumbani. Sasa na hii gesi haitaishia hapo, Tanzania ijayo ambayo Mheshimiwa anasema ya viwanda anasema vitu vya uhakika. Sasa hivi hili

bomba kubwa linasafirisha kwa siku, *70 million cubic feet of natural gas per day*, lakini *capacity yake ni 784 million cubic feet of natural gas per day!* Hili bomba sasa hivi likianza kufanya kazi likijaa kabisa kufanya kazi na kugundua gesi lazima tupeleke mikoani. Kwa hiyo, hata mikoa itapata hii gesi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mengine, Kiwanda cha Mbolea cha Kilwa chenyewe kimepanga kuzalisha tani 3,800 kwa siku. Uwekezaji wake ni dola za Marekani bilioni moja nukta tisa. Sasa ndugu yangu wa Lindi ukisema tunapataje faida, kuna Kiwanda cha Mbolea kinakuja *investment one point nine billion US dollars* na bado unasema hujui utafaidikaje, saa zingine ndiyo maana huwa unaniona mzee nakaa kimya, nashindwa tu niseme nini sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi yale ya gesi siyo mengi kiasi hicho, huyu anahitaji *104 million cubic feet of natural gas per day*, kwa miaka 20 anakuwa kama amekuna upele tu, hajatumia gesi yoyote, wala kule msianze kuwa na masikitiko gesi yetu, yaani hazidishi TCF moja, havushi trillioni moja ya gesi kwa miaka 20. Ndiyo maana hata wale wa Mtwara wanaweza vile vile wakaanzisha hicho kiwanda na LNG ndugu yangu ukisema huoni faida ndiyo itakuwa *investment* kubwa katika historia ya nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende Dangote mmeiongelea sana, Dangote wameshindwana na TPDC bei, yeye anataka dola *tano* kwa *unit* TPDC inasema nne lakini wameshakubaliana watajenga *pipe* atatumia. Makaa ya mawe aliagiza South Africa mara moja tu! Tumemzuia atumie mawe ya Ngaka, gypsum nayo tumemzuia atumie gypsum za hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba la Uganda mmeliongelea tutalifanyia kazi, *finally* tunafanyia kazi, wiki ijayo tutaonana tena kulijadili tena. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, niye madini. Nyamongo ndugu yangu Heche tulikaa, ndiyo maana akiongea mimi natulia tu! Tuliweka Tume, tutakwenda pale itakuwa wazi. Sasa hayo yote aliyokuwa anaongea humu sijui yako kwenye ile ripoti, kwa hiyo atulie tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, Mererani *tanzanite*, tunajua kuna matatizo ya kufa na kupona lakini tunalifanyia kazi vile vile. Lakini kwa *tanzanite*, Watanzania sisi wenyewe tuliomo humu huwa tunasema wazawa, wazawa walio na hiyo kitu ni wazawa! Ndiyo maana siku nyingine nilisema, jamani hata mzawa, mgeni wote wanaweza kuwa sio wazuri. Sasa sijui mzawa akikuibia dola kumi na Mhindi akikuibia dola kumi yupi amekuibia nyingi? (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, haya kodi, katika mikataba na kodi za madini, ni kweli kwamba kuna migodi ambayo haijaanza kulipa kodi ya mapato (*Corporate Tax*), lakini karibu yote sasa tunaisimamia wataanza kulipa.

Vile vile Waheshimiwa mmetoa wazo la TMAA, TANSORT na TRA na hilo tunalichukua twende kulifanyia kazi. Wachimbaji wadogo, tumewapatia mlezi wao ni STAMICO, maeneo tunatoa na tutaendelea kutoa. Jumapili iliyopita nilikuwa nimekaa na watu wa World Bank watatoa karibu dola milioni 400 kuwasaidia. Kwa hiyo tunaendelea kuwasaidia sana, isipokuwa na nyie muwahimize walipe kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimalizie na hili la Mheshimiwa Zitto, alisema jamani mafuta mbaani ya siku tano ndege hazitui hapa. Nimepewa hapa takwimu inaonesha hadi sasa tuna lita milioni 8,749,810, haya yanatutosha mpaka Juni, sasa huyu aliyekwambia yamebaki ya siku tano yeye mwenyewe kaleta barua anasema anayo ya siku ngapi? Anayo ya siku 16. Ndiyo mambo nasema haya mambo magumu kidogo, alimwambia ana tano, huyo huyo kaleta barua nina ya siku 16. Kwa hiyo, tunachokifanya ni kwamba tunachukua tahadhari, tunashukuru sana tutaleta mafuta mengine tuhakikishe kwamba mafuta yapo. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huyu aliyesema mafuta yake ni machafu kuna sehemu ya hifadhi ya mafuta yake TBS imekuta ni masafi. Kwa hiyo, kuna mengine ana mchafu, huku ana masafi, niwaeleze hawa wa mafuta hii ni biashara ngumu, ni lazima tunavyoijadili humu tuwe makini sana. Huyu aliyelea ndiye amepatia PUMA, amepatia OILCOM, amepatia TOTAL, amepatia GAPCO. GAPCO ni safi, TOTAL safi, OILCOM safi, PUMA ndiyo analalamika, lakini sehemu ya shehena yake haina hiyo contamination na TBS wanaendelea kufanya utafiti na kujaribu kutafuta nini kimetokea. Lakini mafuta yapo, tunachukua tahadhari yasije yakaisha kabla, meli nyingine inakuja tarehe 13 Juni, kwa hiyo tunataka kuhakikisha tuna mafuta mengi kabla ya tarehe 13 Juni. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimemaliza sasa? Bunge lako lilikaa, aah! Sorry! Bado bado. (Kicheko)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijatoa hoja, kuna moja hapa limebaki la hawa wa magwangala lakini nilitatu. Jamani haya mabaki kuja kukaa dunia ya karne ya 21 unang'ang'ana kabisa mtu apewe mabaki ya mgodi, kusema kweli haiendani, kweli! Inaweza kuwa hamna kitu humu. Ni wananchi na CHADEMA ndiyo mlimtuma...

**WABUNGE FULANI:** Aliombwa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Aliombwa? Wananchi ndiyo walimwomba. Mnyika sasa kama...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ongea na kiti.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Ooh samahani, lakini unajua Mheshimiwa Mnyika, kijana wangu huwa mara nyingi kabla sijamaliza nampatia swali la kichwa. Je, nimpatie, nisimpe?

**WABUNGE FULANI:** Mpe

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Nimpe, nisimpe?

**WABUNGE FULANI:** Mpe!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya naomba kutoa hoja. (Makofi/Kicheko)

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA, NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono. Nitawahoji baadaye, Katibu.

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

#### **KAMATI YA MATUMIZI**

**NAIBU SPIKA:** Kamati ya matumizi, tukae, katibu

**NDG. CHARLES MLOKA –KATIBU MEZANI:**

#### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Kif. 1001 - Admin. and HR Mgt... .. Sh. 4,770,307,000/=

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumeletewa orodha hapa ya watu ambao wangependa kuongea kwenye mshahara wa Waziri, tutaanza na kutoka CCM, Mheshimiwa George Malima Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, sina shida na mshahara wa Mheshimiwa Waziri ila naomba tu kidogo maelezo kwa *substation* ya Zuzu kupitia njia ya umeme inayoitwa Mpwapwa feeder, ndio inayogawa umeme maeneo ya Wilaya ya Chamwino, Gairo, Kongwa, Mpwapwa mpaka Kibakwe. Sasa kuna uwezekano mkubwa njia ni ndefu na imechakaa sasa na ndiyo maana umeme unakatika mara kwa mara katika maeneo hayo. Sasa nina ombi kwa Mheshimiwa Waziri, je, anaweza kutusogezea kituo cha kupooza umeme cha *grid* aidha kiwe Mpwapwa au Kongwa?



Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawezekana ikapunguza kukatikakatika kwa umeme katika maeneo hayo katika Wilaya karibu nne au tano hivi, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ni kwamba, haya ni mambo ya kitaalam namuahidi kwamba nina timu yangu ya TANESCO na Jumatatu kabla ya kuelekea Dar es Salaam watapita maeneo hayo aone kitaalam sehemu ipi inawezekana kutatua tatizo hilo.

**MWENYEKITI:** Naona Mheshimiwa Lubeleje ameridhika na majibu, Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kushika mshahara wa Waziri iwapo sitapata maelezo yanayoridhisha. Suala la usambazaji umeme vijijini ni suala nyeti sana kwa sisi Wabunge wote na Watanzania wote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba melezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri suala la Mfuko wa REA, ni *ring fenced* na kumekuwa kuna *concern* baina ya Wabunge kwamba kumekuwa kuna *delay* ya ku-*disburse* hela kutoka Hazina kwenda kwenye Mfuko wa REA. Sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri atakaposimama atoe *assurance beyond reasonable doubt* kwamba *going forward* changamoto hii haitakuwepo na hizi hela zitakuwa zinaenda moja kwa moja kwenye Mfuko wa REA ili wananchi wetu wapate umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ningependa kupata *clarification* ya namna REA Phase III.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashungwa unaunganisha au ni kitu kimoja?

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Ni kitu kimoja.

**MWENYEKITI:** Maana mshahara wa Waziri huwa ni sera sasa ukichanganya mambo hapo kidogo itatupa tabu.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Sehemu ya pili, ya *issue* ni *clarification* ya REA Phase III. Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Waziri wametoa *clarification* nzuri kwamba sasa hivi umeme umepita kwenye vijiji vyetu maeneo ya barabarani, ningependa kupata *commitment* kutoka Serikalini kwamba REA Phase III haitaendelea kusambaza maeneo ya barabarani bali itaingia ndani ya vijiji ili wananchi wetu vijijini wapate umeme. Nashukuru. (Makofi)



**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kwenye kusambaza umeme ni sawasawa kama ambavyo unajenga barabara, kwanza unaanza na *main road*. Kwa hiyo, kitu cha kwanza cha kushukuru ni kwamba umeme mwingi umeingia kwenye kijiji yaani *high tension* na sisi tunajua kwamba tunalazimika sasa, *REA Phase III* ni lazima twende ndani zaidi na hata hivyo kwenye *Phase III* kuna kwenda ndani lakini bado kuna kurudi nyuma kwa vile vijiji vilivyorukwa ili tushushe umeme kwa kufunga *transformer*. Kwa hiyo, namhakikishia kwamba na hizi fedha na zingine tunazotafuta hali itakuwa ni tofauti sana, lakini cha muhimu njia kuu imefika kijijini mwako. Hili la fedha bahati nzuri ninaye aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha hapa, naomba atusaidie kujibu sasa hivi ni Waziri wa Kilimo ana majibu mazuri zaidi yangu mimi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niweke wazi kwamba mimi ni *care taker* wa Wizara ya Fedha kwa hiyo hapa nakaimu Wizara ya Fedha ambapo Waziri wa Fedha na Naibu wake hawapo. Hii ni *commitment* ya Wizara ya Fedha kwamba kipindi kilichopita ni sawa tulishatengeneza sera ya *ring fencing*, lakini kiutendaji fedha zote ambazo ziko *ring fenced* zilikuwa bado zinakaa kwenye Mfuko ule ule. Matumizi yakianza kutumika *first charge* ikitoka *second charge* zinakuwa zinatoka kwenye fungu lile lile. Kwa hiyo, inatoka mishahara, linatoka deni la Taifa, kinachobaki ndiyo kinaanza kukumbukwa kwenye *ring fencing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa sasa na kuanzia tarehe Mosi Julai, fedha zote ambazo ziko *ring fenced* za *REA* pamoja na za Mifuko mingine kama ya *TANROADs* hazitakuwa zinawekwa tena kwenye Mfuko Mkuu ambako matumizi mengine pia yanatumika. Kwa maana hiyo, hakutatokea tena utaratibu wa fedha ambazo zilitengwa kwa ajili ya *REA* kuchanganywa na matumizi mengine, zitakuwa zinakwenda moja kwa moja kwenye akaunti maalum, zikishakusanywa zinakwenda moja kwa moja kwenye akaunti maalum. Hivyo, Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na Wizara zingine ambazo zina Mifuko Maalum hazitapata tena usumbufu wa fedha zilizokuwa *ring fenced* kutumika kwenye matumizi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Innocent Bashungwa arudishe tu shilingi ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini ikizingatiwa Wabunge wote hata wa Upinzani walikuwa wanajinadi kutumia umeme aliopeleka Mheshimiwa Profesa Muhongo ili wapate kura. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Alikuwa hajatoa shilingi na nadhani amesharidhika na majibu. Mheshimiwa John Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kuna jambo nitaliombea ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na iwapo ufafanuzi hautajiridhisha nitaomba nipewe nafasi ya kutoa hoja ya kuondoa shilingi. Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni wakati wa kujibu maswali na hata nje ya Bunge kwenye vyombo vya habari amekuwa akisema kwamba Tanzania haikukosa fedha za *compact II* za MCC kwenye sekta ya nishati kwa maana ya umeme bali ni fedha ambazo zilikuwa zinahusika na masuala ya maji na barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninao ushahidi wenye kuonesha kwamba Tanzania iliomba kiasi cha dola milioni 472.8 ambazo ni zaidi ya bilioni 800 ambazo tuko kwenye hatari ya kuzikosa na Mheshimiwa Waziri aeleze ni sababu zipi zinazofanya hizi fedha tuna hatari ya kuzikosa, fedha ambazo zilikuwa zisaidie miradi ifuatayo:-

*Power sector reform project* dola milioni 39.3; *TANESCO transformation project* dola milioni 88.3, *Access electricity project* dola milioni 219; *Zanzibar project* dola milioni 58.6 na *Productive uses project* dola milioni 7.0.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni fedha nyingi sana kwa miradi mikubwa kweli ambapo tungezipata Waziri aeleze ni vigezo vipi ambavyo tumeshindwa kuvifikia vya *MCC compact II* na kwa nini amekuwa akitoa maelezo ya uongo Bungeni juu ya suala hili na namna gani jambo hili litamalizika kwa maslahi ya wananchi kwa miradi yote hiyo. Naomba majibu ya Mheshimiwa Waziri. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti siyo kwamba hiyo *document* ni ya ajabu hata mimi ninayo hapa na kwa ufahamisho ni mimi niliitengeneza Marekani nikiwa nimekaa na mtu wa MCC na Waziri wa Marekani, kwa hiyo, siyo kitu kigeni. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa jibu langu linabaki pale pale, watu walikuwa wanalalamika, wanasema umeme vijijini yaani REA imekosa fedha za MCC na REA haina fedha za MCC, kama hapa hamna, ukweli ndio huo. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja ya kuondoa shilingi. Hapa nilipo nina barua pepe, ambayo inatoka kwa Laston Msongole Mratibu wa MCA Tanzania II kwenda kwa vigogo kadhaa wa Wizara isipokuwa Waziri hakuwa *copied*, inasema yafuatayo na ndiyo maana nasema

Waziri anasema uongo, Bwana Masanja nimemsikia Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini anavyojibu maswali Bungeni juu ya *MCC Compact II* na kabla ya hapo niliona alivyokuwa anajibu maswali ya waandishi wa habari juu ya athari za kusitishwa kwa *Compact II* kuna *distortion* kubwa za msingi. Kwanza si kweli kwamba *compact* tuliyokubaliana, Wizara ya Nishati na Madini mlishiriki kikamilifu, hati ilikuwa iishie Sekta ya Maji na Barabara. *Documents* za *negotiation* zilizofanyika Washington wote tunazo pamoja nanyi. *Compact* hii ilikuwa *exclusive* kwa ajili ya Sekta ya Nishati hususan umeme kwa fedha zote zilikuwa zimeahidiwa USD dola 472.8 milioni. Angalia *attachments* hizo, ninazo nyaraka za nyongeza, nisitumie muda mrefu kwenda kwenye nyaraka za nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanaendelea kusema mjue kwa vyovyote vile itakavyokuwa ukweli huu ukiwekwa wazi ninyi ndio mtakaobeba mzigo wa kumpotosha Waziri wenu. Kwa hiyo, maana yake ni nini; Waziri umepotoshwa katika maelezo yako na umekuwa ukitoa maelezo ya uongo ndani na nje ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa jambo la msingi ambalo nataka lijadiliwe, Waziri hujajibu bado vitu vilivyofanya Tanzania kuwe na hati hati ya kuzikosa hizi fedha, kwa sababu fedha ikikosekana zina athari kwenye miradi ya maendeleo niliyoitaja. Natoa shilingi tujadili kwa sababu fedha hizi zinahitajika kwa miradi mbalimbali ya maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja jambo hili lijadiliwe. (*Makofi*)

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda Mheshimiwa Mwijage, halafu aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Simbachawene halafu Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Sakaya wanatosha. Tutaanza na, Mheshimiwa Ester Bulaya tafadhali tuendeleo na kikao, tutaanza na Mheshimiwa Mwijage.

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge nimekuwa nikihudhuria Bunge, nimekuwa nikimsikiliza Waziri wa Nishati na Madini akijibu maswali, lakini nimekuwa Naibu wa Waziri wa Nishati na Madini, Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, umeme wa *REA* tumeutolea jasho, tumeutolea jasho sisi ndiyo tuliweka tozo kwa kufuata maelekeo ya ilani ya chama chetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo Msongole anayeitwa Msongole ni kuwadi wa wapi, tumeamua sisi tutajenga umeme wetu pesa iko hapa, hakuna kitu

ambacho Mheshimiwa Waziri amezungumza kwa kupotosha huyo Msongole anayeandika meseji anayeandika *e-mail* anamtishia nani? Watanzania wanalipa shilingi mia kwa kila lita ya mafuta, kwa ajili ya umeme wao. Watanzania wanajua tumeongeza bei ya mafuta ya taa, Watanzania wanajua huu umeme wa REA ni umeme wa kwetu na tutaendelea kutoza tozo na tutajiwezesha sisi wenyewe lazima mjenge uwezo wa kujitegemea, *over dependency syndrome* hata viwanda hamtaviweza lazima muweze Watanzania tukubaliane tunakwenda na umeme tunaozungumzia ni wa REA. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu kama hawezi kukusindikiza akakufikisha, aondoke arudi, kama MCC waliona tuna upungufu watuache tutatembea kwa nguvu zetu, walikuja kutusaidia, waache waondoke. (Makofi/vigelegele)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nasimama kuunga hoja ya Mheshimiwa Mnyika, kuhusiana na suala la miradi ya MCC ndani ya michango iliyokuwa inatolewa tangu jana tumeshuhudia Waheshimiwa Wabunge, wakiwa wanamtaka Mheshimiwa Waziri, awathibitishie ni kwa namna gani miradi ambayo ilikuwa ndani ya MCC itaweza kuhudumiwa na Serikali ndani ya michango hii humu na hata tukifuata *hansard paper* itaonesha hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi kuamkia jana Mheshimiwa Waziri mwenyewe ndani ya Bunge hili alisema , mradi wa MCC ni kama mtu unalima shamba, ulikuwa una heka zako nane, akaja mtu akakwambia kwamba naongeza heka mbili, zile heka nane unaweza ukazilima, lakini zile heka mbili asipokupa hela hutazilima na kwenye hili kuongezewa heka mbili kwenye kulima ni faida kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kitu ambacho tayari kweli kweli ni faida kwa Watanzania. Kwa hiyo, kitendo cha Serikali kuruhusu zile heka mbili zikakatizwa kwa sababu ya kushindwa kutimiza masharti ya kuweza kupata zile fedha ni hasara kwa Watanzania. Kwa hiyo, siyo kweli Waziri atuambie kwamba ile ilikuwepo, tatizo ni kwamba tumeshindwa kuzitumia, kwa hiyo, tukubali lazima Waziri aweze kutueleza hayo. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada Mkuya Salum.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nadhani na mimi nitoe mchango katika suala hili ambalo lilianza toka Bunge lililopita. *Of course* Tanzania ili-pass vigezo vyote kwa ajili ya ku-access fedha hizi za MCC. Kinachotokea sasa hivi kupata fedha za MCC ni mchakato na sisi

Tanzania maana yake hatutaweza kusimama kuendelea, *simply* kwa sababu wenzetu wa MCC wanaona kuna upungufu katika *point* za *good governance* Tanzania. Sisi wenyewe kama nchi tunaona tunakwenda sawa na ni kweli kwamba, nadhani kwa *speed* ambayo tunakwenda tutaweza kabisa kufidia lile pengo ambalo MCC watasema kwamba basi hawataki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, *point* wanazo ni vigezo kwenye *good governance* na wao ni muono wao sisi kama nchi tunaona tunakwenda sawa na naamini Mheshimiwa Mnyika, tutafika tutakwenda na nadhani ni utaratibu tu wa kawaida nchi kama wao wafadhili wanaona kwamba tuwanyime msaada tunaweza tukasimama tutakwenda kwa miguu yetu. Siku zote tunachotaka kusema hapa kwamba, Tanzania sasa hivi lazima tujitegemee na hizi changamoto tunazopata zinatufunza kwamba Tanzania tusimame twende mbele tuweze kujitegemea kwa mapato yetu sisi wenyewe. Nadhani Mheshimiwa Waziri alikuwa yuko sahihi kwamba tunaweza kwenda mbele katika suala hili. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Taifa letu liweze kuheshimika ni lazima tujenge uwezo wetu wa ndani wa kujitegemea. Ili Taifa letu liweze kuwa na hadhi na heshima tunayokusudia ya kwenda kwenye uchumi wa kati, ni lazima isiwe eti nongwa tunaponyimwa msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivi ni lini wenzetu wa upande wa pili wamewahi kuulilia misaada ambayo tumenyimwa? Hivi ni kwa nini huu unadaiwa kwa nguvu sana na kuonekana mna uchungu sana kwa kuukosa huu msaada? Hivi kweli Msongole na Waziri tumwamini nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hapa mtoa hoja anachotaka kutuambia ni kwamba, Mheshimiwa Waziri tusimwamini, tumwamini huyo Msongole, ambaye hatumjui, hatumfahamu, hatumuoni hapa! Ni ukweli kabisa kwamba, tutatekeleza miradi ya REA kwa nguvu yetu na Waziri amesema tumeongeza fedha kwa ajili ya miradi vijijini nyingi kuliko hata ilivyokuwa wakati wowote huko nyuma, kwa kutumia fedha zetu za ndani. Hivyo ndivyo tutakavyojenga Taifa linaloheshimika, lakini sio kwa kuulilia misaada! Mbona mnaulilia huu, una nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutafuata maneno ya Mheshimiwa Waziri ambaye tunaweza au Bunge linaweza kumwajibisha; nitashangaa kama Bunge litamfuata huyu Mwasongole, sijui nani, ambaye hatumjui hapa! *(Makofi)*

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika. Kuna wakati mnasikitisha sana yaani mtu kama

Mheshimiwa Saada anaongea anapiga *bush* tu! Mheshimiwa Saada, pesa hizi mlienda kuomba za nini kama mlikuwa hamtaki huo msaada kwanza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja hapa, Mheshimiwa Mnyika amesema hizi pesa kulikuwa na pesa za REA au hakuna pesa za REA? Hiyo ndiyo hoja hapa! Sasa mnapiga *around the bush*! Mheshimiwa Waziri juzi, Mheshimiwa Muhongo nakuheshimu, wewe niache nizungumze! Juzi amesema hapa ametoa mfano wakati anajibu swali la Mheshimiwa Msigwa kwamba, ulikuwa unalima heka nane mtu akaja mtu kukuongezea heka mbili, ina maana anakiri kwamba, mle kuna pesa za REA! Sasa badala ya kujibu hoja hapa, mradi wa umeme huu, badala ya kujibu hii hoja anaanza...

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)

**MHE. JOHN W. HECHE:** Tulieni!

**MWENYEKITI:** *Order!* Waheshimiwa tusikilizane!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie watulie!

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tusikilizane! Mheshimiwa Heche malizia!

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, waambie watulie!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni kukiri kwamba, kulikuwa na pesa za umeme au hakuna pesa za umeme, basi! Mambo mengine ya kelele kelele, wana-*twist*, *twist* haisaidii na Jumatatu mnaenda kuomba tena msaada mwingine! (*Makofi*)

(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Nishati ameweka vizuri sana kwenye sentensi yake. Ninachoshangaa kwanza kama kuna mtu amefuatilia kwa makini alichosema Waziri, anashangaa hapa tunabishania nini! Waziri anachosemea kulikuwa na *parallel initiatives*, yeye anachosema hakikuwepo ni kwenye REA na wote tunajua hapa fedha tuliyoongeza kupeleka kwenye REA, hiki kiko wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini cha pili, Mheshimiwa Mnyika mara nyingi nimekuwa nikijua ana-*reason* vitu, hivi kweli, unaweza ukatuletea *e-mail* ambayo haikuwa *verified* popote ukachukulia kama ni *official document* ya kuweza kutumia hapa! Eeh! Mara ngapi tumekuwa tukiona watu



wakitengeneza *e-mails* na kuzisambaza kwa vitu na baadaye zinakuwa haziko *verified!* Tunawezaje kutumia *e-meil* na mtu yeyote anayeweza akaunganisha majina tu na akaandika na akasema, halafu na wewe unaita *direct* kwenye mjadala ambao ni *very sensitive* wa kujadili masuala ya Kitaifa! Hiyo na yenyewe ni kutokuwa *fair!* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niseme maelezo ya Mheshimiwa Waziri yanajitosheleza na yako *professional* na yana ukweli na yako *backed* na *facts*. Kwenye hili lingine ambalo limeletwa kwa heshima zote kwa Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Mnyika, hapa hapakuwa mahali pake kwa sababu, alichokisemea Mheshimiwa Waziri ni tofauti na kile ambacho amekiongelea. Hiyo, *e-mail* ambayo ameikota leo hii tukisema tunatumia hiyo, tukianza ku-*recall e-mails* nyingine hata yeye mwenyewe ambazo zimewahi kuandikwa juu yake atakataa kwamba, *e-mails* hizo kuna watu wamezitengeneza kuzileta hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Mnyika, rudisha shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili Mheshimiwa Waziri aendelee kulitumikia Taifa. Hakuna haja ya kuweka jambo la aina hiyo katika suala la msingi ambalo liko *backed* na *fact* hapa. (Makofi)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu tuongee kama Watanzania halafu tuwe waangalifu kujifunza Kiingereza kizuri. Kabla na sasa inabidi vingine tuviongee ambavyo hata mlikuwa hampaswi kuvifahamu. Siku mbili kabla ya Bodi kufanya maamuzi haya, Mwenyekiti wa Bodi ya MCC ni Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Marekani; siku mbili kabla nimefanya kikao cha masaa zaidi ya manne nikiwa naelezwa na Wamarekani wenyewe, siyo vizuri kueleza kwamba, nini kitaamuliwa kwenye hiyo Bodi. Kwa hiyo, nilijua nini kitaamuliwa na kwa sababu zipi na wote tunafahamu sababu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaombwa...

**WABUNGE FULANI:** Sababu ni uchaguzi wa Zanzibar.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Yes sababu ilikuwa ni uchaguzi wa Zanzibar! Yes, sawa, wakasema, tena niende mbali zaidi! Sasa ni kwamba, hapa *statement* ya Wamarekani na walivyofanya hiyo *decision*, John Kerry ambaye ni *Foreign Secretary*, neno lililotumiwa ndio maana mtu aking'ang'ania hili neno la Kiingereza, wao MCC wame-suspend hawaja-cancel! Wame-suspend, sasa wcha tuongee kama Watanzania.



Mheshimiwa Mwenyekiti, hii sio mara ya kwanza, wakati wa *East Germany* na *West Germany* walitaka kutupatia masharti Mwalimu alikataa! Ujerumani ya Magharibi ilitushutumu kwa nini tunashirikiana na Ujerumani ya Mashariki, ikatuwekea masharti, Mwalimu hakukubali hayo masharti, tukakataa, wakakatisha msaada wao, lakini baadae wakarudi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo Marekani tunayoiamini kwamba, maamuzi yao ni mazuri sana tuangalie Cuba na USA nini kimetokea juzi! Uhasama umekwisha! Kwa hiyo, ndugu zangu ni kwamba, sisi tutaenda wenyewe kama Taifa, fedha za REA narudia kusema, narudia na niko palepale fedha za REA hazina mchango wa MCC hata senti moja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, alichosema Mheshimiwa Mnyika kwamba, REA inapokea fedha za MCC siyo kweli na hoja hii ifutwe.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kuhusu Utaratibu!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika ni zamu yako sasa kufunga hoja yako kwa hiyo, Utaratibu haupo! Naomba ufunge hoja!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nafunga hoja kwa kusema kwanza Mheshimiwa Waziri amesema uwongo kwa sababu mimi katika maelezo yangu yote hakuna mahali ambapo nilisema kwamba, fedha hizi ni fedha za REA. Nilichokisema ni kwamba...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walionge  
bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Chukueni Hansard!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, wewe ongea na mimi! Waheshimiwa tusikilizane! Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari...

**MWENYEKITI:** Wewe ongea na Kiti! Wewe ongea na Kiti!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna shaka, naongea na wewe! Niko tayari hapa itolewe *Hansard* tuthibitishe mimi na Mheshimiwa Waziri nani amesema uwongo! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichokisema ni kwamba, Mheshimiwa Waziri amekuwa akinukuliwa akisema *MCC Compact II* ni kwa ajili ya masuala ya barabara na maji, si umeme! Nikatoa maelezo hapa yenye kuonesha miradi ya

umeme tunayoikosa na ni miradi mingi! Sio tu ya vijijini na mpaka Dar-es-Salaam kuna miradi tunaikosa! Mpaka Zanzibar kuna miradi tunaikosa! Miradi ya Dola milioni 472! Dola milioni 472, yani zaidi ya bilioni 800 ni fedha nyingi sana kuzikosa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninyi ambao ndio mmetembeza bakuli, ndiyo ombaomba! Serikali ya CCM ndiyo ambayo imekuwa ikiombaomba ikishindwa kujitegemea, leo mnataka kuonesha kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Nenda Mirembe.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eti mnatetea maslahi, ni unafiki tu, tuache unafiki huyu Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesema...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika, dakika moja umalizie hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri mwenyewe amesema kwenye maelezo yake, hata MCC hata REA Phase III amesema anakwenda Jumatatu kwenda kuomba hela! Umesema Waziri unakwenda kuomba hela sehemu nyingine! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini yote haya nihitimishe kwa kusema kwamba, mko tayari ninyi kwa gharama ya uchaguzi wa Zanzibar, nchi hii ikose miradi kwa gharama ya uchaguzi wa Zanzibar.

**MBUNGE FULANI:** Nenda Mirembe!

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shilingi hii siirudishi, ili iwe kwenye record kwamba, kwa gharama za kukosa Utawala Bora, kuvuruga uchaguzi, kuvunja haki za binadamu, mko tayari Tanzania ikose misaada na iko siku hali hii itawahukumu itakapowaondoa madarakani. Ahsante sana! Siirudishi shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Mnyika, nadhani umeshikilia shilingi kwa hiyo, ngoja tuhoji! Waheshimiwa Wabunge kuwe na order! Halafu naomba sana msiwashe microphones tafadhali. Sasa nitawahoji hoja ya Mheshimiwa Mnyika imetolewa!

**MHE. JOHN HECHE:** Yule Mhindi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Heche, tafadhali! Mheshimiwa Heche naomba ukae, Mheshimiwa Heche!

**MBUNGE FULANI:** Njoo basi.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Tokaaa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge naomba tutulie! Nitawahoji! Wanaokubaliana na Hoja ya Mheshimiwa Mnyika ya kutoa shilingi sasa waseme...

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ametoa hoja Waheshimiwa!

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge waliongea  
bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ametoa hoja! Nitawahoji! Waheshimiwa Wabunge tusikilizane! Msijibizane wenyewe! Tusikilizane, Mheshimiwa Esther tafadhali! sasa nawahoji. Waliosema Siyo wameshinda! Kwa hiyo, Shilingi ya Mheshimiwa Waziri inabaki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Watu wengine watakaozungumza kwenye hii hoja nitawasoma, lakini kabla ya hapo, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1) nitaongeza nusu saa, ili tuweze kumalizia Kamati ya Matumizi. Sasa nitamwita Mheshimiwa Magdalena Sakaya!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia nilizungumzia suala la uwepo wa makaa ya mawe katika nchi yetu ya Tanzania na namna ambavyo kwa miaka karibu 20 Serikali imekuwa inasuasua kutokuwa na miradi ya kimkakati kuhakikisha kwamba, makaa haya yanatumika, hasa kwa ajili ya nishati ya matumizi ya nyumbani ili kuokoa misitu ambayo inaharibika kwa speed kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana labda ni muda haukutosha Mheshimiwa Waziri kueleza, lakini ningepomba tupate ufafanuzi ni kwa nini kwa miaka yote makaa ambayo tunayo kule Mbinga na maeneo mengine tumeshindwa kuweka mchakato yakatumika kama nishati kwa ajili ya matumizi ya nyumbani? Ahsante.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani katika kuhitimisha hoja yangu nilisema kwamba, tuna mchanganyiko wa nishati, *energy mix* au *energy matrix*. Tulivyojipanga ni kwamba kwa sasa hivi kuwekeza kwa haraka sana tutatumia gesi, ndiyo maana tuna uhakika wa hizo *megawatt* tunazosisema kwa sababu, gesi asilia ya ujazo wa trilioni futi moja unaweza ukazalisha *megawatt* 5,000. Kwa hiyo, hata ule wa baharini tusipouchimba tusipoleta huu wa nchi kavu tuna *TCF* 10.8 ambazo ni *megawatt* zaidi ya 50,000. Kwa hiyo, tunaongea kitu cha uhakika, lakini tunavyokwenda mbele tunataka tupunguze matumizi ya gesi, gesi itumike kwenye viwanda na sehemu nyingine na badala yake tuongeze matumizi ya makaa ya mawe na matumizi ya umeme wa maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siyo kwamba, hatujui makaa ya mawe yako wapi yako kiasi gani! Miaka 10 nyuma tuliweka makisio kwamba, *reserves* zetu ni tani bilioni tano, sasa hivi nadhani zimefika 10. Mgodi uliokuwepo ulikuwa wa Kiwira uliwahi kufikisha *megawatt* 20 ukashuka mpaka *megawatt* moja. Sasa tarehe 30 Agosti, ndicho nilichokisema hicho, natengeneza *document* ya kuleta watu wa kushindana na hawa watu tutawaelekeza; Kiwira tunataka *megawatt* 200 wewe unatupa ofa gani? Huko Mbinga unakosema, kote tumekwenda tuna ramani, tunajua hayo madini yalipo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kwamba, hizi *megawatt* elfu 10 au 15 unazozisikia tunazitaja makaa ya mawe yamo sana. Sasa kuna suala la kuyatumia majumbani, hapa ni lazima uyafanyie utafiti uangalie *sulphur content* kusudi usije ukatengeneza *toxic gas* kama *sulphur dioxide* wakati unayachoma. Ndiyo maana hata wale akinamama wa kule Mbinga niliwakuta wanatengeneza yale makaa tukaenda kuyafanyia utafiti pamoja na *COSTECH* kuangalia *sulphur content* tukakuta iko chini, lakini vilevile kuna *ash content*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimfahamishe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, makaa ya mawe kwenye mipangilio yetu ni muhimu sana na tutayatumia kwa wingi sana. Kwa sasa hivi ile uliyokuwa unasema unaona magari yanapita, sijui yanaenda wapi, mgodi ambao unazalisha makaa mengi sasa hivi ni mgodi wa Ngaka, una uwezo wa kuzalisha tani nusu milioni kwa mwaka, ndio maana tunailazimisha Dangote itumie makaa ya Ngaka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutatumia makaa hata ya huko Mbinga tutayatumia kwa wingi sana. Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya, nilikusikia kama umesema ulitaka maelezo ya ziada! Hayajakuridhisha? Haya, endelea!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini kwa umuhimu wa suala hili naomba niseme kwamba, nitatoa Shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri amesema sasa hivi kipaumbele kwanza ni kwenye suala la gesi, lakini hivi sasa tunavyoongea kuna gesi! Gesi kile kidumu kimoja kinaenda kwenye 56,000/= au 58,000/=, jaribu kupiga mahesabu kile kina kilo 15, ni Watanzania wangapi ambao wana uwezo wa kutumia gesi sasa hivi kwa ajili ya kupikia? Kwa ajili ya kuchemshia maharage, kupikia vyakula vyote vya Watanzania nani mwenye uwezo wa kuweza kuitumia gesi? Kwa hiyo, pamoja na uwepo wa gesi hiyo, lakini bado wanaotumia ni wachache! Ndio maana mpaka sasa hivi asilimia kubwa ya Watanzania wanatumia mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kusema kwamba kipaumbele ni kwenye suala la gesi, bado nasema kwamba kwa upande wa viwandani sawa, lakini kwa matumizi ya nyumbani bado. Mheshimiwa Waziri anasema kwamba kote wamefika, Ngaka wamefikia, wamefika na kule Mbinga. Kufika na kuona siyo *solution*, yameonekana miaka mingi iliyopita, *solution how can you use it, that is the problem?* (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kwenda kuyatembelea, yako kwenye ramani, ziko kibao, lakini tatizo kama yanafahamika na yanajulikana kwa nini hayapewi kipaumbele cha matumizi ili tuweze kuokoa rasilimali zetu za misitu ambayo tunakwenda kwenye jangwa? Hiyo ndiyo *point* yangu, nimeshatoa hoja.

**WABUNGE FULANI:** Toa hoja.

**MWENYEKITI:** Hujatoa Mheshimiwa Sakaya haya sasa toa hoja.

**MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shilingi kwa ajili ya suala hili.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Profesa Maghembe, halafu Mheshimiwa Mhagama, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda halafu Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Riziki, tunaanza na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza niseme suala alilozungumza Mheshimiwa Sakaya linao msingi kwamba ni nishati ambayo kweli tunaihitaji katika matumizi ya nyumbani, lakini ninalotaka kupingana naye ni hili moja kwamba Serikali haijafanya jitihada zozote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyofahamu hasa katika mgodi wa Ngaka, kwanza mpaka sasa hivi kwa mujibu wa majibu ambayo ameyatoa Mheshimiwa Waziri kila siku ukiwa njiani unatoka Makambako mpaka Songea lazima utakutana na malori makubwa yaani makubwa mpaka tunasema sasa hivi barabara zetu zinaharibika. Tani kwa tani kwa ajili ya kusafirisha kwenda Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo kuna jitihada ambazo tayari kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi Barabara sasa ya kutoka Kitai –Lutui, mpaka bandari ya Ndumbi, itaanza kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa ajili ya kuwezesha kufika hayo makaa kiurahisi zaidi kule Kyela. Bandari ya Ndumbi tayari imeshaanza kutengenezwa, kwa hiyo, naona kwamba kimsingi kupanga ni kuchagua, kama tunavyosema fedha zetu zinakwenda kwa mipango ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa huwezi kuwekeza kila mahali halafu kote usipate matunda. Naamini kwamba mipango iliyokaa ni mizuri tuanze na hiyo gesi ambayo tayari tumeshaanza kuitumia na tumeona matunda yake na muda ukifika ukihitaji makaa basi itakuwa ni muda muafaka. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Sakaya na bahati nzuri sisi tunakuamini kwa michango yako tushirikiane irudishe shilingi. Ahsante sana.

**MHE. RIZIKI SHAHARI MNGWALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Naomba niseme vile vile kama neno ambalo Waziri amelitumia sana tuzungumze kama Watanzania na nimesimama hapa kumuunga mkono Mheshimiwa Sakaya kwenye hoja yake kwamba lazima paonekane utashi tangu mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye hoja yake amesema hapa na akaeleza vizuri kabisa hata hiyo gesi mnayosema ndiyo tumeanzia huko, tumewekeza huko, lakini haiendi kutatua matatizo haya ya Watanzania ya kila siku na haiondoi janga na hatari kubwa iliyo mbele yetu ya kuharibu na kumaliza misitu yetu. Hiyo ndiyo *point*, sasa mkipinda kona, mkienda vile tunasema kila siku acheni misamiati, *gymnastic* hizo za *thematics* hazitufikishi popote Waheshimiwa. Hebu tuangalie hoja, tutoe majibu kwenye hoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Sakaya, jibu halijatolewa na hayo maelezo pia mengine ambayo yalisapoti kwa upande ule. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja ya Mheshimiwa Sakaya. Lengo alilopendekeza Mheshimiwa Sakaya msingi wake ni sawasawa na ni mzuri, kwamba kuongeza utumiaji wa makaa ya mawe na gesi nyumbani kutapunguza ukataji wa miti kwa kutengeneza mkaa, jambo hili ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini alichoeleza Mheshimiwa Waziri ni kwamba jambo hili la kutumia mkaa kama nishati ya nyumbani ni lazima lifanyiwe utafiti vizuri kwa sababu yako mambo mawili ambayo ni muhimu kuyazingatia. Jambo la kwanza kuchoma mkaa wa mawe kuna uwezekano wa kuzalisha *sulphur dioxide* nyingi ambayo ni hatari kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kukamilisha utafiti huu na kuangalia njia ambazo zinaweza kupunguza uzalishaji wa *sulphur dioxide* nyumbani sasa makaa hayo yanaweza kutumika. Hata hivyo, liko jambo lingine ambalo ni la kitaalam ni kwamba katika kutumia makaa ya mawe joto ambalo litatokea katika kuyachoma ni kubwa sana ukilinganisha na joto la mkaa huu wa miti na hivyo tunatakiwa tuangalie upya hata vile vifaa ambavyo tunatumia kwa kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, la kufanya tumhimize Mheshimiwa Waziri, aharakishe utafiti unaohusiana na mambo haya ambayo ni muhimu sana, halafu tuondoke uko kwenye mkaa wa miti, tufuate mkaa wa mawe. Kwa hiyo, namwomba dada yangu Sakaya kwa sasa na kwa sababu haiko tayari, ni chakula ambacho hakijaiva, amruhusu Mheshimiwa Waziri aongeze uharaka wa kufanya utafiti ili tuweze kupata nishati hii mbadala. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A.BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namuunga mkono Mheshimiwa Magdalena Sakaya nitoe shilingi ya baba yangu pale. Wabunge kama mtakubaliana nami, tujjulize hapa kati ya makaa ya mawe na gesi kipi kilianza kugundulika. Ni kweli kwamba hatujatoa kipaumbele katika kufanya utafiti wa kutosha na kuhakikisha tunaanza kutumia makaa yetu ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, marehemu Mheshimiwa Deo Filikunjombe, Mungu amrehemu alikuwa akizungumzia sana makaa ya mawe ya Linganga na Mchuchuma katika kipindi chake chote cha Ubunge. Haya kwenye Ilani ya CCM yamewekwa tangu na katika kila aina ya Mpango, lakini hatuoni jitihada



za dhati za kuona ni kiasi gani tunaweza tukatumia makaa ya mawe katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wa Mtwara wamesema, leo Dangote ananunua makaa ya mawe South Africa, tungetengeneza mazingira ya kutosha gesi *plus* makaa ya mawe yangepunguza matatizo ambayo tunayo sasa hivi. Ni *commitment* tu hapa, hii miaka 20 ambayo imepita tumepanga, hatukuweza kufanikiwa mbali na Kamati yetu ya PAC chini ya Mheshimiwa Zitto Kabwe ikafanikisha hata kumpata huyo Mchina. Hatujui mpaka sasa hivi mambo yanaendaje? Mambo haya hayana vyama, ni utaifa, ni hoja nzuri tu ya Mheshimiwa dada yangu Magdalena Sakaya, hili nalo tutaanza kutukanana? 20 years imepita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Magdalena. (*Makofi*)

**WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Lengo la Mheshimiwa Sakaya nadhani anasukumwa na taaluma yake na upenzi wake wa mazingira, yeye analenga kwenye kuhifadhi. Sasa naomba tuongozwe na uhalisia na takwimu, hizo presha za wahifadhi ndiyo zimetupelekea kutumia mkaa wa mawe na baadhi ya viwanda vikiwemo vya Morogoro vikalazimishwa kutumia mkaa wa mawe. Kwa hiyo, mkaa wa mawe unatumika lakini matumizi ya LPG, watu wasichanganye hii gesi ya Mtwara na LPG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mtaalam wa petroli Tanzania, sasa tunatumia LPG kuliko kiasi, Waheshimiwa Wabunge niwaambie, matumizi ya mkaa mjini ndio yanaharibu misitu. Magunia zaidi ya 80,000 huchomeka Dar es Salaam, lakini Dar es Salaam sasa inabadilika kwenda kwenye gesi, hawa warasimu wa Dar es Salaam wenye kipato cha kati wakiweza kutumia gesi misitu yetu itapona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taasisi yangu ya TIRDO ndiko utafiti unafanyika wa namna ya kutumia huu mkaa wa mawe. Kama alivyosema Profesa Maghembe haya mambo yana madhara, hatuwezi kuwa-*subject* watu kwenye madhara, lakini kuna mradi wa kutengeneza mzunguko wa gesi, hii *compress natural gas*. Katika miji ya Dar es Salaam iko na Lindi, iko na Mtwara, yako kwenye maandiko ya Profesa, ukiyasoma imeelezewa, kuna mpango mkubwa kuitoa Dar es Salaam kwenye mkaa kwa kutumia *compress natural gas*, yote hayo yameeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na mtazamo wa Mheshimiwa Sakaya wa kuhifadhi mazingira, lakini mipango iko hapa. Halafu mambo ya Dangote wasiyalete hapa, tunajua kwa nini Dangote alikwenda kuleta mkaa, ni

wakati barabara zetu zimeanguka ndio maana ukimuuliza Mheshimiwa Kolimba akawa anaisisitiza Serikali kwamba tutengeneze barabara kutoka Mchuchuma na Liganga kusudi iweze kuleta mkaa wa mawe wanapohitaji. Mheshimiwa Sakaya rudisha shilingi ya Mheshimiwa Muhongo tupate umeme na kwenye Jimbo lako umeme unakwenda kushughulikiwa na ninapozungumza Mpanda muanze kutengeneza zile nguzo za Mheshimiwa Sakaya umeme uwake. (Makofi/Kicheko)

**MHE. ALLY M. KEISSY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana. Nataka kutoa ufafanuzi, kuna Wabunge wengi na wananchi wengi wanadhani kwamba ile gesi ya Mtwara unaweka moja kwa moja kwenye mitungi na unashusha bei ya mitungi. Ie gesi ya mitungi inatoka kwenye *petrol*, tungegundua *petrol* na dizeli ndio tungepata ile gesi ya mitungi. Kwa hiyo, kusema kwamba kwa sababu gesi ya Mtwara tumepata, ndiyo bei ya mitungi itashuka, ndugu zangu mnapozungumza kitu muwe na ufahamu. (Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile gesi ya Mtwara haihusiki na matumizi ya majumbani kwenye mitungi yetu, kwa hiyo naunga hoja ya Mheshimiwa Waziri, toa shilingi sitegemei kama bei itashuka mpaka tugundue *petrol* ndiyo italeti ile gesi. (Makofi)

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufafanuzi uliotolewa na ndugu Keissy na Mheshimiwa Mwijage ni ufafanuzi mzuri kwa sababu mtoa hoja alijichanganya akadhani hii gesi ya Mtwara ndiyo inawekwa kwenye mitungi, siyo hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ambacho nikisema ni kwamba, makaa ya mawe tunayatumia. Sasa hivi huko Mbeya *Cement* inatumia na Tanga *Cement* wanatumia, ndiyo maana unaona yale malori mahali ambapo hatujaanza kutumia ni kuzalisha umeme mwingi, huo ndio nimesema tarehe 30, badala ya kuita mtu mmoja mmoja tunaingia mikataba mibovu, nimesema tuiweke wazi watu washindane.

Mheshimiwa Mbunge labda nikueleze kitu ambacho siyo lazima nikueleze, ilibidi tukatishe huyu mtu aliyekuwa amepita, unajua hata hizi tenda zetu siyo nzuri, alikuwa amepita mtu ambaye hana uwezo wa kifedha na kitaalam tukakataa. Sisi Wizara tumekataa tukawambia *STAMICO* huyu hana uwezo wa fedha, hana uwezo wa teknolojia, atatumia Kiwira kwenda kutafuta fedha tutaingia kesi. Ndiyo maana tunataka kufanya ushindani wa wazi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye mambo ya mazingira, ni hivi, kwanza dunia ya sasa na nimeona kwamba tutakuja kuelimishwa hapa *Sustainable Development goals. United Nations* yote, dunia nzima yote sasa hivi

kila mtu anakukataza kutumia makaa ya mawe kuzalisha umeme, lakini *projection* China mpaka mwaka 2040 asilimia 30 ya umeme wao utatokana na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuja kuangalia sisi nchi za Kiafrika kuingia kwenye mtego wa kuzuia kutumia makaa ya mawe, tunapiga hesabu hata *carbon per capital* yaani uchafuzi wa mazingira, yaani unatoa zile *toxic gases carbon dioxide* na ni ngapi kwa mtu mmoja kwa mwaka. Ndiyo maana sisi Tanzania hata hiyo *Sustainable Development Millennium Goals*, Tanzania ndio iliwakilisha Afrika kutengeneza. Niliwaeleza japokuwa sisi Tanzania tumeiwakilisha Afrika, sisi tutatumia makaa ya mawe kwa sababu *pollution* yetu *carbon per capital ni zero point one, two tones per person per annum*, tunacheza na tarakimu tu hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tutatumia makaa ya mawe na tayari tunayatumia. Nakuomba ndugu yangu rudisha shilingi ili uweze ukafaidika na umeme. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya naona ana–*smile* labda amesharudisha shilingi, Mheshimiwa Sakaya karibu.

**MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka niweke rekodi sawa, suala lililosemwa na Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Waziri kwamba nimejichanganya, sikujichanganya. Nimesema kwamba sasa hivi Serikali inazungumza habari ya gesi, gesi, lakini hata gesi iliyopo kwa sasa hivi wanayoitumia ni wachache! Nilikuwa nataka kusema kwamba, hata hiyo gesi inayotoka Mtwara ikifika Dar es Salaam bado kwa sababu haitakuwa bure itauzwa, watakaoitumia ni wachache, kwa hiyo lazima tutafute rasilimali ambayo itakuwa *cheap* kwa kila Mtanzania kuweza kumudu. Ndiyo hicho kitu nilikuwa nasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichotaka hapa ni *commitment* ya Serikali kwamba ni ukweli kwamba tunazo nishati mbalimbali, tuna umeme, gesi, mafuta ya taa na vitu vingine, lakini *still* misitu inaharibika. Kwa hiyo, lazima tupate *commitment* kwa namna gani tunaweza tukahoji matumizi ya makaa ya mawe, lini au utaratibu gani utawekwa ili angalau makaa ya mawe yakiwepo ichanganywe sasa na huyu anayetumia gesi na anayetumia kidogo mafuta ya taa angalau tuokoe misitu hiyo ndio hoja yangu. Kwa hiyo, naomba *commitment* ya Serikali, sio kwamba nimejichanganya.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sakaya umerudisha shilingi au bado umeshikia shilingi?

**MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti naomba *commitment* ya Serikali, sija rudisha shilingi.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kidogo nimsaidie, jamani tuongee mambo ya kitaalam, wewe unasema unatunza mazingira, halafu unataka kuunguza makaa ya mawe yazalishe *carbondioxide*, hiyo unatunzaje mazingira? Siwezi kutoa *commitment* nitakuwa siyo mwanasayansi siwezi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wabunge kwa sababu Mheshimiwa Sakaya pamoja na maelezo ya ziada aliyotoa Mheshimiwa Waziri yeye hakuridhika. Kwa hivyo, nitawahoji. Waliosema siyo wameshinda, kwa hivyo shilingi ya Mheshimiwa Waziri inaendelea kubaki. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)

**MHE. RASHID M. CHUA CHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Juhudi za Serikali za kupanua huduma ya umeme tunazona lakini kuna jambo lingine ambalo ni jambo *serious* sana, nalo ni kukatikakatika kwa umeme. Naona si vyema tukaiacha bajeti hii inapita moja kwa moja bila kupata *commitment* ya Serikali katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umeme si nzuri katika baadhi ya Maeneo na inawezekana hakuna hata Mbunge mmoja anayeweza kusimama akasema kwake umeme haukatiki. Ka maana hiyo basi tunapozungumzia umeme kwa mfano, umeme wa gesi tunazungumzia chanzo chake katika Mikoa ya Kusini, Mtwara na Lindi ambao kimsingi umeme unakatika kila siku zaidi ya mara tatu. Sasa hivi tunapozungumza hususan katika Majimbo yetu kule Masasi peke yake umeme umeshakatika mara mbili tunasubiri ya tatu na ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itoe kauli ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua muda wetu unakimbia sana ili tupate muda wa Waziri kuweza kujibu naomba ufupishe hoja yako tafadhali.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa naomba Serikali itoe kauli hili jambo litakwisha lini la kukatika katika kwa umeme katika Mikoa ya Kusini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ufafanuzi kidogo tu kwa Mheshimiwa Chuachua kuhusiana na suala hili la kukatikakatika kwa umeme. Katika jibu langu la msingi nimeeleza, kwanza

kabisa tunakubaliana kwamba ni kweli kuna maeneo bado umeme unakatikakatika na sababu za msingi tumezieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, za kwanza kuna nguzo ambazo ni mbovu TANESCO wanaendelea kurekebisha na kwa sasa hivi hatua ambayo Serikali imechukua TANESCO imeanzisha kampuni tanzu, ya kutengeneza concrete pole, kwa hiyo, itaanza sasa kutengeneza nguzo ambazo ni za concrete, ambazo hazitakuwa zinaanguka, sasa kuanguka kwa nguzo kwa sehemu nyingine, kunasababisha pia kukatika katika kwa umeme, hilo ni la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, ni low voltage kwamba umeme tulionao kwa sasa ni wa kiwango cha chini, kwa maeneo mengi sana tunatumia kilovolt 132 ambao ndio wa juu. Sasa mkakati wa kuondokana na hivyo, tumesema kuanzia mwakani umeme wa kilovolt 400 unaanza kutengenezwa, kwa hiyo, kufikia mwaka 2018/2019 uhakika wa umeme kukatikakatika utakuwa umekoma kabisa hapa nchini. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chuachua ameelewa, kwa hiyo tunakushukuru.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muda uliobaki sasa hatutaweza kuendelea na mjadala. Pamoja na kwamba majina ya watu ambao wangependa kusema katika kifungu hiki. Kwa hiyo, tutaingia kwenye utaratibu wa kupitisha mafungu yote, kwa mujibu wa Kanuni ya 104. (Makofi)

## **FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI**

Kif. 1001 - Admin. and HR. Mgt. ... ..	.sh. 4,770,307,000/=
Kif. 1002 - Finance and Accounts ... ..	.sh. 1,097,940,000/=
Kif. 1003 - Policy and Planning ... ..	.sh. 1,161,400,000/=
Kif. 1004 - Internal Audit Unit ... ..	.sh. 539,939,000/=
Kif. 1005 - Legal Services ... ..	.sh. 718,805,000/=
Kif. 1006 - Govt. Communication Unit ... ..	.sh. 591,274,000/=
Kif. 1007 - Procurement Mgt. Unit ... ..	.sh. 520,966,000/=
Kif. 1008 - Environment Management Unit ...	.sh.455,100,000/=
Kif.1009 - Mgt. Information System ... ..	.sh.966,480,000/=
Kif. 2001- Minerals ... ..	.sh. 23,919,450,000/=
Kif. 2002 - Madini Institute ... ..	.sh. 2,156,876,000/=
Kif. 2004 - TZ. Diamond (TANSORT)... ..	.sh. 510,204,000/=
Kif. 2005 - Estern Zone . ... ..	.sh. 1,153,156,000/=
Kif. 2006 - Western Zone ... ..	.sh.645,300,000/=
Kif.2007 - Lake Zone ... ..	.sh.858,474,000/=
Kif. 2008 - Northern Zone ... ..	.shs.940,672,000/=
Kif.2009 - Southern Zone ... ..	.sh.564,830,000/=
Kif.2010 - Central Western Zone ... ..	.sh.757,760,000/=

Kif. 2011 - Central Zone ... ..sh.603,170,000/=

Kif. 2012 - Southern Western Zone ... ..sh.589,830,000/=

Kif. 2013 - Lake Victoria Eastern Zone ... .. sh.628,270,000/=

Kif. 2014 - Lake Nyasa Zone ... .. sh.631,496,000/=

Kif. 3001 - Energy and Petroleum ... ..sh. 21,447,149,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

## MIPANGO YA MAENDELEO

### FUNGU 58 - WIZARA YA NISHATI NA MADINI

**MWENYEKITI:** Katibu hebu soma upya.

Kif. 2001- Minerals ... ..sh. 18,600,000,000/=

Kif. 2002 - Madini Institute .. .. sh. 6,000,000,000/=

Kif. 3001 - Energy and Petroleum ... ..sh. 1,031,754,669,000/=

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

**NDG. CHARLES MLOKA - KATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

(Bunge lilirudia)

**NAIBU SPIKA:** Tukae, mtoa hoja taarifa.

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Hivyo basi, naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (Makofi)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Yalipitishwa na Bunge)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nichukue nafasi hii, kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa bajeti yao kupita kwa kishindo. Pia nichukue nafasi hii kuwataka Wizara hii tena kwa sababu Bunge limepitisha maombi ya bajeti kama mlivyoyaleta na linataraji wakati ule ambapo majukumu yake ya kuisimamia Serikali yatakapofika, basi wataletewa taarifa ambazo zitakuwa zinaendana na kile ambacho wamekipitisha leo.

Lingine tangazo dogo, linatoka kwa Mheshimiwa Lucia Michael Mlowe ambae amepoteza pochi ndogo nyeusi, ndani yake kulikuwa na *diary* ambayo ina kadi za benki na vitambulisho, anaomba mtu yeyote aliyeiona tafadhali ampatie au apeleke Ofisi ya Katibu halafu yeye atapatiwa. Ama kama hukuiona lakini ukaiona mahali tukitoka hapa tafadhali kadi zake za benki ziko humo atahitaji taarifa zake.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kusema hayo, upo mwongozo ulikuwa umeombwa leo asubuhi na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, kuhusu suala la Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, kutojibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja kwa ukamilifu.

Waheshimiwa Wabunge, mchana wa leo tarehe 20 Mei, 2016 kabla ya kusitisha shughuli za Bunge, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini aliomba mwongozo wa Spika, bila kutaja Kanuni husika kuhusu majibu ya swali namba 205 ambalo lilielekezwa katika kujua ni kwa namna gani Serikali imejipanga kuboresha nyumba za askari Magereza na Polisi, kwani jibu lililotolewa linahusu uboreshaji wa nyumba za Polisi pekee.

Katika maelezo yake Mheshimiwa Selasini alieleza ifuatavyo nanukuu:

“Askari Magereza wa nchi hii, wanaishi katika hali duni sana na nitoe mfano tu katika Jimbo langu wanaishi katika vibanda vya mabanzi, ambavyo kule tunajengea nyumba za nguruwe. Huu ni udhalilishaji mkubwa sana, ni kwa nini usitolewe mwongozo kwamba kwa ajili ya Polisi uletwe mchanganuo na ionekane kwamba Polisi watajengewa kiasi gani na Magereza kiasi gani, tena kwenye maeneo yapi, ambayo hawa askari wa magereza wanaishi kwa kudhalilika.”

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuombwa Mwongozo huo, kiti kilielekeza kwa majibu kuwa, majibu ya Mwongozo huo yatatolewa baadaye.

Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya ufafanuzi zaidi, naomba kurejea swali namba 205 liloulizwa na Mheshimwa Devotha Mathew Minja, kama ifuatavyo:-



Askari wa Jeshi la Polisi na Magereza wanaoishi katika nyumba chakavu zisizokuwa na hadhi, ikilinganishwa na kazi zao wanazozifanya kwa jamii; je, Serikali ina mpango gani kuwaboresha askari makazi?

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitia kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge, ilibainika kuwa si kwamba swali la Mheshimiwa Mbunge halikujibiwa kikamilifu na Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ila majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusu swali husika, hayakutoa mchanganuo wa nyumba ngapi zitajengwa kwa upande wa Askari wa Jeshi la Magereza.

Hivyo kwa kuzingatia Mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Mbunge na uzito wa swali lililoulizwa kiti kimeamua kuelekeza swali hilo lirudiwe kuulizwa katika kikao cha tarehe 23 Mei, 2016, Ili Serikali iweze kutoa majibu kwa ufasaha zaidi ikiwa ni pamoja na kutoa mchanganuo wa nyumba ngapi za askari magereza zitajengwa na katika maeneo gani, huo ndio mwongozo wa kiti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, naambiwa hapa Mheshimiwa aliyepoteza pochi ameshapatiwa na ameshasainishwa, kwa hiyo ameshaipata.

Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho tarehe 21 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi.

*(Saa 2.29 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumamosi,  
Tarehe 21 Mei, 2016, Saa Tatu Asubuhi)*